# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU


## IMEANDIKWA NA: SHEIKH MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYA

## IMETAFSIRIWA NA: SHEIKH HASAN MWALUPA

### IMEHARIRIWA NA: USTADH ABDALLAH MOHAMED

### IMEPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: UKHT PILI RAJABU


### UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI

Kitabu hiki kilichoko mikononi mwako hivi sasa ni juhudi ya miaka mingi sana ya watu waliojitolea kuona kazi hii imefanikiwa bila ya kumsahau Marhum Abu Muhammad wa London.

Kama lilivyo jina la Tafsiri ndivyo ilivyo Tafsiri yenyewe ambayo mwanachuoni huyu mahiri kabisa aliyeifafanua ni mtu aliyebobea katika fani zote ambazo mfasiri (Mfafanuzi) anatakiwa awe nazo.

Sheikh Muhammad Jawad Mughniyya ameonesha cheche zake katika vitabu vingi alivyoviandika katika maudhui mbali mbalimbali na hivyo kujipatia wasomaji wengi sana.

Msomi huyu, mwenye fikra huru na anayetetea kile anachokiamini, ni mtu mwenye mawazo mapana na kuyaangalia mambo kwa undani sana, kipaumbele chake ni katika maslahi ya umma huu na amejaribu sana kwenda na wakati.

Sifa kubwa pekee ya mwanachuoni huyu ni kuwa yeye hakujihusisha sana na kung'ang'ania madhehebu fulani tu, labda hii yatokana na wadhifa wake wa ukadhi aliokuwa nao katika nchi ya Lebanon ambayo ina madhehebu mengi, ambapo sula la madhehebu ni nyeti nchini humo, hata hivyo yeye aliweza kuamua matatizo ya watu kwenye ofisi yake kulingana na madhehebu yao pale walipomwendea. Hiyo ilimsaidia sana hata kuweza kutoa kitabu kitwacho Al-Fiqh a'laa madhaahabil-khamsah (Fikhi ya madhehebu matano) yaani ya Hanafi, Maaliki, Shafi, Hambali na Shia (ambacho twataraji kitatoka kwa lugha ya kiswahili hivi karibuni Inshaallah).

Jambo lililotupa msukumo wa kukifasiri kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili ni zile faida nyingi atakazozipata msomaji na kujua mambo mengi na ya ajabu yaliyo mapya kwake ambayo si rahisi kuyapata kwa wafasiri wengine.

Msomaji atapata faida katika fani za Sayansi, Siasa, Historia, Mashairi, visa vizuri, na Saikolojia miongoni mwa mengine; ndiyo maana msomaji atashangaa kidogo anapoisoma Tafsiri hii atakapoona mwandishi amewataja na kuwanukuu watu kama kina Mfalme Edward, wanasayansi kama kina Enstein, wasanii kama Charlie Champlin (Mchekeshaji maarufu), na wengineo, hali inayoifanya tafsiri hii kuwa ni ya kipekee kabisa.

Mtindo alioutumia mwandishi ni sahali uliokusudiwa watu wa tabaka mbalimbali, wanavyuoni na watu wa kawaida.

Nia yetu ni kukigawanya kitabu hiki bure lakini tumelazimika kukiuza kwa bei nafuu ili kurudisha gharama za uchapishaji.

Mwisho: Shukrani kubwa iwaendee bila ya kuwataja watu waliojitolea usiku na mchana, jopo la wafasiri, wahariri, wachapaji, waliotupa moyo na kutoa maoni yao na walioisimamia ili kuhakikisha kwamba kitabu kimemfikia msomaji.

## MAKOSA YA CHAPA

Sikumbuki kama nimewahi kusoma kitabu kilichotoka kupigwa chapa, cha zamani au cha sasa, bila ya kukuta makosa ya chapa, Nafikiri sitasoma kitabu kisichokuwa hivyo. Nimejaribu sana kuliepuka hilo katika tungo zangu, lakini sikufanikiwa.

Nilikuwa sifikirii kama ninaweza kuona makosa haya katika maandishi ya msahafu mtukufu, kama yale yaliyo katika baadhi ya chapa; kwa mfano neno yabswutu kwa swad, badala ya yabsutu kwa sin, na katika chapa ya Tafsir Arrazi ya Misr ya mwaka 1935, Sura ya (2:146), Imeandikwa La Ya'alamuun, (hawajui) badala ya Ya'alamuun (wanajua). Mfano wa makosa haya hausameheki.

Katika Tafsir Al-Manar, chapa ya Pili, sura (5:212), imeandikwa Fawqahum ila yawmil qiyama badala ya Fawqahum yawamal qiyama. Hatuwezi kusema kosa hili ni kubwa zaidi kuliko lile.

Lakini mkosaji atatuletea udhuru kwa msemo mashuhuri huko kwetu Jabal amil 'Makosa ya chapa.'

Katika Tafsiri Majmau chapa ya Urfan, Sura (46:15), imeandikwa: Hatta idha balagha arbai' na sanah badala ya: Hattaidha balagha ashuddahu arbai ' na sanah"

Kusema hivi sio kama ninajitetea kutokana na makosa ya chapa atakayoyakuta msomaji katika kitabu hiki, ijapokuwa naomba msamaha kama litatokea hili, lakini makusudio yangu hasa ni kumwambia yule atakayefungua macho yake kwenye makosa ya matamko na kuufungia macho uzuri wa maana.

Vilevile ninamwambia yule ambaye siku moja aliniambia: "Vitabu vyako vimejaa makosa ya chapa.” Kama kwamba hakuna kitu chochote katika vitabu hivyo isipokuwa makosa ya chapa tu. Wote hao ninawaambia: Mungu awasamehe na aniongoze mimi na nyinyi.

Vyovyote iwavyo, mimi ninaomba msamaha kutokana na makosa ya kifikra na ya chapa. Anasema Amirul Muminiin (a.s): **"Watu wote ni wapungufu wenye kuchanganyikiwa, isipokuwa yule aliyehifadhiwa na Mwenyezi Mungu."** Na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye mwenye jukumu la kunikubalia yale niliyoyapatia na kunisamehe niliyakosea, kwa jaha ya Mtume na kizazi chake, ziwashukie rehema na amani (Amin).

**MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYAH**

1

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

Sura Ya Arubaini Na Sita: Surat Al-Ahqaf. Imeshuka Makka. Ina Aya 35.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

حم ﴿١﴾

1. Haa miim.

تَنزِيلُ الْكِتَابِ مِنَ اللَّـهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ﴿٢﴾

2. Uteremsho wa Kitabu umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

مَا خَلَقْنَا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ وَأَجَلٍ مُّسَمًّى وَالَّذِينَ كَفَرُوا عَمَّا أُنذِرُوا مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾

3. Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake ila kwa haki na kwa muda uliowekwa. Na wale waliokufuru wanayapuuza yale wanayoonywa.

قُلْ أَرَأَيْتُم مَّا تَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّـهِ أَرُونِي مَاذَا خَلَقُوا مِنَ الْأَرْضِ أَمْ لَهُمْ شِرْكٌ فِي السَّمَاوَاتِ ائْتُونِي بِكِتَابٍ مِّن قَبْلِ هَـٰذَا أَوْ أَثَارَةٍ مِّنْ عِلْمٍ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿٤﴾

4. Sema: Je, mnawaona wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu? Nionyesheni wameumba nini katika ardhi; au wana shirika katika mbingu? Nileteeni Kitabu kilicho kuwa kabla ya hiki, au athari yoyote ya ilimu, ikiwa mnasema kweli.

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُو مِن دُونِ اللَّـهِ مَن لَّا يَسْتَجِيبُ لَهُ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَن دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ ﴿٥﴾

5. Na ni nani mpotofu mkubwa kuliko yule anayeomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ambaye hatamjibu mpaka Siku ya Kiyama, Na wala hawatambui maombi yao.

وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِعِبَادَتِهِمْ كَافِرِينَ ﴿٦﴾

6. Na watakapokusanywa watu watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao.

## IKO WAPI DALILI IKIWA NYINYI NI WA KWELI?

**Aya 1-6**

### MAANA

Haamiim. Uteremsho wa Kitabu umetoka kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

Imetangulia kwa herufi zake katika Juz. 25 (45:1) na Juz. 23 (39:1).

Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake ila kwa haki na kwa muda uliowekwa.

Mwenyezi Mungu ni mwenye hekima, haumbi kitu ila kwa hikima, na ni muhali kuumba kwa mchezo. Ameuumba ulimwengu na yaliyomo ndani yake kwa hikima na malengo sahihi. Akauwekea muda maalum wa kwisha kwake; baada yake ni hisabu na malipo katika nyumba ya pili.

Umetangulia mfano wake katika Juz. 21 (30:8).

Na wale waliokufuru wanayapuuza yale wanayoonywa.

Mwenyezi Mungu anawahofisha wakosefu na siku ya Kiyama na vituko vyake, na akawawekea dalili wazi, lakini wakakataa isipokuwa inadi na jeuri.

Je, mnawaona wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu? Nionyesheni wameumba nini katika ardhi; au wana shirika katika mbingu?

Maana ni kuwa nipeni habari enyi waabudu masanamu, ni jambo gani liliowafanya muyafanye masanamu ni miungu na kuyaabudu. Je, ni kwa kuwa yameumba kitu katika ardhi na mbinguni au yalishirikiana na Mwenyezi Mungu katika kuumba mbingu au sehemu yake?

Nileteeni Kitabu kilicho kuwa kabla ya hiki cha Qur'an; kama vile Tawrat, Injil n.k., kinachosema kuwa masanamu ni washirika wa Mwenyezi Mungu katika kuumba kwake au kuwa yanaweza kuwaombea kwa Mungu au kuwa na utajo wowote.

Au athari yoyote ya ilimu, ikiwa mnasema kweli.

Ikiwa hamna dalili ya nukuu yoyote, je mnayo dalili ya kiakili kusadikisha myasemayo na kuyafanya sahihi mnayoyaabudu?

Umetangulia mfano wake katika Juz. 22 (35:40).

## KUABUDU MASANAMU WAKATI MAENDELEO YA KUFIKA ANGANI

**Unaweza kuuliza**: Kwa nini Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametilia umuhimu sana kuwarudi wenye kuabudu masanamu na mizimu kwenye Aya hii na nyinginezo, na hali hili sio jambo zito sana na liko wazi kabisa? Kuupinga uungu wa masanamu si ni jambo liliowazi; sawa na kuukanusha upofu na uoni na giza na nuru?

**Jibu**: Kuyatukuza masanamu na kuyaabudu, kumekua ni sehemu ya maisha ya mtu kuanzia zama na Nuh (a.s) mpaka zama za Muhammad **(s.a.w.w)**, ambapo baina ya wawili hao kuna maelefu ya miaka; bali mpaka hivi sasa kwenye maendeleo ya kufika angani, bado masanamu yameenea mashariki mwa ardhi na magharibi yake.

Masanamu yaliyoko kwenye nyumba za ibada, siku hizi, kwenye njia panda na kwenye vilele vya milima. Pia mapicha kwenye kuta yaliyoenea huku na huko na kwenye vitabu vya kumbukumbu si ni aina ya kuabudu masanamu?

Umetukuka ukuu wa Muhammad **(s.a.w.w)** katika kumtukuza mtu kwa kumsafisha na ibada ya masanamu yaliyotengenezwa na mikono yake. Mshairi anasema:

Namshangaa insani mchonga jiwe ambaye
Hulifanya rahamani Mungu aabudiwaye
Huku adhani moyoni hudhuru na kumfaaye
Si aabudu mikono ilochonga hilo jiwe
Hayo si ndio maono lau ataka ajuwe
Basi na iwe mikono ya kuabudu si jiwe

Ndiyo imechonga jiwe kama anavyoelewa

Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanaowaomba, badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawatawaitikia mpaka Siku ya Kiyama.

Makusudio ya kusema 'mpaka siku ya Kiyama,' ni milele na kutowezekana kujibu kabisa. Maana ni kuwa hakuna mjinga aliyepotea zaidi kuliko yule anayeabudu kisichosikia anayeita wala kumjibu anayeomba.

Na wala hawatambui maombi yao.

Washirikina wanaabudu masanamu, lakini masanamu hayana habari nao, wala hayana hisia yoyote.

Na watakapokusanywa watu watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao.

Vile vile siku ya Kiyama wakati watu watakapofufuliwa kwa hisabu na malipo, miungu ya washirikina itajitenga nao na kuwakataa. Tazama Juz.11 (10:28).

وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ قَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ هَـٰذَا سِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٧﴾

7. Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi, wale waliokufuru husema juu ya haki inapowajia: Huu ni uchawi ulio wazi.

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ ۖ قُلْ إِنِ افْتَرَيْتُهُ فَلَا تَمْلِكُونَ لِي مِنَ اللَّـهِ شَيْئًا ۖ هُوَ أَعْلَمُ بِمَا تُفِيضُونَ فِيهِ ۖ كَفَىٰ بِهِ شَهِيدًا بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۖ وَهُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿٨﴾

8. Au wanasema: Ameizua! Sema: Ikiwa nimeizua mimi, basi nyinyi hamwezi kunifaa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Yeye anajua zaidi hayo mnayoropokwa; anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi. Na Yeye ni Mwingi wa Maghufira, Mwenye kurehemu.

قُلْ مَا كُنتُ بِدْعًا مِّنَ الرُّسُلِ وَمَا أَدْرِي مَا يُفْعَلُ بِي وَلَا بِكُمْ ۖ إِنْ أَتَّبِعُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ وَمَا أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٩﴾

9. Sema, mimi si kioja miongoni mwa Mitume. Wala sijui nitakavyofanywa mimi wala nyinyi. Mimi nafuata niliyopewa Wahyi tu, wala mimi si chochote ila ni mwonyaji, mwenye kubainisha.

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِن كَانَ مِنْ عِندِ اللَّـهِ وَكَفَرْتُم بِهِ وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِّن بَنِي إِسْرَائِيلَ عَلَىٰ مِثْلِهِ فَآمَنَ وَاسْتَكْبَرْتُمْ ۖ إِنَّ اللَّـهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠﴾

10. Sema: Mwaonaje yakiwa haya ni kweli yametoka kwa Mwenyezi Mungu, nanyi mmeyakataa, na alishuhudia shahidi miongoni mwa Wana wa Israili juu ya mfano wa haya, na akaamini, na nyinyi mnafanya kiburi? Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu.

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ آمَنُوا لَوْ كَانَ خَيْرًا مَّا سَبَقُونَا إِلَيْهِ ۚ وَإِذْ لَمْ يَهْتَدُوا بِهِ فَسَيَقُولُونَ هَـٰذَا إِفْكٌ قَدِيمٌ ﴿١١﴾

11. Na wale ambao wamekufuru waliwaambia wale ambao wameamini: Lau hii ingelikuwa ni heri, wasingelitutangulia. Na walipokosa kuongoka kwayo basi wakasema: Huu ni uzushi wa zamani.

وَمِن قَبْلِهِ كِتَابُ مُوسَىٰ إِمَامًا وَرَحْمَةً ۚ وَهَـٰذَا كِتَابٌ مُّصَدِّقٌ لِّسَانًا عَرَبِيًّا لِّيُنذِرَ الَّذِينَ ظَلَمُوا وَبُشْرَىٰ لِلْمُحْسِنِينَ ﴿١٢﴾

12. Na kabla yake kilikuwapo Kitabu cha Musa, kuwa kiongozi na chenye rehema. Na hiki ni Kitabu chenye kusadikisha cha lugha ya kiarabu, ili kiwaonye wale waliodhulumu, na kiwe ni bishara kwa watendao mema.

## AU WANASEMA WAMEYATUNGA?

**Aya 7 – 12**

### MAANA

Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi, wale waliokufuru husema juu ya haki inapowajia: Huu ni uchawi ulio wazi.

Makusudio ya ishara zetu na haki ni Qur'an. Maana ya zilizo wazi ni kuwa Aya za Qur'an ziko wazi hazikufunganafungana. Lakini pamoja na kuwa Qur'an iko wazi na kudhihiri dalili kuwa ni haki, bado wazushi, walio mataghuti na wapenda anasa wameipa sifa ya uchawi ulio waziwazi. Si kwa lolote ila ni kwa kuwa imewafanya wao kuwa sawa na watu wengine. Umetangulia mfano wa hayo katika Aya kadhaa huko nyuma.

Au wanasema: Ameizua! Sema: Ikiwa nimeizua mimi, basi nyinyi hamwezi kunifaa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu.

Je, washirikina wanadai kuwa umeizua hii Qur'an ewe Muhammad **(s.a.w.w)**? Waambie: vipi nimzulie Mungu uwongo na hali mimi ndiye ninayemuhofia zaidi? Je, mtanikinga na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na adhabu yake ikiwa nitasema uwongo au kumzulia? Aliyasema haya Mtume kutegemea vile wanavyomjua yeye jinsi anavyochukia uwongo na tabia nyinginezo mbaya.

Yeye anajua zaidi hayo mnayoropokwa; anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi.

Hakifichiki kitu katika kauli zenu na vitendo vyenu nanyi mtahisabiwa navyo; na Mwenyezi Mungu ananijua mimi na nyinyi, kwa hiyo anashudia ukweli na uaminifu kwangu na anashuhudia uwongo na hiyana kwenu

Na Yeye ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

Atawasamehe na kuwachanganya kwenye rehema yake ikiwa mtatubia na kurejea.

Sema: mimi si kioja miongoni mwa Mitume.

Mimi si wa kwanza kufikisha ujumbe wa Mungu. Wamenitangulia mitume na manabii wengi

Wala sijui nitakavyofanywa mimi wala nyinyi.

Mtume **(s.a.w.w)** anajua hali yake na hali ya washirikina huko Akhera. Kwa sababu Mwenyezi Mungu alimpa habari ya hilo; kama zinavyoeleza Aya kadhaa; mbali ya kuwa ilimu hii ni katika nyenzo za utume. Zimekuja Hadith mutawatir, kwamba Mtume aliwabashiria pepo watu kadhaa.

Kwa hiyo basi Maana ya Aya ni kuwa Mtume hajui yatakayowatokea katika maisha ya duniani na atawatia mtihani gani Mwenyezi Mungu. Vile vile hajui kuwa Mwenyezi Mungu atawaadhibu hapa duniani au ataahirisha adhabu yao mpaka siku ya ufufuo.

Mimi nafuata niliyopewa Wahyi tu, wala mimi si chochote ila ni mwonyaji mwenye kubainisha.

Sio kazi ya muonyaji kujua ilimu ya ghaibu; isipokuwa yeye anafikisha anayopewa wahyi na Mwenyezi Mungu kuhusiana na yale yatakayowatokea washirikina.

Ieleweke kuwa Aya hii ilishuka kabla ya kushuka Aya inayosema kuwa mwisho ni wa dini ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wajapochukia washirikina. Au pengine ni miongoni mwa mifumo ya kutoa mwito kwa hikima na mawaidha mazuri.

Sema: Mwaonaje yakiwa haya ni kweli yametoka kwa Mwenyezi Mungu, nanyi mmeyakataa, na alishuhudia shahidi miongoni mwa Wana wa Israili juu ya mfano wa haya, na akaamini, na nyinyi mnafanya kiburi? Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu madhalimu.

Sura hii tuliyo nayo imeshuka Makka isipokuwa Aya hii tuliyo nayo, ilishuka Madina kwa ajili ya Abdullah bin Salim, aliposilimu Madina. Yeye alikuwa mwanachuoni mkubwa wa Wana wa Israil. Haya ndiyo yaliyoelezwa kwenye tafsiri nyingi.

Maana ni sema ewe Muhammad kuwaambia wale wanaodai kuwa Qur'an ni uchawi uliozushwa, hebu niambieni itakuwaje hali yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ikithibiti kuwa Qur'an ni haki na kweli na akaiamini mwana wa chuoni katika wana wa Israil; kama vile Abdullah bin Salam ambaye anatambua siri za wahyi na kushuudia kuwa mafunzo ya Qur'an ni kama mafunzo ya Tawrat iliyoteremshwa na Mwenyezi Mungu kwa Musa? Basi mtakuwaje mkibaki na upotevu wenu na inada yenu? Je mjidhulumu kwa hiyari yenu na kujianika kwenye adhabu ya Mwenyezi Mungu?

Na wale ambao wamekufuru waliwaambia wale ambao wameamini: Lau hii ingelikuwa ni heri, wasingelitutangulia.

Watu wengi walioitikia mwito wa Mtume **(s.a.w.w)**, mwanzo mwanzo wa mwito wa Uislamu, walikuwa ni miongoni mwa wanyonge. Kwa hiyo mamwinyi wakaifanya hiyo ni sababu ya kuituhumu risala ya Mtume. Kwa sababu, wanavyodai, ni kuwa haki ni ile inayokubaliwa na vigogo, wala sio kuwa watu wajulikane kwa kuwa na haki. Kila wanalolilifanya matajiri ndio haki na wanalolilifanya wengine ni batili. Hayo ndiyo madai yao, lakini kila mwenye kuipinga haki itamshinda.

Ndio maana hazikupita siku mtumwa wa kihabeshi akapanda kwenye mgongo wa Al-Ka'aba akinadi Lailaha illallah Muhammadurrasulullah (Hakuna Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu, Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu). Na Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** akayavunja masanamu na kuyatupa chini ya nyayo zake huku akisema: "Haki imefika na batili imeondoka, hakika batili ni yenye kuondoka."

Katika Tafsir Arrazi, imeandikwa kuwa mjakazi wa Amru alisilimu na alikuwa akimpiga mpaka anachoka. Basi makafiri wakasema: "Kama Uislamu ungelikuwa ni kheri asingetutangulia majakazi wa Amru." Lakini Amru mwenyewe alisilimu badaye, akapigana vita vya Roma na Fursi.

Na walipokosa kuongoka kwayo basi wakasema: Huu ni uzushi wa zamani.

Wanazungumziwa makafiri wa kikuraishi. 'Kwayo' ni hiyo Qur'an. Mataghuti waliisifu kuwa ya zamani, kwa vile, kwa madai yao, wanasema ni ngano za watu wa kale zilizopitwa na wakati.

Walisema hivi sio kwa lolote isipokuwa wao hawaamini isipokuwa masilahi yao na chumo lao tu, na Qur'an inapinga na kupiga vita hayo.

Na kabla yake kilikuwapo Kitabu cha Musa, kuwa kiongozi na chenye rehema. Na hiki ni Kitabu chenye kusadikisha cha lugha ya kiarabu, ili kiwaonye wale waliodhulumu, na kiwe ni bishara kwa watendao mema.

Qur'an ni kama Tawrat iliyomshukia Musa. Vitabu vyote hivyo viwili vinaongoza kwenye haki na ni rehema kwa mwenye kuviamini na avitumia kwa mujibu wake. Tawrat ilitoa habari za kuja Muhammad:

الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِندَهُمْ فِي التَّوْرَاةِ وَالْإِنجِيلِ يَأْمُرُهُم بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ عَنِ الْمُنكَ رِ

﴿١٥٧﴾

"Ambaye wanamkuta ameandikwa kwao katika Tawrat na Injili, ambaye anawaamrisha mema na anawakatazamaovu." Juz. 9 (7:157).

Vile vile Qur'an inaisadikisha Tawrat hii na inatamka kwa lugha yenu, enyi waarabu, ikimuonya na adhabu yule atakayefanya uovu na kumpa habari njema za thawabu yule mwenye kufanya wema. Basi vipi mara mnasema ni uchawi na mara nyingine ni ngano za watu wa kale; mbona hamyasemi hayo kwa Tawrat?

2

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّـهُ ثُمَّ اسْتَقَامُوا فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٣﴾

13. Hakika wale waliosema: Mola wetu ni Mwenyezi Mungu; kisha wakawa na msimamo, hawatakuwa na hofu, wala hawatahuzunika.

أُولَـٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ خَالِدِينَ فِيهَا جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾

14. Hao ndio watu wa Peponi, watadumu humo, ni malipo kwa waliyokuwa wakiyatenda.

وَوَصَّيْنَا الْإِنسَانَ بِوَالِدَيْهِ إِحْسَانًا ۖ حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا ۖ وَحَمْلُهُ وَفِصَالُهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا
حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ أَشُدَّهُ وَبَلَغَ أَرْبَعِينَ سَنَةً قَالَ رَبِّ أَوْزِعْنِي أَنْ أَشْكُرَ نِعْمَتَكَ الَّتِي أَنْعَمْتَ عَلَيَّ وَعَلَىٰ
وَالِدَيَّ وَأَنْ أَعْمَلَ صَالِحًا تَرْضَاهُ وَأَصْلِحْ لِي فِي ذُرِّيَّتِي ۖ إِنِّي تُبْتُ إِلَيْكَ وَإِنِّي مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٥﴾

15. Na tumemuusia mtu awafanyie wema wazazi wake wawili. Mama yake amebeba mimba yake kwa taabu, na akamzaa kwa taabu. Na kubeba mimba kwake na kumwachisha ziwa ni miezi thalathini. Hata anapofika kukomaa kwake, na akafikilia miaka arubaini. Husema: Mola wangu! Nizindue nishukuru neema yako uliyonineemesha na wazazi wangu, na nipate kutende mema unayoyaridhia. Na unitengenezee dhuriya zangu. Hakika mimi nimetubu kwako, na hakika mimi ni miongoni mwa Waislamu.

أُولَـٰئِكَ الَّذِينَ نَتَقَبَّلُ عَنْهُمْ أَحْسَنَ مَا عَمِلُوا وَنَتَجَاوَزُ عَن سَيِّئَاتِهِمْ فِي أَصْحَابِ الْجَنَّةِ ۖ وَعْدَ
الصِّدْقِ الَّذِي كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿١٦﴾

16. Hao ndio tunaowatakabalia bora ya vitendo walivyovitenda. Na tunayasamehe mabaya yao, watakuwa miongoni mwa watu wa Peponi. Miadi ya kweli hiyo waliyoahidiwa.

## KUWAFANYIA WEMA WAZAZI WAWILI

**Aya 13 – 16**

### MAANA

Hakika wale waliosema: Mola wetu ni Mwenyezi Mungu; kisha wakawa na msimamo, hawatakuwa na hofu, wala hawatahuzunika.

Katika Juz. 17 (21:103) Mwenyezi Mungu amesema: "Hiyo fazaa kubwa haitawahuzunisha. Na Malaika watawapokea: Hii ndiyo siku yenu mliyokuwa mkiahidiwa."

Na katika Aya hii tuliyo nayo, anasema Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuwa: hao ni wale walioshikamana na dini ya Mwenyezi Mungu kiitikadi, kikauli na kivitendo katika maisha ya duniani. Jumla hii imetajwa hivi ilivyo na tumeifafanua zaidi katika Juz. 21 (41:30).

Hao ndio watu wa Peponi, watadumu humo, ni malipo kwa waliyokuwa wakiyatenda.

Hao ni wale walioamini na wakawa na msimamo. Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: 'Kwa waliyokuwa wakiyatenda,' ni msisitizo wa kuwa hakuna imani wala msimamo bila ya matendo.

Na tumemuusia mtu awafanyie wema wazazi wake wawili. Mama yake amebeba mimba yake kwa taabu, na akamzaa kwa taabu.

Yaani amepata matatizo mengi alipokuwa na mimba, wakati wa kumzaa na hata kwenye malezi pia. Kuna riwaya inayosema kuwa haki ya mama ni zaidi ya haki ya baba, kwa sababu alimbeba wakati ambapo hakuna yoyote wa kumbeba, akamkinga kwa masikio na macho na viungo vyote, akiwa na furaha. Akakubali awe na njaa, lakini mwanawe ashibe, awe na kiu lakini anywe, awe uchi lakini avae. Basi shukrani na wema ziwe kwa kiasi hicho.

Mwanzoni mtoto alikuwa akiona kuwa ni wajibu wake kuwasikiliza na kuwatii, wazazi wake, lakini sasa mtoto anaona kuwa ni lazima wazazi wake wamtii na kumnyenyekea mtoto na kusikiliza amri zake. Yametangulia maelezo ya kuwafanyia wema wazazi wawili katika Juz. 1(2:83), Juz. 5 (4:36), Juz. 8 (6:151) na Juz. 15 (17:23).

Na kubeba mimba kwake na kumwachisha ziwa ni miezi thalathini.

Tukiunganisha Aya hii na ile isemayo:

وَفِصَالُهُ فِي عَامَيْنِ ﴿١٤﴾

"Na kumwachisha ziwa miaka miwili." Juz. 21 (31:14),

Inatubainikia kuwa uchache wa muda wa mimba ni miezi sita. Kwa sababu tukiondoa miaka miwili ya kunyonyesha inabakia miezi sita kwa uchache. Elimu ya utabibu ya kisasa imethibitisha nadharia hii.

Sheikh Al-Maraghi Almasri katika tafsiri yake anasema: "Wa kwanza kuvumbua hukumu hii ni Ali (K.W.)."

Na amepokea Muhammad bin Is-haq, mwenye kitabu cha As-Sira, kwamba mtu mmoja alimuoa mwanamke akamzalia mtoto wa mimba ya miezi sita kamili. Akamshitakia Uthman. Alipoletewa, akaamuru arujumiwe (apigwe kwa mawe).

Ali alipopata habari alimjia akamwambia: **"Kwani husomi Qur'an? "** Uthman akasema, kwa nini nasoma. Akamwambia: **"Hukusikia kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na kubeba mimba kwake na kumwachisha ziwa ni miezi thalathini." Na ile isemayo "Na kumwachisha ziwa miaka miwili."**

**Kwa hiyo baada ya miaka miwili, hakuna kinachobaki ila miezi sita?"** Uthman akasema: Wallah! Sikujua hivyo.

Hebu nileteeni huyo mwanamke. Basi wakamkuta amezaa. Akasema Muammar bin Abdallah: "Wallah! Hakuna kunguru kwa kunguru wala yai kwa yai lilifonana kuliko mtoto huyu alivyofanana na baba yake. " Baba yake alipomuona, akasema: "Huyu ni mwanangu, wallah, sina shaka"

Hata anapofika kukomaa kwake na akafikilia miaka arubaini,

Anapofikia baleghe mtu kwa kutoa manii au kwa miaka[1]1, na akawa ni mwenye akili, katika matumizi yake, basi anakuwa na yale waliyo nayo watu wazima na ni juu yake kutekeleza taklifa zote za sharia.

Hata hivyo wafasiri wamesema kuwa Aya hii inaashiria maudhui mengine ambayo ni kukomaa mtu akili na mwili, kwa dalili ya kuli yake

1. Shafi na Hambali wanasema kuwa baleghe inathibiti kwa kufikisha miaka 15 kwa mvulana na msichana. Malik wanasema ni miaka17 kwa mvulana na msichana. Hanafi wakasema 18 kwa mvulana na 17 kwa msichana na Imamiya wakasema 15 kwa mvulana na 9 kwa msichana.

Mwenyezi Mungu: 'Na akafikia miaka arubaini,' ambapo anafikia ukomo wa nguvu zake.

Vyovyote iwavyo miaka haitoshi kumfanya mtu kuwa na ukomavu wa akili ikiwa hakupitia uzoefu mwingi.

Sio mbali kuwa kutajwa miaka arubaini katika Aya ni kuashiria kuwa, aghalabu, mtu katika miaka hii anapitia majaribio yenye manufaa. Wafasiri na wanahistoria wanasema kuwa Mwenyezi Mungu hakumtuma Mtume ila baada ya kufikisha miaka arubaini, isipokuwa Isa na Yahya.

Husema: Mola wangu! Nizindue nishukuru neema yako uliyonineemesha na wazazi wangu, na nipate kutenda mema unayoyaridhia.

Mwenye akili hutaka tawfiki na msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kuweza kutekeleza shukrani kwake kwa kumtii na kumnyenyekea.

Neema kubwa zaidi ni kuongozwa kwenye haki na kuitumia inavyotakikana. Ama kule kuweko mtu sio neema kwake wala kwa mwingine akiwa si nyenzo ya kufanya matendo mema.

Imetangulia Aya hii kwa herufi zake katika Juz. 19 (27:19).

Na unitengenezee dhuriya zangu.

Watoto ni mzigo mkubwa kwa wazazi, bali malezi yao na matakwa yao ni janga hasa. Lakini, maskini, baba anasahau taabu zote hizi ikiwa Mwenyezi Mungu atamneemesha kizazi chema, vinginevyo itakuwa ni majanga na masaibu makubwa.

Hakika mimi nimetubu kwako, na hakika mimi ni miongoni mwa Waislamu.

Hapa kuna ishara kuwa Mwenyezi Mungu hakubali toba ya mwenye dhambi wala haitikii dua yake ila akitubia dhambi zake na akawa na msimamo katika vitendo vyake na kauli yake.

Hao ndio tunaowatakakabalia bora ya vitendo walivyovitenda.

Makusudio ya bora ya vitendo ni visivyokuwa vitendoviovu. Kwa vile vitendo viovu anavisamehe; kama alivyovyosema: Na tunayasamehe mabaya yao, kwa sababu wametubia na kufanya ikhlasi. Watakuwa miongoni mwa watu wa Peponi; yaani watakuwa pamoja nao.

Miadi ya kweli hiyo waliyoahidiwa, kuwa matendo yao yatakubaliwa, kusamehewa makosa yao na kuingia Peponi. Ahadi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kweli na kauli yake ni haki.

وَالَّذِي قَالَ لِوَالِدَيْهِ أُفٍّ لَّكُمَا أَتَعِدَانِنِي أَنْ أُخْرَجَ وَقَدْ خَلَتِ الْقُرُونُ مِن قَبْلِي وَهُمَا يَسْتَغِيثَانِ
اللَّـهَ وَيْلَكَ آمِنْ إِنَّ وَعْدَ اللَّـهِ حَقٌّ فَيَقُولُ مَا هَـٰذَا إِلَّا أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿١٧﴾

17. Na ambaye amewaambia, wazazi wake Ah! Nanyi! Je, mnanitisha kuwa nitafufuliwa, na hali vizazi vingi vimekwishapita kabla yangu! Na hao humwomba msaada Mwenyezi Mungu: Ole wako! Amini! Hakika miadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli. Na yeye husema: Hayakuwa haya ila ni ngano za watu wa kale.

أُولَـٰئِكَ الَّذِينَ حَقَّ عَلَيْهِمُ الْقَوْلُ فِي أُمَمٍ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِم مِّنَ الْجِنِّ وَالْإِنسِ إِنَّهُمْ كَانُوا
خَاسِرِينَ ﴿١٨﴾

18. Hao ndio ambao imehakikishwa kauli juu yao; kama mataifa yaliyokwishapita kabla yao miongoni mwa majini na watu. Hakika hao wamekuwa wenye kuhasirika.

وَلِكُلٍّ دَرَجَاتٌ مِمَّا عَمِلُوا ۖ وَلِيُوَفِّيَهُمْ أَعْمَالَهُمْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٩﴾

19. Na wote watakuwa na daraja zao mbali mbali kwa waliyoyatenda, na ili awalipe kwa vitendo vyao, na hawatadhulumiwa.

وَيَوْمَ يُعْرَضُ الَّذِينَ كَفَرُوا عَلَى النَّارِ أَذْهَبْتُمْ طَيِّبَاتِكُمْ فِي حَيَاتِكُمُ الدُّنْيَا وَاسْتَمْتَعْتُمْ بِهَا فَالْيَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنْتُمْ تَسْتَكْبِرُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَبِمَا كُنْتُمْ تَفْسُقُونَ ﴿٢٠﴾

20. Na siku wale waliokufuru watakapoonyeshwa Moto: Nyinyi mlitwaa vitu vyenu vizuri katika maisha yenu ya dunia, na mkastarehe navyo. Basi leo mnalipwa adhabu ya fedheha kwa mlivyokuwa mkitakabari katika ardhi bila ya haki, na kwa mlivyokuwa mkifanya ufuska.

## ALIYEWAAMBIA WAZAZI WAKE AKH!

**Aya 17 – 20**

### MAANA

Na ambaye amewaambia, wazazi wake Ah! Nanyi! na akawaambia: Je, mnanitisha kuwa nitafufuliwa, na hali vizazi vingi vimekwishapita kabla yangu!

Ni nani mtoto huyu anayezungumziwa na Qur'an na kusema kuwa ni kafiri mwenye kuwaudhi wazazi wake?

**Jibu**: Mwenyezi Mungu hakumtaja mtu hasa. Dhahiri ya Aya inaonyesha kwamba makusudio yake ni kila mtoto anayeikanusha siku ya mwisho, naye akiwa na wazazi wanaojitahidi kumpa nasaha, kumwongoza na kumhadharisha na ghadhabu za Mwenyezi Mungu na adhabu yake, lakini bado anaona kusumbuliwa na kuwaambia: Poteleeni mbali! Vipi mtu ataweza kutoka kaburini na hali amekuwa mchanga? Je, ameshawahi kutokewa na hivyo mwingine asiyekuwa mimi katika zama zozote?

Aya hii inawaelekea vijana wengi wa kisasa, kama vile imewashukia wao. Lau kama watauliza na kujadiliana kwa kukusudia maarifa na kuongoka kwenye uhakika, basi itakuwa ni wajibu wetu tuwakaribishe na maswali na majadiliano yao; na tufanye bidii kubwa kadiri tunavyoweza ili tuwakinaishe, kwa kuifanyia kazi kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

لَتُبَيِّنُنَّهُ لِلنَّاسِ وَلَا تَكْتُمُونَهُ ﴿١٨٧﴾

"Lazima mtakibainisha kwa watu wala hamtakificha." Juz. 4 (3:187).

Na pia kuwa wao wana haja zaidi ya kuongozwa na kubainishiwa.

Na hao wazazi humwomba msaada Mwenyezi Mungu na humwambia mtoto wao: Ole wako! Amini! Hakika miadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli.

Wanamwomba msaada Mwenyezi Mungu kutokana na kufuru ya mtoto wao na kumsisitiza kwamba ufufuo ni kweli. Mara nyingi mwito wa wazazi kwa mtoto unakuwa kama kawaida tu, lakini neno 'humwomba msaada Mwenyezi Mungu,' linaonyesha jinsi wanavyoona uchungu na masikitiko kwa kufuru ya mtoto wao aliyewaasi na ujeuri wake. Lakini pamoja na yote hayo anang'ng'nia upotevu na yeye husema:

Hayakuwa haya ila ni ngano za watu wa kale.

Anawajibu wazazi wake pamoja na huruma zao kwake na nasaha zao: Maneno yenu haya hayana maana yoyote ispokuwa porojo tu. Hivi ndivyo vijana wengi wa kileo wanavyowangalia baba zao na mama zao. Ajabu ni

kuwa kijana lau atayasikia haya kutoka kwa kijana mwenzake asingelikuwa na msimamo huu wa dharau.

Hao ndio ambao imehakikishwa kauli juu yao kama mataifa yaliyokwishapita kabla yao miongoni mwa majini na watu.

'Hao,' ni kila mwenye kuifanyia inadi haki na akapinga mwito wa wenye ikhlasi. Kuhakikishiwa kauli juu yao ni neno la adhabu. Hii ni desturi ya Mwenyezi Mungu katika uma zilizotangulia, wawe maji- ni au watu.

Hakika hao wamekuwa wenye kuhasirika, kwa vile waliuacha mwito wa haki na wakamzibia masikio mtoa nasaha aliyemwaminifu.

Na wote watakuwa na daraja zao mbali mbali kwa waliyoyatenda, na ili awalipe kwa vitendo vyao, na hawatadhulumiwa.

Daraja za watu, siku ya Kiyama, zitatofautiana kulingana na matendo yao yalivyokuwa duniani. Tafisiri wazi zaidi inayofafanua Aya hii, ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

يَوْمَ تَجِدُ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ مِنْ خَيْرٍ مُّحْضَرًا وَمَا عَمِلَتْ مِن سُوءٍ ﴿٣٠﴾

"Siku ambayo kila nafsi itakuta heri iliyoitenda imehudhurishwa, na iliyoyatenda katika uovu." Juz. 4 (3:30).

Na siku wale waliokufuru watakapoonyeshwa Moto; yaani watakapoadhibiwa, na Malaika wa adhabu watawaambia:

Nyinyi mlitwaa vitu vyenu vizuri katika maisha yenu ya dunia, na mkastarehe navyo.

Mlikusanya mamilioni ya pesa mlizozipora kisha mkazirundika, mkajijengea viwanda na majumba marefu kwa hisabu ya wanyonge, mkatumia yote kwenye raha na starehe, bila ya kuiwekea akiba siku hii ya leo.

Basi leo mnalipwa adhabu ya fedheha kwa mlivyokuwa mkitakabari katika ardhi bila ya haki, na kwa mlivyokuwa mkifanya ufuska.

Mlionyeshwa haki mkaifanyia kiburi, mkajitukuza na mkaijaza ardhi dhulma na ufisadi. Basi onjeni uchungu wa ubaya wenu kama mlivyoonja utamu wake jana.

Katika Tafsir ya Sheikh Al-Maraghi, kuna maelezo kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alipokuwa akitaka kusafiri, mtu wa mwisho kumuaga katika familia alikuwa ni Fatima, na mtu wa kwanza kumjulia hali, anaporudi safirini, alikuwa ni Fatima. Siku moja aliporudi kutoka katika vita alikwenda nyumbani kwa Fatima, kama desturi yake.

Akaona pazia ya sufu nzito mlangoni na akawaona Hasan Na Husein wamevishwa vikuku vya fedha, basi akarudi bila ya kuingia. Fatima akaona kuwa hakuingia kutokana na aliyoyaona. Basi akaiondoa ile pazia na vikukuu akavipeleka kwa baba yake naye akawapa masikini na akasema: "Hawa ndio watu wa nyumba yangu – akiwashiria Fatima na waliomo nyumbani mwake – wala sipendi wale vizuri vyao katika maisha yao ya dunia."

3

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

وَاذْكُرْ أَخَا عَادٍ إِذْ أَنذَرَ قَوْمَهُ بِالْأَحْقَافِ وَقَدْ خَلَتِ النُّذُرُ مِن بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّـهَ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٢١﴾

21. Na mtaje ndugu wa kina A'di, alipowaonya watu wake kwenye vilima vya mchanga. Na kwa yakini waonyaji wengi walitokea kabla yake na baada yake: kuwa msimwabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hakika mimi ninawahofia na adhabu ya siku iliyo kuu.

قَالُوا أَجِئْتَنَا لِتَأْفِكَنَا عَنْ آلِهَتِنَا فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَا إِن كُنتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٢٢﴾

22. Wakasema: Je, umetujia ili ututenge mbali na miungu yetu? Basi tuletee hayo unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli.

قَالَ إِنَّمَا الْعِلْمُ عِندَ اللَّـهِ وَأُبَلِّغُكُم مَّا أُرْسِلْتُ بِهِ وَلَـٰكِنِّي أَرَاكُمْ قَوْمًا تَجْهَلُونَ ﴿٢٣﴾

23. Akasema: Hakika ujuzi uko kwa Mwenyezi Mungu tu. Mimi ninawafikishia niliyotumwa, lakini ninawaona kuwa nyinyi ni watu mnaofanya ujinga.

فَلَمَّا رَأَوْهُ عَارِضًا مُّسْتَقْبِلَ أَوْدِيَتِهِمْ قَالُوا هَـٰذَا عَارِضٌ مُّمْطِرُنَا ۚ بَلْ هُوَ مَا اسْتَعْجَلْتُم بِهِ ۖ رِيحٌ فِيهَا عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٢٤﴾

24. Basi walipoliona wingu likielekea kwenye mabonde yao, walisema: Wingu hili ni la kutunyeshea mvua! Kumbe, haya ni hayo mliyoyahimiza, ni upepo ndani yake imo adhabu chungu!

تُدَمِّرُ كُلَّ شَيْءٍ بِأَمْرِ رَبِّهَا فَأَصْبَحُوا لَا يُرَىٰ إِلَّا مَسَاكِنُهُمْ ۚ كَذَٰلِكَ نَجْزِي الْقَوْمَ الْمُجْرِمِينَ ﴿٢٥﴾

25. Unaangamiza kila kitu kwa amri ya Mola wake. Wakawa hawaonekani ila nyumba zao tu. Hivyo ndivyo tunavyowalipa watu wakosefu.

وَلَقَدْ مَكَّنَّاهُمْ فِيمَا إِن مَّكَّنَّاكُمْ فِيهِ وَجَعَلْنَا لَهُمْ سَمْعًا وَأَبْصَارًا وَأَفْئِدَةً فَمَا أَغْنَىٰ عَنْهُمْ سَمْعُهُمْ وَلَا أَبْصَارُهُمْ وَلَا أَفْئِدَتُهُم مِّن شَيْءٍ إِذْ كَانُوا يَجْحَدُونَ بِآيَاتِ اللَّـهِ وَحَاقَ بِهِم مَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٢٦﴾

26. Na hakika tuliwamakinisha, sio kama tulivyowamakinisha nyinyi, Na tuliwapa masikio, na macho, na nyoyo; na hayakuwafaa kitu masikio yao, wala macho yao, wala nyoyo zao, Kwani hao walikuwa wakizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, na yakawazunguka yale waliyokuwa wakiyafanyia stihizai.

وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا مَا حَوْلَكُم مِّنَ الْقُرَىٰ وَصَرَّفْنَا الْآيَاتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٢٧﴾

27. Na hakika tuliiangamiza miji ilio jirani zenu, na tuliziainisha Ishara ili wapate kurejea.

فَلَوْلَا نَصَرَهُمُ الَّذِينَ اتَّخَذُوا مِن دُونِ اللَّـهِ قُرْبَانًا آلِهَةً ۖ بَلْ ضَلُّوا عَنْهُمْ ۚ وَذَٰلِكَ إِفْكُهُمْ وَمَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٢٨﴾

28. Basi mbona wale waliowashika badala ya Mwenyezi Mungu, kuwa wawakurubishe, hawakuwanusuru? Bali waliwapotea! Na hivyo ndio uwongo wao na waliyokuwa wakiyazua.

## HUD

**Aya 21 -28**

## MAANA

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amekitaja kisa cha Hud, katika Juz. 8 (7:65-72), Juz. 12 (11:50 -60), Juz. 19 (26: 123-140) na katika Juzuu nyinginezo zilizopita na zitakazofuatia. Kwa hiyo hapa tutaja kwa ufupi tu, kwa kutegemea yaliyokwishapita.

Na mtaje ndugu wa kina A'di, alipowaonya watu wake kwenye vilima vya mchanga.

Ewe Muhammad! Watajie watu wako kisa cha Hud na watu wake, ili wapate mawaidha na mazingatio. Walikuwa ni waarabu kama watu wako, walikuwa na nguvu zaidi na mali, na nyumba zao zilikuwa karibu na mji wako, kwa vile waliishi kwenye vichuguu vya mchanga – sehemu ya Yemen iliyoshikana na Hijaz; kama ilivyosemekana.

Na kwa yakini waonyaji wengi walitokea kabla yake na baada yake.

Makusudio ya waonyaji ni mitume. Maana ni kuwa waambie ewe Muhammad, kuwa vile vile Hud hakuwa Mtume wa mwanzo wala wa mwisho, bali Mwenyezi Mungu alituma mitume wengi kabla ya Hud na baada yake. Na alikuwa akiwaonya watu wake kwa maneno yale yale ya kila Nabii:

Kuwa msimwabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hakika mimi ninawahofia na adhabu ya siku iliyo kuu, ikiwa mtabakia na upotevu na shirki mliyo nayo.

Wakasema: Je, umetujia ili ututenge mbali na miungu yetu? Basi tuletee hayo unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli.

Yaani wewe Hud unataka tuache kuabudu masanamu na tuabudu Mungu mmoja, si ni jambo la ajabu hili! Tena unatuhofisha na adhabu, si utuletee haraka basi ikiwa vitisho vyako ni vya kweli?

Akasema: Hakika ujuzi uko kwa Mwenyezi Mungu tu. Mimi ninawafikishia niliyotumwa, lakini ninawaona kuwa nyinyi ni watu mnaofanya ujinga.

Mola wangu ameniamarisha niwaonye na adhabu, basi nikatii amri, nikawaonya. Ama kuwa lini itatokea adhabu hiyo, ni ya aina gani au ikoje, anaiujua Mwenyezi Mungu tu, mimi sijui lolote katika hayo. Isipokuwa nina uhakika kabisa kuwa nyinyi ni watu mliozama kwenye ujinga na upotevu.

Basi walipoliona wingu likielekea kwenye mabonde yao, walisema: Wingu hili ni la kutunyeshea mvua!

Waliidhania adhabu kuwa ni mawingu, wakafurahi kuwa watanyeshewa mvua, Kwa hiyo wakabashiriana kupata rutuba na mavuno.

Basi Hud akawaambia au hali halisi ikaonyesha:

Kumbe, haya ni hayo mliyoyahimiza, ni upepo ndani yake imo adhabu chungu! Unaangamiza kila kitu kwa amri ya Mola wake.

Wakaona mawingu angani ambayo dhahiri yake ni rehema na undani wake ni adhabu, wakadanganyika na dhahiri na wakaghafilika na

yanayojificha yanayokuja ghafla. Basi adhabu ikawanyakua wakiwa wamelewa amani na matamanio. Huu ndio mwisho wa mwenye kuyatii matamanio yake.

Wakawa hawaonekani ila nyumba zao tu amabazo zimekuwa ni makaburi ya miili yao. Mwenye akili ni yule anayepata mawaidha na mfano wa watu hawa, akahofia mashiko ya Mwenyezi Mungu wakati wa nema na raha na akatarajia rehema yake wakati wa shida na karaha.

Hivyo ndivyo tunavyowalipa watu wakosefu duniani na Akhera au Akhera peke yake kulingana na inavyotaka hikima yake.

Na hakika tuliwamakinisha, sio kama tulivyowamakinisha nyinyi.

Tuliwaangamiza akina A'd walipoasi na kupetuka mipaka, na tulikuwa tumewapa nguvu na mali kwa namna ambayo hatukuwapa nyinyi mfano wake enyi vigogo wa kikuraishi. Hivi hamuogopi kuwapata yaliyowapata A'd na wengineo katika uma zilizopita?

Na tuliwapa masikio, na macho, na nyoyo; kama tulivyowapa nyinyi, na hayakuwafaa kitu masikio yao, wala macho yao, wala nyoyo zao, kwa sababu hawakunufaika nayo, bali walikuwa kama wendawazimu, viziwi, mabubu na vipofu kwenye ukumbusho na hadhari.

Basi enyi watu wa Makka msighurike na masikio, macho na akili zenu. Kwani yote hayo hayawatafaa kitu itakaposhuka adhabu.

Kwani hao walikuwa wakizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, na yakawazunguka yale waliyokuwa wakiyafanyia stihizai.

Waliipinga haki pamoja na dalili zake na wakaidharau na watu wake. Wakaingia kwenye uovu na upotevu; malipo yao yakawa ni maangamizi na kuvunjika.

Na hakika tuliiangamiza miji ilio jirani zenu, na tuliziainisha Ishara ili wapate kurejea.

Maneno yanaelekezwa kwa washirikina wa Makka. Makusudio ya miji ni watu wa miji hiyo ambao ni akina A'd na Thamud na wanaopakana nao.

Kuzianisha Ishara ni kuwabainishia aina za dalili na mawaidha, na walihadharishwa kwa kauli na vitendo ili wawaidhike na wakome, lakini wakakataa isipokuwa ukafiri, basi ikawathibitikia adhabu na wakabomolewa kabisa.

Basi mbona wale waliowashika badala ya Mwenyezi Mungu, kuwa wawakurubishe, kwa Mwenyezi Mungu, hawakuwanusuru? Bali waliwapotea! Na hivyo ndio uwongo wao na waliyokuwa wakiyazua.

'Hivyo' ni hivyo kutookoa masanamu na kwamba hayamsaidii aliyekuwa akiyaabudu wakati wa dhiki. Maana ni kuwa kauli ya washirikina kuwa sanamu ni muombezi wetu mbele ya Mwenyezi Mungu na muokozi wetu, ni uzushi.

وَإِذْ صَرَفْنَا إِلَيْكَ نَفَرًا مِّنَ الْجِنِّ يَسْتَمِعُونَ الْقُرْآنَ فَلَمَّا حَضَرُوهُ قَالُوا أَنصِتُوا فَلَمَّا قُضِيَ وَلَّوْا إِلَىٰ قَوْمِهِم مُّنذِرِينَ ﴿٢٩﴾

29. Na tulipokuletea kundi la majini kusikiliza Qur'an. Basi walipoihudhuria walisema: Nyamazeni! Na ilipomalizwa, walirudi kwa kaumu yao kwenda kuwaonya.

قَالُوا يَا قَوْمَنَا إِنَّا سَمِعْنَا كِتَابًا أُنزِلَ مِن بَعْدِ مُوسَىٰ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ وَإِلَىٰ طَرِيقٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٣٠﴾

30. Wakasema: Enyi kaumu yetu! Sisi tumesikia Kitabu kilichoteremshwa baada ya Musa, kinachosadikisha yaliyo kuwa kabla yake, na kinachoongoza kwenye Haki na kwenye Njia iliyonyooka.

يَا قَوْمَنَا أَجِيبُوا دَاعِيَ اللَّـهِ وَآمِنُوا بِهِ يَغْفِرْ لَكُم مِّن ذُنُوبِكُمْ وَيُجِرْكُم مِّنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣١﴾

31. Enyi kaumu yetu! Muitikieni Mwenye kuitia kwa Mwenyezi Mungu, na mumwamini, Mwenyezi Mungu atawasamehe, na atawakinga na adhabu chungu.

وَمَن لَّا يُجِبْ دَاعِيَ اللَّـهِ فَلَيْسَ بِمُعْجِزٍ فِي الْأَرْضِ وَلَيْسَ لَهُ مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءُ أُولَـٰئِكَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٣٢﴾

32. Na asiyemwitikia mwitaji wa Mwenyezi Mungu basi hatashinda katika ardhi, wala hatakuwa na walinzi mbele yake. Hao wamo katika upotovu ulio dhahiri.

## MAJINI WANASIKILZA QUR'AN

**Aya 29 – 32**

### MAANA

Na tulipokuletea kundi la majini kusikiliza Qur'an. Basi walipoihudhuria walisema: Nyamazeni! Na ilipomalizwa, walirudi kwa kaumu yao kwenda kuwaonya.

Miongoni mwa wadhifa wa akili ni kuhukumu uwezekeano wa kuweko kitu au kutokuweko. Ikihukumu uwezekano wa kuweko, basi inakimbilia kuthibitisha kuweko kwake kwa kutumia nyenzo, zinazoafikiana na maumbile ya kitu kinachotakiwa kuthibitishwa, kwa hisia na majaribio.

Kikiwa ni katika mambo ya kiakili, basi njia yake itakuwa ni akili. Na kikiwa ni katika mamabo ya ghaibu –sio kuweko Mungu – basi njia yake itakuwa ni wahyi tu. Ukielezea basi itakuwa ni lazima kukubaliana nao.

Hakuna mwenye shaka kwamba akili haikatai kuweko viumbe vilivyo mbali nasi na vinavyotofautiana na tunayoyajua na tuliyoyazoea. Bali tuna uhakika kuwa tusiyoyajua ni mengi zaidi kuliko tunayoyajua; miongoni mwa hayo ni majini. Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameyataja katika Aya kadhaa; kama vile:

وَأَنَّا مِنَّا الصَّالِحُونَ وَمِنَّا دُونَ ذَٰلِكَ ﴿١١﴾

"Na hakika katika sisi wako wema na wengine katika sisi ni kinyume na hayo." (72:11).

Mwenyezi Mungu alipeleka kundi katika hao wema kwa Mtume Mtukufu **(s.a.w.w)**, wakamsikia akisoma Qur'an, wakaanza kuambiana: 'Hebu nyamazeni na mzingatie maana yake.' Basi wakanyamaza na kusikiliza kwa makini. Wakaona uongofu na nuru, wakamwamini Muhammad **(s.a.w.w)**. Mtume alipomaliza kusoma walirudi haraka kwa watu wao kuwaonya na kuwapa bishara ya Uislamu.

Wakasema: Enyi kaumu yetu! Sisi tumesikia Kitabu kilichoteremshwa baada ya Musa, kinachosadikisha yaliyo kuwa kabla yake, na kinachoongoza kwenye Haki na kwenye Njia iliyonyooka

Waliwaambia watu wao kuwa tumesikia Kitabu kutoka kwa Muhammad **(s.a.w.w)** kinachofanana na kile alichoteremshiwa Musa, nacho kinasadikisha yale waliyokuja nayo manabii, ya kuamini tawhid na ufufuo. Vile vile kinaongoza kwenye usawa na kufanya heri:

فَقَالُوا إِنَّا سَمِعْنَا قُرْآنًا عَجَبًا ﴿١﴾ يَهْدِي إِلَى الرُّشْدِ فَآمَنَّا بِهِ وَلَن نُّشْرِكَ بِرَبِّنَا أَحَدًا ﴿٢﴾

"Wakasema: hakika tumesikia Qur'an ya ajabu. Inaongoza kwenye uwongofu kwa hiyo tumeiamini na hatutamshirikisha yeyote na Mola wetu." (72:1-2).

Ikiwa sisi hatujawaona majini walioathirika na Qur'an na kuiamini, lakini tumewaona wataalamau na watu wenye akili wengi wakiathirika na matamshi ya Qur'an kwa kiasi cha kusikia matamshi yake tu; tena wakaamini imani isiyokuwa na shaka kuwa inatoka kwa Mwenye hekima Mjuzi.

Enyi kaumu yetu! Muitikieni Mwenye kuitia kwa Mwenyezi Mungu, na mumwamini, Mwenyezi Mungu atawasamehe, na atawakinga na adhabu chungu.

Itikieni mwito wa haki na mumfuate anayeutoa mwito huo; Mwenyezi Mungu atawasamehe dhambi zenu na atawaingiza katika rehema yake na kuwaokoa na ghadhabu yake na adhabu yake.

Na asiyemwitikia mwitaji wa Mwenyezi Mungu basi hatashinda katika ardhi, wala hatakuwa na walinzi mbele yake. Hao wamo katika upotovu ulio dhahiri.

Hakuna kumkimbia Mwenyezi Mungu isipokuwa kwake tu wala hakuna kuokoka na adhabu yake isipokuwa kwa ikhlasi na matendo mema.

Hao wamo katika upotevu ulio dhahiri.

'Hao' ni hao wasioitikia mwito wa Mwenyezi Mungu, na asiyemwitikia atakuwa ameiacha njia ya haki na uongofu.

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّـهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَعْيَ بِخَلْقِهِنَّ بِقَادِرٍ عَلَىٰ أَن يُحْيِيَ الْمَوْتَىٰ
بَلَىٰ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٣﴾

33. Je, hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, aliyeziumba mbingu na ardhi, na hakuchoka kwa kuziumba, kuwa ni Muweza wa kuwafufua wafu? Kwa nini? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.

وَيَوْمَ يُعْرَضُ الَّذِينَ كَفَرُوا عَلَى النَّارِ أَلَيْسَ هَـٰذَا بِالْحَقِّ قَالُوا بَلَىٰ وَرَبِّنَا قَالَ فَذُوقُوا الْعَذَابَ
بِمَا كُنتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٣٤﴾

34. Na siku makafiri watakapoonyeshwa Moto, Je, haya si kweli? Watasema: Kwani? Tunaapa kwa Mola wetu! Atasema: Basi onjeni adhabu kwa sababu ya mliyokuwa mkikataa.

فَاصْبِرْ كَمَا صَبَرَ أُولُو الْعَزْمِ مِنَ الرُّسُلِ وَلَا تَسْتَعْجِل لَّهُمْ كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَ مَا يُوعَدُونَ لَمْ
يَلْبَثُوا إِلَّا سَاعَةً مِّن نَّهَارٍ بَلَاغٌ فَهَلْ يُهْلَكُ إِلَّا الْقَوْمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٣٥﴾

35. Basi subiri, kama walivyosubiri Mitume wenye azma, Wala usiwahimizie. Siku watakayoyaona waliyoahidiwa, itakuwa kama kwamba

hawakukaa ila saa moja ya mchana. Huu ndio ufikisho! Kwani huangamizwa isipokuwa walio watu mafasiki?

## JE, HAYA SI KWELI?

**Aya 33 – 35**

### MAANA

Je, hawaoni ya kwamba Mwenyezi Mungu, aliyeziumba mbingu na ardhi, na hakuchoka kwa kuziumba, kuwa ni Muweza wa kuwafufua wafu? Kwa nini? Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.

Ulimwengu huu wa ajabu unajulisha uweza wa muumba na ukuu wake. Vile vile unajulisha, tena kwa njia bora, kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ana uwezo wa kuwafufa wafu. Kwa vile sabu inayoleta mambo hayo mawili ni moja, ambayo ni uweza wa mwenye kukiambia kitu 'kuwa' na kikawa. Imam Ali (a.s) anasema: **"Namshangaa anayekanusha ufufuo wa pili na hali anaona ufufuo wa kwanza!"**

Maana ya Aya hii yametangulia katika makumi ya Aya na yatakuja mengine mengi; miongoni mwayo ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Je, tulichoka kwa umbo la kwanza?" (50:15). Basi tutachoka vipi na umbo la pili?

Na siku makafiri watakapoonyeshwa Moto, yaani watakapoadhibiwa na kuaambiwa: Je, haya, mliyokuwa mkiyakanusha hapo mwanzo, si kweli? Watasema: Kwani? Tunaapa kwa Mola wetu! ni kweli.

Walikanusha duniani ambapo kunawadhuru kukana na wamekubali Akhera ambapo hakuwanufaishi chochote kukiri kwao.

Atasema: Basi onjeni adhabu kwa sababu mlikuwa mkikataa; bali mliwadharau wale walioamini hisabu ya Mwenyezi Mungu na adhabu yake. Mfano wa Aya hii ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:Na ungeliona watakaposimamishwa mbele ya Mola wao, Akasema: Je, si kweli haya? Watasema: Kwa nini? Tunaapa kwa Mola wetu. Atasema: Basi onjeni adhabu kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyakataa." Juz. 7 (6:30).

Basi subiri, kama walivyosubiri Mitume wenye azma,

Kwenye tafsiri nyingi imeelezwa kuwa mitume wenye azma (Ululu-azm) ni watano: Nuh, Ibrahim, Musa, Isa na Muhammad. Kila mmoja wao alikuwa na sharia mahususi aliyoiwajibisha Mwenyezi Mungu kutumiwa na viumbe wote wakati wake mpaka afike mtume mwingine kati ya hao watano.

Akija anafuta sharia ya yule aliyemtangulia katika wale watano, mpaka kufikia sharia ya Muhammad **(s.a.w.w)**, Bwana wa mitume na mwisho wa manabii. Hiyo haiwezi kufutwa hadi siku ya kiyama. Ama manabii wengine wasiokuwa hao ululu-azm, walikuwa wakitumia sharia ya waliyemtangulia katika hao watano.

Kuna riwaya za Ahlul-bayt zinazozungumzia hili na kuashirwa na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

شَرَعَ لَكُم مِّنَ الدِّينِ مَا وَصَّىٰ بِهِ نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهِ إِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ وَعِيسَىٰ ﴿١٣﴾

"Amewapa sharia ya Dini aliyomuusia Nuhu na tuliyokupa wahyi wewe, na tuliyowausia Ibrahim na Musa na Isa," Juz. 25 (42:13).

Ambapo amewahusu kuwataja hao watano na kutaja neno sharia. Na 'wewe' ni wewe Muhammad.

Wala usiwahimizie adhabu. Siku watakayoyaona waliyoahidiwa itakuwa kama kwamba hawakukaa ulimwenguni ila saa moja ya mchana.

Maneno yanaelekezwa kwa Muhammad **(s.a.w.w)**, na wanaoambiwa ni wale walioikanusha risala yake. Makusudio ya yale mliyoahidiwa ni adhabu ya Jahannam. Maana ni kuwa usifanye haraka ewe Muhammad **(s.a.w.w)** ya kutaka wale waliokufuru waadhibiwe, kwa sababu itawapata tu huko Akhera. Huku kukaa kwao duniani hata kukirefuka, lakini watapoiona adhabu wataona kama kwamba ni kitambo kidogo tu.

Mfano wa Aya hii ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

مَتَاعٌ قَلِيلٌ ثُمَّ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ ۚ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿١٩٧﴾

"Ni starehe ndogo. Kisha makazi yao ni Jahannam ni mahali pabaya pa kushukia."

Juz. 4 (3:197).

Imam Ali (a.s) anasema: **"Hakika dunia ni starehe za siku kidogo, zinaondoka kama yanavyoondoka mangati au kama yanavyopotea mawingu."**

Huu ndio ufikisho!

Yaani Qur'an ni ufikisho wa risala za Mwenyezi Mungu Mtukufu, nayo ni hoja tosha ya mawaidha yake na ni ponyo kwa anayetaka mwongozo na uongofu.

Kwani huangamizwa wengine isipokuwa walio watu mafasiki?

Hapana!

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي مَقَامٍ أَمِينٍ ﴿٥١﴾ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٥٢﴾

"Hakika wenye takua watakuwa katika mahali pa amani. Katika mabustani na chemchem."

Juz. (44:51-52).

## MWISHO WA SURA YA ARUBAINI NA SITA: SURAT AL-AHQAF

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

Sura Ya Arubaini Na Saba: Surat Muhammad. Ina Aya 38. Aya zote au nyingi zimeshuka Madina.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّهِ أَضَلَّ أَعْمَالَهُمْ ﴿١﴾

1. Wale waliokufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, Yeye atavipotoa vitendo vyao.

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَآمَنُوا بِمَا نُزِّلَ عَلَىٰ مُحَمَّدٍ وَهُوَ الْحَقُّ مِن رَّبِّهِمْ ۙ كَفَّرَ عَنْهُمْ
سَيِّئَاتِهِمْ وَأَصْلَحَ بَالَهُمْ ﴿٢﴾

2. Na wale walioamini, na wakatenda mema, na wakaamini aliyoteremshiwa Muhammad - nayo ni Haki iliyotoka kwa Mola wao - atawafutia maovu yao na ataitengeneza hali yao.

ذَٰلِكَ بِأَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا اتَّبَعُوا الْبَاطِلَ وَأَنَّ الَّذِينَ آمَنُوا اتَّبَعُوا الْحَقَّ مِن رَّبِّهِمْ ۚ كَذَٰلِكَ يَضْرِبُ
اللَّهُ لِلنَّاسِ أَمْثَالَهُمْ ﴿٣﴾

3. Hayo ni kwa sababu wale waliokufuru wamefuata upotovu, na walioamini wamefuata Haki iliyotoka kwa Mola wao. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyowapigia watu mifano yao.

فَإِذَا لَقِيتُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبَ الرِّقَابِ حَتَّىٰ إِذَا أَثْخَنتُمُوهُمْ فَشُدُّوا الْوَثَاقَ فَإِمَّا مَنًّا بَعْدُ وَإِمَّا
فِدَاءً حَتَّىٰ تَضَعَ الْحَرْبُ أَوْزَارَهَا ۚ ذَٰلِكَ وَلَوْ يَشَاءُ اللَّهُ لَانتَصَرَ مِنْهُمْ وَلَٰكِن لِّيَبْلُوَ بَعْضَكُم بِبَعْضٍ ۗ
وَالَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَلَن يُضِلَّ أَعْمَالَهُمْ ﴿٤﴾

4. Basi mnapokutana na waliokufuru wapigeni shingo, mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu. Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vitue mizigo yake. Ndio hivyo. Na lau angelitaka Mwenyezi Mungu angeliwashinda mwenyewe, lakini haya ni kwa sababu awatie katika mitihani nyinyi kwa nyinyi. Na waliouliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu hatazipoteza amali zao.

سَيَهْدِيهِمْ وَيُصْلِحُ بَالَهُمْ ﴿٥﴾

5. Atawaongoza na awatengezee hali yao.

وَيُدْخِلُهُمُ الْجَنَّةَ عَرَّفَهَا لَهُمْ ﴿٦﴾

6. Na atawaingiza katika Pepo aliyowajulisha.

## AMININI TULIYOMTEREMSHIA MUHAMMAD

**Aya 1 – 6**

### MAANAA

Wale waliokufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, Yeye atavipotoa vitendo vyao.

Neno 'kuzuilia' tumelifasiri kutokana na neno la kiarabu 'swaddu' lenye maana ya kupinga na pia lina maana ya kuzuuilia. Likifasiriwa kwa maana

ya kwanza, itakuwa kukufuru na kupinga ni kwa maana moja na uunganishi utakuwa ni wa kitafsiri. Ikiwa litafasiriwa 'kuzuiliwa' maana yake itakuwa wao hawakuamini na pia wamewazuia watu wengine wasiamini. Hii ndio dhahiri inayofahamishwa na Aya.'Kuvipotoa vitendo vyao,' ni kuvibatilisha; kama kwamba havikuwaokoa.

Maana ni kuwa mwenye kuupinga Uislamu na akawazuia watu wengine wasiuamini, Mwenyezi Mungu hatamkubalia chochote. Kwa sababu Uislamu ni sharti la msingi la thawabu za Akhera. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَمَا مَنَعَهُمْ أَن تُقْبَلَ مِنْهُمْ نَفَقَاتُهُمْ إِلَّا أَنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّـهِ وَبِرَسُولِهِ ﴿٥٤﴾

"Na hawakuzuiliwa kukubaliwa michango yao, ila ni kwamba wao wamemkufuru Mwenyezi Mungu na Mtume wake." Juz. 10 (9:54).

Na wale walioamini, na wakatenda mema, na wakaamini aliyoteremshiwa Muhammad - nayo ni Haki iliyotoka kwa Mola wao - atawafutia maovu yao na ataitengeneza hali yao.

Neno hali hapa tumelifasiri kutokana na neno la kiarabu 'bal' ambalo pia lina maana ya moyo.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kusema kuwa hatawakubalia makafiri, sasa anasema kuwa mwenye kufanya amali njema akiwa anamwamini Mwenyezi Mungu na Qur'an isiyo na shaka, atamkubalia na atamsamehe dhambi zake akitubia na pia atamtengenezea vizuri mambo yake duniani kwa tawfiki na heri na Akhera atamtia Peponi.

Hayo ni kwa sababu wale waliokufuru wamefuata upotovu, na walioamini wamefuata Haki iliyotoka kwa Mola wao.

'Hayo' ni hayo ya thawabu za watenda mema na adhabu ya watenda uovu. Maana ni kuwa haki ina wenyewe na batili ina wenyewe. Na Mwenyezi Mungu (s.w.t) atamlipa kila mmoja stahiki yake, hakika yeye ana habari ya wanayoyafanya.

Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyowapigia watu mifano yao akibainisha thawabu za mtenda mema na mfano wa watenda mema wenzake, ili awe na yakini ya wema wake na uongofu wake na kumbainishia muovu mfano wa adhabu ya waovu wenzake, ili aweze kujikanya na kuongoka.

Basi mnapokutana na waliokufuru wapigeni shingo mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu. Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vitue mizigo yake.

Aya hii ni miongoni mwa mama wa Aya na katika Aya zilizo wazi wazi na maudhui yake ya vita ni muhimu. Kwa hiyo kwanza tutafsiri misamiati yake kisha tubainishe maana yanayopatikana:

Makusudio ya kukutana ni kupamabana na maadui wa Uislamu katika vita. Kupiga shingo ni kinaya cha kuua; iwe ni kwa kukata shingo au vinginevyo. Mwenyezi Mungu amehusisha kutaja shingo kwa vile ni katika viungo muhimu. Kuwadhoofisha ni kuwaua sana na kuwakamata.

Kufunga pingu ni kuwafunga imara au kutia jela ili wasikimbie wakawarudishia mpira nyinyi. Kuwachilia kwa hisani ni kuwaachilia kwa fidia au bila ya kutoa fidia. Kutua vita mizio yake ni adui kusalimu amri na kutupa silaha. Kwa sababu mizigo ya vita ni silaha.

Maana ya Aya kwa ujumla ni maadui wa dini waking'ang'ania kufuru na mkapambana nao kwa vita, basi wapigeni ili isiwashike huruma na mpambane nao kwa uimara mpaka muwakamate.

Mkishawakamata basi muwazuie barabara ili wasiwaponyoke wasije wakawageukia. Baada ya hapo mwenye hiyari atakuwa ni Mtume au naibu wake, kuwaachia mateka kwa fidia au bila fidia kulingana na masilahi yalivyo wakati huo.

Ilivyo hasa maana ya Aya hii na ile simayo:

مَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَن يَكُونَ لَهُ أَسْرَىٰ حَتَّىٰ يُثْخِنَ فِي الْأَرْضِ ﴿٦٧﴾

"Haimfalii Nabii yoyote kuwa na mateka mpaka awe ameshinda sawasawa katika ardhi."

Juz. 10 (8:67),

Ni moja tu; yaani hakuna mateka ila baada ya kuwashinda vitani.

Ndio hivyo. Na lau angelitaka Mwenyezi Mungu angeliwashinda mwenyewe, lakini haya ni kwa sababu awatie katika mitihani nyinyi kwa nyinyi.

'Ndio hivyo,' ni ishara ya aliyoyabainisha Mwenyezi Mungu – kupigana na maaduia wa Mwenyezi Mungu na kuwachukua mateka. Maana ni kuwa lau Mwenyezi Mungu angelitaka kuwatesa maadui zake katika dunia bila ya vita angeliweza kuwaangamiza kwa askari wa kutoka mbinguni, lakini Mwenyezi Mungu amewaamuru waumini kupigana jihadi na kuwajaribu kwa makafiri, ili vidhihirike vitendo vya yule mwenye kustahiki thawabu na adhabu.

Na waliouliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu hatazipoteza amali zao.

Mwenyezi Mungu anapigana vita na mwenye kumuasi kwa kumtumia mwenye kumtii. Akiuliwa mtiifu, damu yake haiendi bure. Vipi isiwe hivyo na hali atakuwa shahidi wa njia ya Mwenyezi Mungu na kwa ajili yake? Ni nani anayemtekelezea Mwenyezi Mungu kuliko yule aliyemafanyia ikhlasi na akafanya kwa ajili yake?

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amebainisha ujira wa waliofanya kwa ajili yake kwa kusema: "Hatapoteza amali zao," bali itawarudia wao heri. Hiyo ni kwa kuwa Atawaongoza peponi kwenye mashukio yao, sawa na walivyokuwa wakiongoka kwenye nyumba zao za duniani na awatengezee hali yao, siku ile mtu atakapomkimbia ndugu yake na mama yake na wanawe.

Na atawaingiza katika Pepo aliyowajulisha mito yake, matunda yake, makasri yake, mahurilaini wake na mengineyo yanayotamaniwa na nafsi na yale yanayoburudisha macho.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَنصُرُوا اللَّـهَ يَنصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ ﴿٧﴾

7. Enyi mlioamini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atawanusuru ataithibitisha miguu yenu.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا فَتَعْسًا لَّهُمْ وَأَضَلَّ أَعْمَالَهُمْ ﴿٨﴾

8. Na waliokufuru, basi kwao ni maangamizo, na atavipoteza vitendo vyao,

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَرِهُوا مَا أَنزَلَ اللَّـهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ ﴿٩﴾

9. Hayo ni kwa sababu waliyachukia aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi akaviangusha vitendo vyao.

أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَيَنظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الَّذِي نَ مِن قَبْلِهِمْ دَمَّرَ اللَّـهُ عَلَيْهِمْ وَلِلْكَافِرِينَ أَمْثَالُهَا ﴿١٠﴾

10. Je, hawatembei katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa waliokuwa kabla yao? Mwenyezi Mungu aliwaangamiza. Na kwa makafiri hawa itakuwa mfano wa hayo.

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّـهَ مَوْلَى الَّذِينَ آمَنُوا وَأَنَّ الْكَافِرِينَ لَا مَوْلَىٰ لَهُمْ ﴿١١﴾

11. Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini. Na makafiri hawana mlinzi.

إِنَّ اللَّـهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِ ن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَالَّذِينَ كَفَرُوا يَتَمَتَّعُونَ وَيَأْكُلُونَ كَمَا تَأْكُلُ الْأَنْعَامُ وَالنَّارُ مَثْوًى لَّهُمْ ﴿١٢﴾

12. Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza ambao wameamini na wakatenda mema katika Bustani zipitiwazo na mito chini yake. Na ambao wamekufuru hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makazi yao.

وَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ هِيَ أَشَدُّ قُوَّةً مِّن قَرْيَتِكَ الَّتِي أَخْرَجَتْكَ أَهْلَكْنَاهُمْ فَلَا نَاصِرَ لَهُمْ ﴿١٣﴾

13. Na miji mingapi iliyo kuwa na nguvu zaidi kuliko mji wako huu uliokutoa; nao tuliwateketeza na wala hawakuwa na wa kuwanusuru.

أَفَمَن كَانَ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّهِ كَمَن زُيِّنَ لَهُ سُوءُ عَمَلِهِ وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُم ﴿١٤﴾

14. Je, mwenye kuwa na dalili kutoka kwa Mola wake ni kama aliyepambiwa uovu wa vitendo vyake, na wakafuata hawa zao?

## MKIMNUSURU MWENYEZI MUNGU ATAWANUSURU

**Aya 7 – 14**

### MAANA

Enyi mlioamini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atawanusuru ataithibitisha miguu yenu.

Kuithibitisha miguu ni kinaya cha uimara. Aya hii ni dalili wazi kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) yuko pamoja na watu wa haki na uadilifu; anawasaidia na kuwashika mkono. Maana ya Aya hii yako kwenye Aya nyingi; kama vile:

فَإِنَّ حِزْبَ اللَّـهِ هُمُ الْغَالِبُونَ ﴿٥٦﴾

"Basi kundi la Mwenyezi Mungu ndio watakaoshinda." Juz. 6 (5:56).

إِنَّ اللَّـهَ مَعَ الَّذِينَ اتَّقَوا وَّالَّذِينَ هُم مُّحْسِنُونَ ﴿١٢٨﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wenye uchamungu Na wale ambao wanatenda mema" Juz. 14 (16:128),

إِنَّ اللَّـهَ يُدَافِعُ عَنِ الَّذِينَ آمَنُوا ﴿٣٨﴾... وَلَيَنصُرَنَّ اللَّـهُ مَن يَنصُرُهُ إِنَّ اللَّـهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٤٠﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu huwakinga walioamini. Na hakika Mwenyezi Mungu humnusuru yule anayemnusuru Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mtukufu." Juz. 17 (22:38,40).

Nusra inayotoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) iko namna nyingi; miongoni mwazo ni hizi zifutazo:

• Kuwashinda maadui kwa vita na nguvu ya silaha; kama alivyowashinda Mtume wa Mwenyezi Mungu vigogo wa kikuraishi na dhulma yao na wengineo.

• Kushinda kwa adhabu itokayo mbinguni; kama vile kimbunga tufani n.k.

• Kushinda kwa nguvu ya hoja na dalili katika mijadala.

• Kushinda kwa shani na utajo wa kudumu duniani.

• Nusra ya Akhera siku ile zitakosawijika nyuso.

وَتَرَى الْمُجْرِمِينَ يَوْمَئِذٍ مُّقَرَّنِينَ فِي الْأَصْفَادِ ﴿٤٩﴾

"Na utawaona wahalifu siku hiyo wamefungwa katika minyororo." Juz. 13 (14:49).

Kwa vile katika Aya tuliyo nayo nusra haikufungwa na sifa ya aina yoyote, basi inatubainikia kuwa makusudio ya nusura katika Aya hii ni nusra yoyote. Hakuna mwenye shaka kuwa itakuwa tu, hata kama ni huko Akhera kusiko na shaka. Kwa hiyo basi hakuna nafasi ya kutaaradhi au kuuliza kuwa vipi Mwenyezi Mungu amewaahidi wenye haki nusra yake, lakini historia imejaa dhulma na ujeuri waaliofanyiwa wema na wenye ikhlasi.

Yametangulia maelezo kuhusu maudhui haya katika Juz. 17 (22:38) kifungu cha "Mwenyezi Mungu huwakinga walioamini."

## DOLA YA KIISLAMU

Kwa mnasaba wa Aya hii tutadokeza yafuatayo: Kuna vikundi siku hizi vinadai kusimamisha dola ya Kiislamu. Ni mwislamu gani leo, mwenye ikhlasi ya Mwenyezi Mungu anayekataa Uislamu uwe na serkali yake inayotekeleza hukumu za Qur'an na waislamu wawe na umoja utakaowaokoa na utengano?

Lakini tujiulize: Je, dola hii itapatikana kwa kiasi tu cha kusimamisha bendera na kuinua nembo? Au kwa kuweko vilemba vingi kwenye vichwa vya wajinga na wenye undani?

Je, inawezekana kuwaunganisha Waislamu milioni 700 walioenea mashariki na magharibi mwa ardhi huku wakiwa na makabila, madhehebu na siasa mbalimbali; hawa wameukumbatia ujamaa, wale ubepari na wengine wakiwa na siasa zisizofungamana na upande wowote?

Kama itapatikana dola hiyo ya waarabu au wasiokuwa waarabu je, itaweza kukabili majukumu yake na kutatua matatizo ya waislamu katika nchi nyingine. Kisha je, dola hii ni ya kisunni au kishia au ya wote wawili?

Majibu ya maswali haya tuwachie wataalamu wenye ikhlasi[1].

Hakika waislamu wamepatwa na udhalili mwingi na kushindwa. Kule kushindwa mnamo tarehe 5 June inatosha kuwa ni udhalili na utwevu. Sababu ya kwanza na ya mwisho ya kushindwa huko ni utengano. Dawa pekee ya hilo ni maarufu kwa wote – kusimama safu moja dhidi ya maadui wenye ushirikiano waliojipanga na kujitokeza kwenye vita vya mwezi June.

Mwenye kumfanyia ikhlasi Mwenyezi Mungu na akataka kuwanasihi waislamu kwa ukweli kabisa basi na afanye juhudi zake zote kwa ajili ya kuwasaidia waislamu kujikomboa na nguvu ya ufisadi ya ndani na nje.

---

1. Ikumbukwe mwandishi aliandika katika miaka ya 1970.

Wakishajikomboa na kuwa na uhuru kamili, hapo ndipo wenye ikhlasi wanaweza kufikiria serikali ya kiislamu au nyingine yenye kuridhiwa na Mwenyezi Mungu na yenye masilahi kwa waislamu.

Ishara yetu hii inatiliwa nguvu na kauli ya Imam Ali (a.s): **"Hakika uzushi wenye kutatiza ni maangamizi ... na katika utawala wa Mungu kuna hifadhi ya mambo yenu basi upeni utiifu wenu au Mwenyezi Mungu atawaondolea utawala wa kiislamu."**

Ikiwa utawala wa kiisalamu uliwaondokea wahenga kwa sababu ya utengano wao, je utaweza kuturudia sisi tuliotengana zaidi.

**Unaweza kuuliza**: Je, ni kweli yanayosemwa kuwa chimbuko la fikra ya dola ya kiislamu ni uzayuni ili kuitakasa dola yake ya kidini na ya kibaguzi? Ili waweze kusema kuwa hata waislamu nao pia wanataka dola ya kidini?

**Jibu**: Hakika dini ya kiyahudi ni dini ya uadui wa maisha na ubinadamu. Kwa sababu, katika itikadi yao, Mwenyezi Mungu ni Mungu wa kikabila, hajishughulishi na walimwengu wengine wote isipokuwa Israil peke yake, na kwamba watu wengine wote wameumbwa kuwatumikia wao; kama ilivyoelezwa katika kitabu Alkanzul marsud cha Dkt. Yussuf Hanna Naasrullah na kitabu Albaqau lilyahud cha mzayuni Rose Marine.

Ama Uislamu ni dini ya maisha, huruma na ubaindamu kwa ujumla. Hakuna kitu kinachofahamisha hivyo zaidi kuliko Aya na Hadithi zinazotangaza waziwazi kuwa uislamu unaongoza kwenye usawa zaidi na kwamba unatilia mkazo kwenye akili na maumbile na ni wajibu kuitikia mwito wa Mwenyezi Mungu na Mtume, kwa sababu ni mwito wa maisha bora.

Maana ni kuwa Uislamu ni dini ya kilimwengu ya kiakili; yaani unajishughulisha na mtu kama mtu wa namna yeyote, hata kama ni myahudi, kwa sharti ya kutomfanyia uadui nduguye mtu.

Sasa haya ni wapi kwa wapi na dini ya Mayahudi waliojiita taifa teule la Mwenyezi Mungu?

Na waliokufuru, basi kwao ni maangamizo, hawataona isipokuwa hizaya na maangamizi na atavipoteza vitendo vyao, haitawarudia heri yoyote.

Hayo ni kwa sababu waliyachukia aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi akaviangusha vitendo vyao.

Walimchukia Mtume **(s.a.w.w)** na Qur'an si kwa lolote ila ni kwa vile aliwatakia haki na wao wanaichukia, basi wakawa ni wenye hasara. Kupotea na kuanguka kuna maana moja, nako ni kupotea na kutofaa amali. Mwenyezi Mungu amekariri ili kuashiria kuwa kuikufuru Qur'an na kuichukia ni kupotea amali.

Je, hawatembei katika ardhi wakaona ulikuwaje mwisho wa waliokuwa kabla yao?

Jinsi washirikina walivyokadhibisha risala ya Muhammad **(s.a.w.w)**, huku wakiona athari ya waliopita na wakisikia kuwa Mwenyezi Mungu aliwaadhibu walipowakadhibisha mitume?

Aya hii imetangulia kwa herufi zake katika Aya kadhaa.

Mwenyezi Mungu aliwaangamiza wao, watoto wao, wake zao na mali zao.

Na kwa makafiri hawa itakuwa mfano wa hayo.

Hukumu ya Mwenyezi Mungu kwa mataghuti ni moja – ikiwa atawaangamiza wa mwanzo kwa sababu ya uasi wao, basi wengine pia atawaangamiza kwa sababu hiyo hiyo.

Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa walioamini. Na makafiri hawana mlinzi.

'Hayo' ni hayo ya kuangamizwa. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu aliwaangamiza makafiri wakiwa hawana wa kuwasaidia, lakini waumini, msimamizi wao ni Mwenyezi Mungu, akiwakinga na kuwaaneemesha.

Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza ambao wameamini na wakatenda mema katika Bustani zipitiwazo na mito chini yake.

Maana yako wazi na imekwishatangulia katika Aya kadhaa huko nyuma.

Na ambao wamekufuru hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makazi yao.

Wao ni sawa na wanyama, wanakula tu na wala hawafikirii chochote. Kwa hiyo mwisho wao ni Jahannam makazi mabaya kabisa.

Imam Ali (a.s) anasema: **"Mimi sikuumbwa ili nijishughulishe na kula vizuri. kama mnyama aliyefungwa ambaye hamu yake ni lishe yake tu, au asiyefungwa ambaye shughuli yake kuu ni kuchakura majaa kwa ajili ya lishe yake na kucheza nayo anavyotaka."**

Na miji mingapi iliyo kuwa na nguvu zaidi kuliko mji wako huu uliokutoa; nao tuliwateketeza na wala hawakuwa na wa kuwanusuru.

Hili ni karipio kwa wale waliopanga njama za kumuua Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, akalazimika kuuhama mji wake wa Makka na kuelekea Madina. Tazama Juz. 9 (8:30).

Katika Tafsir Attabariy, imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas, kwamba Mtume alipotaka kuutoka mji wa Makka alisema: ''Wewe ni mji wa Mwenyezi Mungu unaopendeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu. Na wewe ni mji wa Mwenyezi Mungu unaopendeza zaidi kwangu. Lau sikuwa washirikina wamenitoa nisingelikutoka.'' Ndipo Mwenyezi Mungu (s.w.t) akateremsha Aya hii.

Je, mwenye kuwa na dalili kutoka kwa Mola wake ni kama aliyepambiwa uovu wa vitendo vyake, na wakafuata hawaa zao?

Yule mwenye kuichukua haki kutoka katika chimbuko lake na akawa na busara, hayuko sawa mbele ya Mwenyezi Mungu na yule anayeipima haki kwa hawaa yake na malengo yake, huku akijiona kuwa yeye ndiye mtu mwenye matendo mema zaidi kuliko wengine.

5

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

مَّثَلُ الْجَنَّةِ الَّتِي وُعِدَ الْمُتَّقُونَ ۖ فِيهَا أَنْهَارٌ مِّن مَّاءٍ غَيْرِ آسِنٍ وَأَنْهَارٌ مِّن لَّبَنٍ لَّمْ يَتَغَيَّرْ طَعْمُهُ
وَأَنْهَارٌ مِّنْ خَمْرٍ لَّذَّةٍ لِّلشَّارِبِينَ وَأَنْهَارٌ مِّنْ عَسَلٍ مُّصَفًّى ۖ وَلَهُمْ فِيهَا مِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ وَمَغْفِرَةٌ مِّن
رَّبِّهِمْ ۖ كَمَنْ هُوَ خَالِدٌ فِي النَّارِ وَسُقُوا مَاءً حَمِيمًا فَقَطَّعَ أَمْعَاءَهُمْ ﴿١٥﴾

15. Mfano wa Pepo waliyoahidiwa wenye takuwa ina mito ya maji yasiyoharibika, Na mito ya maziwa. Na mito ya mvinyo yenye utamu. Na mito ya asali iliyosafishwa. Na wao humo watakuwa na kila namna ya matunda, na maghufira kutoka kwa Mola wao. Basi je, hao ni kama watakaodumu Motoni? Na wakinyweshwa maji yanayochemka yatakayokata matumbo yao.

وَمِنْهُم مَّن يَسْتَمِعُ إِلَيْكَ حَتَّىٰ إِذَا خَرَجُوا مِنْ عِندِكَ قَالُوا لِلَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ مَاذَا قَالَ آنِفًا ۚ
أُولَـٰئِكَ الَّذِينَ طَبَعَ اللَّـهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ ﴿١٦﴾

16. Na wapo miongoni mwao wanaokusikiliza, mpaka wakiondoka kwako huwauliza waliopewa ilimu: Amesema nini sasa hivi? Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao, na wakafuata hawaa zao.

وَالَّذِينَ اهْتَدَوْا زَادَهُمْ هُدًى وَآتَاهُمْ تَقْوَاهُمْ ﴿١٧﴾

17. Na ambao wameongoka anawazidishia uongofu.

فَهَلْ يَنظُرُونَ إِلَّا السَّاعَةَ أَن تَأْتِيَهُم بَغْتَةً ۖ فَقَدْ جَاءَ أَشْرَاطُهَا ۚ فَأَنَّىٰ لَهُمْ إِذَا جَاءَتْهُمْ ذِكْرَاهُمْ
﴿١٨﴾

18. Kwani wanangojea jengine isipokuwa iwafikie Saa kwa ghafla? Basi sharti zake zimekwisha kuja. Na itapowajia kutawafaa wapi kukumbuka kwao?

فَاعْلَمْ أَنَّهُ لَا إِلَـٰهَ إِلَّا اللَّـهُ وَاسْتَغْفِرْ لِذَنبِكَ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ ۗ وَاللَّـهُ يَعْلَمُ مُتَقَلَّبَكُمْ
وَمَثْوَاكُمْ ﴿١٩﴾

19. Basi jua ya kwamba hapana mola ila Mwenyezi Mungu. Na omba maghufira kwa dhambi zako na za waumini wanaume na waumini wanawake. Na Mwenyezi Mungu anajua mahali penu pa kwenda na kurudi na mahali penu pa kukaa.

## SIFA ZA PEPO

**Aya 15 – 19**

### MAANA

Mfano wa Pepo waliyoahidiwa wenye takuwa ina mito ya maji yasiyoharibika.

Makusudio ya mfano wa pepo ni sifa zake. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu anawapa habari waja wake kwamba miongoni mwa sifa za pepo ni kuwa ndani yake mna mito ya maji yanayobaki na asili yake bila ya kubadilishwa na chochote.

Na mito ya maziwa isiyoharibika ladha yake wala rangi au harufu yake. Na mito ya mvinyo yenye utamu kwa wanywao. Ni tamu mdomoni wala hauleweshi. Na mito ya asali iliyosafishwa kutokana na masega na mengineyo. Na wao humo watakuwa na kila namna ya matunda yakiwemo yale ambayo hayana mfano wake duniani.

Katika baadhi ya vitabu vya kisufi imeandikwa kuwa Makusudio ya maji hapa ni ilimu, maziwa ni matendo, mvinyo ni mahaba na asali ni utamu wa maarifa na kuwa karibu na Mwenyezi Mungu.

Tumekwishatangulia kusema mara nyingi kwamba kila kinachokuja katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu inapasa kukichukulia kwa dhahiri yake mpaka ithibitike kinyume kutokana na nakili au akili. Hapa akili haikatai chochote katika sifa za pepo zilizotajwa. Kwa hiyo basi ni wajibu kuchukulia dhahiri yake na kubaki hivyo hivyo.

**Unaweza kuuliza**: Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja mara kadhaa katika Kitabu chake kuwa watu wa Peponi watastarehe kwa ladha za kimaana, sio za kihisia; kama vile Kupendwa na kuridhiwa na Mwenyezi Mungu na kuinuliwa daraja zao kwake. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

﴿فِي مَقْعَدِ صِدْقٍ عِندَ مَلِيكٍ مُّقْتَدِرٍ ﴿٥٥﴾

"Katika makao mazuri karibu na Mfalme Mwenye uwezo." (54:55)

Na kauli yake:

﴿سَيَجْعَلُ لَهُمُ الرَّحْمَـٰنُ وُدًّا ﴿٩٦﴾

"Mwingi wa rehema atawajaalia mapenzi." Juz. 16 (19:96).

Sasa je, kuna wajihi gani wa kuchanganya Aya zile zinazofahamisha neema ya Peponi inayokuwa kwa ladha za kihisia na zile zinazofahamisha ladha ya kimaana?

**Jibu**: hakuna kizuizi cha kuzuia kuchanganya zote mbili na kutumia ufahamisho wote. Kwa hiyo watu wa Peponi watastarehe kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu na kuinuliwa daraja zao mbele yake; vile vile watastarehe na vitu vizuri katika vyakula na vinywaji.

Mula Sadra anasema katika Asfar: "Ama Pepo iko kama ilivyojulishwa na Kitabu na sunna kwa kufuatana na dalili. Ndani yake hamtakuwa na mauti wala uzee, ghamu au maradhi. Hakuna kuisha wala kuondoka.

Ni nyumba ya cheo na utukufu. Wakazi wake hawatapata tabu wala kuchoka. Humo watapata kila kinachotamaniwa na nafsi na kuburudisha macho na watadumu humo.

"Wakazi wake watakua karibu na Mwenyezi Mungu, ni mawalii wake ni wapenzi wake na ni watu wa karama yake. Na kwamba wao watakuwa na daraja bora; miongoni mwao kuna watakaostarehe kwa tasbih na takbir, na wengine watastarehe kwa ladha za hisia; kama vile aina ya vyakula, vinywaji na matunda. Pia makochi, mahurilaini na kutumikiwa na vijana. Vile vile kukaa kwenye mito na mazulia na kuvaa hariri nyepesi na nzito. Kila mmoja ataburudika kulingana na hamu yake."

Na maghufira kutoka kwa Mola wao.

Wale wanaostarehe na anasa za dunia huko watahisabiwa hisabu nzito: Ama watu wa Peponi wao watakuwa kwenye neema wakiwa kwenye amani ya hisabu ya Mwenyezi Mungu na adhabu yake.

Basi je hao ni kama watakaodumu Motoni?

Hapa kuna maneno ya kukadiriwa yanayofahamika kutokana na mfumo wa maneno; kukadiriwa kwake ni je, atakayedumu Peponi ni sawa na atakayedumu Motoni? Hapana hawalingani sawa.

Na wakinyweshwa maji yanayochemka yatakayokata matumbo yao.

Vipi watakuwa sawa na hali watu wa Peponi watakunywa maji matamu, maziwa, mvinyo na asali safi; na watu wa motoni watakunywa usaha na maji moto yanayotokota matumboni?

Na wapo miongoni mwao wanaokusikiliza, mpaka wakiondoka kwako huwauliza waliopewa ilimu: Amesema nini sasa hivi?

Yaani miongoni mwa watu wanaokusikiliza wewe Muhammad wako makafiri au wanafiki na wanapotoka wanasema kwa dharau kuwaambia wale waliohudhuria katika maulama wa watu wa kitabu: ati amesemaje huyo sasa hivi? Sisi hatukufahamu. Je nyinyi mmefahamu kitu? Hii ndio tabia ya yule asiyeona chochote isipokuwa matamanio yake tu.

Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao, na wakafuata hawa zao.

Kauli yake Mwenyezi Mungu (s.w.t): 'Na wakafuata matamanio yao,' inaashiria jawabu la swali; Kwanini Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao? Ndio majibu yakawa, kwa vile hawa zao zimememea kwenye nyoyo zao mpaka ikawa kama kwamba Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu yake au amewaumba bila ya nyoyo; kama anavyosema Mwenyezi Mungu:

﴿فَلَمَّا زَاغُوا أَزَاغَ اللَّـهُ قُلُوبَهُمْ ﴿٥﴾﴾

"Walipopotoka Mwenyezi Mungu alizipotoa nyoyo zao" (61:5).

Na ambao wameongoka anawazidishia uongofu.

Waumini waliutafuta uongofu kwa ukweli na ikhlas, kwa hiyo Mwenyezi Mungu amekuwa ndio muongozi na mlezi wao; akawazidishia elimu ya heri na akawapa ulinzi wake na tawfiki yake kwenye yale yaliyo na heri ya dunia yao na Akhera yao. Haya ndiyo Makusudio ya na anawapa takua yao.

Kwani wanangojea jengine isipokuwa iwafikie Saa ya Kiyama kwa ghafla?

Wanaambiwa wale waliosema kwa dharau: Ati amsema nini sasa hivi? Walisema hivi wakiwa wameghafilika kabisa na siku ambayo itawanyakuwa ghafla na wasimame mbele ya Mwenyezi Mungu kwa ajili ya hisabu.

Basi sharti zake zimekwisha kuja.

Makusudio ya sharti hapa ni dalili na hoja mkataa za ufufuo. Zimekuja katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu na mdomoni mwa Muhammad **(s.a.w.w)** kwa mifumo mbalimbali wala hazikuacha udhuru wowote kwa mkanushaji.

Na itapowajia kutawafaa wapi kukumbuka kwao?

Maana ni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwakumbusha duniani, lakini wakakataa, na watakapofufuliwa na kuona adhabu watakumbuka na kujuta, lakini wakati huo hakutafaa chochote kukumbuka kwao.

Basi jua ya kwamba hapana Mola ila Mwenyezi Mungu Yeye anahuisha na kufisha na kuadhibu na kutoa adhabu. Sio mbali kuwa maana ya hapana mola isipokuwa Mwenyezi Mungu hapa, ni lingania Mwenyezi Mungu na umoja wake.

Na omba maghufira kwa dhambi zako na za waumini wanaume na waumini wanawake.

Kuomba maghufira kwa dhambi ni jambo linalopendeza kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na ni jambo linalotakina hasa; ni sawa kuweko na dhambi au la.

Na Mwenyezi Mungu anajua mahali penu pa kwenda na kurudi matendo ya duniani na mahali penu pa kukaa mtakapoacha matendo yenu au kwenda zenu Akhera; kama ilivyosemekana.

Vyovyote iwavyo ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) anajua hali ya waja wake duniani na Akhera na pale wanapokuwa katika harakati na wanapotulia.

وَيَقُولُ الَّذِينَ آمَنُوا لَوْلَا نُزِّلَتْ سُورَةٌ ۖ فَإِذَا أُنزِلَتْ سُورَةٌ مُّحْكَمَةٌ وَذُكِرَ فِيهَا الْقِتَالُ ۙ رَأَيْتَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ يَنظُرُونَ إِلَيْكَ نَظَرَ الْمَغْشِيِّ عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ ۖ فَأَوْلَىٰ لَهُمْ ﴿٢٠﴾

20. Na wanasema wale ambao wameamini: Kwa nini haiteremshwi Sura? Na inapoteremshwa Sura iliyo waziwazi na vikatajwa ndani yake vita, utawaona wenye maradhi katika nyoyo zao. wanakutazama mtazamo wa anayezimia kwa mauti. Basi ole wao.

طَاعَةٌ وَقَوْلٌ مَّعْرُوفٌ ۚ فَإِذَا عَزَمَ الْأَمْرُ فَلَوْ صَدَقُوا اللَّـهَ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُمْ ﴿٢١﴾

Utiifu na kauli njema. Na jambo likishaazimiwa, basi wakiwa ni wakweli kwa Mwenyezi Mungu, bila ya shaka itakuwa ni heri kwao.

فَهَلْ عَسَيْتُمْ إِن تَوَلَّيْتُمْ أَن تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَتُقَطِّعُوا أَرْحَامَكُمْ ﴿٢٢﴾

22. Basi yanayotarajiwa kwenu mkitawala ndio mtafanya ufisadi katika nchi na mtaukata udugu wenu?

أُولَـٰئِكَ الَّذِينَ لَعَنَهُمُ اللَّـهُ فَأَصَمَّهُمْ وَأَعْمَىٰ أَبْصَارَهُمْ ﴿٢٣﴾

23. Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewalaani, na akawatia uziwi, na akawapofoa macho yao.

## UTIIFU NA KAULI NJEMA

**Aya 20 – 23**

### MAANA

Na wanasema wale ambao wameamini: Kwa nini haiteremshwi Sura?'' Na inapoteremshwa Sura iliyo waziwazi na vikatajwa ndani yake vita, utawaona wenye maradhi katika nyoyo zao wanakutazama mtazamo wa anayezimia kwa mauti.

Hapa kuna kukadiria maneno kuwa: Kwa nini haiteremshwi sura ya vita? Dalili ya kukadiria huku ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: 'Na vikatajwa ndani yake vita.' Hali hii watu wa nahw wanaiita ufahamisho unaofahamishwa na wa pili. Iliyo waziwazi ni kutaja vita waziwazi. Maradhi hapa ni shaka na unafiki.

Maana ni kuwa waumini wenye ikhlasi walikuwa wakitamani Qur'an iwaamrishe jihadi ya kupigana na makafiri na waovu. Wanapoitwa walikuwa wakienda haraka kujitolea nafsi zao katika njia ya Mwenyezi Mungu, huku wakiwa na furaha ya kukutana na Mwenyezi Mungu na thawabu zake.

Ama wale walio na maradhi nyoyoni mwao ambao ni wanafiki, walikuwa wakichukia sana jihadi na vita, na inapoteremshwa Aya ya vita basi mishipa inawasimama kwa hofu wakimwangalia Mtume kwa mtazamo wa hofu, kama anayeangalia mauti yakimjia.

Basi ole wao.

Wafasiri wengi wamesema maana ya neno Awla hapa ni 'ole wao' ambalo pia lina maana ya bora. Mfumo wa maneno unakubaliana na maana hii ya ole wao.

Utiifu na kauli njema.

Haya ni maneno yanayoanza tena. Maana yake ni kuwa kumtii Mwenyezi Mungu na kauli njema atakayoikubali Mtume ni bora kwao kuliko kukijaza kifua na unafiki na kumtazama Mtume kwa jicho la chuki na hofu.

Na jambo likishaazimiwa, basi wakiwa ni wakweli kwa Mwenyezi Mungu, bila ya shaka itakuwa ni heri kwao.

Lau wanafiki wangelimfanyia ikhlasi Mwenyezi Mungu na wakaitikia mwito wa Mtume inapokuja amri ya vita na ikawa ni lazima, ingelikuwa ni heri ya dunia yao na Akhera yao. Lakini walikataa isipokuwa ufisadi.

Basi yanayotarajiwa kwenu mkitawala ndio mtafanya ufisadi katika nchi na mtaukata udugu wenu?

Nyinyi wanafiki mmedhihirisha Uislamu kwa kujilazimisha na kuogopa nguvu yake. Huenda mkipata nguvu na utawala mtaijaza ardhi ufisadi kwa ibada ya masanamu na kumwaga damu, kupora mali na kuvunja udugu.

Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewalaani kwa kuwaweka mbali na rehema, na akawatia uziwi, na akawapofoa macho yao.

Walipoutilia uziwi mwito wa haki na kuufumbia macho ndio Mwenyezi Mungu naye akawatia uziwi na kuwapofua. Kwa maneno mengine ni kuwa walifuata njia ya maangamizi kwa hiyari yao ndio Mwenyezi Mungu akawaangamiza:

وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَـٰكِن ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ ...﴿١٠١﴾

"Na hatukuwadhulumu, lakini wamejidhulumu wenyewe" Juz. 12 (11:101).

6

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

أَفَلَا يَتَدَبَّرُونَ الْقُرْآنَ أَمْ عَلَىٰ قُلُوبٍ أَقْفَالُهَا ﴿٢٤﴾

24. Je, Hawaizingatii hii Qur'an? Au kwenye nyoyo zipo kufuli?

إِنَّ الَّذِينَ ارْتَدُّوا عَلَىٰ أَدْبَارِهِم مِّن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْهُدَى الشَّيْطَانُ سَوَّلَ لَهُمْ وَأَمْلَىٰ لَهُمْ ﴿٢٥﴾

25. Kwa hakika ambao wanarudi kwa migongo yao baada ya kuawabainikia uwongofu, Shetani huyo amewashawishi na amewacheleweshа.

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا لِلَّذِينَ كَرِهُوا مَا نَزَّلَ اللَّهُ سَنُطِيعُكُمْ فِي بَعْضِ الْأَمْرِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِسْرَارَهُمْ
﴿٢٦﴾

26. Hayo ni kwa sababu waliwaambia waliochukia aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu: Tutawatii katika baadhi ya mambo. Na Mwenyezi Mungu anajua siri zao.

فَكَيْفَ إِذَا تَوَفَّتْهُمُ الْمَلَائِكَةُ يَضْرِبُونَ وُجُوهَهُمْ وَأَدْبَارَهُمْ ﴿٢٧﴾

27. Basi itakuwaje Malaika watakapowafisha wakawa wanawapiga nyuso zao na migongo yao!

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمُ اتَّبَعُوا مَا أَسْخَطَ اللَّهَ وَكَرِهُوا رِضْوَانَهُ فَأَحْبَطَ أَعْمَالَهُمْ ﴿٢٨﴾

28. Hayo ni kwa sababu wao waliyafuata yaliyomchukiza Mwenyezi Mungu na wakachukia yanayomridhisha. Basi akaviangusha vitendo vyao.

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ أَن لَّن يُخْرِجَ اللَّهُ أَضْغَانَهُمْ ﴿٢٩﴾

29. Je, ambao wana maradhi nyoyoni mwao wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu hatazidhihirisha chuki zao?

وَلَوْ نَشَاءُ لَأَرَيْنَاكَهُمْ فَلَعَرَفْتَهُم بِسِيمَاهُمْ وَلَتَعْرِفَنَّهُمْ فِي لَحْنِ الْقَوْلِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ أَعْمَالَكُمْ
﴿٣٠﴾

30. Na lau tungelipenda, tungelikuonyesha hao na ungeliwatambua kwa alama zao. Na bila ya shaka utawajua kwa namna ya usemi Na Mwenyezi Mungu anavijua vitendo vyenu.

وَلَنَبْلُوَنَّكُمْ حَتَّىٰ نَعْلَمَ الْمُجَاهِدِينَ مِنكُمْ وَالصَّابِرِينَ وَنَبْلُوَ أَخْبَارَكُمْ ﴿٣١﴾

31. Na bila ya shaka tutawajribu mpaka tuwajue wapignao jihadi katika nyinyi na wanaosubiri. Nasi tutazijaribu habari zenu.

## JE HAWAIZINGATI QUR'AN?

**Aya 24 – 31**

### MAANA

Je, Hawaizingatii hii Qur'an? Au kwenye nyoyo zipo kufuli?

Wanaambiwa wanafiki. Kwa sababu Aya hii na ilie iliyo kabla yake inawazungumzia wao. Dalili zote zilizokuja katika Qur'an, za kuweko Mwenyezi Mungu katika kuumbwa mbingu na ardhi, hoja wazi za utume wa Muhammad **(s.a.w.w)**.

Ubaya wa shirki, dhulma na ufisadi katika ardhi, yote hayo yako wazi hayakufumbwafumbwa; kuongezea athari ya mfumo wa Qur'an katika moyo wa msomaji na msikilizaji anavyopata hisia. Basi makafiri wananini hawaathiriki na muujiza huu? Je, wamekosa usikizi na macho au nyoyo zao zimefungwa na kufuli na kutu.

Kwa hakika ambao wanarudi kwa migongo yao baada ya kuawabainikia uwongofu, Shetani huyo amewashawishi na amewacheleweshа.

Neno kurudi tumelifasiri kutokana na neno la kiarabu Irtaddu (kuritadi) lenye maana ya kuamini haki kisha kuikanusha. Pia kuijua haki kwa dalili mkataa kisha kuikanusha kwa matamanio ya nafsi, kunaingia katika hukumu ya kuritadi, kwa sababu kuijua haki ni sawa na kuiamini na kuichukia ni sawa na kuiritadi.

Ama mwenye kuficha ukafiri na akadhihirisha imani huyo ni mnafiki na murtadi vile vile. Ni mnafiki kwa vile amedhihirisha kinyume na yaliyo moyoni mwake na ni murtadi kwa kuwa duniani anakuwa kama mumin na Akhera anakuwa kafiri; kama kwamba yeye ni mumin na wakati huo huo ni murtadi.

Tamko la Aya limegusia aina zote tatu. Kwa sababu dalili za dhahiri zilizosimaia kwenye Tawhid, ufufuo na utume wa Muhammad **(s.a.w.w)** ndio hoja aliyoikusuduia Mwenyezi Mungu kwa kusema: 'Baada ya kuwabainikia uongofu,' lakini shetani aliwadanganya kwa unafiki na kuiritadi haki na kuipinga. Akawaahidi ahadi ya uwongo na kuwatia wasiwasi wa tamaa na matamanio.

Hayo ni kwa sababu waliwaambia waliochukia aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu: Tutawatii katika baadhi ya mambo.

Waliosema ni wanafiki na waliochukia ni mayahudi waliokuwa majirani wa Mtume. Kwa sababu mayahudi ndio watu wanaochukia zaidi kila kilichoteremshwa na Mwenyezi Mungu; hasa Qur'an. Maana ni kuwa wanafiki waliwambia mayahudi: sisi tuko pamoja na nyinyi kuhusu Muhammad na tunashirikiana nanyi katika kumpiga vita; isipokuwa hali haituruhusu kutangaza uadui wetu kwake. Kwa hiyo tuacheni tujionyeshe kuwa ni waislamu na tutakuwa pamoja nanyi kwenye njama dhidi yake.

Na Mwenyezi Mungu anajua siri zao.

Yaani siri za mayahudi na za wanafiki, kwa sababu kwake hakifichiki chochote katika ardhi wala mbinguni.

Basi itakuwaje Malaika watakapowafisha wakawa wanawapiga nyuso zao na migongo yao!

Wamekimbia jihadi kwa kuogopa mauti, je wataweza kuyakimbia mauti na mapigo yake? Na ufufuo na vituko vyake.

Hayo ni kwa sababu wao waliyafuata yaliyomchukiza Mwenyezi Mungu na wakachukia yanayomridhisha.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) atawaadhibu wakati wa mauti na baada yake vile vile, kwa vile waliathirika na yale yanayomchukiza Mwenyezi Mungu kuliko yale yanayomridhisha.

Basi akaviangusha vitendo vyao, havitawafaa kitu.

Je, ambao wana maradhi nyoyoni mwao wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu hatazidhihirisha chuki zao?

Wanafiki walificha chuki na uadui kwa Mtume na maswahaba; wakawadhihirishia upendo na utii; wakadhani kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) hatadhihirisha wanayoyaficha vifuani mwao.

Na lau tungelipenda tungelikuonyesha hao na ungeliwatambua kwa alama zao.

Kukuonyesha ni kukutambulisha na kutambua ni kuwatambua kwa alama zao. Lengo la kugawanya huku kunakofanana na kukaririka ni kusisitiza kuwa Mtume hapitwi na kitu anachofahamishwa na Mwenyezi Mungu. Lakini asiyekuwa Mtume anaweza kukosea katika kufahamu kwake.

Dhahiri ya Aya inafahamisha kuwa ilishuka kabla ya Mtume kuwafahamu wanafiki, kutokana na neno 'lau,' lakini Mtume **(s.a.w.w)** aliwatambua baadae kutoka na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

Na bila ya shaka utawajua kwa namna ya usemi wao.

Namna ya usemi ni kule kumaanisha kwake; kama vile udhuru wa uwongo waliokuwa wakiutoa wanafiki na jinsi wanavyowalaumu watu wema na kuwasifu washari na mengineyo yanayojiachia mdomoni yanayaofahamisha ria na unafiki.

Imepokewa Hadith kutoka kwa Anas: "Hakufichika mnafiki kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, baada ya Aya hii." Vile vile Nabii **(s.a.w.w)** alikuwa akiwajuwa wanafiki kwa vitendo vyao. Walikuwa wakiikimbia jihadi na wakiona uzito kujitolea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Na Mwenyezi Mungu anavijua vitendo vyenu.

Hili ni kemeo kwa kila anayedhihirisha heri na kuficha shari.

Na bila ya shaka tutawajaribu mpaka tuwajue wapignao jihadi katika nyinyi na wanaosubiri. Nasi tutazijaribu habari zenu.

Mwenyezi Mungu anawajua wanaopigana jihadi na walio na subira kabla ya kuwafanyia majaribio, lakini anafanya hivi kwa kuamrisha na kukataza ili amdhihirishe na amtambulishe muovu na mwema kwa vitendo ambavyo vinastahiki adhabu au thawabu.

Imeelezwa katika Nahjul-balagha: "Mwenyezi Mungu anataka mumnusuru na hali yeye ana majeshi ya mbinguni na ardhini na Yeye ni Mwenye nguvu Mwenye hekima. Na anataka mukopeshe na Yeye ana hazina za mbingu na ardhi na Mwenye kujitosha Mwenye kusifiwa…Anataka kuwajaribu ninani wenu mwenye matendo mema zaidi.

Basi harakisheni matendo yenu mtakuwa jirani na Mwenyezi Mungu."

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّـهِ وَشَاقُّوا الرَّسُولَ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْهُدَىٰ لَن يَضُرُّوا اللَّـهَ شَيْئًا وَسَيُحْبِطُ أَعْمَالَهُمْ ﴿٣٢﴾

32. Hakika ambao wamekufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu na wakakinzana na Mtume baada ya kuwabainikia uwongofu, hawatamdhuru Mwenyezi Mungu kwa lolote, na ataviangusha vitendo vyao.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّـهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَلَا تُبْطِلُوا أَعْمَالَكُمْ ﴿٣٣﴾

33. Enyi ambao mmeamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake! Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume; wala msiviharibu vitendo vyenu.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّـهِ ثُمَّ مَاتُوا وَهُمْ كُفَّارٌ فَلَن يَغْفِرَ اللَّـهُ لَهُمْ ﴿٣٤﴾

34. Hakika ambao wamekufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, kisha wakafa na hali ni makafiri, Mwenyezi Mungu hatawaghufiria.

فَلَا تَهِنُوا وَتَدْعُوا إِلَى السَّلْمِ وَأَنتُمُ الْأَعْلَوْنَ وَاللَّـهُ مَعَكُمْ وَلَن يَتِرَكُمْ أَعْمَالَكُمْ ﴿٣٥﴾

35. Basi msilegee na kuita kwenye suluhu. Na hali nyinyi ndio mko juu; Na Mwenyezi Mungu yuko pamoja nanyi, Wala hatawanyima malipo ya vitendo vyenu.

إِنَّمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَلَهْوٌ وَإِن تُؤْمِنُوا وَتَتَّقُوا يُؤْتِكُمْ أُجُورَكُمْ وَلَا يَسْأَلْكُمْ أَمْوَالَكُمْ ﴿٣٦﴾

36. Hakika uhai wa duniani ni mchezo na upuzi. Na mkiamini na mkawa na takua, atawapa ujira wenu, Wala hawaombi mali zenu.

إِن يَسْأَلْكُمُوهَا فَيُحْفِكُمْ تَبْخَلُوا وَيُخْرِجْ أَضْغَانَكُمْ ﴿٣٧﴾

37. Akiwaomba hizo na akiwashikilia mtafanya ubakhili, na atatoa chuki zenu.

هَا أَنتُمْ هَـٰؤُلَاءِ تُدْعَوْنَ لِتُنفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّـهِ فَمِنكُم مَّن يَبْخَلُ وَمَن يَبْخَلْ فَإِنَّمَا يَبْخَلُ عَن نَّفْسِهِ وَاللَّـهُ الْغَنِيُّ وَأَنتُمُ الْفُقَرَاءُ وَإِن تَتَوَلَّوْا يَسْتَبْدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُونُوا أَمْثَالَكُم ﴿٣٨﴾

38. Ehee! Nyinyi mnaitwa mtumie katika njia ya Mwenyezi Mungu, Na wapo katika nyinyi wanaofanya ubakhili. Na anayefanya ubakhili basi anajifanyia ubakhili mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, na nyinyi ndio wahitaji. Na mkigeuka atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi.

## MSIBATILISHE AMALI ZENU

**Aya 32 – 38**

### MAANA

Hakika ambao wamekufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu na wakakinzana na Mtume baada ya kuwabainikia uwongofu, hawatamdhuru Mwenyezi Mungu kwa lolote, na ataviangusha vitendo vyao.

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alilingania kwenye Uislamu kwa dalili na ubainifu; wakakaukataa watu wa masilahi na wakawazuia watu wasiukubali Uislamu kwa kutumia nguvu, mali na propaganda za uwongo.

Lakini Mwenyezi Mungu alimpa nguvu Mtume wake, akaidhihirisha dini yake na akaviangusha vitendo vya wahaini.

Hadi leo Uislamu na waislamu wanakabiliana sana na nguvu za shari. Zilizo hatari zaidi ni baadhi ya dola zinazobeba jina la Uislamu huku zikishirikiana na adui mkubwa zaidi, mkoloni wa kizayuni. Umefika wakati, sasa, waislamu waondoe vumbi la chuki na mfarakano ili waweze kuungana pamoja dhidi ya adui yao mwenye ushirikiano na wenzake.

Enyi ambao mmeamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake! Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume; yaani fanyeni mambo kwa imani yenu.

Kwa hiyo kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: 'Mtiini Mwenyezi Mungu,' baada ya kusema: 'Enyi ambao mmeamini,' ni sawa na kauli yake:

فَمَن كَانَ يَرْجُو لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا ﴿١١٠﴾

“Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake basi naatende matendo mema.” Juz. 16: (18:110).

Wala msiviharibu vitendo vyenu kwa shirki na unafiki wala kwa masimbulizi na udhia au kwa maovu ambayo huondoa mema. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ اللَّـهُ مِنَ الْمُتَّقِينَ ﴿٢٧﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu huwapokelea wamchao tu.” Juz. 6 (5:27).

Kuna Hadith isemayo: “Mwenyezi Mungu hakubali matendo ila kwatakua.” Imam Ali (a.s) anasema: **“Kwenye matendo, kuweni ni wenye kujishughulisha zaidi na kukubaliwa matendo.”**

Hakika ambao wamekufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, kisha wakafa na hali ni makafiri, Mwenyezi Mungu hatawaghufiria huko Akhera. Kwa sababu Mwenyezi Mungu (s.w.t.) atawafufua watu kulingana na walioyofia na atawahisabu kulingana na walivyomaliza uhai wao kwenye ukafiri au imani.

Umetangulia mfano wake katika Juz. 2 (2:161) na Juz. 3 (3:91).

### QUR’AN NA SIASA YA VITA

Basi msilegee na kuita kwenye suluhu.

Matukio yamethibitisha kwamba mwenye kulegea mbele ya adui yake na akaogopa kumkabili basi ndio amempa silaha atayompigia na kujifanya mnyonge kwake. Imam Ali (a.s) anasema: **“Kuogopa ni kuvunjika moyo na kuona haya ni kusumbuka.”**

Tazama Juz. 22 (33: 59-62) kifungu ‘Vita vya nafsi.’

Siasa nzuri ya vita ni kuwa mkakamavu mtu mbele ya adui yake, vile vile asipuuze nguvu za adui, bali ajiandae vizuri na amkabili kwa uimara kabisa bila ya kujali mashaka na tabu atakayoipata.

Qur’an imeandika siasa hii kwa kusema: “Basi msilegee na kuita kwenye suluhu.” Yaani msilegee mbele ya adui mkasalimu amri kwenye nguvu zao na utaghuti wao.

Pia kauli yake: “Na waandalieni nguvu vile muwezavyo.” Juz. 10 (8:60). Yaani msidharau nguvu zao; mjifunge kibwebwe kwa kila nguvu mliyo nayo ya watu na ya kiuchumi.

Na hali nyinyi ndio mko juu; yaani mtashinda, lakini mpaka muungune na kuwa safu moja kumkabili adui wenu na adui wa Mwenyezi Mungu; vinginevyo mtashindwa na haitabakia hata harufu yenu; kama inavyosema Qur’an katika Juz. 10 (8:46).

Na Mwenyezi Mungu yuko pamoja nanyi, mkiitikia mwito wake wa jihadi kwa hali na mali, ili tamko la Mwenyezi Mungu liwe juu ili neno la haki liwe juu na neno la batili liwe chini. Ama yule mwenye kupenda raha na akasalimu amri kwenye nguvu ya upotevu na ufisadi, basi Mwenyezi Mungu ataachana naye na kumwachia aliyejisalimisha naye

Wala hatawanyima malipo ya vitendo vyenu kuanzia nafsi, watu au mali iliyotoka kwa ajili ya dini, nchi au haki yoyote. Muhanga huu hauwezi kwenda burebure; bali ni heshima ya dini na nchi katika maisha ya duniani na ni akiba Akhera mbele ya Mwenyezi Mungu.

**Unaweza kuuliza**: Kauli yake Mwenyezi Mungu: “Basi msilegee na kuita kwenye suluhu na hali nyinyi ndio mko juu,” si inajulisha waziwazi

kwamba mwenye nguvu anafaa kumdhibiti mnyonge bila ya kuwa na huruma naye wala kuwa na suluhu naye? Bila shaka hili linapingana na ubinadamu na uadilifu, wala haliafikiani na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا ادْخُلُوا فِي السِّلْمِ كَافَّةً ﴿٢٠٨﴾

"Enyi ambao mmeamini! Ingieni kwenye usalama nyote" Juz. 2 (2:208)?

**Jibu**: kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Basi msilegee na kuita kwenye suluhu na hali nyinyi ndio mko juu," maana yake ni ikiwa mtapata balaa ya adui aliye mnyama asiyekuwa na kipimo cha haki wala uadilifu wala hajilazimishi na kanuni wala ahadi na pia hafahamu lugha yoyote isipokuwa nguvu. Mkifikiwa na adui wa aina hii basi nilazima mkabiliane; msimwogope wala msiwe na huruma katika haki. Kummaliza adui huyu ni kuimaliza shari na kuleta heri ya wote.

Ajabu ya sadfa! Imetokea wakati nikiandika maneno haya leo hii 8 April 1970, Israil, ikitumia ndege aina Phantoum ya Amerika na makombora yake, imeshambulia shule ya msingi ya Bahrul-baqar katika Jamhuri ya Umoja wa Kiarabu[1]1, na kuua watoto 47, na kujeruhi kadhaa, wenye umri wa kati ya miaka 6 hadi 12.

Bila shaka U.S.A. ndiyo inayobeba majukumu ya kuuliwa watoto wadogo wasiokuwa na hatia yoyote. Na pia majukumu ya mashambulizi ya mfano huo yaliyotokea katika kiwanda cha Aba Za'abal yaliyowaacha wahanga 33 majeruhi na waliouawa.

Amerika ndio yenye majukumu, kwa vile ndiyo iliyoisheheni Israil kwa silaha na mali na ikaamrisha iwafanyie waarabu; kama hiyo yenyewe inavyoifanyia Vietnam. Vyombo vya habari vimenukuu kuwa jeshi la Amerika limesambaratisha mji mzima katika Vietnam. Hakuokoka katika mji huo mtoto wala mwanamke. Mji huu na mashule yake unahusiana vipi na vita?!

Je, usalama utakuweko na wanyama hawa? Jamani! Pengine labda maana ya usalama yawe ni kusalimu amri kwa madhalimu na waasi!

Hakika uhai wa duniani ni mchezo na upuzi kwa mwenye kuipondokea na akahadaika na ubatilifu wake; bali ni shari hasa kwa mwenye kuanzisha vita kwa ajili ya dunia. Na ni nyumba ya heri kwa mwenye kuwaidhika nayo na akaifanya ni maandalizi ya Akhera yake.

Na mkiamini na mkawa na takua atawapa ujira wenu.

Kuunganisha takua na imani kunafahamisha kuwa kuamini tu na kusadikisha hakuna malipo mbele ya Mwenyezi Mungu; bali hapana budi kuweko na vitendo pamoja na imani. Ufafanuzi zaidi wa Aya hii ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ إِنَّا لَا نُضِيعُ أَجْرَ مَنْ أَحْسَنَ عَمَلًا ﴿٣٠﴾

1. Jina hili lilikuwa likitumiwa na nchi mbili za kiarabu Misr na Syria zilizoungana mwaka 1958 ikiwa ni mwanzo wa umoja wa wa nchi za Kiarabu; kama ilivyokuwa ndoto ya Jamal Abdulnasser na kuvunjika mwaka 1961 kutokana na mapinduzi ya kijeshi yaliyotokea Damscus. Hata hivyo Misr iliendelea kutumia jina hili hadi 1970, ilipobadilisha na kujiita Jamhuri ya Kiarabu ya Misr. Mauji ya watoto yalitokea upande wa Misr mkoa wa mashariki katika mji wa Husseynia. –Vyanzo vya habari za tovuti.

“Hakika wale ambao wameamini na wakatenda mema, hakika sisi hatupotezi ujira wa anayefanya mazuri.”Juz. 15 (18:30)

Wala hawaombi mali zenu. Na akiwaomba hizo na akiwashikilia mtafanya ubakhili, na atatoa chuki zenu.

Makusudio ya hawaombi ni hawataki mtoe mali yote wala kutoa mali nyingi ya kuwadhuru. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) amejaalia fungu la mafukara katika mali ya matajiri na akachunga kiwango cha kutosheleza mahitaji na vile vile masilahi ya watowaji wasidhurike.

Lau kuwa Mwenyezi Mungu, ambaye imetukuka hekima yake, angeliwataka matajiri zaidi kiwango hiki na akawahimiza kutoa, basi wangelizuia na wangekua na chuki na Uislamu na Nabii.

Ehee! Nyinyi mnaitwa mtumie katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Kundi la wafasiri wamesema kuwa Makusudio ya njia ya Mwenyezi Mungu ni jihadi. Usahihi ni kuwa inakusanya kila lililo na radhi ya Mwenyezi Mungu na masilahi ya watu kwa namna moja au nyingine.

Na wapo katika nyinyi wanaofanya ubakhili. Na anayefanya ubakhili basi anajifanyia ubakhili mwenyewe.

Bakhili anamnyima Mwenyezi Mungu na kujilimbikizia mwenyewe, lakini natija inakuwa kinyume na anavyotaka; pale anapoiweka nafsi yake kwenye ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na kuinyima radhi zake na thawabu zake. Tazama kifungu; ‘Mali ndio sababu ya ugomvi’ mwanzo wa Juz. 4 (3:92).

Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, na nyinyi ndio wahitaji wa fadhila zake na rehma zake. Hakupata ukwasi mja yeyote ila kwa sababu inayotoka kwake. Ama Yeye Mwenyezi Mungu ni mkwasi kwa dhati yake sio kwa kufaidika, ni mtendaji sio kwa kutumia ala, na ni mkadiriaji sio kwa kufikiria.

Na mkigeuka atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi.

Kama mkiupinga mwito wa Mwenyezi Mungu na mkang’ang’ania uasi na ujeuri basi atawaondoa na awalete wengine watakaomsabihi na kumsifu bila ya kumuasi na lolote. Umetangulia mfano wake katika Juz. 13 (14:19) na Juz. 22 (35:16).

## MWISHO WA SURA YA ARUBAINI NA SABA: SURAT MUHAMMAD

7

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

Sura Ya Arubaini Na Nane: Surat Al-Fath. Imeshuka Makka. Ina Aya 29.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا ﴿١﴾

1. Hakika tumekupa ushindi wa dhahiri

لِّيَغْفِرَ لَكَ اللَّـهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ وَيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ وَيَهْدِيَكَ صِرَاطًا مُّسْتَقِيمًا ﴿٢﴾

2. Ili Mwenyezi Mungu akughufirie dhambi yako iliyotangulia na ijayo, na akutimizie neema zake, na akuongoze katika njia iliyonyooka.

وَيَنصُرَكَ اللَّـهُ نَصْرًا عَزِيزًا ﴿٣﴾

3. Na Mwenyezi Mungu akunusuru nusura yenye nguvu.

هُوَ الَّذِي أَنزَلَ السَّكِينَةَ فِي قُلُوبِ الْمُؤْمِنِينَ لِيَزْدَادُوا إِيمَانًا مَّعَ إِيمَانِهِمْ وَلِلَّـهِ جُنُودُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَكَانَ اللَّـهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٤﴾

4. Yeye ndiye aliyeteremsha utulivu katika nyoyo za waumini ili wazidi imani juu ya imani yao. Na Mwenyezi Mungu ana majeshi ya mbingu na ardhi; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye ujuzi, Mwenye hikima.

لِّيُدْخِلَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَيُكَفِّرَ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَكَانَ ذَٰلِكَ عِندَ اللَّـهِ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٥﴾

5. Ili awaingize waumini wanaume na waumini wanawake katika Bustani zipitiwazo na mito chini yake, wadumu humo, na awafutie maovu yao. Na huko ndiko kufuzu kukubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

## TUMEKUPA USHINDI

**Aya 1 – 5**

### MAANA

Hakika tumekupa Ushindi wa dhahiri.

Neno 'ushindi' tumelifasiri kutokana na neno la kiarabu 'Fat-h' ambalo lina maana nyingine zaidi ya hiyo. Lakini Makusudio yake hapa ni ushindi, kwa sababu ndiyo yanayokuja akilini mwanzo, na pia kwamba Nabii **(s.a.w.w)** alisema: **"Nimeteremshiwa Aya inayopendeza zaidi kwangu kuliko dunia na yaliyomo**. Kisha akasoma: "Hakika tumekupa Ushindi wa dhahiri". Maana ni kuwa tumekupa ushindi ewe Muhammad ushindi wa dhahiri.

Wametofautiana wafasiri kuhusu aina ya ushindi wenyewe. Tabariy ameishilia na kauli nne na Razi akaishilia na tano. Wafasiri wengi wamesema kuwa Makusudio ya ushindi hapa ni ushindi wa Suluhu ya Hudaybiya. Kwa sababu sura hii ilishuka baada ya mkataba wa amani aliowekeana Mtume na watu wa Makka, sehemu ya Hudaybiya.

Hata hivyo kauli iliyo na nguvu kwetu ni kuwa Makusudio ya ushindi hapa ni kuwa juu Uislamu, kuwa na nguvu waislamu na kudhalilika maadui wake wanafiki na washirikina. Kwa sababu ushindi katika Aya ni wa kiujmla haukufungwa na Hudaybiya, kuiteka Makka, kuwashinda waroma na wafursi au kwengineko.

Kwa hiyo basi Aya hii itakuwa inarudufu ile isemayo:

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾

"Yeye ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na dini ya haki, ili ipate kushinda dini zote, ijapokuwa washirikina wamechukia." Juz. 10 (9:33).

Kwa maneno mengine ni kuwa ushindi ni wa kiujmla sio wa kiaina.

Ili Mwenyezi Mungu akughufirie dhambi yako iliyotangulia na ijayo.

**Unaweza kuuliza**: lini Nabii alifanya dhambi mpaka asamehewe na Mwenyezi Mungu? Iko wapi isma ya manabii ya kuepukana na dhambi? Itakuwaje ushindi ndio iwe sababu ya maghufira? Kuna uhusiano gani baina ya ushindi na maghufira?

**Jibu**: Makusudio ya dhambi hapa sio dhambi ya Mtume kiuhakika na kiuhalisi. Itakuwaje na hali yeye ni mwenye kuhifadhiwa na madhambi na makosa. Makusudio ni kuwa washirikina wlikuwa wakiamini kuwa Mtume ana dhambi kutokana na mwito wake wa Tawhid, mwito wa kutupiliwa mbali ushirikina na kupiga vita kuiga waliopita.

Ama Makusudio ya maghufira ni kuwa washirikina hawa walikuja kugundua kuwa Muhammad **(s.a.w.w)** hana dhambi na kwamba yeye ni Mtume wa kweli na wa haki na wao ndio waliokuwa na dhambi kwa kumtuhumu na risala yake.

Yaani Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alitoa mwito wa Tawhid akikosoa ibada ya masanamu na kupiga vita dhulma na unyanyasaji na mengine ya ufisadi wa kijahilia na maigizo yake. Ni dhambi gani iliyokubwa zaidi kwa jahili na wengineo kuliko kumkosoa na kumtia ila na vitu vyake vitakatifu vya kidini na ada ya mababu zake ambayo ndio desturi yake?

Lakini baada Mwenyezi Mungu kuidhihirisha dini yake na kumnusuru Nabii wake kwa dalili na hoja na kuingia watu kwenye dini ya Mwenyezi Mungu makundi makundi, wakiwemo washirikina waliokuwa wakimuona Mtume ni mwenye hatia kwao na kwa miungu yao, iliwabainikia kuwa Muhammad **(s.a.w.w)** ni mkweli na wao ni wakosefu.

Kwa ufupi ni kuwa makusudio ya dhambi ya Mtume ni dhambi yake kwa madai ya maadui zake washirikina, sio dhambi halisi. Na makusudio ya msamaha ni msamaha wao kwa lile walilodai kuwa ni dhambi; yaani toba yao kwa walivyomdhania Mtume.

Ama kuinasibisha dhambi kwa Mtume, katika dhahiri ya maneno, na kunasibisha msamaha kwa Mwenyezi Mungu, hilo ni jambo sahali, kwamba majazi yanatoa upeo wa hilo na zaidi.

Kuhusu uhusiano wa ushindi na maghufira, uko wazi – kwamba ushindi ndio sababu ya kufichuka ukweli wa Mtume na kuepuka kwake dhambi – iliyodaiwa - waliyomtuhumu nayo washirikina kabla ya ushindi.

Na akutimizie neema zake kwa kukupa ushindi dhidi ya madui zako na kuinua shani yako duniani.

Na akuongoze katika njia iliyonyooka ambayo ni sharia ya Mwenyezi Mungu inayodhamini heri ya watu na masilahi yao, kila wakati na kila mahali.

Na Mwenyezi Mungu akunusuru nusura yenye nguvu.

Nusura yenye nguvu ni ile inayokuwa kwa haki na kwa ajili ya haki na kwa jihadi iliyowekewa sharia sio kwa njama au mapinduzi wala kwa msaada wa waovu.

Yeye ndiye aliyeteremsha utulivu katika nyoyo za waumini ili wazidi imani juu ya imani yao.

Makusudio ya utulivu ni kuridhia na kutulia kimwamko. Kwa sababu matukio yametuonyesha kuwa utulivu wa kijahili unaishia pabaya. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu ameipa nguvu dini yake akampa ushindi Nabii wake ili wafurahi waumini, nyoyo zao zitulie, wazidi kuwa na yakini na Mola wao, wamtegemee Nabii wao na kuwa na nguvu katika dini yao.

Na Mwenyezi Mungu ana majeshi ya mbingu na ardhi.

Hii ni kinaya cha ukuu wa uweza; vinginevyo Mwenyezi Mungu hahitajii walimwengu, kwa sababu Yeye ni kukiambia kitu kuwa kinakuwa.

Hapa kuna ishara kwamba lau Mwenyezi Mungu angelitaka angeliwaangamiza washirikina bila jihadi na vita, lakini ni kwa ajili ya kuwajaribu waja ili ajulikane nani mzuri zaidi wa matendo.

Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye ujuzi, Mwenye hikima katika kuumba kwake na kupangilia kwake.

Ili awaingize waumini wanaume na waumini wanawake katika Bustani zipitiwazo na mito chini yake, wadumu humo, na awafutie maovu yao. Na huko ndiko kufuzu kukubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

Tabari anasema: iliposhuka "Hakika tumekupa Ushindi wa dhahiri," waumini walimwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**: Pongezi ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amekwishakubainishia atakavyokufanyia, je na sisi? Ndio ikashuka kauli yake Mwenyezi Mungu: "Ili awaingize waumini wananume na waumini wanawake…" mpaka mwisho.

Hata kama riwaya itakuwa si sahihi, lakini hakuna mwenye shaka kwamba Mwenyezi Mungu anasamehe maovu ya wanaoutubia na kuwangiza waumini katika rehema yake na pepo yake. Na atakayeingia Peponi atakuwa amefuzu fungu lenye kutosheleza.

وَيُعَذِّبَ الْمُنَافِقِينَ وَالْمُنَافِقَاتِ وَالْمُشْرِكِينَ وَالْمُشْرِكَاتِ الظَّانِّينَ بِاللَّـهِ ظَنَّ السَّوْءِ عَلَيْهِمْ دَائِرَةُ السَّوْءِ وَغَضِبَ اللَّـهُ عَلَيْهِمْ وَلَعَنَهُمْ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَهَنَّمَ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿٦﴾

6. Na awaadhibu wanafiki wanaume na wanafiki wanawake, na washirikina wanaume na washirikina wanawake, wanaomdhania Mwenyezi Mungu dhana mbaya. Utawafikia mgeuko mbaya, na Mwenyezi Mungu awakasirikie, na awalaani, na awaandalie Jahannamu. Na hayo ni marudio maovu kabisa.

وَلِلَّـهِ جُنُودُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَكَانَ اللَّـهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿٧﴾

7. Na Mwenyezi Mungu ana majeshi ya mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye ujuzi, Mwenye hikima.

إِنَّا أَرْسَلْنَاكَ شَاهِدًا وَمُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ﴿٨﴾

8. Hakika tumekutuma uwe shahidi na mbashiri na muonyaji.

لِّتُؤْمِنُوا بِاللَّـهِ وَرَسُولِهِ وَتُعَزِّرُوهُ وَتُوَقِّرُوهُ وَتُسَبِّحُوهُ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٩﴾

9. Ili mumwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mumsaidie, na mumhishimu, na mumsabihi asubuhi na jioni.

## NA AWAADHIBU WANAFIKI

**Aya 6 – 9**

### MAANA

Na awaadhibu wanafiki wanaume na wanafiki wanawake, na washirikina wanaume na washirikina wanawake, wanaomdhania Mwenyezi Mungu dhana mbaya. Utawafikia mgeuko mbaya, na Mwenyezi Mungu awakasirikie, na awalaani, na awaandalie Jahannamu. Na hayo ni marudio maovu kabisa.

Ubaya ni shari na ufisadi. Makusudio ya dhana mbaya kwa Mwenyezi Mungu ni kudhani kuwa, ambaye imetukuka hekima yake, hatafufua walio katika makaburi na kwamba hataunusuru uislamu na Nabii wa uislamu na mengineyo wanayoyadhania wanafiki na washirikina.

Maana kwa ujumla ni kuwa Mwenyezi Mungu, kama alivyowaandalia watu wa imani Peo yenye neema, vile vile amewaandalia wale waliomdhania vibaya, kama waanafiki na washirikana, shari itakayowazunguka kila upande, hasira, laana na mwisho mbaya – moto wa Jahannam usiokwisha wakafa wala hautapunguzwa.

Na Mwenyezi Mungu ana majeshi ya mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye ujuzi, Mwenye hikima.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliitaja Aya hii alipowaashiria watu wa imani na malipo yao katika Aya iliyotangulia. Hapa tena ameitaja akiwaashiria wanafiki na washirikina. Lengo la kukaririka huku ni kutanabahisha kwamba Yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu ni muweza wa kuwaneemesha na kuwaadhibu, ili mja amtii Mwenyezi Mungu kwa kutarajia thawabu zake na ajiepushe na kumuasi kuhofia adhabu yake.

Hakika tumekutuma uwe shahidi na mbashiri na muonyaji.

Kesho Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** atashuhudia mbele ya Mwenyezi Mungu kwamba yeye amewafikishia waja yale aliyopewa wahyi, akawabashiria watiifu kuokoka na akawaonya waasi na maangamizi.

Imetangulia kwa herufi zake katika Juz. 22 (33:45).

Ili mumwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mumsaidie, na mumhishimu, na mumsabihi asubuhi na jioni.

Mumsaidie na mumhishimu ni Mtume. Imesemekana kuwa ni Muisaidie na muihishimu dini, lakini maana yote ni sawa. Mumsabihi Mwenyezi Mungu. Makusudio ya tasbihi ya asubuhi na jioni ni swala tano.

Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu alimtuma Muhammad kwa viumbe ili wamwamini Mwenyezi Mungu na risala ya Muhammad **(s.a.w.w)** wamsaidie kwa kupigana jihadi katika njia yake Mwenyezi Mungu na wamuhishimu kwa kuhishimu hukumu za Mwenyezi Mungu kwa kuzitii na kuzitumia na pia wadumu kwenye Swala tano.

إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّـهَ يَدُ اللَّـهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ ۚ فَمَن نَّكَثَ فَإِنَّمَا يَنكُثُ عَلَىٰ
نَفْسِهِ ۖ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِمَا عَاهَدَ عَلَيْهُ اللَّـهَ فَسَيُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٠﴾

10. Hakika wanaokubai, kwa hakika wanambai Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi hakika anaivunja kwa kuidhuru nafsi yake; na anayetekeleza aliyomuahadi Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atampa ujira mkubwa.

سَيَقُولُ لَكَ الْمُخَلَّفُونَ مِنَ الْأَعْرَابِ شَغَلَتْنَا أَمْوَالُنَا وَأَهْلُونَا فَاسْتَغْفِرْ لَنَا ۚ يَقُولُونَ بِأَلْسِنَتِهِم مَّا
لَيْسَ فِي قُلُوبِهِمْ ۚ قُلْ فَمَن يَمْلِكُ لَكُم مِّنَ اللَّـهِ شَيْئًا إِنْ أَرَادَ بِكُمْ ضَرًّا أَوْ أَرَادَ بِكُمْ نَفْعًا ۚ بَلْ
كَانَ اللَّـهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿١١﴾

11. Watakuambia mabedui waliobaki nyuma: imetushughulisha mali yetu na ahali zetu, basi tuombee msamaha. Wanasema kwa ndimi zao yasiyokuwamo nyoyoni mwao. Sema: Ni nani awezaye kuwasaidia na chochote kwa Mwenyezi Mungu akitaka kuwadhuru au akitaka kuwanufaisha? Bali Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda.

بَلْ ظَنَنتُمْ أَن لَّن يَنقَلِبَ الرَّسُولُ وَالْمُؤْمِنُونَ إِلَىٰ أَهْلِيهِمْ أَبَدًا وَزُيِّنَ ذَٰلِكَ فِي قُلُوبِكُمْ وَظَنَنتُمْ
ظَنَّ السَّوْءِ وَكُنتُمْ قَوْمًا بُورًا ﴿١٢﴾

12. Lakini mlidhani kwamba Mtume na waumini hawatarudi kabisa kwa ahali zao, na mkapambiwa hayo katika nyoyo zenu, na mkadhania dhana mbaya, na mmekuwa watu wanaoangamia.

وَمَن لَّمْ يُؤْمِن بِاللَّـهِ وَرَسُولِهِ فَإِنَّا أَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ سَعِيرًا ﴿١٣﴾

13. Na asiyemwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi kwa hakika tumewaandalia makafiri Moto mkali.

وَلِلَّـهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ يَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ ۚ وَكَانَ اللَّـهُ غَفُورًا رَّحِيمًا
﴿١٤﴾

14. Na ni wa Mwenyezi Mungu ufalme wa mbingu na ardhi. Humsamehe amtakaye, na humwadhibu amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghufira, Mwenye kurehemu.

## BAIA YA RIDHWAN CHINI YA MTI

**Aya 10 – 14**

### KISA KWA UFUPI

Hakika wanaokubai, kwa hakika wanambai Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi hakika anaivunja kwa kuidhuru nafsi yake; na anayetekeleza aliyomuahadi Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atampa ujira mkubwa.

Aya hii inaashiria Baiatur-ridhwan Baia iliyoridhiwa iliyokuwa chini ya mti. Kisa chake ni kama ifuatavyo:

Hadi kufikia mwaka wa sita wa Hijra, washirikina ndio waliokuwa wakitawala Makka na Nyumba takatifu. Mwishoni mwa mwaka huo Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alitoka Madina Munawwara pamoja na waislamu 1400 kuelekea Makka Mukkarrama kufanya Umra wakiwa hawana fikra yoyote ya vita.

Walipofika sehemu inayoitwa Hudaybiyya, Abu Sufyani alipata taarifa ya kufika kwao. Kwa hiyo akawakusanya makuraishi na wakapitisha azimio la kuwazuia waislamu wasiingie Nyumba takatifu (Al-Ka'aba) kwa nguvu ya silaha. Wakawakusanya wapanda farasi wakiongozwa na Khalid Bin Al-Walid.

Wakapishana wajumbe baina ya Mtume **(s.a.w.w)** na wao. Ujumbe wa makuraishi ulimtaka Mtume arudi Madina wala asiingie Makka, Mtume naye akawajibu kuwa sisi hatukuja kupigana na yoyote, tumekuja kuzuru Nyumba takatifu tu na atakayetuzuia tutapigana naye.

Urwa Bin Mas'ud alikuwa ni mmoja wa wajumbe wa makuraishi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, akaona maswahaba wakionyesha aina kwa aina ya mapenzi kwa Mtume, hakutawadha ila waligombania mabaki ya udhu wake na hakutema mate ila waliyachukua mate yake; hata unywele wake ukianguka tu walikuwa wakiugombania.

Basi akarudi akiwa ameshangaa sana kwa aliyoyaona akasema: "Enyi makuraishi jamani! Mimi nilimuona Kisra kwenye Ufalme, Kaizari na Najashi, lakini sikuona kwao ufalme kwa watu wao unaonafana na Muhammad kwa sahaba zake. Mimewaona hawawezi kumwacha kwa jambo lolote. Hebu fikirieni vizuri!"

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alimtuma Uthman kwa Makuraishi kwa vile yuko karibu na Abu sufyan na akamwambia: ''Waambie sisi hatukuja kwa vita; tumekuja kuzuru hii nyumba tukitukuza heshima na miko yake. Tuna wanyama tutawachinja kisha twende zetu.''

Uthman alipowapelekea habari hii wakasema: ''Haiwezekani kabisa.'' Ikawa hakuna habari za Uthman, ukatokea uvumi kuwa ameuawa. Mtume aliposikia uvumi huu akasema: Hatuondoki mpaka tupigane na watu hawa.

Akatoa mwito wa kuungwa mkono akiwa amekaa chini ya mti. Basi saha- ba zake wakambai (kiapo cha utii) haraka sana kwamba watamtii na wako tayari kufa katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliisifu baia hii kuwa ni bai yake hasa, na kwamba ameichukua kwa mkono wake, atakayevunja ahadi hii atakuwa amemfanyia hiyana Mwenyezi Mungu na kujiletea hasira zake na atayeiteleza kikamilifu atakuwa karibu na Mola na mwisho mzuri.

Jina maarufu la baia hii ni Baia iliyoridhiwa (Baiatur-ridhwan) au Baia ya mti (Bai'atu-shajara). Pia inaitwa Baia iliyoridhiwa chini ya mti kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu katika Aya ya 18 ya sura hii tuliyo nayo: "Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewaridhia waumini walipokubai chini ya mti."

Makuraishi walipoona ukakamavu wa Mtume walikuja chini kufanya suluhu. Wakakakubaliana kwamba waislamu wasiingie Makka mwaka ule mpaka mwaka unaofuatia wakaingia kufanya Umra na kukaa siku tatu bila ya kuwa na silaha isipokuwa panga kwenye ala zake.

Mtume **(s.a.w.w)** akamwita Ali bin Abi Twalib na akamwambia: ''Andika Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.'' Mjumbe wa makuraishi akapinga ana akesema: Andika kwa jina lako ewe Mola wangu. Akakubali Mtume na Ali akaandika. Nabii akaendelea kusema: Andika, haya ndiyo waliyokubaliana Muhammad

Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mjumbe wa makuraishi akapinga tena, na kusema: Andika jina lako na la baba yako. Ali akasita.

Mtume akamwambia na wewe yatakupata mfano wake; akiwa anamwashiria suala la mahakimu wawli katika vita vya Siffin. Na hiyo ni miongoni mwa ilimu ya ghaibu aliyompa wahyi Mwenyezi Mungu Mtume wake mtukufu, ambayo ni miongoni mwa nguvu ya hoja ya utume wake na ukweli katika utume wake.

Walipomaliza kutiliana sahii mkataba wa Hudaybiyya, Mtume na maswahaba walitoa Ihramu zao, wakachinja na wakanyoa vichwa vyao. wakabaki siku kadhaa pale Hudaybiyya kisha wakarudi zao Madina.

Mwaka uliofuatia Nabii na Maswahaba walieleka Makka kufanya Umra. Wakaingia huku wakipiga Takbira hii kwa sauti: la ilaha illa Allah, nasara abdah, waazza jundah, wakhadhalal-ahazaba wahdah (hapana Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu, hali ya kuwa pekee yake, amemnusuru mja wake, amelipa nguvu jeshi lake, na amevidhalilisha vikosi hali ya kuwa peke yake).

Wakababakia Makka siku tatu wakitufu na kuchinja. Umra huu unaitwa Umra wa kulipa, kwa sababu unachukua nafasi ya umra ule waliozuiliwa na washirikina. Ilishuka Aya kwa umra huo kama ilivyoelezwa katika Aya ya 28 ya sura hii tuliyo nayo: "Hakika Mwenyezi Mungu amemhakikishia Mtume wake ruiya ya haki. Bila ya shaka mtauingia Msikiti Mtakatifu, Inshallah, kwa amani, na hali mmenyoa vichwa vyenu na mmepunguza. Hamtakuwa na hofu."

## MABEDUI WALIOBAKI NYUMA

Watakuambia mabedui waliobaki nyuma: Imetushughulisha mali yetu na ahali zetu, basi tuombee msamaha.

Mtume **(s.a.w.w)** alipotaka kutoka kwenda Makka mwaka ule wa Hudaybiyya. Waislamu walimhimiza wasafiri naye, lakini baadhi ya mabedui wanaoishi kando kando ya Madina na wanafiki wengine walikataa kutoka pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, wakidhania kuwa Makuraishi hawatamruhusu Muhammad **(s.a.w.w)** kuingia Makka. Wakaambiana: Hatuna haja ya kujiingiza kwenye hatari hii.

Bada ya kutimia mkataba, Mwenyezi Mungu alimwambia Mtume wake: utakaporudi Madina wale waliobaki nyuma watatoa visababu, kuwa kuangalia familia zao na mali zao ndiko kulikowazuia kufuatana nawe na watakuomba msamaha wa uongo na wakinafiki. Pia watakutaka uwaombee msamaha kwa Mwenyezi Mungu awaridhie na kuwasamehe yaliyopita.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) akawakadhibisha kwa kusema: Wanasema kwa ndimi zao yasiyokuwamo nyoyoni mwao; kama ilivyo kawaida ya wanafiki.

Sema: Ni nani awezaye kuwasaidia na chochote kwa Mwenyezi Mungu akitaka kuwadhuru au akitaka kuwanufaisha?

Mnamwambia uwongo Mwenyezi Mungu na hali Yeye anajua siri zenu na dhahiri zenu? Tena heri yenu na shari yenu iko mikononi mwake. Ni nani atakayemzuia akiwatakia heri au shari?

Bali Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda na tena anamjulisha Mtume wake kuwa nyinyi mnadhihirisha yasiyokuwa nyoyoni mwenu.

Lakini mlidhani kwamba Mtume na waumini hawatarudi kabisa kwa ahali zao, na mkapambiwa hayo katika nyoyo zenu.

Mlimwacha Mtume mkidhani kuwa Mwenyezi Mungu hatamnusuru Nabii wake na wale waliokuwa pamoja naye na kwamba ushindi utakuwa wa maadui wa Mwenyezi Mungu dhidi ya vipenzi vyake.

Na mkadhania dhana mbaya kuwa waislamu wanakwenda kwenye mauti tu. Wala hakuna tegemeo la dhana isipokuwa wasiwasi wa shetani tu, kwamba Mwenyezi Mungu hataitia nguvu dini yake na kumnusuru Mtume wake. Na mmekuwa watu wanaoangamia. Kila mwenye kukubali uongozi wa shetani basi ataongozwa kwenye maangamizi.

Na asiyemwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi kwa hakika tumewaandalia makafiri Moto mkali. watadumu humo wala hawatapata wa kuwasaidia.

Na ni wa Mwenyezi Mungu ufalme wa mbingu na ardhi.

Hakuna mfalme mwingine asiyekuwa Yeye wala hakuna hila wala nguvu isipokuwa kwake. Mwenye kumfanyia ikhlasi na akamtegemea Yeye basi atamtoshea. Na mwenye kuelekea kwa mwinginewe basi atamwachia huyo.

Humsamehe amtakaye yule anayestahiki maghufira, kwa sababu ni hakimu, ni muhali kwake kumsamehe anayemwga damu kidhulma, akavunja mashule ya watoto wadogo na akapora vyakula vya wenye njaa. Na humwadhibu amtakaye anayestahiki adhabu; wala Mola wako si mwenye kuwadhulumu waja.

Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghufira, Mwenye kurehemu yule anayejihurumia yeye na mwingine; vinginevyo asiye na huruma naye hahurummiwi. Na madhalimu hawana wa kuwanusuru.

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

سَيَقُولُ الْمُخَلَّفُونَ إِذَا انطَلَقْتُمْ إِلَىٰ مَغَانِمَ لِتَأْخُذُوهَا ذَرُونَا نَتَّبِعْكُمْ ۖ يُرِيدُونَ أَن يُبَدِّلُوا كَلَامَ اللَّـهِ ۚ قُل لَّن تَتَّبِعُونَا كَذَٰلِكُمْ قَالَ اللَّـهُ مِن قَبْلُ ۖ فَسَيَقُولُونَ بَلْ تَحْسُدُونَنَا ۚ بَلْ كَانُوا لَا يَفْقَهُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٥﴾

15. Waliobaki nyuma watasema: Mtapokwenda kuchukua ngawira, tuacheni tuwafuate! Wanataka kuyabadili maneno ya Mwenyezi Mungu. Sema: Hamtatufuata kabisa! Mwenyezi Mungu alikwishasema hivi zamani. Hapo watasema: Bali nyinyi mnatuhusudu. Bali walikuwa hawafahamu ila kidogo.

قُل لِّلْمُخَلَّفِينَ مِنَ الْأَعْرَابِ سَتُدْعَوْنَ إِلَىٰ قَوْمٍ أُولِي بَأْسٍ شَدِيدٍ تُقَاتِلُونَهُمْ أَوْ يُسْلِمُونَ ۖ فَإِن تُطِيعُوا يُؤْتِكُمُ اللَّـهُ أَجْرًا حَسَنًا ۖ وَإِن تَتَوَلَّوْا كَمَا تَوَلَّيْتُم مِّن قَبْلُ يُعَذِّبْكُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٦﴾

16. Waambie walioachwa nyuma katika mabedui: Mtakujaitwa kwenda pigana na watu wakali kwa vita; mpigane nao au wasalimu amri. Basi mkimtii, Mwenyezi Mungu atawapa ujira mzuri; na mkigeuka kama mlivyogeuka kwanza, atawaadhibu kwa adhabu chungu.

لَّيْسَ عَلَى الْأَعْمَىٰ حَرَجٌ وَلَا عَلَى الْأَعْرَجِ حَرَجٌ وَلَا عَلَى الْمَرِيضِ حَرَجٌ ۗ وَمَن يُطِعِ اللَّـهَ وَرَسُولَهُ يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ۖ وَمَن يَتَوَلَّ يُعَذِّبْهُ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٧﴾

17. Kipofu hana tabu, wala kiguru hana tabu, wala mgonjwa hana tabu. Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, atamuingiza katika Mabustani yapitiwayo na mito chini yake. Na atakayegeuka atamuadhibu kwa adhabu chungu.

## TUACHENI TUWAFUATE

**Aya 15 – 17**

### MAANA

Waliobaki nyuma watasema: Mtapokwenda kuchukua ngawira, tuacheni tuwafuate!

Ni wale wale waliokataa kutoka na Mtume alipoelekea Makka mwishoni mwa mwaka wa sita, ambao amewakusudia Mwenyezi Mungu katika Aya iliyotangulia. Mtume aliwahimiza wafuatane naye, lakini wakawahofia makuraishi kwa visingizio vya familia na mali.

Baada ya Mtume kurudi Hudaybiyya alikaa Madina hadi mwanzo mwanzo wa mwaka wa saba, akaenda kupigana Khaybara. Huko waislamu walipata ngawira nyingi sana, zilzioamsha tamaa ya waliobaki nyuma. Wakamwambia Mtume na wale aliokuwa nao: tuchukueni na sisi kwenye ngawira hizo. Leo wanataka kutoka na jana walipoitwa walijitia kushughulika na watu wao na mali wakihofia jihadi. Haya ndiyo mantiki ya kila aliyetekwa na tamaa na asione jingine ila hiyo tu.

Wanataka kuyabadili maneno ya Mwenyezi Mungu.

Wanaotaka ni hao hao waliobaki nyuma. Makusudio ya maneno ya Mwenyezi Mungu hapa ni ahadi yake Mwenyezi Mungu Mtukufu

kuwanyima ngawira waliobaki nyuma, ambayo ameiashiria kwa kusema: “Mtapo kwenda kuchukua ngawira.”

Lakini Mwenyezi Mungu, ambaye imetukuka hikima yake, hakutubainishia ngawira yenyewe.

Je, ni ngawira za Khaybara au yinginezo. Hata hivyo wafasiri wamesema kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliwaahidi watu wa Baia iliyoridhiwa kuwa ngawira ya Khaybara itawahusu wao tu. Razi anasema: Hii ndio kauli mashuhuri kwa wafasiri. Maraghi naye akasema: “ni habari sahaihi.” Hili haliko mbali, kwa sababu vita vya Khaybar ndivyo vya kwanza baada ya mkataba wa Hudaybiyya.

Vyovyote iwavyo ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimwamrisha Nabii wake awaambie waliobaki nyuma: Sema: Hamtatufuata kabisa kuchukua ngawira kwa sababu nyinyi mlikataa kufuatana nasi Makka mkihofia vita. Mwenyezi Mungu alikwishasema hivi zamani kuwa hamna fungu la ngawira.

Hapo watasema: Bali nyinyi mnatuhusudu.

Hapana, sivyo kabisa! Mwenyezi Mungu hakutunyima ngawira bali nyinyi ndio mnaotunyima kwa chuki na husuda kwetu.

Bali walikuwa hawafahamu ila kidogo.

Hili ni jawabu la Mwenyezi Mungu Mtukufu kutokana na kauli yao ‘bali mnatuhusudu.’ Sio kama mlivyodai, ni kutojua kwenu na uasi wenu kwenye hukumu nyingi.

Waambie walioachwa nyuma katika mabedui ambao walikataa kutoka na Mtume kwenda Makka: Mtakujaitwa kwenda pigana na watu wakali kwa vita.

Aliyewaita ni Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**. Baada ya vita vya Khaybar, Mtume aliwaita kwenye vita vya Hunayn, Taif na Tabuk.

Mpigane nao au wasalimu amri.

Yaani wakali ambao mtaitwa mkapigane nao watahiyarishwa mambo mawili na Mtume: Upanga au Uislamu. Basi je, mtaitikia mwito wa Mtume au mtarudi kwenye visigino vyenu kama mlivyofanya hapo mwanzo? Kwa maneno mengine ni kuwa kupambana kwenu na wakali wa vita ndio uthibitisho wa ukweli wenu sio kuchukua ngawira.

Basi mkimtii, Mwenyezi Mungu atawapa ujira mzuri; ngawira duniani na Pepo Akhera. Au Pepo na daraja ya juu mbele ya Mwenyezi Mungu kwa yule atakayeuawa.

Na mkigeuka kama mlivyogeuka kwanza, atawaadhibu kwa adhabu iliyo chungu.

Kuna adhabu gani chungu zaidi kuliko adhabu ya Jahannam?

Kipofu hana tabu, wala kiguru hana tabu, wala mgonjwa hana tabu.

Makusudio ya tabu hapa ni dhambi. Maana ni kuwa hakuna dhambi kwa watu wa aina zote hizi tatu kama wakibaki nyuma ikiwa ni vita vya kutoa mwito wa uislamu.

Ama jihadi ya kujikinga na adui na kumzuia na uchokozi wake, hivyo ni lazima kwa wote wanaume kwa wanawake, watu wazima kwa watoto, na wazima na walemavu. Kila mtu ni kwa kadiri ya nguvu zake.

Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, atamuingiza katika Mabustani yapitiwayo na mito chini yake. Na atakayegeuka atamuadhibu kwa adhabu chungu.

Maana yako wazi – ni Pepo kwa mtiifu na Moto kwa muasi.

Maana haya yamekaririka kwenye makumi ya Aya, kwa mnasaba wa kutaja heri na shari, kutanabahisha kwamba Mwenyezi Mungu ni mwadilifu, kwamba mtu hataachwa bure na kwamba yeye atakutana na Mwenyezi Mungu kwa matendo yake. Ni matendo tu ndio yatakua maudhui ya hisabu na kipimo cha malipo.

لَّقَدْ رَضِيَ اللَّـهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنزَلَ السَّكِينَةَ
عَلَيْهِمْ وَأَثَابَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿١٨﴾

18. Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewaridhia waumini walipokubai chini ya mti, na alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawalipa kwa ushindi wa karibu.

وَمَغَانِمَ كَثِيرَةً يَأْخُذُونَهَا وَكَانَ اللَّـهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٩﴾

19. Na ngawira nyingi watakazozichukua. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

وَعَدَكُمُ اللَّـهُ مَغَانِمَ كَثِيرَةً تَأْخُذُونَهَا فَعَجَّلَ لَكُمْ هَـٰذِهِ وَكَفَّ أَيْدِيَ النَّاسِ عَنكُمْ
وَلِتَكُونَ آيَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ وَيَهْدِيَكُمْ صِرَاطًا مُّسْتَقِيمًا ﴿٢٠﴾

20. Mwenyezi Mungu amewaahidi ngawira nyingi mtakazozichukua, basi amewatangulizia hii, na akaizuia mikono ya watu isiwafikie. Na ili hiyo iwe ni Ishara kwa waumini, na akawaongoza njia iliyonyooka.

وَأُخْرَىٰ لَمْ تَقْدِرُوا عَلَيْهَا قَدْ أَحَاطَ اللَّـهُ بِهَا وَكَانَ اللَّـهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرًا ﴿٢١﴾

21. Na nyingine hamjaweza kuzipata, Mwenyezi Mungu amekwishazizingira. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.

وَلَوْ قَاتَلَكُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوَلَّوُا الْأَدْبَارَ ثُمَّ لَا يَجِدُونَ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿٢٢﴾

22. Na lau makafiri wangelipigana nanyi basi bila ya shaka wangeligeuza migongo, kisha wasingelipata mlinzi wala msaidizi.

سُنَّةَ اللَّـهِ الَّتِي قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلُ وَلَن تَجِدَ لِسُنَّةِ اللَّـهِ تَبْدِيلًا ﴿٢٣﴾

23. Ni desturi ya Mwenyezi Mungu iliyokwishapita zamani, hutapata mabadiliko katika desturi ya Mwenyezi Mungu.

وَهُوَ الَّذِي كَفَّ أَيْدِيَهُمْ عَنكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ عَنْهُم بِبَطْنِ مَكَّةَ مِن بَعْدِ أَنْ أَظْفَرَكُمْ عَلَيْهِمْ وَكَانَ
اللَّـهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرًا ﴿٢٤﴾

24. Na Yeye ndiye aliyeizuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao, katika bonde la Makka baada ya kuwapa ushindi juu yao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona myatendayo.

## WALIPOKUBAI CHINI YAMTI

**Aya 18 – 24**

### MAANA

Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewaridhia waumini walipokubai chini ya mti.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anaashira Baia iliyoridhiwai chini ya mti, kwamba Yeye yuko radhi nayo na watu wake. Yamekwishatangulia maelezo ya Baia hii katika Aya 10 ya Sura hii.

Na alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawalipa

Wanaelezewa watu wa baia. Nyoyo zao zilijaa ukweli na ikhlasi kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Makusudio ya utulivu ni raha na utulivu wa moyo. Ushindi wa karibu ni mkataba wa Hudaybiyya ambao miongoni mwa athari zake ni kuingia waislamu Makka kufanya umra, pamoja na kuchukia makuraishi. Kuna riwaya isemayo kuwa Umar bin Al- khattwab alimuuliza Nabii **(s.a.w.w)**: **"Ni ushindi huu ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Mtume akasema: "Ndio."**

Wafasiri wengi wamesema kuwa makusudio ya ngawira nyingi, ni ngawira za Khaybara. Kwa sababu Khaybara ilikuwa mashuhuri kwa ngawira nyingi na mashamba. Lakini kauli yenye nguvu ni kila ngawira walizopata watu wa Baia iliyoridhiwa, kwa sababu Mwenyezi Mungu (s.w.t) amesema ngawira kiujumla bila ya kuifunga na jambo maalum.

Maana yake kwa ufupi ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliwaneemesha watu wa Baia iliyoridhiwa kwa utulivu na neema nyingi, kwa sababu Yeye alijua kuwa wao wana ikhlasi katika dini yao na ukweli wa azma yao ya jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

Kila mafanikio waliyoyapata waislamu na kuwapeleka mbele ni katika Athari za nguvu za Mwenyezi Mungu, uweza wake na hekima yake katika mipangilio.

Mwenyezi Mungu amewaahidi ngawira nyingi mtakazozichukua.

Ngawira nyingi hapa ni kila nyara walizozipata waislamu zama za Mtume **(s.a.w.w)**. Kwa hiyo basi tofauti ya ngawira zilizotajwa kwenye Aya iliy- otangulia ni kuwa zile zilizowahusu watu wa Baia iliyoridhiwa na hizi ni za waislamu wote kila mahali na kila wakati.

Basi amewatangulizia hii.

Hii ni ishara ya suluhu ya Hudaybiyya. Kwa sababu suluhu hii ndiyo iliy- otangulia. Ama ngawira za Khaybara zilikuwa baada ya suluhu. Lau si neno hii, tungelisema iliyotangulia ni suluhu pamoja na Khaybar.

Na akaizuia mikono ya watu isiwafikie.

Tabari anasema, wametofautiana watu wa taawili kuhusu neno 'watu' hapa. Ikasemekana ni mayahudi wengine wakasema ni makuraishi. Tuonavyo sisi makusudio ni maadui wa Uislamu waliojaribu kuumaliza na kuwamaliza Waislamu. Hakuna lililowazuia isipokuwa udhahifu.

Na ili hiyo iwe ni Ishara kwa Waumini.

'Hiyo' ni suluhu ya Hudaybiyya. Mwenyezi Mungu ameifanya ni alama kwa waumini kuwa Mwenyezi Mungu yuko pamoja nao na anawanusuru na maadui zao. Hazikupita siku ila ikawabainikia waumini kuwa mkataba wa Hudaybiyya ulikuwa ni heri kwao na shari kwa washirikina.

Na akawaongoza njia iliyonyooka kwenye kila yaliyo na manufaa yenu ya dunia na Akhera.

Na nyingine hamjaweza kuzipata, Mwenyezi Mungu amekwishazizingira.

Yaani Mwenyezi Mungu amewaahidi ngawira mnazoweza kuzipata hivi sasa, vile vile amewaahidi nyingine msizoweza kuzipata hivi sasa, lakini Mwenyezi Mungu amewahifadhia, na mtazipata baadae, iwe karibu au mbali.

Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu, hashindwi kuwapa nyara zaidi ya mnavyofikiria na kutegemea.

Na lau makafiri wangelipigana nanyi basi bila ya shaka wangeligeuza migongo, kisha wasingelipata mlinzi wala msaidizi.

Kama kwamba muulizaji aliuliza itawezekana vipi waislamu wapate nyara za makafiri, na hali wao wana nguvu na ni wengi wanaopigania nafsi zao?

Ndio Mwenyezi Mungu (s.w.t) akajibu kuwa Yeye yuko pamoja na waumini na anawakinga. Mwenyezi Mungu hashindwi na jambo. Ama makafiri hawana kimbilio isipokuwa upanga au kukimbia.

Ni desturi ya Mwenyezi Mungu iliyokwishapita zamani, hutapata mabadiliko katika desturi ya Mwenyezi Mungu.

Ni desturi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa mitume waliopita kuwashin- da maadui zao. Kama muulizajai atauliza, mbona hii haiafikiani na Aya zinazoelezea waziwazi kuwa mayahudi walikuwa wakiwaua manabii bila ya haki? Majibu yake yako kwenye Juz. 17 22: (38 – 41).

Na Yeye ndiye aliyeizuia mikono yao kwenu, na mikono yenu kwao, katika bonde la Makka baada ya kuwapa ushindi juu yao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona myatendayo.

'Yeye' ni Mwenyezi Mungu. Waliozuiwa mikono ni makafiri. Imesemekana kuwa Makusudio ya bonde la Makka ni Hudaybiyya, kwa vile mji huo uko karibu na Makka.

Wengine wakasema ni Makka yenyewe. Maana haya ndiyo yanayokuja haraka kwenye fahamu, kutokana na neno bonde.

Maana ni kuwa enyi waislamu mmeingia Makka, uliokuwa mji mkuu wa shirki na kitovu cha washirikina mkiwa washindi bila ya vita.

Hii ni katika fadhila za Mwenyezi Mungu na neema yake kubwa kwenu. Kwa sababu Yeye ndiye aliyewazuia kupigana kwa kuwatia hofu katika nyoyo zao na akawazuia nyinyi kupigana nao kwa kuwakataza.

Suluhu ya Hudaybiyya ilikuwa mwaka wa sita wa Hijra, Umra ya kulipa ukawa mwaka wa saba na kuiteka Makka kukawa katika mwaka wa nane.

9

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

هُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَالْهَدْيَ مَعْكُوفًا أَن يَبْلُغَ مَحِلَّهُ ۚ وَلَوْلَا رِجَالٌ
مُّؤْمِنُونَ وَنِسَاءٌ مُّؤْمِنَاتٌ لَّمْ تَعْلَمُوهُمْ أَن تَطَئُوهُمْ فَتُصِيبَكُم مِّنْهُم مَّعَرَّةٌ بِغَيْرِ عِلْمٍ ۖ لِّيُدْخِلَ اللَّـهُ
فِي رَحْمَتِهِ مَن يَشَاءُ ۚ لَوْ تَزَيَّلُوا لَعَذَّبْنَا الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٢٥﴾

25. Hao ndio waliokufuru na wakawazuia msiingie Msikiti Mtakatifu, na wakawazuilia dhabihu kufika mahala pao pa kuchinjwa. Na lau si wanaume waumini na wanawake waumini msiowajua kuwa mtawasaga na mkaingia matatani kutokana nao bila ya kujua. Ili amuingize amtakaye katika rehema yake. Lau wangelipambanuka bila ya shaka tungeli waadhibu waliokufuru kwa adhabu chungu.

إِذْ جَعَلَ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي قُلُوبِهِمُ الْحَمِيَّةَ حَمِيَّةَ الْجَاهِلِيَّةِ فَأَنزَلَ اللَّـهُ سَكِينَتَهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ وَعَلَى
الْمُؤْمِنِينَ وَأَلْزَمَهُمْ كَلِمَةَ التَّقْوَىٰ وَكَانُوا أَحَقَّ بِهَا وَأَهْلَهَا ۚ وَكَانَ اللَّـهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٢٦﴾

26. Pale wale ambao wamekufuru walipotia katika nyoyo zao hasira, hasira za kijinga, Mwenyezi Mungu aliteremsha utulivu juu ya Mtume wake na juu ya waumini, na akawalazimisha neno la takua. Na wao walikuwa ndio wenye haki nalo na wenye kustahili. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

## WALIOWAZUIA NA MSIKITI MTAKATIFU

**Aya 25 – 26**

### MAANA

Hao ndio waliokufuru na wakawazuia msiingie Msikiti Mtakatifu, na wakawazuilia dhabihu kufika mahala pao pa kuchinjwa.

Katika kufasiri Aya ya 10 ya sura hii tulisema kuwa mnamo mwaka wa sita wa Hijra washirikina walimzuia Mtume **(s.a.w.w)** na maswahaba wasiuzuru Msikiti Mtakatifu. Inasemekana walikuwa na ngamia sabini wa kuchinja Makka. Hao ndio aliowakusudia Mwenyezi Mungu kwa kusema: "na wakawazuilia dhabihu kufika mahala pao pa kuchinjwa."

Vile vile katika Aya 24 tukasema kuwa waislamu waliiteka Makka bila ya vita mnamo mwaka wa nane. Kwa sababu Mwenyezi Mungu alitizitia hofu nyoyo za washirikina kutokana na waislamu.

Aya tuliyo nayo hivi sasa inaelezea maana haya na kusisitiza kuwa watu wa Makka hawakujizuia kupigana na Mtume **(s.a.w.w)** na maswahaba wake, walipoingia Makka, isipokuwa ni kwa kuwaogopa waislamu. Dalili ya hilo – kama ilivyoweka wazi Aya – ni kuwa hawa ndio walewale waliowazuia waislamu jana kuingia Msikiti Mtakatifu na kuchinja ili wale mafukara.

Kisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) akaashiria baadhi ya faida za kutopigana Makka, kwa kusema:

1. Na lau si wanaume waumini na wanawake waumini msiowajua kuwa mtawasaga na mkaingia matatani kutokana nao bila ya kujua.

Mtume **(s.a.w.w)** alipoingia Makka kuiteka, hapo walikuweko waislamu wanaume na wanawake, waliokuwa hawajulikani wala huwezi kuwatofautisha na wshirikina kwa vile walikuwa wakificha imani yao kuhofia maadui wa uislamu. Lau vita vingechachamaa, madhara yake yangeliwakumba waislamu na makafiri. Hilo lingeliwatia tabu waislamu; kama vile kutoa fidia ya kuua kwa makosa, kuongezea maadui watapata la kusema kuwa waislamu wanauana wenyewe kwa wenyewe.

2. Ili amuingize amtakaye katika rehema yake.

Makusudio ya rehema hapa ni Uislamu. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliizuia mikono isipigane Makka, kwa sababu anajua kuwa baadhi ya wakazi wake washirikina wataongoka na kusilimu. Na ilitokea hivyo kweli.

Lau wangelipambanuka bila ya shaka tungeliwaadhibu waliokufuru kwa adhabu chungu.

Yaani lau wangelijulina waislamu na makafiri, Mwenyezi Mungu angeliwaruhusu kupigana na na makafiri na angeliwateremshia adhabu kali.

Pale wale ambao wamekufuru walipotia katika nyoyo zao hasira, hasira za kijinga.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anawaashiria vigogo wa kishirikina waliomzuia Nabii **(s.a.w.w)** kuzuru Msikiti mtakatifu. Si kwa lolote ila ni kwamba nyoyo zao zimejaa taasubi na kiburi.

Hili pekee linatosha kuruhusiwa kuuawa, lakini Mwenyezi Mungu (s.w.t) akaizuia mikono ya waumini kuwachunga wale wanaoficha imani yao na waislamu watakaopatikana baadaye.

Mwenyezi Mungu aliteremsha utulivu juu ya Mtume wake na juu ya waumini, na akawalazimisha neno la takua. Na wao walikuwa ndio wenye haki nalo na wenye kustahili.

Makusudio ya utulivu hapa ni kuridhia na subira nzuri. Kuwalazimisha ni kuwawajibishia. Ama neno la takua imesemekana ni tamko la ilaha illa Allah… (hapana Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu….). lakini lenye nguvu ni kuwa makusudio yake ni kufanya takua.

Maana ni kuwa Mtume **(s.a.w.w)** alikubali suluhu ya Hudaybiyya pamoja na kiburi cha washirikina na ujeuri wao. Baadhi ya maswahaba walichukia suluhu na wakataka kupigana tu, lakini Mwenyezi Mungu akawapa subira nzuri pamoja na ufedhuli wa washirikina, akawaamrisha wakubali suluhuu na wairidhie.

Wakasikia na wakafanya yanayowajibisha imani na takua. Hilo si la kushangaza kwa vile wao ndio wanaostahiki na ndio aula kulitumia. Walikwishapigana jihadi na wakajitolea mara nyingi katika njia ya Mwenyezi Mungu na wakafanya subira ya kiungwana.

Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

Anawajua wenye takua na wenye hatia, kila mmoja atamlipa kwa aliyoyachuma na wao hawatadhulumiwa.

لَّقَدْ صَدَقَ اللَّـهُ رَسُولَهُ الرُّؤْيَا بِالْحَقِّ ۖ لَتَدْخُلُنَّ الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ إِن شَاءَ اللَّـهُ آمِنِينَ مُحَلِّقِينَ
رُءُوسَكُمْ وَمُقَصِّرِينَ لَا تَخَافُونَ ۖ فَعَلِمَ مَا لَمْ تَعْلَمُوا فَجَعَلَ مِن دُونِ ذَٰلِكَ فَتْحًا قَرِيبًا ﴿٢٧﴾

27. Hakika Mwenyezi Mungu amemhakikishia Mtume wake ruiya ya haki. Bila ya shaka mtauingia Msikiti Mtakatifu, Inshallah, kwa amani, na

hali mmenyoa vich- wa vyenu na mmepunguza. Hamtakuwa na hofu. Alijua msiyoyajua. Mbali na haya aliwapa ushindi ulio karibu.

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ ۚ وَكَفَىٰ بِاللَّـهِ شَهِيدًا ﴿٢٨﴾

28. Yeye ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uwongofu na dini ya haki, ili aitukuze juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi.

مُّحَمَّدٌ رَّسُولُ اللَّـهِ ۚ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ ۖ تَرَاهُمْ رُكَّعًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ
فَضْلًا مِّنَ اللَّـهِ وَرِضْوَانًا ۖ سِيمَاهُمْ فِي وُجُوهِهِم مِّنْ أَثَرِ السُّجُودِ ۚ ذَٰلِكَ مَثَلُهُمْ فِي التَّوْرَاةِ ۚ وَمَثَلُهُمْ فِي
الْإِنجِيلِ كَزَرْعٍ أَخْرَجَ شَطْأَهُ فَآزَرَهُ فَاسْتَغْلَظَ فَاسْتَوَىٰ عَلَىٰ سُوقِهِ يُعْجِبُ الزُّرَّاعَ لِيَغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ
وَعَدَ اللَّـهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنْهُم مَّغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا ﴿٢٩﴾

29. Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu na walio pamoja naye, wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao. Utawaona wakirukuu na kusujudu wakitafuta fadhila na radhi za Mwenyezi Mungu. Alama zao zi katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Tawrat na mfano wao katika Injili ni kama mmea uliotoa chipukizi lake, kisha ukalitia nguvu, ukawa mnene, ukasimama sawa juu ya shina lake, ukawapendeza wakulima, ili kuwakasirisha kwa ajili yao makafiri. Mwenyezi Mungu amewaahidi walioamini na wakatenda mema katika wao maghufira na ujira mkubwa.

## MRUIYA YA MTUME

**Aya 27 – 29**

### MAANA

Hakika Mwenyezi Mungu amemhakikishia Mtume wake ruiya ya haki. Bila ya shaka mtauingia Msikiti Mtakatifu, Inshallah, kwa amani, na hali mmenyoa vichwa vyenu na mmepunguza. Hamtakuwa na hofu.

Dhahiri ya Aya na Hadith mutawatir zinafahamisha kuwa Mtume **(s.a.w.w)** aliota kuwa yeye na swahaba zake wameingia Makka kwa amani, wakatufu nyumba kongwe; vile wanavyotaka, wengine wakiwa wamenyoa na wengine wamepunguza. Basi Mtume akawaelezea swahaba zake alivyoona usingizini. Wakafurahi na kufikiria kuwa mwaka huhuo wataingia Makka. Mtume akaenda nao Makka lakini wakazuiliwa Hudaybiyya na wakarudi Madina; kama tulivyokwishaeleza.

Hapo wanafiki wakawa wamepata la kusema: "Haya iko wapi ndoto? Hatukunyoa, hatukupunguza wala hatukuona Msikiti? Wakasahau au wakajitia kusahau kuwa Mtume hakutaja muda. Mmoja akamuuliza Mtume: si umesema hakika utauingia Msikiti Mtakatifu kwa amani? Akasema ndio, lakini sikusema ni mwaka huu.

Mwaka uliofuatia, ambao ulikuwa ni mwaka wa saba wa Hijra, waislamu waliingia Makka kufanya Umra, wakatufu Al-Ka'aba wanavyotaka, akanyoa mwenye kunyoa na kupunguza mwenye kupunguza. Wakabaki hapo siku tatu kisha wakarejea Madina. Ndio ikashuka kauli yake Mwenyezi Mungu: "Hakika Mwenyezi Mungu amemhakikishia Mtume wake ruiya," yalipojitokeza yale aliyoota Mtume na kuwaambia:

Alijua msiyoyajua.

Mwenyezi Mungu alijua masilahi ya kuuahirisha umra baada ya mkataba wa Hudaybiyya, jambo ambalo waislamu hawakulijua; ambayo ni kuepusha vita, kusilimu washirikina wengi waliomzuilia Mtume na maswahaba.

Mbali na haya aliwapa ushindi ulio karibu.

'Haya' ni kuhakika ndoto ya kuingia Makka kwa amani. Makusudio ya ushindi ni mkataba wa Hudaybiya au ni huo na kuichukua Khaybara. Maana ni kuwa suluhu hii na kuiteka Khaybara kulikofanyika baada siku kidogo, kulifanyika kabla ya kuhakikika ndoto. Mambo hayo mawili ni ushindi mkubwa sawa na kuingia Makka.

Yeye ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uwongofu na Dini ya haki, ili aitukuze juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi.

Makusudio ya Mtume ni Muhammad **(s.a.w.w)**. Uwongofu na dini ya haki ni Uislamu. Ulitukuka na kuenea mashariki mwa ardhi na magharibi yake. Kwa sababu unatoa mwito wa kutenda kwa ajili maisha bora na kukataza kila ambalo litakuwa ni kikwazo katika njia ya kufikia hilo.

Umetangulia mfano wake katika Juz. 10 (9:33).

## MASWAHABA NA QUR'AN

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amesimulia katika Kitabu chake Kitakatifu kuwa Musa Bin Imran aliwalingania wana wa Israil kwenye vita wakamwambia:

فَاذْهَبْ أَنتَ وَرَبُّكَ فَقَاتِلَا إِنَّا هَاهُنَا قَاعِدُونَ ﴿٢٤﴾

"Basi nenda wewe na Mola wako mkapigane, sisi tutakaa hapa." Juz. 6 (5:24).

Pia alisimulia kuwa watu wa Bwana Masih walijaribu kumuua na kumsulubu na wanafunzi wake wakamwambia: Je Mola wako anaweza kututeremshia chakula kutoka mbinguni; aliposema: Mcheni Mwenyezi Mungu. Wakasema: Tunataka kula katika hicho Tazama Juz. 7 (5:111-112).

Na akateremsha Sura nzima mbali ya Aya nyinginezo kadhaa kuwashutumu maswahaba wanafiki, lakini vile vile aliteremsha Aya nyingi za kuwasifu maswahaba wema wenye takua; miongoni mwa Aya hizo ni ya 18 ya sura hii tuliyo nayo, tuliyoifasiri punde tu na ile isemayo:

وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُم بِإِحْسَانٍ رَّضِيَ اللَّـهُ عَنْهُ مْ
وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتَهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٠٠﴾

"Na waliotangulia wa kwanza katika wahajiri na Ansari, na wale waliowafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu yuko radhi nao na wao wako radhi naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito chini yake, watadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa." Juz. 11 (9:100).

Na pia kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu na walio pamoja naye, wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao.

Waovu huungana katika kutafuta windo, na wanapolipata wanauana wao kwa wao kugombania kulila. Lakini wenye ikhlasi wao wako wako pamoja tu wakati wote, hawatofautiani. Ni ndugu katika dini wakihurumiana na kusaidiana; ni kama familia moja, wanasaidiana kwenye haki na watu wake na wanapiga vita ubatilifu na wanachama wake.

Hii ndio sifa halisi ya swahaba wa Muhammad **(s.a.w.w)** kwa ushahidi wake Mwenyezi Mungu Mtukufu pale alipowasifu wao na Mtume kuwa wanakasirika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na wanaridhia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Haya ameyatambua Dkt. Twaha Hussein, mwanafasihi ambaye huwa anafahamika kwa ishara na dalili. Anasema katika kitabu chake: Mir-atul-islam (Kioo cha uaislamu): "Uislamu wa manabii haukuwa ni twaa ya dhahiri isipokuwa uaislamu wao ulikuwa mpana wenye kina na wa ukweli zaidi ya inavyowezekana kuwa Uislamu. Na Uislamu wa waliokuwa wema katika Maswahaba haukuwa na ufinyu unaosimama mbele ya utii ulio dhahiri, isipokuwa ulikuwa ni mpana na wenye kina zaidi ya hivyo."

Kisha Dkt. akampigia mfano Ammar Bin Yasir kwa Uislamu huu wa kina, akasema: "Ammar bin Yasir alikuwa akipigana pamoja na Ali katika Siffin kwa hamasa, naye akiwa ni mzee wa miaka tisini au kupita. Alikuwa akipigana kwa imani, yaani kwamba yeye anaitetea haki. Siku alipouawa alikuwa akiwahimiza watu huku akisema: Ni nani atakayekwenda Peponi? Leo nitakutana na wapenzi Muhammad na kikosi chake."

Anaendelea kusema: "Kuuawa kwa Ammar kulikuwa ni kumthibitisha Ali na walio wema katika maswahaba zake na kumuweka kwenye shaka Muawiya na waliokuwa pamoja naye. Hiyo ni kwa sababu Wahajiri wengi na Answar walimuona Mtume **(s.a.w.w)** akipapasa kichwa cha Ammar na kumwambia: Masikini ewe mwana wa Sumayya, kitakuua kikundi kiovu."

Utawaona wakirukuu na kusujudu.

Yaani mandhari yanamfanya muangaliaji awaone kuwa wao ni watu wa kurukuu na kusujudu, hata kama wakati huo hawako hivyo.

Wakitafuta fadhila na radhi za Mwenyezi Mungu. Alama zao zi katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu.

Makusudio ya athari ya kusujudu hapa sio ile alama nyeusi inayoonekana kwenye paji la uso, hapana kwa sababu alama hizi nyingi ni za kinafiki na ria; isipokuwa makusudio yake ni usafi na uangavu unaonekana usoni kutokana na athari ya ibada.

Maana ni kuwa maswahaba walirukuu na kusujudu kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu na thawabu zake na kuhofia ghadhabu zake na adhabu zake. Athari hiyo, ukiichunguza, inajitokeza katika nyuso zao kiuhakika, kwa sababu ibada ya ikhlasi ya Mungu inaleta utwahara na usafi katika nafsi ya mja mwenye ikhlasi na kujitokeza kwa ukamilifu usoni; sawa na inavyojitokeza huzuni na furaha.

Huu ndio mfano wao katika Tawrat na mfano wao katika Injili ni kama mmea uliotoa chipukizi lake, kisha ukalitia nguvu, ukawa mnene, ukasimama sawa juu ya shina lake.

Hiki ni kinaya cha maswahaba wa Mtume **(s.a.w.w)**; mwanzo wanakuwa wachache kisha wanazidi na kuwa wengi. Ufafanuzi wa mfano huu ni kuwa Tawrt na Injili zimetoa bishara ya Muhammad **(s.a.w.w)**, zikawasifia maswahaba zake kama mmea unaokuwa, ukazaa matunda na yakawa mengi pamoja na matawi yake, yakashikana vizuri na ukawa una nguvu. Ukawapendeza wakulima kwa uzuri wake na kukua kwake.

Ili kuwakasirisha kwa ajili yao makafiri.

Sio mbali kuwa makusudio ya wakulima hapa ni Mtume, maadamu mmea ni swahaba zake, kwa sababu yeye ndiye aliyewainua kufikia mahali walipo; na kwa fadhila yake wameshinda vita wakati wake na baadae. Na kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja wakulima badala ya mkulima kwa kumtukuza Mtume **(s.a.w.w)**.

Ikumbukwe kwamba tunayasema haya kwa njia ya uwezekano tu wa kukisia

Mwenyezi Mungu amewaahidi walioamini na wakatenda mema katika wao maghufira na ujira mkubwa.

Maana yake yako wazi. Umetangulia mfano wake katika Juz. 6 (5:9).

## JE, SHIA ITHANAASHARIA WANA TAFSIRI YA NDANI?

Mwanafasihi wa Misr, Dkt Mustafa Mahmud, alitoa mfululizo wa makala 13, katika jarida la Sabahul-khayr. Katika makala hizo alizungumzia muujiza wa Qur'an, kisa cha kuumba[1] na maudhui mengine ya ghaibu.

Kisha yakakusanywa makala katika kitabu kilichoitwa: Muhawalatu lifahmi asriy lilqur'an (Kujaribu kuifahamu Qur'an kisasa). Kikachapishwa na kutolewa mnamo mwezi wa tatu au wa nne mwaka 1970.

Katika makala ya 'Mungu mmoja na dini moja,' mtungaji aliwachanganya Shia Ithnaashariya pamojana vikundi vinavyofasiri Qur'an kwa undani, na kwamba wao ni sawa na Al-babiyya na Al-khawarij, wakifasiri Qur'an kwa tafsiri ya undani.

Basi nikamwandikia barua kwamba Shia Ithanaasharia, wako mbali zaidi ya watu wote na fikra hii ya uzushi na upotevu na kwamba vitabu vyao vinashudia hilo na vimejaa kwa watu. Nikamtajia baadhi ya vitabu hivyo na jinsi masheikh wa Azhar wenye insafu walivyosema kuhusu Shia Imamia; kama vile marehemu Sheikh Shaltut na wengineo waliounukuliwa na jarida la Al-islam, linalotolewa Misr na Darut-taqrib.

Katika jioni ya 15-4-1970, nilisikia mlio wa simu, akawa ni Dkt. Mustafa Mahmud akizungumza kutoka Triumph Hotel ya Beirut…Tukawa pamoja kwa mara ya kwanza. Tukazungumza kuhusu kitabu chake Allahu wal-insan (Mwenyezi Mungu na mtu) na majibu yangu Allahu wal-aql (Mwenyezi Mungu na akili).

Basi nikamwalika nyumbani kwangu siku iliyofuatia. Mazungumzo yetu yalikuwa juu Uislamu na tafsiri za ndani. Miongoni mwa maneno aliyoyasema mwana fasihi huyu ni: "Baadhi ya Shia wanafasiri "Amezichanganya bahari mbili kwa kuzikutanisha[2]." kuwa ni Ali na Fatima."

Nikwambia: Je, ni mantiki na ni sawa kweli kulihusisha kundi lenye mamilioni ya wafuasi kwa kauli ya mmoja wao, anayejiwakilisha yeye mwenyewe tu? Je, ni lazima ikiwa sheikh mmoja atafasiri Aya ya Qur'an kwa undani, ndio taifa zima lihisabiwe wanafasiri Qur'an kwa undani? Ikiwa malenga mmoja wa Misr atafasiri ubeti wa shairi kialama, je, ni sawa kusema kuwa malenga wote wa Misri wanafasiri mashairi kialama? Niliendelea kumwambia: "Hakika Shia Ithnaasharia wana vitabu vya kiitikadi vinavyokubalika; kama vile Awail al-maqalat cha Sheikh Mufid,

1. Pia aliwahi kuzungumzia mdundo wa ndani wa Qur'an. Tazama Juz. 22 (36:1-6).
2. Sura 55:19.

Qawaidul-aqai cha Nasruddin Attusi na sherehe yake cha Allama Hill na yaliyoelezwa katika Sharhut Tajrid minat Tawhid…"

Nilikuwa nikikutana na Tafsiri ya kiundani ya masheikh wa kisunni wakati nikifanya utafiti wa rejea, lakini nilikua nikizipuuza, kwa vile zilikuwa haziendani na malengo ya tafsiri yangu. Basi Dkt. Alipotoa hoja ya bahari mbili, nilijaribu sana kukumbuka angalau tafsiri moja tu ili nipinge manaeno ya Dkt. Lakini kumbukumbu zangu ziliniangusha wakati nilipokuwa nazihitajia sana. Basi tukaendelea na maudhi mengine.

Ilikuwa ni sadfa wakati tukijadilina, kuwa ninafasiri sura hii ya Al-fat-h. Siku iliyofuatia nikafika kwenye Aya isemayo: "Ni kama mmea uliotoa chipukizi lake, kisha ukalitia nguvu, ukawa mnene, ukasimama sawa juu ya shina lake," Mara nikasoma tafsiri za Kissuni: Ruhul-bayan ya Isamil Haqqi na Ats-hil ya Alhafidh bin Ahamd Al-Kalabi. Wote ni wa kissuni, ninawanukuu: "Ni kama mmea uliotoa chipukizi lake Kwa Abu Bakr, kisha ukalitia nguvu kwa Umar, ukawa mnene kwa Uthman, ukasimama sawa juu ya shina lake kwa Ali."

Basi niliyoyaona katika tafsiri hizi yakanikumbusha niliyoyasoma zamani katika kitabu Hayatu Al-imam Abu Hanifa (Maisha ya Imam Abu Hanifa) cha Sayyid Afifi, kwamba Suyut amesema: "Wamesema maulama kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alimbashiria Imam Malik katika Hadith isemayo: "Inakurubia watu kupiga matumbo ya farasi wakitafuta ilimu, hawatapata mwanachuoni aliye mjuzi zaidi kuliko mwanachuoni wa Madina."

Akambashiria Shafii katika Hadith: "Msiwatukane makuraishi kwani mwanachuoni wake ataijaza ardhi ilimu." Akambashiria Abu hanifa kwenye Hadith: "Lau kama ilimu itakuwa imeangikwa juu ya Thureya wangeliifuata watu katika wafursi."

Basi hapo hapo nikampigia simu Dkt, nikamsomea tafsiri mbili na kumuuliza: je, utaniruhusu nizinasibishe tafsiri hizi kwa masunni wote, niwafanye wao na Wahabiy kuwa ni sawa, kama ulvyofanya wewe kwa Shia kwa kuwa tu mmoja wao amesema?

Basi hakunijibu kitu isipokuwa: "Tamam … tamam." (sawa … sawa).

## MWISHO WA SURA YA ARUBAINI NA NANE: SURAT AL-FATH

10

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

Sura Ya Arubaini Na Tisa: Surat Al- Hujurat. Imeshuka Madina. Ina Aya 18.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kure-hemu

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُقَدِّمُوا بَيْنَ يَدَيِ اللَّـهِ وَرَسُولِهِ وَاتَّقُوا اللَّـهَ إِنَّ اللَّـهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١﴾

1. Enyi ambao mmeamini! Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ
بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَن تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنتُمْ لَا تَشْعُرُونَ ﴿٢﴾

2. Enyi mlioamini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaanguka, na hali hamtambui.

إِنَّ الَّذِينَ يَغُضُّونَ أَصْوَاتَهُمْ عِندَ رَسُولِ اللَّـهِ أُولَـٰئِكَ الَّذِينَ امْتَحَنَ اللَّـهُ قُلُوبَهُمْ لِلتَّقْوَىٰ لَهُم
مَّغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٣﴾

3. Kwa hakika ambao wanateremsha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amezitia mtihani nyoyo zao kwa takua. Hao watakuwa na maghufira na ujira mkubwa.

إِنَّ الَّذِينَ يُنَادُونَكَ مِن وَرَاءِ الْحُجُرَاتِ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٤﴾

4. Hakika ambao wanakuita nyuma ya vyumba, wengi wao hawana akili.

وَلَوْ أَنَّهُمْ صَبَرُوا حَتَّىٰ تَخْرُجَ إِلَيْهِمْ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُمْ وَاللَّـهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٥﴾

5. Na lau wao wangelingojea mpaka uwatokee ingelikuwa kheri kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

## MSINYANYUE SAUTI ZENU KULIKO SAUTI YA NABII

**Aya 1 – 5**

### MAANA

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anawakumbusha waumini mambo haya yafutayo:-

1. Enyi ambao mmeamini! Msitangulie mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Msifanye haraka kusema au kufanya tendo lolote linaoamabatana na dini na masilahi ya uma, mpaka alipitishe Mwenyezi Mungu kupitia Mtume wake mtukufu.

Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

Katika Nahjul-balagha imeandikwa: “Mche Mwenyezi Mungu kwa baad-hi ya takua hata kama ni kidogo. Na weka sitara baina yako na Mwenyezi Mungu hata kama ni nyembamba.”

Kwa uchache kabisa wa mtu kumcha Muumba wake ni kujizuia kusema: Lau Mwenyezi Mungu angelihalalisha hili ambalo ameliharamisha au angeliharamisha lile alilolilihalalisha. Au kusema afadhali Nabii angelifanya hivi au asingelifanya vile alivyofanya na mengineyo ya ujeuri na ujinga.

2. Enyi mlioamini! Msinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii.

Si jambo zuri kuinua sauti bila ya dharura. Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema: "Na uinamishe sauti yako. Hakika sauti mbaya zaidi ni ya punda." Juz. 21 (31:19). Sikwambii tena ikiwa ni kuinua sauti mbele ya wakubwa na kwenye vikao vyao. Na Mtume mtukufu **(s.a.w.w)** ni bwana wa manabii na mtukufu wa viumbe wote.

3. Wala msiseme naye kwa kelele kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaanguka, na hali hamtambui.

Mnapozungumza na Nabii msizungumze kama mnavyozungumza nyinyi. Mwenye kufanya hivyo atakuwa amebatilisha imani yake bila ya kutaka wala kujua. Na mwenye kubatilika imani yake ndio vimebatilika vitendo vyake na atakuwa mikononi mwa waliopata hasara.

Kwa hakika ambao wanateremsha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amezitia mtihani nyoyo zao kwa takua – yaani amezisafisha nyoyo zao kwa matendo mema - Hao watakuwa na maghufira na ujira mkubwa.

Mwenyezi Mungu huwajaribu waja wake kwa aina mbalimbali ya mitihani, ili apate mawaidha mwenye kuwaidhika na ajikanye mwenye kukanyika. Mwenye kuwaidhika na akawa na subira Mwenyezi Mungu humtakasa, humuongoza njia ya usawa na humneemesha kwa maghufira na ujira wa wenye kuwa na subira.

Aya inaashiria kwamba kuzungumza kwa adabu na kwa inavyotakikana ni katika imani. Imam Ali (a.s) anasema: **"Imani ya mja hainyooki mpaka unyooke moyo wake na moyo haunyooki mpaka unyooke ulimi wake.**

Hakika ambao wanakuita nyuma ya vyumba, wengi wao hawana akili.

Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa na wake tisa, kila mmoja alikuwa na chumba chake kilichojengwa kwa makuti ya mtende, mlangoni kukiwa na pazia ya manyoya.

Wafasiri wanasema kuwa mabedui walikuja Madina na wakasimama nyuma ya vyumba vya Mtume wakaanza kuita kwa sauti: Ewe Muhammad **(s.a.w.w)** tutokee! Mtume akangoja kidogo; kisha akawatokea. Mwenyezi Mungu amewataja kuwa wengi wao hawakujua walichokuwa wakikifanya, kutokana na ubedui na ushamba.

Na lau wao wangelingojea mpaka uwatokee ingelikuwa kheri kwao, kwa sababu kungoja na kutofanya haraka kuna malipo na thawabu, kumwdhimisha Mtume wa Mwenyezi Mungu na kuchunga adabu.

Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu. Rehema yake inaenea kwa washamba, walalahoi n.k.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِنَبَإٍ فَتَبَيَّنُوا أَن تُصِيبُوا قَوْمًا بِجَهَالَةٍ فَتُصْبِحُوا عَلَىٰ مَا فَعَلْتُمْ نَادِمِينَ ﴿٦﴾

6. Enyi mlioamini! Akiwajia fasiki na habari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kutojua, na mkawa wenye kujuta kwa mliyoyatenda.

## AKIWAJIA FASIKI NA HABARI YOYOTE, ICHUNGUZENI

**Aya 6**

### MAANA

Enyi mlioamini! Akiwajia fasiki na habari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kutojua, na mkawa wenye kujuta kwa mliyoyatenda.

Imekuwa mashuhuri kwa wafasiri kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alimtuma Walid bin Uqba bin Abu Muit kwa Bani Mustaliq kuchukua Zaka, wakampokea kwa shangwe ya kumzunguka, lakini akadhania kuwa wanataka kumzuia.

Akarudi kwa Mtume **(s.a.w.w)** na kumwambia: wamenizuia na kunifukuza. Basi Mtume **(s.a.w.w)** akakasirika na baadhi ya swahaba zake wakamwambia tuwashambulie? Ndio ikashuka Aya hii kuwaondolea tuhuma Bani Mustaliq. Kuna sababu nyingine ya kushuka Aya hii.

Sisi hatutegemei lolote katika sababu za kushuka Aya ila ikithibiti kwa nukuu ya Qur'an au Hadith mutawatir. Zaidi ya hayo ni kuwa kudhania Walid shari hakuwezi kusababisha ufasiki; isipokuwa ni kukosea na kutatizika. Mwenye kukosea haitwi fasiki.

Vyovyote itakavyokuwa sababu za kushuka, lakini Aya haishilii kwenye sababu hiyo, bali inaenda mbali zaidi, kwa vile sababu haiwezi kuhusisha isipokuwa inaenea. Itakuwa sababu inatajwa kwa ajili ya jambo fulani ambalo halihusishi tamko. Kwa hiyo niwajibu kuichukulia dhahiri ya Aya, ambayo inafahamisha uharamu wa kuyachukulia maneno ya fasiki bila ya kuchunguza na kuthibitisha habari yake, kuhofia kuingia kwenye hatari; kama kuwadhuru wengine na kujuta, na majuto ni mjukuu.

Tunapata tafsiri ya Aya hii katika kauli ya Imam Ali (a.s): **"Mwenye kufuata njia iliyo wazi atakunywa maji, na mwenye kuacha atahangaika."**

Kundi la masheikh wa kisunni na kishia wameitumia Aya hii kuwa ni dalili ya wajibu wa kuchukulia kauli ya mwenye kutegemewa bila ya sharti la kuchunguza ukweli wake. Baadhi yao wameitolea dalili kwa maneno ya undani yaliyojifungafunga.

Iko wazi kuwa Aya imechukua msingi wa kiujumla wa kupima habari ambayo haifai kuitegema ila baada ya uthibitisho na hiyo ni habari ya fasiki. Vile vile habari inayotegemwa bila ya uthibitisho ambayo ni habari ya mwenye kutegemewa.

Kwa sababu Mwenyezi Mungu ameshartiza kuitegemea habari ya fasiki kwa ubainifu na uthibitisho, lakini hakuitaja habari ya mwenye kutegemewa. Lau ingelikuwa ni wajib kuichunguza habari ya mwenye kuaminika basi angeliitaja. Kwa kuwa haikutajwa basi sharti hiyo haipo.

Tuanavyo sisi ni kuwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Akiwajia fasiki na habari yoyote, ichunguzeni," inafahamisha tu wajibu wa kuichunguza na kuithibitisha habari ya fasiki wala haifahimishi wajibu huo kwa habri ya mwenye kuaminika. Sisi tuko na wale wasemao kuwa kuitegemea habari ya mwenye kuaminika bila ya uchunguzi ni njia wanayoitumia wenye akili wa kale na wa sasa.

Hata hivyo kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Msije mkawasibu watu kwa kutojua, na mkawa wenye kujuta kwa mliyoyatenda," inafahamisha kuwa habari yoyote ambayo hatuna wasiwasi nayo kuingia katika matatizo na haramu, basi inafaa kuitumia bila ya kumwangalia mtoaji habari.

Kimsingi ni kuwa tusiamini habari ila ikiwa inatoka kwa mwenye kuaminika au tuithibitishe na kuichunguza ikiwa inatoka kwa fasiki.

وَاعْلَمُوا أَنَّ فِيكُمْ رَسُولَ اللَّـهِ لَوْ يُطِيعُكُمْ فِي كَثِيرٍ مِّنَ الْأَمْرِ لَعَنِتُّمْ وَلَـٰكِنَّ اللَّـهَ حَبَّبَ إِلَيْكُمُ الْإِيمَانَ وَزَيَّنَهُ فِي قُلُوبِكُمْ وَكَرَّهَ إِلَيْكُمُ الْكُفْرَ وَالْفُسُوقَ وَالْعِصْيَانَ أُولَـٰئِكَ هُمُ الرَّاشِدُونَ ﴿٧﴾

7. Na jueni kuwa yuko kati yenu Mtume wa Mwenyezi Mungu. Lau angeliwatii katika mambo mengi, bila ya shaka mngelitaabika. Lakini Mwenyezi Mungu amewapendezea Imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na akauchukiza kwenu ukafiri, na upotovu, na uasi. Hao ndio walioongoka.

فَضْلًا مِّنَ اللَّـهِ وَنِعْمَةً وَاللَّـهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٨﴾

8. Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na neema zake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima.

## MWENYEZI MUNGU AMEWAPENDEKEZEA IMANI

**Aya 7 – 8**

### MAANA

Na jueni kuwa yuko kati yenu Mtume wa Mwenyezi Mungu na mtukufu wa wa mwanzo na wa mwisho. Basi ni juu yenu kumwadhimisha wala msimpe habari isipokuwa ya ukweli.

Lau angeliwatii katika mambo mengi, bila ya shaka mngelitaabika.

Hii ni amri kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ikielekezwa kwa wau- mini kuwa wamsikilize Mtume na wamtii, wala wasimshauri lile analolijua kutoka kwa Mwenyezi Mungu, ambalo wao hawalijui. Lau angeliwaitikia kwenye mambo mengi wanayomwambia wangelitaabika na kuingia kwenye tabu na dhambi.

Lakini Mwenyezi Mungu amewapendezea Imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na akauchukiza kwenu ukafiri, na upotovu, na uasi. Hao ndio walioongoka.

Mwenyezi Mungu amewaamrisha waja wake wamwamini Yeye na wamtii, akawabainishia uzuri wa imani na utiifu, akatumia kila njia kuwahimiza hilo na akamwahidi malipo na thawabu kubwa mwenye kuamini na akatenda mema. Vile vile amewakataza ukafiri na uasi, akabainisha hasara zake na akamtishia kwa adhabu mwenye kukufuru na kuasi na akazisifia adhabu hizo kwa namna ambayo haiwezi kufikirika akilini ila baada ya kubainishwa. Ni mtu gani anayeweza kufikiria adhabu ambayo si mauti wala uhai.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewatuma Mitume wake kwa watu ili wafikishe amri, makatazo ahadi na kiaga chake. Kuna wale wanaoitikia kihaki na kiukweli, wengine wakapinga na kufanya inadi na kuna wale waliotikia kuhofia masilahi yao na tamaa ya ngawira.

Wale waliomwitikia Mwenyezi Mungu na Mtume kihaki na kiukweli ndio aliowakusudia katika kauli yake: "Amewapendezea Imani, na akaipamba katika nyoyo zenu." Yaani ameipendekeza na kuipamba kutokana na kueleza uzuri wa imani na kivutio cha thawabu nyingi. Akauchukiza ukafiri kwa kueleza mabaya yake na tishio la adhabu chungu.

**Unaweza kuuliza**: Mwenyezi Mungu (s.w.t) amelibainisha hilo kwa waumini na makafiri, kwanini amehusisha kuwataja waumini, kinyume na wengineo?

**Jibu**: Ndio, lakini sio kila mwenye kusikia ubainifu wa Mwenyezi Mungu anauamini na kunufaika nao, wala sio kila mwenye kunasihiwa na Mwenyezi Mungu anakubali nasaha zake. Bali wema wamekubali na waovu wakakataa. Ndio Mwenyezi Mungu (s.w.t) akamtaja na kumsifu mwenye kusikia maneno akafuata mazuri yake na akampuuza mwenye kupinga na akaachana nayo.

Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na neema zake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima.

Hakuna mwenye shaka kwamba mwenye kuchagua uongofu badala ya upotevu ana fadhila na malipo, lakini fadhila kubwa ni ya yule aliyemwandalia njia ya uongofu, akamwongoza na akampa uweza wa kuifuata. Walisema wakale: "Kama si sababu asingelifaulu msababishaji"

وَإِن طَائِفَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ اقْتَتَلُوا فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا ۖ فَإِن بَغَتْ إِحْدَاهُمَا عَلَى الْأُخْرَىٰ فَقَاتِلُوا الَّتِي تَبْغِي حَتَّىٰ تَفِيءَ إِلَىٰ أَمْرِ اللَّـهِ ۚ فَإِن فَاءَتْ فَأَصْلِحُوا بَيْنَهُمَا بِالْعَدْلِ وَأَقْسِطُوا ۖ إِنَّ اللَّـهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ ﴿٩﴾

9. Na ikiwa makundi mawili katika waumini yanapigana, basi yapatanisheni. Na likiwa moja la hayo linadhulumu jingine, basi lipigeni linalodhulumu mpaka lirejee kwenye amri ya Mwenyezi Mungu. Na likirejea basi yapatanisheni kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanaohukumu kwa haki.

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ ۚ وَاتَّقُوا اللَّـهَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١٠﴾

10. Hakika Waumini tu ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mrehemiwe.

## NA IKIWA MAKUNDI MAWILI KATIKA WAUMINI YANAPIGANA

**Aya 9 – 10**

### MAANA

Na ikiwa makundi mawili katika waumini yanapigana, basi yapatanisheni.

Uaislamu una mafunzo na miongozo ya kujenga jamii na kuitengeneza; miongoni mwayo ni wajibu wa kumlinda binadamu damu yake, mali yake, hadhi yake na uhuru wake wa kusema na kutenda. Hakuna yeyote mwenye utawala wa hayo isipokuwa haki. Akitoka kwenye haki na akaingilia haki ya wengine, basi hapo atakuwa amejiondolea kinga ya hayo yeye mwenyewe. Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ ﴿٧٠﴾

“Na hakika tumewatukuza wanadamau.” Juz. 15 (17:70).

Amesema tena kumwambia Mtume wake:

لَّسْتَ عَلَيْهِم بِمُصَيْطِرٍ ﴿٢٢﴾

“Wewe si mwenye kuwatawalia” (88:22).

Akasema tena:

إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَظْلِمُونَ النَّاسَ وَيَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ ﴿٤٢﴾

“Bali njia ya lawama ipo kwa wale wanaowadhulumu watu, na wanafanya jeuri katika ardhi bila ya haki.” Juz. 25 (42:42).

Mafunzo mengine ya Uaislamu ni kuhurumiana na kusaidiana katika yale yaliyo na heri na masilahi kwa wote. Ikiwa itatokea uhasama baina ya makundi mawili ya waumini, basi wajibu wa waumini ni kusuluhisha kwenye misingi ya haki na uadilifu na kuchunga umoja usivunjike.

Kuna Hadith tukufu inayosema: “Je, niwaambie jambo lililo na daraja kubwa zaidi kuliko kufunga, kuswali na kutoa sadaka? Wakasema: Naam! Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Akasema: Ni kuwaunganisha waliotengana”

Na likiwa moja la hayo linadhulumu jingine, basi lipigeni linalodhulumu mpaka lirejee kwenye amri ya Mwenyezi Mungu.

Ikiwa kundi moja litakataa kurudi kwenye haki na likang’ang’ania uchokozi, basi ni juu ya waumini wengine kulihami na dhulma lile kundi linaloonewa, kwa hekima na mawaidha mazuri. Ikiwa lile kundi ovu halitakoma ila kwa vita, basi lipigeni katika mipaka ya sharia inayohakikisha amani ya wote.

Na likirejea basi yapatanisheni kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wanaohukumu kwa haki.

Likitubia lile kundi linaloonea na likaacha kabisa, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira mwenye kurehemu, na hakuna atakayeruhusiwa kulifanyia lolote. Lililobaki ni wajibu wa waumini, kwa juhudi zao waondoe, yaliyotokea kwenye nafsi za pande mbili.

Al-Jassas Al-Hanafi, anasema katika Kitabu Ahkamul-Qur’an akiwa anazungumzia Aya hii: “Ali Bin Abi Twalib alipigana na kundi ovu kwa upanga akiwa pamoja na maswahaba wakubwa wa Badr (Ahlu Badr) waliojulikana. Na alikuwa ni mwenye haki. Hakuna aliyehalifu katika kundi kabisa isipokuwa kundi ovu na wafuaisi wake aliokuwa akipigana nao.”

Na akasema Abu Bakr Al-Malik, Maaruf kwa jina la Ibn –Al-Arabi Al-Muafiri, katika Ahkamul - Qur’an: “Imethibiti kwa maulama wa Kiislamu na imethibiti kwa dalili ya dini kwamba Ali Bin Abu Twalib alikuwa Imam na kwamba kila mwenye kupigana naye ni muovu na kupambana na mtu huyo ni wajibu mpaka arudi kwenye haki.”

## UDUGU WA KIDINI NA UDUGU WA KIBINADAMU

Hakika Waumini tu ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mrehemewe.

Hii ni kusisitiza kuleta suluhu baina ya pande mbili zilzigombana, pamoja na kuashiria kuwa upatanishi huu ni lazima kwa mfungamano wa udugu. Kuna Hadith isemayo: mwislamu ni ndugu wa mwislamu, hamdhulumu, hamtelekezi wala hamtii aibu.

**Unaweza kuuliza:** Kwanini Mwenyezi Mungu (s.w.t) amesema: Hakika waumini tu ni ndugu, na asiseme: Hakika watu wote tu ni ndugu. Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** naye akasema:

"Mwislamu ni ndugu wa mwislamu." Na asiseme: Mtu ni ndugu wa mtu? Tunajua kuwa Mola ni mmoja, asili ni moja, umbile ni moja na usawa baina ya watu ni wajibu. Kwa hiyo upendo unatakikana uwe ni wa jumla sio mahsusi; sawa na rehe- ma ambayo imekienea kila kitu?

Basi mgawanyo huu utakuwa na tofauti gani na ule unaowagawanya binadamu kwa misingi ya kiuchumi; walivyofanya wamarksi, au kuwagawanya kwa misingi ya kijinsia; kama walivyofanya wanazi au kwa misingi ya vita na silaha kama ilivyo siasa ya kimarekani?

Kisha nini kilichosababisha matatizo na maangamizi haya yanayomkabili binadamu leo, hadi kufikia kumalizana, baada ya binadmu kuweza kumiliki nguvu mbaya ya silaha za maangamizi? Je, hii imesabishwa na binadamu kama binadamu au imesabishwa na aina kwa aina za migawanyo?

Hatimaye sasa binadamu wasaidiane kwa misingi ya dini au asasi za kibanadamu?

**Jibu**: Maswali yote haya ni haki, na jibu lake ni moja tu litakoloweza kutosheleza maswali yote haya; nalo ni: Kusaidiana ni wajibu baina ya binadamu wote bila ya kubagua. Huu ndio mwito wa uaislamu hasa, unaofahamishwa na makumi ya Aya na riwaya. Tutatosheka kutaja Aya moja na riwaya moja.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Aya ya 13 ya sura hii: "Enyi watu! Hakika Sisi tumewaumba kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumewafanya mataifa na makabila ili mjuane. Hakika mtukufu zaidi yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni aliye na takua zaidi yenu.

Kwa hiyo mwito wake Mwenyezi Mungu Mtukufu: 'Enyi watu!' pamoja na kusema kwake: 'Kutokana na mwanmmke na mwanamume' na 'aliye na takua zaidi' ni dalili mkataa na wazi kuwa mwito wa Qur'an ni wa kiutu na wa mataifa, unamzingatia mtu ni ndugu wa mtu kwa namna yoyote itakvyokuwa itikadi yake, utaifa wake na jinsia yake.

Mfano wa Aya hii na ufafanuzi wake ni kauli yake Mtume mtukufu **(s.a.w.w)**: "Watu wote wako sawa kama chane za shanuo. Jueni kuwa hakuna ubora wa mwarabu kwa mwajemi wala wa mwajemi kwa mwarabu, wala wa mwekundu kwa mweusi wala wa mweusi kwa mwekundu isipokuwa kwa takua … nyote mnatokana na Adamu na Adam ametokana na mchanga."

Zaidi ya hayo katika Juz.21 (30:30) kuna Aya inayosema kuwa uislamu ni dini ya maumbile na katika Juz. 9 (8:24) kuna Aya inayofahamisha kuwa dini ya Mwenyezi Mungu ni dini ya maisha.

Kwa hali hiyo basi inatubainikia kuwa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na sunna za Mtume wake zinazingatia kuamini utu ni sehemu inayokamilisha kumwamini Mwenyezi Mungu, mitume wake na Vitabu vyake.

Kwa hiyo Makusudio ya mumin katika Aya na mwislamu katika Hadith ni yule anayeamwamini Mwenyezi Mungu na mtu kwa kuwa ni mtu.

Kwa maneno mengine ni kuwa hakuna mzozo wala kupingana baina ya udugu wa kibinadamu na udugu wa kiislamu; huu wa kiislamu unauongeza nguvu ule wa kibinadamu.

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّن قَوْمٍ عَسَىٰ أَن يَكُونُوا خَيْرًا مِّنْهُمْ وَلَا نِسَاءٌ مِّن نِّسَاءٍ عَسَىٰ أَن يَكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ وَلَا تَلْمِزُوا أَنفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوا بِالْأَلْقَابِ بِئْسَ الِاسْمُ الْفُسُوقُ بَعْدَ الْإِيمَانِ وَمَن لَّمْ يَتُبْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿١١﴾

11. Enyi ambao mmeamini! Kaumu isidharau kaumu nyingine, huenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake kwa wanawake wengine, huenda wakawa bora kuliko wao. Wala msitiane kasoro, wala msiitane majina ya kejeli. Na wasiotubu, hao ndio madhalimu.

## KAUMU ISIDHARAU KAUMU NYINGINE

**Aya 11**

### MAANA

Enyi ambao mmeamini! Kaumu isidharau kaumu nyingine, huenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake kwa wanawake wengine, huenda wakawa bora kuliko wao.

Imesemekana kuwa neno Qawm, tulililofasiri kwa maana ya kaumu, kwa maana yake ya kiarabu huwa halitajwi ila kwa wanaume tu, kwa dalili ya kuunganishwa wanawake baada ya neno hilo.

Katika Juz. 19 (25:55-62) tulisema kuwa dhalimu kesho atachukuliwa na Mwenyezi Mungu kuwa ni kafiri ingawaje duniani anachukuliwa kuwa ni mwislamu kama akitamka shahada mbili.

Na mwenye kuwadharau wema atakuwa ni dhalimu na safihi.

Hili Mwenyezi Mungu amelikemea kwa ukali sana; kama aliposema:

فَيَسْخَرُونَ مِنْهُمْ سَخِرَ اللَّـهُ مِنْهُمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٩﴾

"…Wakawafanyia maskhara; Mwenyezi Mungu atawafanyia maskhara na wana wao adhabu iumizayo. " Juz. 10 (9:79).

Pia kauli yake:

إِنَّ الَّذِينَ أَجْرَمُوا كَانُوا مِنَ الَّذِينَ آمَنُوا يَضْحَكُونَ ﴿٢٩﴾ وَإِذَا مَرُّوا بِهِمْ يَتَغَامَزُونَ ﴿٣٠﴾ وَإِذَا انقَلَبُوا إِلَىٰ أَهْلِهِمُ انقَلَبُوا فَكِهِينَ ﴿٣١﴾ وَإِذَا رَأَوْهُمْ قَالُوا إِنَّ هَـٰؤُلَاءِ لَضَالُّونَ ﴿٣٢﴾ وَمَا أُرْسِلُوا عَلَيْهِمْ حَافِظِينَ ﴿٣٣﴾ فَالْيَوْمَ الَّذِينَ آمَنُوا مِنَ الْكُفَّارِ يَضْحَكُونَ ﴿٣٤﴾

"Hakika wale walio na hatia walikuwa wakiwacheka wale ambao wameamini. Wakiwapitia wanakonyezana na wakirudi kwa watu wao walirudi wakishangilia. Na wanapo waona husema: Hakika hawa ndio khasa walio potea. Na wao hawakutumwa wawe walinzi juu yao. Basi leo wale ambao wameamini wanawacheka makafiri" (83: 29-34).

Vile vile amesema:

وَيْلٌ لِّكُلِّ هُمَزَةٍ لُّمَزَةٍ ﴿١﴾

"Ole wake kila mtia kasoro mwenye kusengenya." (104:1).

## VIPI UTAPATA MARAFIKI?

Nimekumbuka, wakati nikifasiri Aya hii, kwamba kiasi cha mika 16 au zaidi iliyopita nilisoma tarjuma ya kitabu: How to win friends and influence people (vipi utapata marafiki na kuathiri nafsi) cha Dayl Karengi.

Vile vile nimekumbuka hekima ya hali ya juu ya Imam Zainul'abidin, inayohusiana na maudhui hii ambayo ina athari zaidi ya kitabu nilichokitaja pamoja na kuwa kimeenea sana na kufasiriwa kwenye lugha nyingi.

Imam, kwenye hekima yake, alikuwa akikusudia kauli yake Mwenyezi Mungu: "Kaumu isidharau kaumu nyingine, huenda wakawa bora kuliko wao." Hekima yenyewe ni hii:

**"Jihadhari na kuzungumza ambayo moyo unayakanya hata kama una udhuru. Kwani sio kila utakayemwambia shari unaweza kumfafanulia udhuru. Aliye mkubwa kuliko wewe muweke daraja ya mzazi, mdogo daraja ya mtoto, na aliye marika daraja ya kaka. Ni nani katika hawa unapenda kumvunjia heshima yake?**

**"Ikiwa shetani atakuingilia kujiona kuwa u mbora zaidi ya mwingine, angalia haya yafutayo: Ikiwa ni mkubwa zaidi yako, sema: amenitangulia kwa imani na matendo mema, kwa hiyo ni bora kuliko mimi. Ikiwa ni mdogo kuliko wewe, sema: nimemtangulia kwa maasi, kwa hiyo yeye ni bora kuliko mimi. Akiwa ni marika yako sema: mimi nina uhakika nimefanya dhambi, lakini nina shaka kuwa yeye amefanya dhambi, basi kwanini niache uhakika nichukue shaka?**

**"Ukiwaona watu wanakutukuza, sema: wamechukulia wema, na ikiwa wanakutenga, sema: kuna makosa nimefanya."**

Imam anaendelea kusema: **"Ukiyafanya haya maisha yako yatakuwa mepesi, utakuwa na marafiki wengi na utakuwa na maadui kidogo, na utafurahi kwa wema wao wala hutasikitika kukutenga."**

Vyovyote watavyosema maulama na wenye hekima kuhisiana na maudhui haya, hawatazidisha kitu kwenye hekima hii fasaha ya hali juu.

Hilo si ajabu kwa vile aliyeisema ni mtoto wa wahyi, hazina ya ilimu ya wahyi na aliyekulia kwenye malezi yake.

Wala msitiane kasoro.

Msitiane ila wala msiwambie wengine lile ambalo hampendi kuambiwa.

Wala msiitane majina ya kejeli.

Mtu asimwite mwenzake kwa jina analolichukia. Mafaqihi wamesema kuwa ikiwa jina halikukusudiwa kasoro wala dharau na ni mashuhuri wa hilo, basi halina ubaya; kama vile Hassan Madafu, n.k.

Ni uovu kutumia jina baya baada ya imani.

Hapa kuna tafsiri mbili: Ya kwanza ni msimwite mumin ewe kafiri! Ya pili, ni uovu huko kumwita mwingine kwa jina asilolipenda. Tafsiri hii ina ngvuvu, kwa wafasiri wengi kuliko ile ya kwanza.

Na wasiotubu, hao ndio madhalimu.

Mwenye kutubia ni kama asiye na dhambi na mwenye kung'ang'ania dhambi atakuwa ameidhulumu nafsi yake. Kwa sababu Mwenyezi Mungu atawaadhibu wenye dhambi.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اجْتَنِبُوا كَثِيرًا مِّنَ الظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ إِثْمٌ وَلَا تَجَسَّسُوا وَلَا يَغْتَب
بَّعْضُكُم بَعْضًا أَيُحِبُّ أَحَدُكُمْ أَن يَأْكُلَ لَحْمَ أَخِيهِ مَيْتًا فَكَرِهْتُمُوهُ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ تَوَّابٌ
رَّحِيمٌ ﴿١٢﴾

12. Enyi ambao mmeamini! Jiepusheni na dhana nyingi. Hakika baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipeleleze, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je, anapenda mmoja wenu kuila nyama ya nduguye aliyekufa? Mnalichukia hilo! Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu.

## DHANA, UJASUSI NA KUSENGENYA

**Aya 12**

### MAANA

Katika Aya iliyotangulia Mwenyezi Mungu (s.w.t) amekataza dharau, kutia ila, kubeza na kuitana majina ya kuchukiza. Na akamkemea mwenye kufanya moja katika hayo. Katika Aya hii anakataza dhana mbaya, ujasusi na kusengenya. Ufafanuzi ndio huu ufuatao:-

### DHANA

Enyi ambao mmeamini! Jiepusheni na dhana nyingi. Hakika baadhi ya dhana ni dhambi.

Sehemu hii ya Aya inawezekana kufanyiwa muhtasari kwa jumla moja tu: "Kila mtu hana hatia mpaka lithibitike kosa lake."

Inawezekana jumla hii kuifafanua kwa urefu, tuweke mpaka wa linalopelekea asili ya dhana, kuwa je, inafaa kuichulia dhana au kuna wajibu wa kujieupusha wakati wote au wakati wa kuweko udhuru na wa kutokuweko ilimu? Na je, kuna udhuru wa kutojua au hakuna?

Ikiwa inafaa kuichukulia dhana, je, tuichukulie dhana vyovyote ilivyo sababu yake na mfungamano wake? Na ikiwa haifai kuichukulia dhana kwa namna yote ile, je ni nyenzo gani za ilimu kwenye hukumu ya sharia na mengineyo katika ilimu ya usul (misingi ya sharia) ambayo tumeimalizia miaka si kidogo kuisoma?

Ni vizuri tuchuke tafsiri ya wastani si kurefusha wala kufupiliza. Kabla ya lolote ni lazima tufanye maandalizi ya kujua toafauti baina ya shaka, dhana na ilimu. Shaka ni kuwa sawa uthibitisho na ukanusho. Dhana ni kuwa na nguvu upande mmoja baina ya hizo mbili, lakini bado kunakuwa na uwezekano kwa upande ule usio na nguvu. Ilimu ni kubainika upande mmoja unaofunga kabisa njia ya upande mwingine.

Unaweza kumdhania mtu heri au shari, ukawa umepatia au umekosea katika dhana yako. Hakuna ubaya kabisa ikiwa utamdhania mwenzako heri, iwe umepatia au umekosea; au iwe litajitokeza hilo kwenye kauli yako na vitendo vyako au lisijitokeze.

Mtume mtukufu **(s.a.w.w)** anasema: **"Wadhanieni waumini heri."** Imam Ali (a.s) anasema: **"Liweke jambo la nduguyo kwenye heri."** Tazama Juz. 1 (2:83) kifungu cha 'Kuchukia usahihi.'

Kwa hiyo basi inatubainikia maana ya kuwa kwanini Mwenyezi Mungu (s.w.t) amesema: "Jiepusheni na dhana nyingi," na wala asisema 'jiepusheni na kila dhana.'

Neno wingi huwa pia linatumiwa kwa maana ya baadhi; na haya ndiyo Makusudio yake kwenye Aya hii; yaani jiepusheni na dhana mbaya.

Dhana mbaya yenyewe sio haramu ikiwa haitajitokeza kwenye kauli au kitendo, wala mwenye dhana hiyo hana majukumu yoyote. Lakini ni lazima asiitolee maamuzi yoyote na aifanye kama haiko. Akiitolea uamuzi na ikajitokeza athari yake kwenye kauli au kitendo, basi atawajibika na atastahili lawama na adhabu.

Hii ndio dhana aliyoikusudia Mwenyezi Mungu aliposema: "Hakika baadhi ya dhana ni dhambi."

Mtume mtukufu **(s.a.w.w)** anasema: **"Mambo matatu hasalimiki nayo yeyote: Kisirani, hasadi na dhana: Ukiona kisirani endelea, ukiona husda usiitake, na ukidhania hakikisha.** Kwa hiyo basi maana ni kuwa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: 'Jiepusheni na dhana nyingi' nikuwa msizitolee maamuzi wala msizitumie; sawa na kauli yake "Asiwafitini shetani."

### UJASUSI

Wala msipeleleze.

Kupeleleza ni kuchunguza siri na makosa kwa njia ya kujificha. Ni haramu kwa Kitabu, Sunna, Ijmai (kongamano la maulama) na kiakili. Na kauli yake:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَدْخُلُوا بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ حَتَّىٰ تَسْتَأْنِسُوا ... ﴿٢٧﴾ فَإِن لَّمْ تَجِدُوا فِيهَا أَحَدًا فَلَا تَدْخُلُوهَا حَتَّىٰ يُؤْذَنَ لَكُمْ... ﴿٢٨﴾

"Enyi ambao mmeamini! Msiingie nyumba zisizo nyumba zenu mpaka muombe ruhusa… na msipomkuta yeyote humo msiingie mpaka mpewe ruhusa." Juz. 18 (24:27-28).

Katika Sunna ni Hadith ya Mtume mtukufu **(s.a.w.w)**: **"Mwenye kukuchungulia ukamtupia kijiwe na ukamtoboa macho yake, basi huna lawama."** Mafaqihi wamekubaliana kwa pamoja kuitumia Hadith hii. Ama akili inauona ujajusi ni vita dhidi ya maisha ya watu na kuingilia uhuru wao na mambo yao yanayowahusu katika mila na desturi.

Nimekumbuka, wakati nikiandika maneno haya, makala ndefu kuhusu maudhui haya, iliyotolewa na gazeti Al-Ahram la 27-6-1969, nililisoma wakati huo, kisha nikalihifadhi katika mafaili ya magazeti. Nililihifadhi na kuliweka akiba ya kulitumia nikilihitajia. Basi nikalisoma tena, mara nikaona mambo ambayo hata kuyawaza tu ni muhali; baadhi yake ni haya yafuatayo:

"Wamarekani hivi sasa wanajua kuwa sio kuwa kuta zao zina masikio tu, bali zina macho na mboni vile vile, kama lilivyosema gazeti la Times. USA wametengeneza kifaa kidogo cha ukubwa wa milimita, kinachoweza kusajili mazungumzo; na mtu anaweza kukiweka kwenye jaketi kama kifungo. Kila mtu anaweza kukitumia na kinagharimu kati ya dola 10 na 15.

Huko New York, wafanyabiashara wameweka matangazo ya biashara kwenye magazeti kuuza vifaa vya kurikodi mazungumzo ya watu majumbani mwao na wanaviuza madukani kama michezo ya watoto. Bei yake haizidi dola 18.

Mtu akiweka kifaa hiki kwenye gari kikielekezwa kwenye jengo basi kitarikodi kila neno linalosemwa kwenye jengo lile. Bali kuna kifaa cha

kusikilizia maneno kisichozidi ukubwa wa punje ya choroko, kinachoweza kuwekwa kwenye kalamu nk, kinatumia betrii ya masaa 18 hadi 50.

Pia wametengeneza kifaa kidogo cha kutuma, kinachoweza kutangaza yanayopita kwenye majumba kwa umbali wa futi 50 na bei yake ni dola 400.

Ajabu ya yote ni kamera zinazopenya ukutani na kupiga picha mambo yote anayoyafanya mtu chooni na hata kwenye giza. Vile vile inawezekana kuchora chale (tattoo) katika mwili wa mtoto wakati anapozaliwa ambayo itafuatilia harakati zake katika maisha yake yote.

Kuna shirika katika Marekani yote linalokusanya habari na harakati binafsi za watu mashuhuri wa siasa, elimu, uandishi uchumi na wengineo na kurikodi maneno yao, na kupiga picha ya vitendo vyao, hata wanapofanya tendo la ndoa na wake zao na wengineo. Mtu anaweza kupata habari hizi kwa dola moja tu. Shirika hili linaitwa Benki ya habari.

Yote hayo yanatokea ikiwa serikali inajua kila kitu, bila ya kufanya lolote, kwa sababu imekuwa ni jambo la kawaida kama vile kuuza magazeti tu." Mwisho wa nukuu ya gazeti.

Haya ni machache katika mengi. Watunzi wameandika vitabu maalum kuhusiana na maudhui haya. Lau wamarekani wangeliyafanya haya kwao tu wenyewe kwa wenyewe, tungeliwaambia wao na wanowatawala: "shauri yenu, kila mji una uhuru wa kujichagulia unavyotaka." Lakini wamarekani wamevuka mipaka, wanafanya ujasusi kwenye nchi nyingine kwa ndege na satalaiti.

Usishangae msomaji. Marekani ni nchi ya maendeleo, demokarasia, bwana mkubwa wa uhuru, na polisi wa ulimwengu.

Tena zaidi ya hayo wanaamini Mwenyezi Mungu… Dalili kubwa kuwa wanamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho ni mauaji ya kinyama waliyoyafanya kwenye kijiji kimoja katika Vietnam ya kusini[1], na kuwasheheneza silaha za kisasa mayahudi ili kuwamaliza wananchi wa Palestina, kuwaua watoto kwa ujumla na kutupa mabomu kwa kutumi ndege za Phantoum kwa watoto wa shule wa Misr! Kweli kabisa USA ni dola kubwa kwenye uwanja huu wa mauaji!

### KUSENGENYA

Wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je, anapenda mmoja wenu kuila nyama ya nduguye aliye kufa? Mnalichukia hilo! Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu.

Kusengenya ni kumtaja mtu kwa jambo asilolipenda. Mtume mtukufu **(s.a.w.w)** anasema: **"Kusengenya ni kumtaja ndugu yako kwa jambo analolichukia. Ikiwa jambo hilo analo huko ni kusengenya na ikiwa hana itakuwa ni kumsingizia."** Na kusingizia ni kukubwa zaidi kuliko kusengenya na kumeharamishwa kwa Kitabu Sunna na Ijmai (kongamano la maulama).

1. Kijiji kisichokuwa na hatia kilichokuwa na wakazi 500, wengi wao wakiwa ni wazee, wanawake na watoto. Wanajeshi wa Mareknai waliwaua wote kwa unya- ma bila ya kubakia yoyote. Hatia hii ilifanyika mwezi wa tatu 1968.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemfananisha mwenye kusengenywa na maiti kwa vile anakuwa hayupo na akaifananisha hishima yake na nyama yake na kumtaja kwa uovu kuwa ndio kula.

Maana ya mnalichukia hilo ni kuwa ikiwa mnaona kinyaa kula nyama ya maiti basi pia muone kinyaa kumsengenya asiyekuwepo, kwa sababu yote mawili hayo yako sawa.

Hakuna jambo linalofahamisha kupungukiwa na udhalili kuliko kusengnya. Imam Ali (a.s) anasema: **"Kusengenya ni juhudi ya asiyejiweza."** Na Mwenyezi Mungu hasamehi kusengenya mpaka asamehe aliyesengenywa. Mafaqihi wameuvua uharamu wa kusengenya kwa wafuatao:-

Mpagani, hakimu dhalimu, mwenye kuudhihirisha ufuska wake, kwa sababu mwenye kulitupa joho la haya hana cha kuficha, kumpa ushauri mwenye kutaka ushauri katika kushirikiana na mtu au kumwakilisha kwenye jambo muhimu, kumtengua shahidi kwa kadhi, na mwenye kudhulumiwa kwa yule aliyemdhulumu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

لَّا يُحِبُّ اللَّـهُ الْجَهْرَ بِالسُّوءِ مِنَ الْقَوْلِ إِلَّا مَن ظُلِمَ ۚ وَكَانَ اللَّـهُ سَمِيعًا عَلِيمًا ﴿١٤٨﴾

"Hapendi Mwenyezi Mungu maneno ya kutangaza uovu ila kwa aliyedhulumiwa."

Juz. 6 (4:148).

Katika Kitabu Al-Makasib cha Sheikh Ansari, imesemwa kuwa sehemu zinazoondolewa uharamu wa kusengenya hazina idadi. Kwa sababu kusengenya kunakuwa haramu ikiwa kutangaza huko hakuna masilahi yenye nguvu. Vinginevyo, basi itakuwa wajibu kutangaza na kueneza kwa kuangalia masilahi yenye nguvu zaidi, kama ilivyo katika kila maasi ya haki za Mwenyezi Mungu na haki za binadamu.Tazama mwanzo wa Juz. 6.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُم مِّن ذَكَرٍ وَأُنثَىٰ وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا ۚ إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ اللَّـهِ أَتْقَاكُمْ ۚ إِنَّ اللَّـهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

13. Enyi watu! Hakika Sisi tumewaumba kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumewafanya mataifa na makabila ili mjuane. Hakika mtukufu zaidi yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni aliye na takua zaidi yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye habari.

قَالَتِ الْأَعْرَابُ آمَنَّا ۖ قُل لَّمْ تُؤْمِنُوا وَلَـٰكِن قُولُوا أَسْلَمْنَا وَلَمَّا يَدْخُلِ الْإِيمَانُ فِي قُلُوبِكُمْ ۖ وَإِن تُطِيعُوا اللَّـهَ وَرَسُولَهُ لَا يَلِتْكُم مِّنْ أَعْمَالِكُمْ شَيْئًا ۚ إِنَّ اللَّـهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٤﴾

14. Mabedui walisema: Tumeamini. Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu. Kwani imani haijaingia katika nyoyo zenu. Na mkimtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hatawapunguzia chochote katika vitendo vyenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّـهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا وَجَاهَدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّـهِ ۚ أُولَـٰئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ ﴿١٥﴾

15. Hakika Waumini ni wale tu waliomwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake tena wasiwe na shaka, na wakapigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Hao ndio wakweli.

قُلْ أَتُعَلِّمُونَ اللَّـهَ بِدِينِكُمْ وَاللَّـهُ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَ مَا فِي الْأَرْضِ وَاللَّـهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١٦﴾

16. Sema: Je, mnamjulisha Mwenyezi Mungu Dini yenu, na hali Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo mbinguni na katika ardhi, na Mwenyezi Mungu anajua kila kitu?

يَمُنُّونَ عَلَيْكَ أَنْ أَسْلَمُوا قُل لَّا تَمُنُّوا عَلَيَّ إِسْلَامَكُم بَلِ اللَّـهُ يَمُنُّ عَلَيْكُمْ أَنْ هَدَاكُمْ لِلْإِيمَانِ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٧﴾

17. Wanakusimbulia kuwa wamesilimu! Sema: Msinisimbulie kwa kusilimu kwenu. Bali Mwenyezi Mungu ndiye anayewasimbulia kwa kuwaongoza kwenye imani, ikiwa nyinyi ni wakweli.

إِنَّ اللَّـهَ يَعْلَمُ غَيْبَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاللَّـهُ بَصِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٨﴾

18. Hakika Mwenyezi Mungu anajua siri za mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayoyatenda.

## MTUKUFU ZAIDI YENU NI MWENYE TAKUA ZAIDI

**Aya 13 – 18**

### MAANA

Enyi watu! Hakika Sisi tumewaumba kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumewafanya mataifa na makabila ili mjuane. Hakika mtukufu zaidi yenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni aliye na takua zaidi yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye habari.

Watu wanajua kuwa baba yao ni Adam na mama yao ni Hawa, lakini lengo la kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Tuewaumba kutokana na mwanamume na mwanamke, ni kuwa watu wote wajue kwamba wao ni ndugu ni udugu wa usawa katika haki na wajibu.

Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu; "Ili mjuane," ni kuwa Makusudio ya kutofautiana kwenu katika miji, nasaba na rangi, sio kuwa muwe vikundi, mchinjane na mjifaharishe kwa mataifa yenu, baba zenu na jinsi zenu, hapana! Sivyo kabisa.

Lengo ni muhurumiane na msaidiane katika yale yaliyo na heri yenu na masilahi yenu. Na mbora kabisa atakuwa yule anayemuogopa Mwenyezi Mungu zaidi na akawanufaisha waja wake.

Aya hii ni mwito kutoka kwenye Qur'an kuwa watu wawe umma mmoja wa kiutu na ulimwengu mmoja unaokusanywa na uadilifu na upendo. Ulimwengu huu ni tegemeo la wenye fikra safi na ni ndoto ya walio wema.

Tuna uhakika kuwa makubaliano ya haki za binadamu, yatabakia kwenye karatasi na yatakuwa ni nadharia tu, ikiwa hautapatikana umoja wa ubinadamu uliotolewa mwito na Qur'an, zaidi ya mika 1300 liliyopita. Amerika na Israil zilitia saini makubaliano ya haki za binadamu, lakini bado ndio za kwanza kuangamiza watu Vietnam na Palestina.

Leo ninapoandika maneno haya 22 April 1970, kamati ya umoja wa mataifa imehakikisha kuwa Israil imevunja haki za binadamu, ikasema waziwazi kuwa Israil imevunja majumba ya wakazi ikaacha miili ya wanaume, wanawake na watoto kwenye kifusi na ikakataa isizikwe. Pia

imevunja sehemu takatifu na mahospitali[1] na kuwaadhibu wenyeji kwa umeme. Watu wazima wanawang'oa viungo, watoto wanawakata mikono na kupasua matumbo yao mbele ya baba zao na mama zao na mengineyo ya kinyama na mauji ya maangamizi.

Mabedui walisema: Tumeamini. Sema: Hamjaamini, lakini semeni: Tumesilimu. Kwani imani haijaingia katika nyoyo zenu. Na mkimtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hatawapunguzia chochote katika vitendo vyenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

Makusudio ya uaislamu hapa ni kutamka shahada mbili. Katika Juz. 1 (2:82), tumetaja tofauti baina ya mumin na mwislamu. Hapa tutamnukuu Dkt Twaha Hussein katika kitabu Mir'atul-islama (Kioo cha uaislamu).

Yeye ni mwanafasihi anayefahamika kwa siri za fasihi, ninamnukuu: "Wakati wa Mtume kulikuweko waumini na waislamu. Basi, niipi tofauti baina imani na Uislamu? Imani kwa dhahiri ya Aya hii ni jambo lilio moyoni ambalo mihimili yake ni ikhlasi kwa Mwenyezi Mungu na kusadikisha, kwa kina ndani ya dhamiri, kila aliloletewa wahyi Mtume.

Natija ya imani hii ni kumwitikia Mwenyezi Mungu na Mtume katika kila wanalolitolea mwito, bila ya kigugumizi, kugwazagwaza, wala kutaradadi, kwa hali yoyote ile itakavyokuwa; iwe kuna matukio au majanga. Mhimili mwingine wa imani hii ni kumwogopa Mwenyezi Mungu kiundani kabisa likitajwa jina lake na kumtegemea kwa undani zinaposomwa Aya zake.

"Ama Uislamu ni twaa ya dhahiri ya kutekeleza wajibu na kujiepusha na yaliyokatwaza; hata kama haitafikia imani ya kweli. Kuna watu wanaosilimu kuhofia ubaya; kama walivyosilimu makuraishi walioachwa bila ya kutekwa nyara siku ya kutekwa Makka. Wengine walasilimu kwa hofu na tamaa; kama walivyofanya mabedui aliowataja Mwenyezi Mungu katika Aya hii."

Hakika Waumini ni wale tu waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake tena wasiwe na shaka, na wakapigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Hao ndio wakweli.

Waumini wa kwelikweli kabisa ni wale wasiokuwa na shaka yoyote kwenye itikadi zao na wanaojitolea kihali na mali, kuihakikisha haki na kuibatilisha batili. Umetangulia mfano wake mara kadhaa; miongoni mwazo ni Juz. 10 (9:88).

Sema: Je, mnamjulisha Mwenyezi Mungu Dini yenu, na hali Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo mbinguni na katika ardhi, na Mwenyezi Mungu anajua kila kitu?

Mabedui walisema tumeamini, ndio Mwenyezi Mungu anawajibu, kuwa hivi mnamjulisha Mwenyezi Mungu imani yenu na hali Yeye anajua siri na yaliyofichika; kila kitu amekizunguka. Tena je imani inakuwa kwa kudai? Inatosha kuwa mtu ni mjinga kuwa hajui uweza wake Mwenyezi Mungu.

---

1. Na leo ninapofasiri maneno haya January 2009. Israil imeyarudia hayohayo huko Gaza. – Mtarjumu.

Wanakusimbulia kuwa wamesilimu! Sema: Msinisimbulie kwa kusilimu kwenu. Bali Mwenyezi Mungu ndiye anayewasimbulia kwa kuwaongoza kwenye imani, ikiwa nyinyi ni wakweli.

Makusudio ya kusimbulia kwake Mwenyezi Mungu ni kuwafanyia hisani, kwa sababu Yeye amekataza masimbulizi, na hawezi kukataza jambo kisha alifanye. Makusudio ya kuongoza kwake kwenye imani ni kutoa mwongozo wa haki na kuipendekeza.

Maana ni kuwa mabedui na walio mfano wao wanaona kuwa wamemfanyia hisani Mola wao na mtume wao kwa dini yao na wanataka walipwe; hali yakuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyewafanyia hisani wao, pale alipowaongoza kwenye haki na kuwahimiza kupitia Mtume wake.

Kwa hiyo wao ndio wamshukuru kwa alivyowafanyia hisani na kuwaneemesha; sio wao wasimbulie na kutaka kulipwa; ikiwa kweli wameamini dini yao na wakafanya ikhlasi kwenye imani yao. Vinginevyo watakuwa wanastahili kutoka kwa Mwenyezi Mungu yale aliyowaandalia waongo na wahaini.

Hakika Mwenyezi Mungu anajua siri za mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayoyatenda.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anajua imani ya kweli na ya uwongo na kuzipamabanua amali zilizokusudiwa dunia na zile zilizokusudiwa radhi ya Mwenyezi Mungu. Aina zote za amali pamoja na imani au kufuru ndio kipimo cha uadilifu wa hisabu na malipo.

## MWISHO WA SURA YA ARUBAINI NA TISA: SURAT AL-HUJURAT

12

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

Sura Ya Hamsini: Surat Qaf. Imeshuka Makka. Ina Aya 45.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

ق ۚ وَالْقُرْآنِ الْمَجِيدِ ﴿١﴾

1. Qaf. Naapa kwa Qur'an tukufu!

بَلْ عَجِبُوا أَن جَاءَهُم مُّنذِرٌ مِّنْهُمْ فَقَالَ الْكَافِرُونَ هَـٰذَا شَيْءٌ عَجِيبٌ ﴿٢﴾

2. Bali wanastaajabu kwamba amewafikia mwonyaji kutoka miongoni mwao, na wakasema makafiri: Hili ni jambo la ajabu!

أَإِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا ۖ ذَٰلِكَ رَجْعٌ بَعِيدٌ ﴿٣﴾

3. Je, tukifa na tukawa udongo? Marejeo hayo ni ya mbali!

قَدْ عَلِمْنَا مَا تَنقُصُ الْأَرْضُ مِنْهُمْ ۖ وَعِندَنَا كِتَابٌ حَفِيظٌ ﴿٤﴾

4. Hakika tunajua kinachopunguzwa na ardhi kutokana nao. Na kwetu kipo Kitabu kinachohifadhi.

بَلْ كَذَّبُوا بِالْحَقِّ لَمَّا جَاءَهُمْ فَهُمْ فِي أَمْرٍ مَّرِيجٍ ﴿٥﴾

5. Lakini waliikadhibisha haki ilipowajia; kwa hivyo wamo katika mambo ya mkorogo.

أَفَلَمْ يَنظُرُوا إِلَى السَّمَاءِ فَوْقَهُمْ كَيْفَ بَنَيْنَاهَا وَزَيَّنَّاهَا وَمَا لَهَا مِن فُرُوجٍ ﴿٦﴾

6. Je, Hawaangalii mbingu zilizo juu yao! Vipi tulivyozijenga, na tukazipamba wala hazina nyufa.

وَالْأَرْضَ مَدَدْنَاهَا وَأَلْقَيْنَا فِيهَا رَوَاسِيَ وَأَنبَتْنَا فِيهَا مِن كُلِّ زَوْجٍ بَهِيجٍ ﴿٧﴾

7. Na ardhi tumeitandaza na tukaiwekea milima, na tukaiotesha mimea mizuri ya kila namna.

تَبْصِرَةً وَذِكْرَىٰ لِكُلِّ عَبْدٍ مُّنِيبٍ ﴿٨﴾

8. Yawe ni busara na ukumbusho kwa kila mja mwenye kuelekea.

وَنَزَّلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً مُّبَارَكًا فَأَنبَتْنَا بِهِ جَنَّاتٍ وَحَبَّ الْحَصِيدِ ﴿٩﴾

9. Na tumeteremsha kutoka mbinguni maji yaliyobarikiwa, na kwa hayo tukaotesha mabustani na nafaka za kuvunwa.

وَالنَّخْلَ بَاسِقَاتٍ لَّهَا طَلْعٌ نَّضِيدٌ ﴿١٠﴾

10. Na mitende mirefu yenye makole yaliyozaa kwa wingi.

رِّزْقًا لِّلْعِبَادِ ۖ وَأَحْيَيْنَا بِهِ بَلْدَةً مَّيْتًا ۚ كَذَٰلِكَ الْخُرُوجُ ﴿١١﴾

11. Ili iwe ni riziki kwa waja wangu. Na tukaifufua kwa maji nchi iliyokuwa imekufa. Kama hivyo ndivyo utakavyokuwa ufufuo.

## NAAPA KWA QUR'AN TUKUFU

**Aya 1 – 11**

### MAANA

Qaf.

Umetangulia mfano wake katika Juz. 1 (2:1).

Naapa kwa Qur'an tukufu!

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameapa kwa Qur'an kudhihirisha ukuu wake, na ameisifu ni tukufu kwa wingi wa manufaa na faida zake.

Bali wanastaajabu kwamba amewafikia mwonyaji kutoka miongoni mwao, na wakasema makafiri: Hili ni jambo la ajabu!

Ndio, ni ajabu katika mantiki ya wale wanaoona kila kitu ni mali, wala hawaoni ubora wowote isipokuwa benki na ardhi.

Umetangulia mfano wake katika Juz. 11(10:2). Juz. 23 (38:4-5).

Je, tukifa na tukawa udongo? Marejeo hayo ni ya mbali!

Walikana ufufuo kwa sababu wao wanashindwa kuuelewa. Sisi tunaamini kushindwa kwao kuuelewa, lakini je, kushindwa kwao kulitambua jambo, ni dalili ya kutokuweko?

Ni mwenye akili gani anayechukia kushindwa kwake kuelewa kitu kuwa hakipo?

Kutatizika kwao kulikotokana na kutojua huku, walikokubainisha kwa kusema: "Ni nani huyo atakayeihuisha mifupa nayo imemung'unyika? Mwenyezi Mungu naye akawajibu:

وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلْقَهُ ۖ قَالَ مَن يُحْيِي الْعِظَامَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٧٨﴾ قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٩﴾

"Sema: Ataihuisha aliyeiumba mara ya kwanza. Na Yeye ni Mjuzi wa kila kuumba."

Juz. (36:78-79).

Maana haya yamekaririka kwenye Aya kadhaa.

Hakika tunajua kinachopunguzwa na ardhi kutokana nao. Na kwetu kipo Kitabu kinachohifadhi.

Kitabu kinachohifadhi ni kinaya cha kuwa Yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu amekizunguka kila kitu kwa ujuzi. Aya hii ni jawabu la kutatizika kulikofanya wakanushe ufufuo. Ufafanuzi wake ni kuwa mwili wa mtu unaliwa na ardhi baada ya mauti na unakuwa chembechembe zinazotawanyika mashariki mwa ardhi na magharibi yake. Vipi zitakuswanywa na kurudishwa ulivyokuwa?

Ndio akajibu Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwamba Yeye anajua kwamba ardhi inakula mili ya wafu na kwamba inatawanyika mashariki mwa ardhi na magharibi yake, lakini pamoja na hayo Yeye anaweza kuikusanya na kuirudishia uhai wake.

### MWENYE KULA NA MWENYE KULIWA

Wanafalsafa na wanatheologia wanakuita kutatizika huku ni kutatizika kwa 'mlaji na mwenye kuliwa.' Mulla Sadra amekutaja katika Juzuu ya nne ya kitabu chake, Al-asfar akasema: "Wametoa hoja kuwa: Ikiwa mtu atamla mtu mwingine, sehemu zilizoziliwa zikirudishwa kwenye mwili wa aliyekula hazitakuwa ni za aliyeliwa, na hapo atakuwa aliyeliwa ama ataadhibiwa au ataneemeshwa kutegemea na aliyemla.

Hayo yamejibiwa katika vitabu vya theologia kwamba ufufuo utakuwa kwa viungo vyao vile vilivyoanza kuumbwa ambavyo ni viungo vya asili kwao; na Mwenyezi Mungu anafihifadhi wala havifanyi ni viungo vya mwingine."

Anaendelea kusema Mulla Sadra kwamba jawabu hili halitoshi. Ukweli ni kuwa kila linalowezekana kiakili na likafahamishwa na wahyi, ni wajibu kuliamini. Na ufufuo ni jambo linalowezekana kiakili na limethibiti kiwahyi. Kwa hiyo niwajibu kulisadiki na kuliamini. Ama wanafalsafa na watu wa mantiki sio maasumu.

Haya ndiyo aliyoyasema mwenye Al-asfar, nayo ndiyo tuliyoyategemea na kuyataja mara kdhaa huko nyuma. Masheikh wamejaribu kuthibitisha ufu- fuo wa kimwili kwa hukumu ya kiakili bila ya kuangalia wahyi, lakini hawakuzidisha ispokuwa uzito na kutatiza.

Lakini waliikadhibisha haki ilipowajia; kwa hivyo wamo katika mambo ya mkorogo.

Makusudio ya haki ni Qur'an. Mwenyezi Mungu ameita, mkorogo hali ya wale waliomwambia Mtume kuwa ni mwenda wazimu, mara ni mchawi, tena ni kuhawani na hata pia wakamwita mshairi. Huko ndikokukorogeka na kuchanganyikiwa hasa.

Je, Hawaangalii mbingu zilizo juu yao! Vipi tulivyozijenga, na tukazipamba wala hazina nyufa.

Makusudio ya kujenga hapa ni kuwa sayari za mbinguni zimepangiliwa kihekima katika kutengenezwa kwake, zimetulia kwenye nidhamu yake na zinakwenda kwa uhakika. Makusudio ya kuzipamba ni uzuri. Ama kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: 'Hazina nyufa' ni kuwa kila sayari katika sayari zake hakuna yenye kasoro; kama alivyosema:

... هَلْ تَرَىٰ مِن فُطُورٍ ﴿٣﴾

"Je, unaona kasoro?" (67:3).

Maana ni kuwa wakadhibishaji hawoni ufufuo kuwa jengo la sayari halifanani na jengo lolote la binadamu. Kwa sababu sayari kadiri itakavyokuwa kubwa, lakini inakuwa ni kitu kimoja kisichokuwa na maunganisho, lakini wajenzi huwa wanaweka tofali juu ya tofali jingine, kati yao kuna utengnisho na mistari, nao hawawezi kujenga jengo kubwa kama hilo la sayari.

Aya hii ni majibu wazi na hoja ya kumnyamzisha yule anayeiweka mbali na kuishangaa fikra ya ufufuo na kusema: "Je, tukifa na tukawa udongo? Marejeo hayo ni ya mbali!"

Majibu yenyewe ni kuwa yule ambaye ameumba sayari bila maunganisho hawezi kushindwa kumfufua mtu baada ya kufa kwake. Kwa sababu hili ni jepesi zaidi kuliko hilo:

لَخَلْقُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ ...﴿٥٧﴾

"Hakika umbo la mbingu na ardhi ni kubwa zaidi kuliko umbo la watu." Juz. 24 (40:57).

Na ardhi tumeitandaza na tukaiwekea milima, na tukaiotesha mimea mizuri ya kila namna.

Yaani tumeitandaza na tukaifanya iwe sawa kwa ajili ya binadamu, tukaweka humo milima ili isiyumbe na tukaotesha aina mbalimbali za mimea inayopendeza kuiona na yenye uzuri wa kuliwa.

Umetangulia mfano wake katika Aya kadhaa; miongoni mwazo ni: Juz.13 (13:3).

Yawe ni busara na ukumbusho kwa kila mja mwenye kuelekea.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameumba ulimwengu na yaliyomo ikiwemo nidhamu na mpangilio ili iwe ni ishara ya ukuu wake Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa mwenye busara na mazingatio. Hapo kuna ishara kuwa mfungamano wa mtu na ulimwengu anaoishi hauishii kwenye maada tu, bali ni kwa moyo pia.

Na tumeteremsha kutoka mbinguni maji yaliyobarikiwa, na kwa hayo tukaotesha mabustani na nafaka za kuvunwa. Na mitende mirefu yenye makole yaliyozaa kwa wingi.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameyaita maji yenye baraka, kwa vile hakuna uhai wa roho wala viwiliwili bila ya maji. Na ameiita mitende mirefu kuashiria kuwa wakati wa kuota mitende inakuwa midogo, kisha inakuwa kwa sababu ambazo Mwenyezi Mungu amezipa maumbile.

Imam Ali (a.s) anasema: **"Haikufahamisha dalili ila kwamba muumba wa chungu ndiye muumba wa mtende kwa umakini wa kukipangila kila kitu."** Yaani umakini wa mpangilio wa kutengenezwa chungu na mtende mkubwa unajulisha kuwa muumba ni mmoja.

Ili iwe ni riziki kwa waja wangu. Kwa vile hawawezi kujiruzuku wenyewe. Na tukaifufua kwa maji nchi iliyokuwa imekufa.

Hii ni mwanzo wa kusema Kama hivyo ndivyo utakavyokuwa ufufuo.

Kwa hiyo kufufua watu baada ya mauti ni sawa na kuufuua kwa maji mji uliokufa. Umetangulia mfano wake katika Aya kadhaa; kama vile Juz. 8 (7:57).

كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَأَصْحَابُ الرَّسِّ وَثَمُودُ ﴿١٢﴾

12. Walikadhibisha kabla yao kaumu ya Nuhu na watu wa Rassi na Thamudi.

وَعَادٌ وَفِرْعَوْنُ وَإِخْوَانُ لُوطٍ ﴿١٣﴾

13. Na A'di na Firauni na ndugu wa Lut.

وَأَصْحَابُ الْأَيْكَةِ وَقَوْمُ تُبَّعٍ ۚ كُلٌّ كَذَّبَ الرُّسُلَ فَحَقَّ وَعِيدِ ﴿١٤﴾

14. Na watu wa Machakani na watu wa Tubbaa'. Wote waliwakanusha Mitume, kwa hivyo kiaga kikathibitika juu yao.

أَفَعَيِينَا بِالْخَلْقِ الْأَوَّلِ ۚ بَلْ هُمْ فِي لَبْسٍ مِّنْ خَلْقٍ جَدِيدٍ ﴿١٥﴾

15. Kwani tulichokakwa kuumba kwa kwanza? Bali wao wamo katika shaka juu ya umbo jipya.

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ وَنَعْلَمُ مَا تُوَسْوِسُ بِهِ نَفْسُهُ ۖ وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ الْوَرِيدِ ﴿١٦﴾

16. Na hakika tumemuumba mtu, na tunayajua yanayoitia wasiwasi nafsi yake. Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingo.

إِذْ يَتَلَقَّى الْمُتَلَقِّيَانِ عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ الشِّمَالِ قَعِيدٌ ﴿١٧﴾

17. Wanapopokea wapokeaji wawili, walioko kuliani na kushotoni.

مَّا يَلْفِظُ مِن قَوْلٍ إِلَّا لَدَيْهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ ﴿١٨﴾

18. Hatamki neno ila karibu yake yupo mwangalizi tayari.

وَجَاءَتْ سَكْرَةُ الْمَوْتِ بِالْحَقِّ ۖ ذَٰلِكَ مَا كُنتَ مِنْهُ تَحِيدُ ﴿١٩﴾

19. Na uchungu wa mauti utamjia kwa haki. Hayo ndiyo uliyokuwa ukiyakimbia.

وَنُفِخَ فِي الصُّورِ ذَٰلِكَ يَوْمُ الْوَعِيدِ ﴿٢٠﴾

20. Na itapulizwa parapanda. Hiyo ndiyo Siku ya Miadi.

وَجَاءَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّعَهَا سَائِقٌ وَشَهِيدٌ ﴿٢١﴾

21. Na itakuja kila nafsi pamoja na na mpelekaji na shahidi.

لَّقَدْ كُنتَ فِي غَفْلَةٍ مِّنْ هَـٰذَا فَكَشَفْنَا عَنكَ غِطَاءَكَ فَبَصَرُكَ الْيَوْمَ حَدِيدٌ ﴿٢٢﴾

22. Kwa hakika ulikuwa umeghafilika na haya; basi leo tumekuondolea pazia lako, kwa hivyo kuona kwako leo ni kukali.

## KWANI TULICHOKA KWA KUUMBA KWA KWANZA?

**Aya 12 – 22**

### MAANA

Walikadhibisha kabla yao yaani kabla ya Muhammad **(s.a.w.w)** kaumu ya Nuh

Kimetangulia kisa cha Nuh katika Juz. 12 (11:27-31).

Na watu wa Rassi.

Rassi ni kisima. Imetangulia ishara yao katika Juz. 19 (25:30-40).

Na Thamudi.

Hao ni watu wa Swaleh. Kisa chao kiko Juz. 12 (11:61-68).

Na A'di.

Hao ni watu wa Hud. Yametangulia masimulizi yao kwenye Juz. 12 (11:50-56).

Na Firauni.

Kisa chake pamoja na Musa na wana wa Israil, kimekaririka mara nyingi; miongoni mwazo ni Juz. 9 (7:103-112).

Na ndugu wa Lut.

Tazama Juz. 8 (7:80-84).

Na watu wa Machakani.

Imetangulia ishara yao katika Juz. 19 (26:176-191).

Na watu wa Tubbaa'.

Yametangulia maelezo yao katika Juz. 25 (45:37).

Wote waliwakanusha Mitume, kwa hivyo kiaga kikathibitika juu yao.

Hiyo ni adhabu ambayo Mwenyezi Mungu aliwaahidi kupitia Mitume wake.

Kwani tulichoka kwa kuumba kwa kwanza mpaka tuchoke na kuumba kwa pili?

"Kama tulivyoanza umbo la kwanza, tutalirudisha tena." Juz. 17 (21:104).

Bali wao wamo katika shaka juu ya umbo jipya.

Umbo jipya ni ufufuo. Shaka ni nzuri, bali wakati mwingine ni dharura, ikiwa ni ya kufanya utafiti na kuchunguza, lakini kukanusha bila ya dalili na kutia shaka tu, huo ni ujinga na upotevu.

Na hakika tumemuumba mtu, na tunayajua yanayoitia wasiwasi nafsi yake. Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingo.

Mwenyezi Mungu yuko karibu na kila kitu kwa kujua kwake, kwa sababu hakuna chochote ila kimetokana na Yeye. Kwa hiyo hakuna kitu kilicho mbali naye. Mwenyezi Mungu amehusisha kutaja mshipa wa shingo

kwa vile uko karibu na mtu kuliko kiungo chochote kingine; kuongezea kuwa ni mhimili wa maisha.

Wanapopokea wapokeaji wawili, walioko kuliani na kushotoni. Hatamki neno ila karibu yake yupo mwangalizi tayari.

Dhahiri ya Aya inaonyesha kuwa Mwenyezi Mungu anamwekea mtu waangalizi wawili; mmoja akiwa upande wa kulia na mwingine wa kushoto wakisajili kila analolitamka. Wafasiri wengi wamesema kuwa waangalizi hawa wawili ni malaika na kwamba yule wa kulia anaandika mema na yule wa kushoto maovu.

Pia inafaa kufasiri kuwa wawili hao ni kinaya cha kuwa mtu ataulizwa anayoyasema na anayoyafanya na kwamba yeye wakati wa hisabu hawezi kuficha au kupinga lolote katika uovu wake, kwa kuweko hoja juu yake.

Tumesema kuwa inafaa tafsiri hii kwa vile inaenda pamoja na ile ya kwanza inayofahamika kutokana dhahiri ya Aya, na natija zao ni moja.

**Unaweza kuuliza**: Mwenyezi Mungu kwa ilimu yake hana haja ya waangalizi na waaandishi. Sasa kuna Makusudio gani ya kuwaweka waangalizi?

**Jibu**: Makusudio ni kuwakabili Mwenyezi Mungu wakosefu kwa lile ambalo hawatakuwa ni hila wala njia ya kulikana. Na kwa mbali Aya inaashiria kuwa haifai kwa kadhi kuhukumu kwa kulijua kwake jambo. Tazama Juz. 24 (41:20).

Na uchungu wa mauti utamjia kwa haki. Hayo ndiyo uliyokuwa ukiyakimbia.

Uchungu wa mauti ni uchungu wa kutoka roho. Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu ‘kwa haki,’ inaashiria kuwa wakati wa kufa, uhakika utamfunukia yule mwenye kukata roho na atajua kwa uhakika kwamba ufufuo ni kweli isiyo na shaka. Neno ‘hayo’ ni ishara ya hayo ya kufufuliwa. Maneno hapa yanelekezwa kwa yule anayekana ufufuo. Makusudio ya kukimbia ni kukana.

Maana ni kuwa ataambiwa yule anayekana ufufuo wakati anapokata roho: huu ndio ufufuo uliokuwa ukiukana. Mfano wake ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿هَٰذَا يَوْمُ الْفَصْلِ الَّذِي كُنتُم بِهِ تُكَذِّبُونَ ﴿٢١﴾

“Hii ndiyo Siku ya upambanuzi mliyokuwa mkiikadhibisha.” Juz. 23 (37:21).

Na itapulizwa parapanda. Hiyo ndiyo Siku ya Miadi.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anaashiria Kiyama:

﴿وَنُفِخَ فِي الصُّورِ فَإِذَا هُم مِّنَ الْأَجْدَاثِ إِلَىٰ رَبِّهِمْ يَنسِلُونَ ﴿٥١﴾

“Na itapulizwa parapanda mara watatoka makaburini wakikimbila kwa Mola wao.”

Juz. 23 (36:51).

Na itakuja kila nafsi pamoja na na mpelekaji na shahidi.

Mpelekaji ni wakuipeleka kwenye mkusanyiko na shahidi ni yule atakayeshuhudia matendo yake.

Kwa hakika ulikuwa umeghafilika na haya; basi leo tumekuondolea pazia lako, kwa hivyo kuona kwako leo ni kukali.

‘Haya,’ ni haya ya hisabu na malipo. Ama kuona kukali makusudio yake ni kuwa uhakika, kwa anayekana ufufuo, utajitokeza wakati wa kufa na baadae; atajua aliyoyakana na atayakana aliyoyajua.

Maana ni kuwa kesho ataambiwa mkanushaji: Ewe muovu! Uliikana siku hii ya leo na ukafuata hawa yako, ukaghafilika na uliyokusudiwa. Basi batili imekuondokea leo, umejua uhakika, lakini ni wakati ambao hakuna kimbilio la kujiepusha na kuungua.

13

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

وَقَالَ قَرِينُهُ هَـٰذَا مَا لَدَيَّ عَتِيدٌ ﴿٢٣﴾

23. Na mwenzake atasema: Haya ndiyo yaliyo tayari kwangu.

أَلْقِيَا فِي جَهَنَّمَ كُلَّ كَفَّارٍ عَنِيدٍ ﴿٢٤﴾

24. Mtupeni katika Jahannamu kila kafiri mwenye inadi.

مَّنَّاعٍ لِّلْخَيْرِ مُعْتَدٍ مُّرِيبٍ ﴿٢٥﴾

25. Azuiaye heri, arukaye mipaka, mwenye kutia shaka.

الَّذِي جَعَلَ مَعَ اللَّـهِ إِلَـٰهًا آخَرَ فَأَلْقِيَاهُ فِي الْعَذَابِ الشَّدِيدِ ﴿٢٦﴾

26. Ambaye amemfanya mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu. Basi mtupeni katika adhabu kali.

قَالَ قَرِينُهُ رَبَّنَا مَا أَطْغَيْتُهُ وَلَـٰكِن كَانَ فِي ضَلَالٍ بَعِيدٍ ﴿٢٧﴾

27. Mwenzake aseme: Ee Mola wetu! Sikumpoteza mimi, bali yeye mwenyewe alikuwa katika upotevu wa mbali.

قَالَ لَا تَخْتَصِمُوا لَدَيَّ وَقَدْ قَدَّمْتُ إِلَيْكُم بِالْوَعِيدِ ﴿٢٨﴾

28. Aseme: Msigombane mbele yangu. Nilikwishawatangulizia kiaga changu.

مَا يُبَدَّلُ الْقَوْلُ لَدَيَّ وَمَا أَنَا بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٢٩﴾

29. Kwangu haibadilishwi kauli, wala Mimi siwadhulumu waja.

يَوْمَ نَقُولُ لِجَهَنَّمَ هَلِ امْتَلَأْتِ وَتَقُولُ هَلْ مِن مَّزِيدٍ ﴿٣٠﴾

30. Siku tutapoiambia Jahannamu: Je, umejaa? Nayo iseme Je, kuna ziada?

وَأُزْلِفَتِ الْجَنَّةُ لِلْمُتَّقِينَ غَيْرَ بَعِيدٍ ﴿٣١﴾

31. Na Pepo italetwa karibu kwa wenye takua, haitakuwa mbali.

هَـٰذَا مَا تُوعَدُونَ لِكُلِّ أَوَّابٍ حَفِيظٍ ﴿٣٢﴾

32. Haya ndiyo mnayoahidiwa. Kwa kila mwenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu ajilindae.

مَّنْ خَشِيَ الرَّحْمَـٰنَ بِالْغَيْبِ وَجَاءَ بِقَلْبٍ مُّنِيبٍ ﴿٣٣﴾

33. Mwenye kumwogopa Mwingi wa Rehema kwa ghaibu, na akaja kwa moyo ulioelekea.

ادْخُلُوهَا بِسَلَامٍ ۖ ذَٰلِكَ يَوْمُ الْخُلُودِ ﴿٣٤﴾

34. Ingieni kwa salama. Hiyo ndiyo siku ya daima.

لَهُم مَّا يَشَاءُونَ فِيهَا وَلَدَيْنَا مَزِيدٌ ﴿٣٥﴾

35. Humo watapata wakitakacho, na kwetu kuna ziada.

## ANAYEKATAZA HERI

**Aya 23 – 35**

**MAANA**

Na mwenzake atasema: Haya ndiyo yaliyo tayari kwangu.

Mwenzake ni yule aliyetajwa katika Aya ya 17- Malaika anayeandika matendo ya yule aliye naye. Maana ni kuwa. Mwandishi huyu atamwambia Mwenyezi Mungu (s.w.t):

Hiki kitabu cha yale uliyonituma. Ndani yake mna mambo yote vile yalivyokuwa: "Na kitabu kitawekwa ndipo utawaona waovu wakiogopa kwa sababu ya yale yaliyomo. Na watasema:

وَيَقُولُونَ يَا وَيْلَتَنَا مَالِ هَـٰذَا الْكِتَابِ لَا يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً إِلَّا أَحْصَاهَا ۚ وَوَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا ۗ وَلَا يَظْلِمُ رَبُّكَ أَحَدًا ﴿٤٩﴾

"Ole wetu! Kina nini kitabu hiki hakiachi dogo wala kubwa ila kinalihesabu? Na watakuta waliyoyafanya yamehudhurishwa. Na Mola wako hadhulumu yoyote." Juz. 15 (18:49).

Mtupeni katika Jahannamu kila kafiri mwenye inadi, Azuiaye heri, arukaye mipaka, mwenye kutia shaka, ambaye amemfanya mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu.

Katika Aya 21, Mwenyezi Mungu (s.w.t) amesema: "Na itakuja kila nafsi pamoja na mpelekaji na shahidi," na katika Aya tuliyo nayo, anasimulia kuwa atamwambia mpelekaji na shahidi, mchukue kwenye Jahannam aliyenishirikisha, akaikufuru haki na akaifanyia inadi, akaipinga heri na akawazulilia watu nayo.

Kisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) atarudia na kusisitiza: Basi mtupeni katika adhabu kali.

Ilivyo ni kuwa hapa Mwenyezi Mungu (s.w.t) amempa sifa ya mwenye kuzuia heri yule mwenye kuruka mipaka, anayetia shaka. Na mahali pengine amempa sifa ya mwenye dhambi:

مَّنَّاعٍ لِّلْخَيْرِ مُعْتَدٍ أَثِيمٍ ﴿١٢﴾

"Azuiaye heri arukaye mipaka, mwenye dhambi" (68:12).

Tukiunganisha Aya hizi na ile isemayo:

إِنَّ شَجَرَتَ الزَّقُّومِ ﴿٤٣﴾ طَعَامُ الْأَثِيمِ ﴿٤٤﴾ كَالْمُهْلِ يَغْلِي فِي الْبُطُونِ ﴿٤٥﴾ كَغَلْيِ الْحَمِيمِ ﴿٤٦﴾

"Hakika Mti wa Zaqqum, Ni chakula cha mwenye dhambi, kama mafuta mazito, hutokota matumboni kama kutokota kwa maji ya moto." Juz. 25 (44:43-46).

Tukiunganisha zote hizo inatubainikia kuwa kosa la kuzuia heri halina mfano na kosa lolote na kwamba adhabu yake haina kipimo.

Mwenzake aseme: Ee Mola wetu! Sikumpoteza mimi, bali yeye mwenyewe alikuwa katika upotevu wa mbali.

Mwenzake huyu sio yule mwenzake wa kwanza. Yule wa kwanza alikuwa ni katika waandishi wema, kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu: "Haya ndiyo yaliyo tayari kwangu."

Ama huyu rafiki wa pili ni katika maibilisi ambao Mwenyezi Mungu amewaashiria kwa kauli yake: "Anayeifanyia upofu dhikri ya Mwingi wa rehema tutamwekea Shetani kuwa ndiye rafiki yake." Juz. 25 (43:36).

Dalili ya kuwa marafiki ni tofauti ni kauli ya rafiki wa pili: "Sikumpoteza." Kwa sababu yule rafiki wa kwanza haiwezekani kupoteza, kwa hiyo hawezi kukana, kwa sababu Mwenyezi Mungu amemchagua kuandika kutokana na uaminifu wake.

Zaidi ya hayo ni kuwa kubishana kesho kutakuwa baina ya wakosefu, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Msigombane mbele yangu." Pia kauli yake: "Siku hiyo marafiki watakuwa maadui, wao kwa wao, isipokuwa wenye takua." Juz. 25 (43:67).

Aseme: Msigombane mbele yangu. Nilikwishawatangulizia kiaga changu.

Maneno yanatoka kwa Mwenyezi Mungu akiyaelekeza kwa mkosefu na rafiki yake shetani. Maana ni kuwa msianze kuambiana, wewe umenipoteza na mwingine naye aseme sikukupoteza. Kwani leo ni siku ya hisabu na malipo; wala mtu hatanufaika na maneno wala na mengine isipokuwa matendo mema tu; nami niliwawapa mwito wake na nikawahadharisha na siku ya leo kwa atakayehalifu, lakini mkakataa isipokuwa ukafiri.

Kwangu haibadilishwi kauli, wala Mimi siwadhulumu waja.

Makusudio ya kauli hapa ni amri yake Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa mpelekaji na shahidi: "Mtupeni katika Jahannam kila kafiri mwenye inadi."

Kutupwa huku kutakuwa tu na ni uadilifu. Kutakuwa, kwa vile ni amri yake Mwenyezi Mungu (s.w.t) wala hakuna mabadiliko katika amri yake. Ni uadilifu kwa sababu mkosefu anastahiki hivyo.

**Unaweza kuuliza**: maulama wengi wamesema kuwa inawezekana kwa Mwenyezi Mungu kuhalifu kiaga (ahadi ya kuadhibu), lakini haiwezekani kuhalifu ahadi; (ahadi ya mazuri) kama ilivyo katika Hadith, aliposema: **"Mwenye kumwahidi yoyote kumlipa uzuri, ni lazima atekeleze, na mwenye kumwahidi ubaya, basi ana hiyari."**

Zaidi ya hayo ni kuwa kiakili ni vizuri kutekeleza ahadi, lakini si vibaya kuhalifu kiaga. Sasa kuna wajihi gani wa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtufu: 'Kwangu haibadilishwi kauli?'

**Baadhi ya maulama wamejibu kuwa**: Mwenyezi Mungu hasamehi hivi hivi tu, bali ni kwa sababu. Pia kusamehe si kubadilisha kauli. Nasi tunaongezea kwenye jawabu hili kuwa makusudio ya kiaga hapa ni kiaga cha adhabu ya mwenye kuzuia heri, na sio kila kiaga. Kwa sababu mruka mipaka huyu mwenye dhambi, tunavyodhani, ni kuwa hana kafara wala muombezi mbele ya Mwenyezi Mungu.

Siku tutapoiambia Jahannamu: Je, umejaa? Nayo iseme Je, kuna ziada?

Hiki ni kinaya cha ukali wa muwako wake na ukali wa adhabu yake, na kwamba haiwi na msongomano wa wenye hatia kwa idadi yoyote watakayokuwa.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameipa Jahannam sifa kadhaa za kutisha zinazosisimua ngozi za wale wanaomwogopa Mola wao. Ama wale walio na maradhi nyoyoni mwao, wanadharau sifa hizo na wale wanaoziamini.

Na Pepo italetwa karibu kwa wenye takua, haitakuwa mbali.

Hii ni njia ya Qur'an, inaunganisha malipo ya muovu na mwema. Huko ni shida na machungu na hapa ni raha na nema na Pepo. Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtufu: 'Haitakuwa mbali,' ni kutilia mkazo neno

kuletwa karibu.Makusudio ya kuletwa karibu Pepo kwa wenye takua ni kuwa ni yao na wao ni wa hiyo.

Haya ndiyo mnayoahidiwa.

Mlijua enyi wenye takua ahadi ya Mwenyezi Mungu naye ameitekeleza. Basi chukueni neema hii isiyokuwa na mpaka wa sifa wala kufikiwa na akili.

Kwa kila mwenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu ajilindae. Mwenye kumwogopa Mwingi wa Rehema kwa ghaibu, na akaja kwa moyo ulioelekea.

Sifa hizi nne ni alama za kujulisha mwenye takua: kuwa ni kutubia akijiweka mbali na maasi, kumhofia Mwenyezi Mungu na kudumu kumtii kwa kutumai thawabu zake, akiwa kwenye imani yake na ikhlasi yake kwenye njia moja; ni sawa awe mbele ya watu au akiwa mbali; kinyume na yule mwenye kujionyesha, mwenye ria.

Anakuwa mvivu akiwa peke yake na na anakuwa mchangamfu mbele ya watu. Huyo ndiye mwenye takua ambaye anamwelekea Mwenyezi Mungu kwa moyo ulio salama.

Kwa maneno mengine ya Imam akimsifu mwenye takua:

"Amemtii anayemwonogoza na akaijiepusha na anayempoteza; akapata njia salama kwa busara ya anayemuonyesha na kutii amri ya anayemwongoza. Akaharakisha kwenye uongofu kabla ya kufungwa milango yake na kuisha nyenzo zake."

Ingieni kwa salama. Hiyo ndiyo siku ya daima. Humo watapata wakitakacho, na kwetu kuna ziada.

Nyinyi wenye takua mtakuwa katika Pepo isiyokatika neema yake, hachoki mkazi wake, hazeeki anayedumu wala hakati tamaa mkazi wake. Mtapata zaidi ya manyoyatamani na kuyapendekeza.

Baada ya hayo, ni kuwa tofauti hii baina ya Pepo na Moto inafichua tofauti iliyopo baina ya wenye takua na wenye hatia na kwamba tofauti yao mbele ya Mwenyezi Mungu ni sawa na tofauti ya Pepo na Moto.

وَكَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُم مِّن قَرْنٍ هُمْ أَشَدُّ مِنْهُم بَطْشًا فَنَقَّبُوا فِي الْبِلَادِ هَلْ مِن مَّحِيصٍ ﴿٣٦﴾

36. Na karne ngapi tuliziangamiza kabla yao waliokuwa na nguvu zaidi kuliko wao. Nao walizunguka katika miji. Je, yako makimbilio?

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَذِكْرَىٰ لِمَن كَانَ لَهُ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ ﴿٣٧﴾

37. Hakika katika hayo kuna ukumbusho kwa mwenye moyo au akatega sikio naye ni shahidi.

وَلَقَدْ خَلَقْنَا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ وَمَا مَسَّنَا مِن لُّغُوبٍ ﴿٣٨﴾

38. Na hakika tumeziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yake katika siku sita; na wala haukutugusa uchovu.

فَاصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ الْغُرُوبِ ﴿٣٩﴾

39. Basi vumilia kwa hayo wasemayo na msabihi Mola wako kabla ya kuchomoza jua na kabla ya kuchwa.

وَمِنَ اللَّيْلِ فَسَبِّحْهُ وَأَدْبَارَ السُّجُودِ ﴿٤٠﴾

40. Na katika usiku msabihi na baada ya kusujudu.

وَاسْتَمِعْ يَوْمَ يُنَادِ الْمُنَادِ مِن مَّكَانٍ قَرِيبٍ ﴿٤١﴾

41. Na sikiliza siku ataponadi mwenye kunadi kutoka pahala karibu.

يَوْمَ يَسْمَعُونَ الصَّيْحَةَ بِالْحَقِّ ذَٰلِكَ يَوْمُ الْخُرُوجِ ﴿٤٢﴾

42. Siku watakaposikia ukelele wa haki. Hiyo ndiyo siku ya kutoka.

إِنَّا نَحْنُ نُحْيِي وَنُمِيتُ وَإِلَيْنَا الْمَصِيرُ ﴿٤٣﴾

43. Hakika Sisi tunahuisha na tunafisha, na kwetu Sisi ndio marejeo.

يَوْمَ تَشَقَّقُ الْأَرْضُ عَنْهُمْ سِرَاعًا ذَٰلِكَ حَشْرٌ عَلَيْنَا يَسِيرٌ ﴿٤٤﴾

44. Siku itapowapasukia ardhi mbio mbio! Mkusanyo huo kwetu ni mwepesi.

نَّحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَقُولُونَ وَمَا أَنتَ عَلَيْهِم بِجَبَّارٍ فَذَكِّرْ بِالْقُرْآنِ مَن يَخَافُ وَعِيدِ ﴿٤٥﴾

45. Sisi tunajua sana wayasemayo. Wala wewe si jabari juu yao. Basi mkumbushe kwa Qur'an anayeogopa kiaga.

## SIKU ATAKAPONADI MWENYE KUNADI

**Aya 36 – 45**

### MAANA

Na karne ngapi tuliziangamiza kabla yao waliokuwa na nguvu zaidi kuliko wao. Nao walizunguka katika miji. Je, yako makimbilio?

Karne ni watu wa zama moja. Maana ni kuwa katika zama zilizopita kulikuwa na uma nyingi zilizokuwa na maendeleo, nguvu na idadi ya watu wengi kuliko wale waliokukadhibisha wewe Muhammad! Pia walikuwa na mawasiliano na miji mingine. Lakini yote hayo hayakuwafaa waliposhukiwa na adhabu, wala hawakupata pa kuikimbia amri ya Mwenyezi Mungu. Je, watu wako hawaogopi kuwasibu yaliyowasibu waliopita?

Maana haya yamekaririka kwenye Aya nyingi; ikiwemo: Juz. 21 (30:9).

Hakika katika hayo kuna ukumbusho kwa mwenye moyo au akatega sikio naye ni shahidi.

Hayo ni hayo ya kukumbushwa maangamizi ya waliopita. Mwenye moyo ni moyo salama. Kutega sikio ni kusikiliza kwa makini. Shahidi ni yule aliyepo kimoyo na kiakili. Maana ni kuwa yale tuliyoyataja ya maangamizi ni mawaidha tosha kwa mwenye busara na akazingatia.

Na hakika tumeziumba mbingu na ardhi na vilivyomo kati yake katika siku sita; na wala haukutugusa uchovu

Siku sita ni kinaya cha mikupuo au maendeleo ya kugeuka ulimwengu kutoka hali moja hadi nyingine. Tazama Juz. 8 (7:54).

Basi vumilia kwa hayo wasemayo, ya ubatilifu na usafihi. Kwa sababu mwisho ni wa wenye kuvumilia uvumilivu wa kiungwana.

Na msabihi Mola wako kabla ya kuchomoza jua. Hiyo ni ishara ya swala ya Alfajiri. Na kabla ya kuchwa, ni swala ya adhuhuri na alasiri.

Na katika usiku msabihi, ni swala ya magharibi na isha. Umetangulia mfano wake katika Juz. 16 (20:130). Na baada ya kusujudu, ni ishara ya uradi baada ya swala na swala za sunna baada ya kumaliza za wajibu.

Na sikiliza siku ataponadi mwenye kunadi kutoka pahala karibu. Siku watakaposikia ukelele wa haki. Hiyo ndiyo siku ya kutoka.

Maneno yanaelekezwa kwa Mtume **(s.a.w.w)**. Siku atakayonadi, hapo kuna maneno ya kukadiriwa; yaani sikiliza masimulizi ya siku atakayonadi;

na wala sio kusikiliza mnadi. Makusudio ya mahala karibu ni kuwa huo mwito watausikia wote; kama kwamba mnadi yuko karibu nao, ingawaje ukelele unatoka mbinguni.

Hapa ndio inatubainikia njia ya kuchanganya na kuafikiana baina ya Aya hii na ile isemayo:

أُولَـٰئِكَ يُنَادَوْنَ مِن مَّكَانٍ بَعِيدٍ ﴿٤٤﴾

"Hao wanaitwa kutoka mahali mbali." Juz. 24 (41:44).

Maana ni kuwa, sikiza tunayokusimulia ewe Muhammad kuhusiana na ukulele wa ufufuo kwa ajili ya hisabu na malipo. Ukulele huu uko mbali, ukitokea mbinguni na uko karibu kwa kuwa unafika kwenye masikio yote, mpaka ya wafu, watatoka makaburini kama nzige waliotawanyika:

هُنَالِكَ تَبْلُو كُلُّ نَفْسٍ مَّا أَسْلَفَتْ ۚ وَرُدُّوا إِلَى اللَّـهِ مَوْلَاهُمُ الْحَقِّ ۖ وَضَلَّ عَنْهُم مَّا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٣٠﴾

"Huko kila nafsi itajua iliyoyatanguliza na watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa haki, na yote waliyokuwa wakiyazua yatawapotea." Juz. 11 (10:30)

Hakika Sisi tunahuisha na tunafisha, na kwetu Sisi ndio marejeo.

Uhai na mauti yako mikononi mwa Mwenyezi Mungu na kwake Yeye ndio marejeo ya viumbe. Umetangulia mfano wake mara nyingi; kama vile katika Juz. 11(10:56).

Siku itapowapasukia ardhi mbio mbio! Mkusanyo huo kwetu ni mwepesi.

Ardhi itawapasukia wa kwanza na wa mwisho, watoke makaburini mwao upesi upesi; wakiwa ni wengi kuliko chunguchungu na machanga. Atakayekuwa na hali nzuri kuliko wengine ni yule atakayepata mahali pa kuweka unyayo wake na pa kuvutia pumzi zake; kama alivyosema Imam Ali (a.s).

Sisi tunajua sana wayasemayo, ya kumkadhibisha Mtume na kukana ufufuo. Wala wewe si jabari juu yao, kuwalazimisha kumwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho. Wewe ni muonyaji tu.

Basi mkumbushe kwa Qur'an anayeogopa kiaga na yule asiyeogopa pia ili utoe hoja. Mwenyezi Mungu amemuhusisha kumtaja anayeogopa kwa kuashiria kuwa yeye ananufaika na ukumbusho zaidi kuliko asiyeogopa:

فَذَكِّرْ إِن نَّفَعَتِ الذِّكْرَىٰ ﴿٩﴾ سَيَذَّكَّرُ مَن يَخْشَىٰ ﴿١٠﴾ وَيَتَجَنَّبُهَا الْأَشْقَى ﴿١١﴾

"Kumbusha ikiwa kutafaa huko kukumbusha. Atakumbuka mwenye kucha na atajiepusha nako muovu." 87: (9-11).

Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: 'Atajiepusha nako muovu,' ni dalili mkataa kuwa amri ya kukumbusha ni ya ujumla, iwe kutafaa au hakutafaa.

**MWISHO WA SURA YA HAMSINI: SURAT QAF**

14

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

Sura Ya Hamsini na Moja: Surat Adh-Dhariyat. Imeshuka Makka. Ina Aya 60.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu

وَالذَّارِيَاتِ ذَرْوًا ﴿١﴾

1. Naapa kwa zinazotawanya sana.

فَالْحَامِلَاتِ وِقْرًا ﴿٢﴾

2. Na zinazobeba mizigo.

فَالْجَارِيَاتِ يُسْرًا ﴿٣﴾

3. Na zinazokwenda kwa wepesi.

فَالْمُقَسِّمَاتِ أَمْرًا ﴿٤﴾

4. Na zinazogawanya amri.

إِنَّمَا تُوعَدُونَ لَصَادِقٌ ﴿٥﴾

5. Hakika mnayoahidiwa bila ya shaka ni kweli.

وَإِنَّ الدِّينَ لَوَاقِعٌ ﴿٦﴾

6. Na kwa hakika dini bila ya shaka itatokea.

وَالسَّمَاءِ ذَاتِ الْحُبُكِ ﴿٧﴾

7. Naapa kwa mbingu zenye umbile zuri.

إِنَّكُمْ لَفِي قَوْلٍ مُّخْتَلِفٍ ﴿٨﴾

8. Hakika nyinyi bila ya shaka mko katika kauli inayokhitalifiana.

يُؤْفَكُ عَنْهُ مَنْ أُفِكَ ﴿٩﴾

9. Anageuzwa nayo mwenye kugeuzwa.

قُتِلَ الْخَرَّاصُونَ ﴿١٠﴾

10. Wazushi wameangamizwa.

الَّذِينَ هُمْ فِي غَمْرَةٍ سَاهُونَ ﴿١١﴾

11. Ambao wameghafilika katika ujinga.

يَسْأَلُونَ أَيَّانَ يَوْمُ الدِّينِ ﴿١٢﴾

12. Wanauliza: Ni lini hiyo siku ya malipo?

يَوْمَ هُمْ عَلَى النَّارِ يُفْتَنُونَ ﴿١٣﴾

13. Ni siku watakayojaribiwa Motoni.

ذُوقُوا فِتْنَتَكُمْ هَٰذَا الَّذِي كُنتُم بِهِ تَسْتَعْجِلُونَ ﴿١٤﴾

14. Onjeni fitna yenu! Haya ndiyo mliyo kuwa mkiyahimiza.

## NAAPA KWA ZINAZOTAWANYA

**Aya 1 – 14**

## MAANA

Naapa kwa zinazotawanya sana, na zinazobeba mizigo, na zinazokwenda kwa wepesi, na zinazogawanya amri.

Katika kufasiri sifa hizi nne kuna rai kadhaa: Kuna waliosema kuwa Makusudio ya zinazotawanya ni pepo, zinazobeba ni mawingu zinazokwenda kwa wepesi ni jahazi na zinazogawanya ni malaika.

Kauli yenye nguvu ni kuwa zote hizi ni sifa za pepo. Ndizo zinazotawanya kwa vile zinatawanya mchanga nk. Akitumia neno hilo, Mwenyezi Mungu Mtufu anasema:

... هَشِيمًا تَذْرُوهُ الرِّيَاحُ ...﴿٤٥﴾

"Majani makavu yaliyokatikakatika yanayopeperushwa na upepo." Juz. 15 (18:45).

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameapa kwa upepo kuashiria manufaa yake, pia kuwa Mwenyezi Mungu anaweza kuapa na kila anachokitaka katika viumbe vyake. Tazama Juz. 23 (37:1-10)

Sifa ya pili ni 'Na zinazobeba mizigo,' Makusudio yake hapa ni kuwa pepo zinabeba mzigo wa mawingu. Anasema Mwenyezi Mungu Mtufu:

سُقْنَاهُ لِبَلَدٍ مَّيِّتٍ ﴿٥٧﴾

"Tunayasukuma kwa ajili ya mji uliokufa." Juz. 8 (7:57).

Sifa ya tatu: 'Na zinazokwenda kwa wepesi,' ni kuwa pepo zinakwenda kwa wepesi zikiwa zinabeba mawingu. Sifa ya nne: 'Na zinazogawanya amri.' Pepo zinatawanya mvua katika ardhi; kama ilivyoelezwa kwenye Juz. 8 (7:57).

Hakika mnayoahidiwa bila ya shaka ni kweli, Na kwa hakika dini bila ya shaka itatokea.

Hili n jawabu la kiapo. Makusudio ya mnayoahidiwa ni uhai baada ya mauti. Na dini ni hisabu na malipo.Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu atawafufua tu walio makaburini, hilo halina shaka. Na kwamba Yeye atamlipa mtu kwa matendo yake. Yakiwa heri basi ni heri na yakiwa shari basi ni shari.

Naapa kwa mbingu zenye umbile zuri.

'Umbile zuri' tumelifasiri kutokana na neno la kiarabu 'Hubuk' ambalo wafasiri wamelitolea kauli nyingi. Lakini iliyo na nguvu ni hii tuliyoifasiri; kwa maana ya kuwa katika maumbile ya mbingu kuna mpangilio, nidhamu, uzuri na kupendeza.

Hakika nyinyi bila ya shaka mko katika kauli inayokhitalifiana.

Msemo unaelekezwa kwa wale wanaomkadhibisha Mtume **(s.a.w.w)** na kauli zao zote ni za mgongano, mkorogano, uwongo na njozi; kama vile kusema kuwa Mtume ni mshairi, mara mwendawazimu na mara nyingine ni mchawi. Na kuhusu Qur'an wakasema ni vigano vya watu wa kale au imetungwa na Muhammad **(s.a.w.w)** n.k.

Anageuzwa nayo mwenye kugeuzwa.

Yaani anageuzwa na dini na haki yule anayeigeuka kwa hawa na ujinga; mfano wake ni sawa na kauli: "Hapofuki na hilo ila kipofu."

Wazushi wameangamizwa.

Hao ni wale aliowabainisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa kusema:

Ambao wameghafilika katika ujinga.

Ujinga na upotevu umewavaa kuanzia kichwani hadi unyayoni, wakazipeleka dhana zao ovyoovyo na bila ya msingi wowote, kwenye ardhi na mbinguni na kwenye ufufuo na malipo. Wakasema kuwa Mwenyezi Mungu ana washirika katika mawe na ana mabinti katika Malaika na wengine aliozaa na majini. Ama ufufuo na hisabu kwao ni upotevu.

Wanauliza: Ni lini hiyo siku ya malipo?

Wenye dharau wanauliza, huo ufufuo utakuwa lini? Mwenyezi Mungu (s.w.t) naye anawajibu:

Ni siku watakayojaribiwa Motoni.

Ufufuo utakuwa siku watakayoonyeshwa moto na kuunguzwa humo. Husemwa kuwa kitu kimejaribiwa, ili kutoa kilichoghushiwa, kikiunguzwa motoni. Malaika wa Motoni watawaambia:

Onjeni fitna yenu! Haya ndiyo mliyokuwa mkiyahimiza.

Hii ndio adhabu mliyokuwa mkihimiza na kuifanyia dharau jana. Je, mmeionaje ladha yake?

إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿١٥﴾

15. Hakika wenye takua watakuwa katika mabustani na chemchem.

آخِذِينَ مَا آتَاهُمْ رَبُّهُمْ ۚ إِنَّهُمْ كَانُوا قَبْلَ ذَٰلِكَ مُحْسِنِينَ ﴿١٦﴾

16. Wakipokea aliyowapa Mola wao. Kwa hakika hao walikuwa kabla ya haya wakifanya mema.

كَانُوا قَلِيلًا مِّنَ اللَّيْلِ مَا يَهْجَعُونَ ﴿١٧﴾

17. Walikuwa wakilala kidogo tu usiku,

وَبِالْأَسْحَارِ هُمْ يَسْتَغْفِرُونَ ﴿١٨﴾

18. Na kabla ya alfajiri wakiomba maghufira.

وَفِي أَمْوَالِهِمْ حَقٌّ لِّلسَّائِلِ وَالْمَحْرُومِ ﴿١٩﴾

19. Na katika mali zao ipo haki ya mwenye kuomba na anayejizuia.

وَفِي الْأَرْضِ آيَاتٌ لِّلْمُوقِنِينَ ﴿٢٠﴾

20. Na katika ardhi zipo Ishara kwa wenye yakini

وَفِي أَنفُسِكُمْ ۚ أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴿٢١﴾

21. Na katika nafsi zenu, Je, hamwoni?

وَفِي السَّمَاءِ رِزْقُكُمْ وَمَا تُوعَدُونَ ﴿٢٢﴾

22. Na katika mbingu ziko riziki zenu na mliyoahidiwa.

فَوَرَبِّ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ إِنَّهُ لَحَقٌّ مِّثْلَ مَا أَنَّكُمْ تَنطِقُونَ ﴿٢٣﴾

23. Basi naapa kwa Mola wa mbingu na ardhi, hakika haya ni kweli kama ilivyo, kuwa nyinyi mnasema.

هَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ ضَيْفِ إِبْرَاهِيمَ الْمُكْرَمِينَ ﴿٢٤﴾

24. Je, imekufikia hadithi ya wageni wa Ibrahim wanaohishimiwa?

إِذْ دَخَلُوا عَلَيْهِ فَقَالُوا سَلَامًا ۖ قَالَ سَلَامٌ قَوْمٌ مُّنكَرُونَ ﴿٢٥﴾

25. Walipoingia kwake wakasema: Salam! Na yeye akasema: Salam! watu nisiowajua.

فَرَاغَ إِلَىٰ أَهْلِهِ فَجَاءَ بِعِجْلٍ سَمِينٍ ﴿٢٦﴾

26. Akaenda kwa ahali yake na akaja na ndama aliyenona.

فَقَرَّبَهُ إِلَيْهِمْ قَالَ أَلَا تَأْكُلُونَ ﴿٢٧﴾

27. Akawakaribisha, akasema: Mbona hamli?

فَأَوْجَسَ مِنْهُمْ خِيفَةً ۖ قَالُوا لَا تَخَفْ ۖ وَبَشَّرُوهُ بِغُلَامٍ عَلِيمٍ ﴿٢٨﴾

28. Akahisi kuwaogopa. Wakasema: Usiwe na khofu, na wakambashiria kupata kijana
mwenye ilimu.

فَأَقْبَلَتِ امْرَأَتُهُ فِي صَرَّةٍ فَصَكَّتْ وَجْهَهَا وَقَالَتْ عَجُوزٌ عَقِيمٌ ﴿٢٩﴾

29. Ndipo mkewe akawaelekea, na ukelele na akapiga uso wake, na kusema: kongwe tasa!

قَالُوا كَذَٰلِكِ قَالَ رَبُّكِ ۖ إِنَّهُ هُوَ الْحَكِيمُ الْعَلِيمُ ﴿٣٠﴾

30. Wakasema: Ndivyo vivyo hivyo alivyosema Mola wako. Hakika Yeye ni Mwenye hikima Mjuzi.

## HAKI YA MWENYE KUOMBA NA ASIYEOMBA

**Aya 15 – 30**

### MAANA

Hakika wenye takua watakuwa katika Mabustani na chemchem. Wakipokea aliyowapa Mola wao. Kwa hakika hao walikuwa kabla ya haya wakifanya mema.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anapokea kutoka kwa wema matendo yao; kama alivyosema:

وَيَأْخُذُ الصَّدَقَاتِ ﴿١٠٤﴾

"Na huzipokea sadaka." Juz. 11 (9:104).

Yaani anazikubali sadaka na kuzilipa. Vilevile watu wema watapokea thawabu walizopewa kwa shangwe na furaha. Kwa maneno mengine ni:

رَّضِيَ اللَّـهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١٩﴾

"Mwenyezi Mungu amewawia radhi na wao wamemwia radhi. Huko ndiko kufuzu kukubwa."
Juz. 7 (5:119).

Walikuwa wakilala kidogo tu usiku, na kabla ya alfajiri wakiomba maghufira.

Walikuwa wakilala usiku, lakini kidogo, na mara nyingi tahajudi yao inaungana na alfajiri, wakifanya tasbihi na istighifari.

Imam Ali (as) anasema katika wasifu wao: **"Ama wakati wa usiku wanatandika miguu yao wakisoma Qur'an kwa mpangilio… wakipitia Aya yenye shauku wanakuwa na tamaa nayo …. Na wakipitia yenye hofu wanaitegea masikio ya nyoyo zao wakidhani kuwa Jahannam inachachati- ka na kuunguruma ndani ya masikio yao; basi wao wanainama kwa migongo yao wakitandika chini mapaji ya nyuso zao, na viganja vyao na ncha za nyao zao (yaani wanasujudu) wakimtaka Mwenyezi Mungu azifungue shingo zao"**

Na katika mali zao ipo haki ya mwenye kuomba na anayejizuia.

Mwenye kuomba ni yule anayeomba watu sadaka, na anayejizuia ni fukara ambaye anajizuia kuomba watu. Huyu amesadikishwa na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtufu:

﴿يَحْسَبُهُمُ الْجَاهِلُ أَغْنِيَاءَ مِنَ التَّعَفُّفِ تَعْرِفُهُم بِسِيمَاهُمْ لَا يَسْأَلُونَ النَّاسَ إِلْحَافًا ﴿٢٧٣﴾

"Asiyewajua anawadhania kuwa ni matajiri kwa kujizuia. Utawafahamu kwa alama zao; hawaombi watu wakan'gan'gania." Juz. 3 (2:273).

Neno 'haki' linafahamisha kuwa fukara ni mshirika wa tajiri katika mali yake. Hilo tumelizungumzia kwa ufafanuzi zaidi katika kifungu cha Zaka kwenye Juz. 3 2: (272-274) na katika Juz. 4 (3: 180-182) kwenye kifungu: 'Matajiri ni mawakala sio wenyewe.'

## MWENYEZI MUNGU NA MAARIFA YA HISIA

Na katika ardhi zipo Ishara kwa wenye yakini na katika nafsi zenu, Je, hamwoni?

Mwenye kupeleleza kwenye viumbe vyote vilivyoko na akachunguza kwa makini, hana budi kujiuliza: ni nani aliyepangilia kwa mpangilio wa uten- genezaji huu? Hatapata jawabu la kukinaisha na tafsiri sahihi isipokuwa kuweko nguvu ya hali ya juu inayoongoza. Ikiwa hatakinai na jibu hili, basi hatapata mbele yake isipokuwa sadfa na umbile pofu. Hakuna mwenye shaka kuwa hii inazidisha ujinga na upofu. Wamaada wanasema kuwa hakuna njia ya maarifa isipokuwa hisia na majaribio.

Na Mwenyezi Mungu haingii kwenye hisia wala majaribio. Kwa hiyo kumwamini hakutegemei dalili, bali ni ujinga na upotevu.

**Tunajibu**: **Kwanza**: hatukubaliani kuwa sababu za maarifa zinakuwa tu kwenye hisia na majaribio; bali kuna maarifa ya kiakili yanayofikiwa kwa nguvu ya dhahania. Na mwenye kuiangusha akili na mazingatio na akakana hoja inayohusiana nayo, atakuwa ameukana utu kabisa. Kwa sababu hakuna utu bila ya akili inayokata.

Zaidi ya hayo ni kuwa mwenye kukana maaarifa ya akili atakuwa ameipinga nafsi yake yeye mwenyewe; kwa kuwa atakuwa ameyakana maarifa ya akili kwa akili, na akatoa dalili ya kutokuweko kitu kwa kuweko kwake.

**Pili**: Hata kama tungekubali kuwa hakuna njia ya maarifa isipokuwa hisia na majaribio, bado tunamthibitisha Mwenyezi Mungu kwa njia hiyo hiyo hasa. Kwamba yuko katika kila mashuhudio ya maumbile.

Ushuhuda huu umefikia ukomo wa uwazi na ufafanuzi na kutufikisha kwenye ilimu ya mwanzilishi, kwa kiasi cha kuangalia tu na kuchunguza bila ya kuhitajia mitambo wala ala zozote.

Lau kungekua kumjua Mwenyezi Mungu kunahitajia mitambo, basi kumwamini Mungu kungelikuwa kwa wataalamu peke yao, na isingelifaa kwa Mwenyezi Mungu kuwambia watu wote: "Enyi watu! Mcheni Mola wenu."

Inajulikana wazi kuwa yeye, ambaye imetukuka hekima yake, amewajibisha imani kwa waja wake wote, lakini baada ya kuwawekea dalili mkataa ya kuondoa udhuru wote wa kutokuweko kwake. Mwenyezi Mungu (s.w.t) amezisimamisha dalili hizi kutokana na maumbile ya kiakili na kwenye hisia vilevile kwa kutumia msingi wa kiakili unaosema: "Ushahidi ni wa mwenye kudai."

Sisi sio tuliojitungia maneno haya wala kukosa adabu; isipokuwa Yeye, ambaye imetukuka hikima yake, ndiye aliyesema:

سَنُرِيهِمْ آيَاتِنَا فِي الْآفَاقِ وَفِي أَنفُسِهِمْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُ الْحَقُّ ﴿٥٣﴾

"Tutawaonyesha Ishara zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli." Juz. 24 (41:53)

Mtu mwenyewe na vilivyo katika upeo ni katika vinavyoshudiwa na vinavyohisiwa vinavyofahamisha kuweko Mwenyezi Mungu. Na kwavyo inadhihiri haki isiyokuwa na shaka.

Mwenye kufuatilia Aya za Qur'an yenye hikima atajikuta yuko mbele ya idadi ya ishara hizi za kilimwengu zinazotoa mwito wa kumwamini Mwenyezi Mungu kwa njia ya maarifa ambayo ni matunda ya hisia na akili; miongoni mwayo ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtufu: "Je, hawatazami ufalme wa mbingu na ardhi na alivyoviumba Mwenyezi Mungu" Juz. 9 (7:185). Yaani vitu vinavyohisiwa na kuguswa.

Kumwamini Mwenyezi Mungu ni imani isiyoonwa na jicho wala kuguswa na mkono, lakini imani hii inalazimishwa na kuwekwa na vinavyoonwa na vinavyoguswa; sawa na anavyoamini daktari mjuzi kuwa kwenye mwili wa binadamu kuna ugonjwa fulani.

Na anaweza kugundua hivyo, kwa kiasi cha kumshika tu mgonjwa, bila ya kutumia darubini au kipimo chochote. Hakuna yeyote awe mumin au mlahidi ila atakuwa anaamini, kwa imani ya mkato, vitu vingi visivyoingia kwenye hisia.

Na katika mbingu ziko riziki zenu na mliyoahidiwa.

Yaani kuna sababu za riziki zenu; kama vile mvua n.k. Wakale walisema: "Lau si mbingu, watu wasingelibakia."

Wametofautiana katika tafsiri ya "mliyoahidiwa." Kuna aliyesema ni Pepo na Moto, mwingine akaseama ni heri na shari na wa tatu akasema ni riziki inayogawanywa.

Rai yetu ni kuwa Makusudio ya ya mliyoahidiwa ni sababu hasa za riziki, kwa dalili ya kuwa, Mwenyezi Mungu Mtufu, ameashiria kwenye Aya kwamba katika ardhi na katika nafsi zetu kuna ishara za kuhisiwa zinazoguswa, zinazomfahaisha Mwenyezi Mungu Mtufu na ukuu wake. Na kimsingi ni kuwa ishara za kuhisiwa katika mbingu zitakuwa ni mvua na sayari na wala sio Pepo, Moto nk.

Basi naapa kwa Mola wa mbingu na ardhi, hakika haya ni kweli kama ilivyo, kuwa nyinyi mnasema.

Razi amesema dhamiri inarudia kwenye Qur'an, kwa hiyo isemwe: 'Hakika hiyo ni kweli;' kama kwamba Mwenyezi Mungu amesema: Hakika Qur'an ni haki wameitamka malaika kama mnavyotamka nyinyi.

Hakuna mwenye shaka kuwa Qur'an ni haki isiyo na shaka na kwamba Jibril ameitamka pia, lakini kuanzia mwanzo wa sura hii hadi hapa tulipo bado haijatajwa Qur'an wala Malaika. Iiyotajwa ni siku ya malipo na hisabu katika Aya 12, kisha Mwenyezi Mungu akataja yaliyo katika ardhi na mbinguni kuwa ni dalili ya kuweko aliyeyaanzisha. Basi bora ni kuirudisha dhamiri kwenye yote haya.

Kwa hiyo basi Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameapa kwa utukufu wake kwamba Mwenyezi Mungu ni haki na ufufuo ni haki, wala haitakikani kutia shaka katika hayo, baada ya kusimama dalili; sawa na

inavyotakikana kwa mtu kutoyatilia shaka aliyoyatamka.
Kuna riwaya inayosema kuwa bedui mmoja aliposikia Aya hii, alisema: "Nani huyo aliyemkasirisha Mwenyezi Mungu Mtufu mpaka akalazimika kuapa?" Haya si mageni kwa ambaye amekulia katika umbile alilozaliwa nalo.

Kwa manasaba wa hayo ni kua watu wa lugha wanasema: matamshi ni aina mbili: ya nje ambayo ni kutamka na ya ndani ambayo ni kufikiria na kutambua. Watu wa mantiki wakasema katika kumwelezea mtu kuwa ni mnyama anayetamka; yaani anayefikiria. Decarte naye anasema: "Mimi ninafikiria, kwa hiyo nipo."

Misingi hii inakanusha shaka ya kuweko mwenye kufikiria, kwa sababu imetoka kwake hasa. Kwa hiyo tunaweza kufasiri kama ilivyokuwa nyinyi mnasema au kama ilivyokuwa nyinyi mnafikiria. Kwa sababu yote mawili, kutamka na kufikiria, yanakanusha shaka ya kuweko mwenye kutamka au kufikiria.

Je, imekufikia hadithi ya wageni wa Ibrahim wanaohishimiwa?

Neno wageni tumelifasiri kutokana na neno la kiarabu dhayf ambalo linatumika kwa mgeni mwanamume au mwanamke, mmoja au wengi.

Makusudio ya wageni wa Ibrahim ni malaika waliokuja kumpa bishara ya kumzaa Is-haq na kuangamizwa kaumu ya Lut. Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewapa sifa ya waheshimiwa kwa kuwa ni waheshimiwa kwake na kwa waja wake waumini.

Walipoingia kwake wakasema: Salam! Na yeye akasema: Salam! watu nisiowajua.

Walimwamkia naye akawarudishia, akasema watu hawa hatuwajui.

Akenda kwa ahali yake na akaja na ndama aliyenona.

Ibrahim alifanya haraka kwenda kwa familia yake, akawaamuru wawaandalie wageni ndama aliyenona. Basi ikawa kama alivyotaka, nyama ikaiva, akawakaribisha, akasema: "Mbona hamli? " Lakini waliendela kutokula, kwa vile wao si watu, hawali chakula.

Akahisi kuwaogopa. Wakasema: Usiwe na khofu, nao wakambashiria kupata kijana mwenye ilimu.

Walimjulisha jambo walilokuja nalo la kumpa habari njema ya kumzaa Is-haq. Ndipo mkewe Sara aliposikia bishara ya Is-haq akawaelekea, na ukelele wa mshangao na akapiga uso wake, kwa furaha na mshangao na kusema: Mimi ni kikongwe tasa! Nitazaa kweli?

Wakasema: Ndivyo vivyo hivyo alivyosema Mola wako. Hakika Yeye ni Mwenye hikima Mjuzi.

Mwenyezi Mungu anajua kuwa wewe ni kikongwe tena tasa, lakini hikima yake inataka kukutunuku mtoto pamoja na uzee wako. Mwenyezi Mungu akilitaka jambo ni kuliambia 'Kuwa na linakuwa.'

Tumefupisha tafsiri ya Aya hizi kwa vile ziko wazi na pia zimekwishatangulia katika Juz. 12 (11: 69-73) na katika Juz. 14 (15:51-56).

15

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

﴿قَالَ فَمَا خَطْبُكُمْ أَيُّهَا الْمُرْسَلُونَ ﴿٣١﴾

31. Akasema: "Basi makusudio yenu ni nini, enyi mliotumwa?

﴿قَالُوا إِنَّا أُرْسِلْنَا إِلَىٰ قَوْمٍ مُّجْرِمِينَ ﴿٣٢﴾

32. Wakasema: Hakika sisi tume tumwa kwa watu wakosefu.

﴿لِنُرْسِلَ عَلَيْهِمْ حِجَارَةً مِّن طِينٍ ﴿٣٣﴾

33. Tuwatupie mawe ya udongo,

﴿مُّسَوَّمَةً عِندَ رَبِّكَ لِلْمُسْرِفِينَ ﴿٣٤﴾

34. Yaliyotiwa alama kutoka kwa Mola wako kwa ajili ya wanaopituka mipaka.

﴿فَأَخْرَجْنَا مَن كَانَ فِيهَا مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٣٥﴾

35. Kwa hivyo tutawatoa katika hao wale walioamini.

﴿فَمَا وَجَدْنَا فِيهَا غَيْرَ بَيْتٍ مِّنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٣٦﴾

36. Lakini hatukupata humo ila nyumba moja tu yenye Waislamu!

﴿وَتَرَكْنَا فِيهَا آيَةً لِّلَّذِينَ يَخَافُونَ الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٣٧﴾

37. Na tukaacha humo Ishara kwa ajili ya wanaoiogopa adhabu chungu.

﴿وَفِي مُوسَىٰ إِذْ أَرْسَلْنَاهُ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ بِسُلْطَانٍ مُّبِينٍ ﴿٣٨﴾

38. Na katika Musa, tulipomtuma kwa Firauni na hoja wazi.

﴿فَتَوَلَّىٰ بِرُكْنِهِ وَقَالَ سَاحِرٌ أَوْ مَجْنُونٌ ﴿٣٩﴾

39. Lakini alipuuza kwa sababu ya nguvu zake na akasema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu!

﴿فَأَخَذْنَاهُ وَجُنُودَهُ فَنَبَذْنَاهُمْ فِي الْيَمِّ وَهُوَ مُلِيمٌ ﴿٤٠﴾

40. Basi tukamkamata yeye na majeshi yake na tukawatupa baharini, na yeye ndiye wa kulaumiwa.

﴿وَفِي عَادٍ إِذْ أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الرِّيحَ الْعَقِيمَ ﴿٤١﴾

41. Na katika A'di tulipowapelekea upepo wa kukata uzazi.

﴿مَا تَذَرُ مِن شَيْءٍ أَتَتْ عَلَيْهِ إِلَّا جَعَلَتْهُ كَالرَّمِيمِ ﴿٤٢﴾

42. Haukuacha chochote ulichokifikia ila ulikifanya kama unga.

﴿وَفِي ثَمُودَ إِذْ قِيلَ لَهُمْ تَمَتَّعُوا حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٤٣﴾

43. Na katika Thamudi walipoambiwa: Stareheni kwa muda mdogo tu.

﴿فَعَتَوْا عَنْ أَمْرِ رَبِّهِمْ فَأَخَذَتْهُمُ الصَّاعِقَةُ وَهُمْ يَنظُرُونَ ﴿٤٤﴾

44. Basi wakaasi amri ya Mola wao, mara kimondo kikawanyakua nao wanaona.

﴿فَمَا اسْتَطَاعُوا مِن قِيَامٍ وَمَا كَانُوا مُنتَصِرِينَ ﴿٤٥﴾

45. Basi hawakuweza kusimama wala hawakuwa wenye kujitetea.

وَقَوْمَ نُوحٍ مِّن قَبْلُ ۖ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَاسِقِينَ ﴿٤٦﴾

46. Na kaumu ya Nuh hapo mbele. Hakika hao walikuwa watu mafasiki.

## BASI MAKUSUDIO YENU NI NINI ENYI MLIOTUMWA?

**Aya 31 – 46**

### MAANA

Akasema: Basi makusudio yenu ni nini, enyi mliotumwa?

Ibrahim (a.s) anawauliza wageni wake baada ya kuwajua ni akina nani, kuwa je, wanakwenda wapi na wanataka nini?

Wakasema: Hakika sisi tumetumwa kwa watu wakosefu; yaani kaumu ya Lut. Walikuwa ni wakosefu waliopituka mipaka, kwani walikuwa wakiwaendea wanaume kwa matamanio badala ya wanawake.

Tuwatupie mawe ya udongo, yaliyotiwa alama kutoka kwa Mola wako kwa ajili ya wanaopituka mipaka.

Tutawaangamiza kwa mawe yaliyotiwa alama yanayotokana na udongo mkavu aliyoyaandaa Mwenyezi Mungu kwa wanaopituka mipaka katika ukafiri dhulma na ufisadi.

Kwa hivyo tutawatoa katika hao wale walioamini ili yasiwasibu yale yatakayowasibu waliopituka mipaka.

Lakini hatukupata humo ila nyumba moja tu yenye Waislamu! Hiyo ni nyumba ya Lut, ukimtoa mkewe aliyekuwa katika walioangamia.

Na tukaacha humo Ishara kwa ajili ya wanaoiogopa adhabu chungu.

Yaani humo mjini mwa watu wa Lut. Makusudio ya ishara ni athari zinazojulisha kuangamia kwao na adhabua yao, ili iwe ni funzo kwa mwenye kutaamali.

Umetangulia mfano wake katika Juz. 8 (7: 80-84) na Juz. 12 (11: 77-83).

Na katika habari za Musa, tulipomtuma kwa Firauni na hoja wazi.

Mwenyezi Mungu alimtuma Musa kwa Firauni akiwa na miujiza ya kutosheleza kumkemea Firauni na upotevu wake, Lakini alipuuza kwa sababu ya nguvu zake.

Alipuuza kwa kughurika na jeshi lake na utawala wake.

Na akasema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu!

Kwa nini Musa ni mchawi au mwendawazimu katika mantiki ya Musa? Ni kwa vile alimwambia wewe si Mungu wa kuabudiwa na akamhadharisha na dhulma na kupituka mipaka.

Basi tukamkamata yeye na majeshi yake na tukawatupa baharini, na yeye ndiye wa kulaumiwa.

Alipituka mipaka na akasema: Mimi ndiye Mola wenu mkubwa, ikawa mwisho wake ni kuangamia na kulaumiwa.

Katika ziada ya maneno ni kuwa huko nyuma tuliashiria sababu za kukaririka. Katika Juz. 16 (20:9-16), tulitaja sababu za kukaririka kisa cha Musa. Ama hapa tunasema: “Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi zaidi.”

Na katika habari za A’di tulipowapelekea upepo wa kukata uzazi.

Mwenyezi Mungu aliwaangamiza A’di na kaumu ya Hud kwa upepo unaovuma, unaobomoa kila kitu. Haukuacha chochote ulichokifikia ila ulikifanya kama unga. Kila unachokipitia unakivunja na kukipondaponda.

Kisa cha Hud na watu wake kimetangulia katika Juz. 8 (7:73-79) na Juz. 12 (11:50-60).

Na katika habari za Thamudi walipoambiwa: Stareheni kwa muda mdogo tu.

Thamud ni watu wa Swaleh. Aya hii inaashiria yaliyoelezwa katika Juz. 12 (11:65): “Basi (Swaleh) akasema: Stareheni katika mji wenu kwa siku tatu. Hiyo ni ahadi isiyokadhibishwa.”

Basi wakaasi amri ya Mola wao, mara kimondo kikawanyakua nao wanaona.

Walimwasi Mwenyezi Mungu na Mtume, ndio Mwenyezi Mungu (s.w.t.) akawateremshia adhabu kutoka mbinguni.

Walipoona zikipomoka nguvu zao, basi hawakuweza kusimama wala hawakuwa wenye kujitetea.

وَإِذَا أَرَادَ اللَّـهُ بِقَوْمٍ سُوءًا فَلَا مَرَدَّ لَهُ ۚ وَمَا لَهُم مِّن دُونِهِ مِن وَالٍ ﴿١١﴾

“Mwenyezi Mungu akiwatakia watu uovu hakuna cha kuwazuia wala hawana mlinzi yeyote badala yake.” Juz. 13 (13:11).

Kisa cha Swaleh kimetangulia katika Juz. 8 (7: 73 – 79) na katika Juz. 12 (11: 61-68).

Na kaumu ya Nuh hapo mbele Mwenyezi Mungu aliwaangamiza kwa dhambi zao.

Hakika hao walikuwa watu mafasiki wakifanya mambo ya kuangamiza na kuvunja miko ya haramu. Kimetangulia kisa cha Nuh, Juz. 8 (7: 59 – 64) Juz. 12 (11: 25-49).

وَالسَّمَاءَ بَنَيْنَاهَا بِأَيْدٍ وَإِنَّا لَمُوسِعُونَ ﴿٤٧﴾

47. Na mbingu tumezifanya kwa nguvu na uwezo na hakika Sisi bila ya shaka ndio wenye kutanua.

وَالْأَرْضَ فَرَشْنَاهَا فَنِعْمَ الْمَاهِدُونَ ﴿٤٨﴾

48. Na ardhi tumeitandaza; basi bora ya watandazaji ni sisi.

وَمِن كُلِّ شَيْءٍ خَلَقْنَا زَوْجَيْنِ لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٤٩﴾

49. Na katika kila kitu tumeumba dume na jike ili mzingatie.

فَفِرُّوا إِلَى اللَّـهِ ۖ إِنِّي لَكُم مِّنْهُ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٥٠﴾

50. Basi kimbilieni kwa Mwenyezi Mungu, hakika mimi ni mwonyaji kwenu wa kubainisha nitokae kwake.

وَلَا تَجْعَلُوا مَعَ اللَّـهِ إِلَـٰهًا آخَرَ ۖ إِنِّي لَكُم مِّنْهُ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٥١﴾

51. Wala msifanye kuwa kuna mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu. Hakika mimi ni mwonyaji kwenu wa kubainisha nitokaye kwake.

كَذَٰلِكَ مَا أَتَى الَّذِينَ مِن قَبْلِهِم مِّن رَّسُولٍ إِلَّا قَالُوا سَاحِرٌ أَوْ مَجْنُونٌ ﴿٥٢﴾

52. Basi ndio hivyo hivyo, hakuwajia kabla yao Mtume ila walisema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu.

أَتَوَاصَوْا بِهِ ۚ بَلْ هُمْ قَوْمٌ طَاغُونَ ﴿٥٣﴾

53. Je, wameusiana kwa haya? Bali hawa ni watu waasi.

فَتَوَلَّ عَنْهُمْ فَمَا أَنتَ بِمَلُومٍ ﴿٥٤﴾

54. Basi waachilie mbali, nawe hulaumiwi.

﴿وَذَكِّرْ فَإِنَّ الذِّكْرَىٰ تَنفَعُ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٥﴾

55. Na kumbusha, kwani ukumbusho huwafaa waumini.

﴿وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

56. Na sikuwaumba majini na watu ila waniabudu.

﴿مَا أُرِيدُ مِنْهُم مِّن رِّزْقٍ وَمَا أُرِيدُ أَن يُطْعِمُونِ ﴿٥٧﴾

57. Sitaki kwao riziki, wala sitaki wanilishe.

﴿إِنَّ اللَّـهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ ﴿٥٨﴾

58. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuruzuku, Mwenye nguvu, Madhubuti.

﴿فَإِنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذَنُوبًا مِّثْلَ ذَنُوبِ أَصْحَابِهِمْ فَلَا يَسْتَعْجِلُونِ ﴿٥٩﴾

59. Hakika waliodhulumu wana fungu lao la adhabu kama fungu la wenzao. Basi wasiniharakishe

﴿فَوَيْلٌ لِّلَّذِينَ كَفَرُوا مِن يَوْمِهِمُ الَّذِي يُوعَدُونَ ﴿٦٠﴾

60. Ole wao walioikanusha siku yao waliyoahidiwa.

## KILA KITU TUMEUMBA DUME NA JIKE

**Aya 47 – 60**

### MAANA

Na mbingu tumezifanya kwa nguvu na uwezo na hakika Sisi bila ya shaka ndio wenye kutanua.

Baadhi ya wafasiri wamesema kuwa Makusudio ya kutanua hapa ni kuwa Mwenyezi Mungu anaipanua riziki kwa viumbe wake kwa mvua.

Lakini maana yanayoafikiana na hali halisi na ufahamisho wa Aya, ni kuwa Makusudio ya ya mbingu ni kwa maana yake yaliyo dhahiri; kuwa ni anga pana iliyo na nyota n.k.

Na Makusudio ya kutanua ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) anaizidisha anga upana kila siku zinavyoendelea kupita.

Wataalamau wanasema kuwa anga inaendela kujivuta kadiri siku zinavyopita, na kwamba ukubwa wa anga ya ulimwengu hivi sasa ni mara kumi zaidi tangu ilipoanza kujivuta. Anasema Sir James Jeans:

"Umbali baina ya makundi ya nyota unafikia miaka milioni moja na nusu ya mwendo wa mwanga. Mwanga unakata masafa ya maili milioni 6 katika mwaka mmoja."

Anasema Camus kuwa imegundulika kutokana na vipimo vikubwa kwamba baina ya nyota kuna masafa ya uwazi yanayokadiriwa kufikia miaka milioni 5 ya mwaka, na kwamba kumehisabiwa makao ya nyota yanayofikia milioni moja, na kuna uwezekano kuwa kuna mkusanyiko mwingine wa makao ya nyota katika masafa yaliyo mbali zaidi. Hayo yanapatikana katika kitabu Attakamul fil Islam, (ukamilifu katika Uislamu) cha Ahmad Amin Al-iraqi Juz. 2 Uk. 67 chapa ya kwanza.

Sisi hatuna hamasa ya Qur'an kuafikiana na sayansi kutokana na hadhari tulizozieleza katika Juz. 1 (2: 2). Lakini hata hivyo hatuwezi kuepuka kusema kuwa Aya hii tukufu ni usadikisho wa ushahidi kuwa muujiza wa Muhammad bin Abdillah **(s.a.w.w)** ni wa pekee na wa milele kati ya miujiza

ya manabii wote na kwamba unazidi kuwa wazi zaidi kadiri sayansi inavyopiga hatua.

Na ardhi tumeitandaza; basi bora ya watandazaji ni sisi.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemwandalia mtu ardhi na akamkunjulia mkono wake humo ili ajenge na afanye mambo ya heri, sio shari na kubomoa. Amemwachia huru mkono wake ili afanye kazi na akampa masharti ya kuuzuia mkono huo dhidi ya ndugu yake binadamu, sio amrushie makombora na mabomu ya sumu kwenye shule za watoto, mahospitalini, na viwandani na kwa kila mwenye kuimba nyimbo ya uhuru na kukataa utumwa isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu tu peke yake.

Na katika kila kitu tumeumba dume na jike ili mzingatie.

Dhahiri ya Aya inafahamisha kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameumba kila jinsi ya kitu katika viumbe vyote mke na mume; iwe ni binadamu, mnyama, mmea au vitu vigumu, kama mawe n.k. Kwa sababu neno 'kila kitu' linaenea kwa vyote.

Hatujui kama wataalamu wameigundua hakika hii au bado wako njiani? Tuliyoyasoma kutoka kwa wataalamu kuhusiana na maudhui haya ni kuwa hakuna chembe yoyote ulimwenguni ila inakuwa imefaungana na kani mbili: chanya na hasi (positive na negative). Yaani nguvu mbili za mvutano. Sijui kama Aya inaafikiana na hali hiyo?

Basi kimbilieni kwa Mwenyezi Mungu, hakika mimi ni mwonyaji kwenu wa kubainisha nitokae kwake.

Kila mwenye kuuzuia mkono wake na kuwaudhi wengine, akasadikisha kauli yake, akaifanyia ikhlasi haki na uadilifu katika vitendo vyake, atakuwa amaeikimbia batili kuiendea haki, atake asitake, lakini muongo mwenye hiyana, huyo ni katika maadui wakubwa wa Mwenyezi Mungu; ajaposoma tahalili na takbiri, akaabudu na kutoa sadaka.

Wala msifanye kuwa kuna mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu. Hakika mimi ni mwonyaji kwenu wa kubainisha nitokaye kwake.

Kuna aina nyingi za shirki; miongini mwazo: ni kuabudu masanamu, kumnasibishia Mungu mtoto, kuwa kigeugeu katika dini na kuwatumikia maadui wa Mwenyezi Mungu na wa ubinadamu kwa kutumia jina la uislamu na kuleta masilahi ya waislamu.

Basi ndio hivyo hivyo, hakuwajia kabla yao Mtume ila walisema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu.

Wakadhibishaji walikwambia wewe, kama vile wa mwanzo walivyoaambia mitume wao.

Je, wameusiana kwa haya? Bali hawa ni watu waasi.

Ni ajabu kufanana wa mwanzo na wa mwisho katika kuwakadhibisha wenye haki na viongozi wema. Je, walikongamana na kuusiana hilo? Hapana hawakukongamana wala hawakuonana au kuungana. Lililowakusanya ni uadui wa batili dhidi ya haki na ujinga dhidi ya ilimu.

Basi waachilie mbali, nawe hulaumiwi.

Usujitoe roho na kufuru yao na uasi wao ewe Muhammad! Wewe hutaulizwa kuhusu dini yao wala kauli zao na vitendo vyao.

Na kumbusha, kwani ukumbusho huwafaa Waumini.

Umuhimu wako ewe Muhammad! Ni kufikisha Qur'an na kuwatolea mawaidha kwayo watu wote. Ikiwa hatanufaika na mawaidha mwenye

kung’ang’ania ukafiri na ufisadi, basi atanufaika nayo mwenye kuitafuta haki ili aiamani na kuitumia kwa mujibu wake.

Na sikuwaumba majini na watu ila waniabudu.

Maana ya kumwabudu Mwenyezi Mungu peke yake ni kuwa huru kwa kutomwabudu mtu, mali, cheo na matamanio yote, na kutonyenyekea isipokuwa kwa haki tu na uadlifu.

Vile vile, kumwabudu Mungu, kunamaanisha kufanya juhudi ya kuinusuru haki na watu wake na kufanya mambo kwa ajili ya dunia na Akhera. Hakuna anayetia shaka kwamba mwenye kufuata njia hii itampeleka kwenye nyumba ya amani.

Kwa hiyo basi lengo la kuumbwa majini na watu ni kuishi maisha mema ya milele katika nyumba ya Mwenyezi Mungu kwa sharti ya kujikomboa na aina zote za utumwa na kufanya mambo mema. Mwenye kupuuza na akazembea, asilaumu ila nafsi yake. Na Mola wako si mwenye kudhulumu waja.

Umetangulia mfano wake katika Juz. 21(31:33-34), kifungu cha: ‘Kwa nini Mungu akamuumba mtu?’

**Unaweza kuuliza**: Utafanya nini na Hadith Qudsi inayosema: “Nilikuwa hazina iliyojificha nikataka nijulikane, basi nikaumba viumbe wakanijua,” si inafahamisha wazi kuwa lengo la kuumbwa ni kumjua Mungu?

**Jibu**: Hadith hii inaafikiana kwa ukamilifu na tafsiri tuliyoitaja. Kwa sababu mwenye kumjua Mwenyezi Mungu kisawasawa, hatahitajia kuwaabudu watu, cheo au mali na atafanya kulinga na radhi ya Mwenyezi Mungu na Pepo yake.

Sitaki kwao riziki, wala sitaki wanilishe.

Ni kama Mwenyezi Mungu, aliyetukuka kabisa, anasema: Sikuwaumba viumbe ili niwatumie kwenye viwanda vyangu na mashamba yangu.

Wala si kwa kuwatuma sokoni kwenda kuniuzia bidhaa zangu; wala pia sikuwaumba kwa ajili ya kuwapiga vita wanaoshindana na mimi katika uporaji na ulanguzi.

Hapana! Mwenyezi Mungu ni mwenye kujitosha na walimwengu wote. Amewaumba ili tu wafanye amali kwa pamoja kwa ajili ya heri yao wote na wapigane jihadi na yule atayejaribu kuingilia uhuru wao, heshima yao na kupora mali zao, ardhi zao na majumba yao.

Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuruzuku, Mwenye nguvu, Madhubuti.

Maana ya kuwa Mwenyezi Mungu ni mwenye kuruzuku ni kuwa yeye aliye Mtukufu, amemuumbia mtu maisha na akampa nyenzo zitakazomwezesha kuvuna matunda kwa ajili ya maisha yake; kama vile akili, nguvu, usikizi na uoni, na akamwambia: shughulika kwa ajili ya dunia yako na Akhera yako, wala usifanye uchokozi, kwani Mwenyezi Mungu hapendi wachokozi.

Ni sawa na mtoto wako kama utampa mali na kumwambia: fanya biashara kwa ajili ya maisha yako na uwe mwaminifu katika muamala wako.

Hakika waliodhulumu wana fungu lao la adhabu kama fungu la wenzao.

Makusudio ya waliodhulumu hapa ni mataghuti ambao walimkadhibisha Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**. Maana ni kuwa fungu la adhabu ya hawa ni sawa na la uma zilizotangulia, walipowakadhibisha mitume wao

Basi wasiniharakishe adhabu ambayo itawshukia tu. Na leo iko karibu sana na kesho.

Ole wao walioikanusha siku yao waliyoahidiwa wanayoiharakisha. Mara ngapi mwenye kuliharakisha jambo, likija anapendelea lisingekuwa!

### MWISHO WA SURA YA HAMSINI NA MOJA: SURAT ADH-DHARIYAT

16

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

Sura Ya Hamsini Na Mbili: Surat At-Tur. Imeshuka Makka. Ina Aya 49.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

وَالطُّورِ ﴿١﴾

1. Naapa kwa Mlima,

وَكِتَابٍ مَّسْطُورٍ ﴿٢﴾

2. Na kitabu kilichoandikwa

فِي رَقٍّ مَّنشُورٍ ﴿٣﴾

3. Katika waraka wa ngozi iliyo kunjuliwa,

وَالْبَيْتِ الْمَعْمُورِ ﴿٤﴾

4. Na kwa Nyumba iliyojengwa,

وَالسَّقْفِ الْمَرْفُوعِ ﴿٥﴾

5. Na kwa sakafu iliyonyanyuliwa,

وَالْبَحْرِ الْمَسْجُورِ ﴿٦﴾

6. Na kwa bahari iliyojazwa.

إِنَّ عَذَابَ رَبِّكَ لَوَاقِعٌ ﴿٧﴾

7. Hakika adhabu ya Mola wako hapana shaka itatokea.

مَّا لَهُ مِن دَافِعٍ ﴿٨﴾

8. Hapana wa kuizuia.

يَوْمَ تَمُورُ السَّمَاءُ مَوْرًا ﴿٩﴾

9. Siku zitakapotikisika mbingu kwa mtikiso,

وَتَسِيرُ الْجِبَالُ سَيْرًا ﴿١٠﴾

10. Na milima iwe inakwenda kwa mwendo mkubwa.

فَوَيْلٌ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُكَذِّبِينَ ﴿١١﴾

11. Basi ole wao siku hiyo wanaokadhibisha,

الَّذِينَ هُمْ فِي خَوْضٍ يَلْعَبُونَ ﴿١٢﴾

12. Ambao wanacheza katika mambo ya upuuzi.

يَوْمَ يُدَعُّونَ إِلَىٰ نَارِ جَهَنَّمَ دَعًّا ﴿١٣﴾

13. Siku wataposukumwa kwenye Moto kwa msukumo wa nguvu.

هَٰذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنتُم بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿١٤﴾

14. Huu ndio ule Moto mliokuwa mkiukadhibisha!

أَفَسِحْرٌ هَٰذَا أَمْ أَنتُمْ لَا تُبْصِرُونَ ﴿١٥﴾

15. Je, huu ni uchawi, au hamuoni?

﴿اصْلَوْهَا فَاصْبِرُوا أَوْ لَا تَصْبِرُوا سَوَاءٌ عَلَيْكُمْ إِنَّمَا تُجْزَوْنَ مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾

16. Uingieni, mkistahamili au msistahamili - ni mamoja kwenu. Hakika mnalipwa kwa mliyokuwa mkiyatenda.

## NAAPA KWA MLIMA

**Aya 1 – 16**

### LUGHA

Anasema Fayruzi Abad katika Kamusi yake Al-Muhit: Neno Tur linatumika kwa maana ya uga wa nyumba, kila mlima na mlima ulio karibu na Ayla unaoitwa mlima Sinai. Pia hutumika kwa milima miwili, mmoja uko Qudus na mwingine ulioko Raasul-ayn. Vile vile mlima ulioko Tiberias.

### MAANA

Naapa kwa Mlima, na kitabu kilichoandikwa katika waraka wa ngozi iliyo kunjuliwa, na kwa Nyumba iliyojengwa, na kwa sakafu iliyonyanyuliwa, na kwa bahari iliyojazwa.

Mlima hapa ni ule mlima Sinai aliozungumza Mwenyezi Mungu na Musa. Pia Mwenyezi Mungu ameapa na mlima huu katika (95:2).

Makusudio ya kitabu chenye kuandikwa ni kila kitabu cha mbinguni. Kwa sababu neno kitabu hapa limekuja kwa kuenea kwenye jinsia yake (nakra). Kulihusisha neno hilo na kitabu maalum kutahitajia maunganishao. Kule kutajwa mlima sinai tu, hakutoshi kuwa makusuidio yawe ni Tawrat.

Makusudio ya kusema kilichoandikwa katika waraka, ni kuwa Mwenyezi Mungu hakuteremsha kitabu ila alikifanya kitumike mikononi mwa watu na kila mtu aweze kukifikia na kukijua kwa ukamilifu. Imam Aliy (a.s) anasema:

**"Nashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake aliyemtuma kwa dini liliyo mashuhuri na kitabu kilichoandikwa."**

Nyumba iliyojengwa ni Al-Kaa'ba. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ ﴿١٢٧﴾

"Na Ibrahim alipoinua misingi ya ile nyumba." Juz. 1 (2:127).

Sakafu iliyonyanyuliwa ni mbingu:

﴿وَجَعَلْنَا السَّمَاءَ سَقْفًا ﴿٣٢﴾

"Na tukaifanya mbingu kuwa sakafu." Juz. 17 (21:32).

Yani iko kama sakafu katika jicho la mwenye kutazama. Bahari iliyojazwa ni kujaa maji:

﴿وَإِذَا الْبِحَارُ سُجِّرَتْ ﴿٦﴾

"Na bahari zitakapojazwa." (81:6).

Mwenyezi Mungu ameapa na vitu hivi vitano kuashiria uweza wake. Tazama Juz. 23 (37:1) kifungu cha: 'Mwenyezi Mungu na kuapa na viumbe vyake.'

Hakika adhabu ya Mola wako hapana shaka itatokea kwa wakosefu. Jumla hii ni jawabu la kiapo. Hapana wa kuizuia; kama yalivyo mauti hakuna wa kuyarudisha ila yule mwenye kuleta uhai na mauti.

Siku zitakapotikisika mbingu kwa mtikiso.

Yaani kani mvutano itaondoka, uzani baina ya sayari utaharibika na kutokea mparaganyo utakaoenea.

Na milima iwe inakwenda kwa mwendo mkubwa. Itakapotikisika mbigu ardhi itatetemeka na milima itaondoka sehemu zake.

Aya mbili hizi zinaashiria kusimama kiyama na kuharibika ulimwengu, ambapo viumbe watakusnywa kwa ajili ya hisabu.

Basi ole wao siku hiyo wanaokadhibisha. Ambao wanacheza katika mambo ya upuuzi.

Waliichezea dunia nayo ikawachezea, lakini hawakuiweza, kwa hiyo ikawapiga mweleka na ikawapeleka haraka kwenye Jahannam ambayo ni makazi mabaya.

Siku wataposukumwa kwenye Moto kwa msukumo wa nguvu.

Watasukumwa kwa nguvu na Malaika wa adhabu watawaambia: Huu ndio ule Moto mlio kuwa mkiukadhibisha! "Ionjeni adhabu iunguzayo. Hayo ni kwa sababu ya yale yaliyokwishatangulizwa na mikono yenu. Na hakika Mwenyezi Mungu si mwenye kuwadhulumu waja." Juz. 10 (8:50-51).

Je, huu ni uchawi, au hamuoni.

Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** aliwahofisha na Moto wa Jahannam wakamwambia wewe ni mchawi. Siku ya malipo Mwenyezi Mungu (s.w.t) atawafanya ni kuni za Jahannam na awaambie, je mmeona sasa? Je, Muhammad ni mchawi? Je, adhabu ya kuungua ni uchawi? Uingieni, mkistahamili au msistahamili - ni mamoja kwenu, adhabu ni hiyo hiyo haipungui wala haiishi. Hakika mnalipwa kwa mliyokuwa mkiyatenda ya dhulma na ufisadi.

﴿إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَنَعِيمٍ ﴿١٧﴾

17. Hakika wenye takua watakua katika Mabustani na neema,

﴿فَاكِهِينَ بِمَا آتَاهُمْ رَبُّهُمْ وَوَقَاهُمْ رَبُّهُمْ عَذَابَ الْجَحِيمِ ﴿١٨﴾

18. Wakifurahi kwa yale aliyowapa Mola wao. Na Mola wao atawalinda na adhabu ya Motoni.

﴿كُلُوا وَاشْرَبُوا هَنِيئًا بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٩﴾

19. Kuleni na kunyweni kwa raha kwa sababu ya mliyokuwa mkiyatenda.

﴿مُتَّكِئِينَ عَلَىٰ سُرُرٍ مَّصْفُوفَةٍ ۖ وَزَوَّجْنَاهُم بِحُورٍ عِينٍ ﴿٢٠﴾

20. Wakiegema viti vya fahari vilivyopangwa safu. Na tutawaoza mahurulaini.

﴿وَالَّذِينَ آمَنُوا وَاتَّبَعَتْهُمْ ذُرِّيَّتُهُم بِإِيمَانٍ أَلْحَقْنَا بِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ وَمَا أَلَتْنَاهُم مِّنْ عَمَلِهِم مِّن شَيْءٍ ۚ كُلُّ امْرِئٍ بِمَا كَسَبَ رَهِينٌ ﴿٢١﴾

21. Na walioamini na dhuriya zao wakawafuata kwa Imani tutawakutanisha nao dhuriya zao, na wala hatutawapunja kitu katika vitendo vyao kila mtu ni rehani wa alichokichuma.

﴿وَأَمْدَدْنَاهُم بِفَاكِهَةٍ وَلَحْمٍ مِّمَّا يَشْتَهُونَ ﴿٢٢﴾

22. Na tutawapa matunda, na nyama kama watavyopenda.

﴿يَتَنَازَعُونَ فِيهَا كَأْسًا لَّا لَغْوٌ فِيهَا وَلَا تَأْثِيمٌ ﴿٢٣﴾

23. Watapeana humo bilauri zisio na (vinywaji) vya upuuzi wala dhambi.

﴿وَيَطُوفُ عَلَيْهِمْ غِلْمَانٌ لَّهُمْ كَأَنَّهُمْ لُؤْلُؤٌ مَّكْنُونٌ ﴿٢٤﴾

24. Na watawapitia watumishi wao kama kwamba ni lulu zilizofichwa.

﴿وَأَقْبَلَ بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ يَتَسَاءَلُونَ ﴿٢٥﴾

25. Wataelekeana wakiulizana.

﴿قَالُوا إِنَّا كُنَّا قَبْلُ فِي أَهْلِنَا مُشْفِقِينَ ﴿٢٦﴾

26. Waseme: Tulikuwa zamani pamoja na ahali zetu tukiogopa.

﴿فَمَنَّ اللَّـهُ عَلَيْنَا وَوَقَانَا عَذَابَ السَّمُومِ ﴿٢٧﴾

27. Basi MwenyeziMungu akatufanyia hisani na akatulinda na adhabu ya upepo wa Moto.

﴿إِنَّا كُنَّا مِن قَبْلُ نَدْعُوهُ إِنَّهُ هُوَ الْبَرُّ الرَّحِيمُ ﴿٢٨﴾

28. Hakika sisi zamani tulikuwa tukimwomba Yeye. Hakika Yeye ndiye Mwema Mwenye kurehemu.

## WATU WA PEPONI

**Aya 17 – 28**

### MAANA

Hakika wenye takua watakua katika Mabustani na neema, Wakifurahi kwa yale aliyowapa Mola wao. Na Mola wao atawalinda na adhabu ya Motoni.

Neno 'wakifurahia' tumelifasiri kutokana na neno fakihina ambalo pia lina maana ya kuwa njema nafsi. Maana zote mbili zinaendana na Pepo na neema. Lakini maana ya kufurahia inaafikiana zaidi na kauli yake Mwenyezi Mungu inayofuatia: Kuleni na kunyweni kwa raha.

Maana ni kuwa walimcha Mwenyezi Mungu duniani, naye amewakinga na adhabu ya Moto na amewafanyia Pepo kuwa ndio malipo yao.

Kuleni na kunyweni kwa raha kwa sababu ya mliyokuwa mkiyatenda.

Nyinyi wacha Mungu, mna haki zaidi ya neema hii, kwa sababu mlifanya kwa ikhlasi. Aya inafahamisha kuwa hakuna heshima yoyote mbele ya Mwenyezi Mungu kwa kiumbe isipokuwa kwa kufanya amali. Ama vyeo nasaba na mali si chochote, ila zikiwa ni nyenzo za heri na masilahi ya umma.

Wakiegema viti vya fahari vilivyopangwa safu.

Kuegema viti pamoja na kuwa faragha, kunafahamisha kutokuwa na matatizo ya maisha na tabu zake.

Na tutawaoza mahurulaini, wanovutia akili na macho kwa uzuri wao na ukamilifu wao. Neema iliyoje!

Na walioamini na dhuriya zao wakawafuata kwa Imani tutawakutanisha nao dhuriya zao.

Hakuna mwenye shaka kwamba watoto wadogo hawataadhibiwa kwa hali yoyote ile; ni sawa wazazi wao wawe wema au waovu, kwa sababu hakuna adhabu bila ya uasi, wala hakuna uasi bila taklifa. Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemwondolea kalamu mtoto mdogo mpaka abaleghe.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amekariri katika Aya kadhaa kauli yake: “Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine.” Juz. 8 (6:164).

Ama kauli ya anayesema kuwa mtoto wa kafiri ataingia motoni, kwa vile kama angeliishi basi angelifuata dini ya baba, kuali hii imeachwa, kwa sababu Mwenyezi Mungu humuhisabu mtu kwa aliyoyatenda, wala hamuhisabu kwa ambayo angeliyatenda.

**Unaweza kuuliza**: Je, watoto wadogo watafufuliwa na kuingia Peponi?

**Jibu**: Hakuna njia ya kujua hilo isipokuwa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Nabii wake. Akili hapa haina nafasi ya kuhukumu; wala hakuna katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu au Hadith mutawatir kwamba watoto wa makafiri watafufuliwa.

Kuna Hadith isemayo: “Hakika waumini wataongozwa kwa baba zao wenye takua siku ya kiyama.” Wafasiri wengi wamesema kuwa watoto wakubwa wa waumini katika kizazi cha wanaomcha Mwenyezi Mungu watakutanishwa na daraja za juu za mababa zao Peponi, hata kama amali zao njema ziko chini, ili wazazi waburudike nao. Wameitolea dalili kauli yao hiyo kwa kauli yake Mwenyezi Mungu:

Na wala hatutawapunja kitu katika vitendo vyao; yaani tutawazidisha karama mababa wala hatutawapunguzia mababa kitu chochote katika thawabu zao na daraja zao.

Shia Imamia, Hanafi, Shafii na Hambali wamesema kuwa mtoto atahukumiwa kuwa ni Mwislamu kutokana na mmoja wa wazazi wake. Akiwa mmoja ni mwislamu na mwingine ni kafiri, basi mtoto atahukumiwa kuwa ni Mwislamu, bila ya kuangalia aliye kafiri ni baba au mama. Lakini Malik wamesema unaozingatiwa ni Uislamu wa baba tu, lakini mama hana athari yoyote ya Uislamu kwa mtoto wake.

Kila mtu ni rehani wa alichokichuma. Yeye peke yake atafuatwa na matendo yake na kwayo ndio atakubaliwa nayo kesho kwa Mungu wala hataulizwa aliyotenda mwingine.

Na tutawapa matunda, na nyama kama watavyopenda.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amehusisha kutaja matunda na nyama, kwa sababu ndio vyakula vikuu.

Watapeana humo bilauri zisio na (vinywaji) vya upuuzi wala dhambi.

Watakunywa vinywaji vya kuchangamsha, lakini visivyokuwa na ulevi au vurugu wala kusababisha dhambi na kuchukuliana maneno.

Na watawapitia watumishi wao kama kwamba ni lulu zilizofichwa.

Kusema kwake Mwenyezi Mungu ‘watumishi wao’ ni ishara yakuwa wao watafuata amri zao na makatazo yao.

Wataelekeana wakiulizana.

Wataulizana ilivyokuwa duniani, Vipi wamestahiki heshima hii kutoka kwa Mwenyezi Mungu?

Umetangulia mfano wake katika Juz. 23 (37:50).

Waseme: Tulikuwa zamani pamoja na ahali zetu tukiogopa.

Tulimwogopa Mwenyezi Mungu duniani kwa kuhofia ghadhabu yake na kutumai thawabu zake, Basi Mwenyezi Mungu akatufanyia hisani kwa rehema yake, akatuhusisha na neema yake na akatulinda na adhabu ya upepo wa Moto unaoambua ngozi na kuunguza nyuso.

Hakika sisi zamani tulikuwa tukimwomba Yeye. Hakika Yeye ndiye Mwema Mwenye kurehemu.

Duniani tulikuwa wema wenye huruma, na Mwenyezi Mungu huku Akhera amekuwa mwema kwetu na Mwenye huruma.

17

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

فَذَكِّرْ فَمَا أَنتَ بِنِعْمَتِ رَبِّكَ بِكَاهِنٍ وَلَا مَجْنُونٍ ﴿٢٩﴾

29. Basi kumbusha! na wewe, kwa neema ya Mola wako, si kuhani wala mwendawazimu.

أَمْ يَقُولُونَ شَاعِرٌ نَّتَرَبَّصُ بِهِ رَيْبَ الْمَنُونِ ﴿٣٠﴾

30. Au wanasema: mshairi, tunamtazamia kupatilizwa na dahari.

قُلْ تَرَبَّصُوا فَإِنِّي مَعَكُم مِّنَ الْمُتَرَبِّصِينَ ﴿٣١﴾

31. Sema: tazamieni, na mimi pia ni pamoja nanyi katika wanaotazamia.

أَمْ تَأْمُرُهُمْ أَحْلَامُهُم بِهَٰذَا أَمْ هُمْ قَوْمٌ طَاغُونَ ﴿٣٢﴾

32. Au akili zao ndio zinawaamrisha haya, au wao ni watu waasi?

أَمْ يَقُولُونَ تَقَوَّلَهُ بَل لَّا يُؤْمِنُونَ ﴿٣٣﴾

33. Au wanasema: Ameitunga? Bali hawaamini tu.

فَلْيَأْتُوا بِحَدِيثٍ مِّثْلِهِ إِن كَانُوا صَادِقِينَ ﴿٣٤﴾

34. Basi na walete masimulizi kama haya ikiwa wao wanasema kweli.

أَمْ خُلِقُوا مِنْ غَيْرِ شَيْءٍ أَمْ هُمُ الْخَالِقُونَ ﴿٣٥﴾

35. Au wao wameumbwa pasipo kutokana na chochote Au wao ndio waumbaji?

أَمْ خَلَقُوا السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ بَل لَّا يُوقِنُونَ ﴿٣٦﴾

36. Au wameziumba mbingu na ardhi? Bali hawana yakini.

أَمْ عِندَهُمْ خَزَائِنُ رَبِّكَ أَمْ هُمُ الْمُصَيْطِرُونَ ﴿٣٧﴾

37. Au wanazo hazina za Mola wako, au wao ndio wenye madaraka?

أَمْ لَهُمْ سُلَّمٌ يَسْتَمِعُونَ فِيهِ فَلْيَأْتِ مُسْتَمِعُهُم بِسُلْطَانٍ مُّبِينٍ ﴿٣٨﴾

38. Au wanayo ngazi ya kusikilizia? Basi huyo msikilizaji wao na alete hoja iliyo wazi!

أَمْ لَهُ الْبَنَاتُ وَلَكُمُ الْبَنُونَ ﴿٣٩﴾

39. Au Yeye Mwenyezi Mungu ana wasichana, na nyinyi mna wavulana?

أَمْ تَسْأَلُهُمْ أَجْرًا فَهُم مِّن مَّغْرَمٍ مُّثْقَلُونَ ﴿٤٠﴾

40. Au wewe unawaomba ujira, kwa hiyo wanaelemewa na gharama?

أَمْ عِندَهُمُ الْغَيْبُ فَهُمْ يَكْتُبُونَ ﴿٤١﴾

41. Au wanayo ilimu ya ghaibu, nao wanaandika?

أَمْ يُرِيدُونَ كَيْدًا فَالَّذِينَ كَفَرُوا هُمُ الْمَكِيدُونَ ﴿٤٢﴾

42. Au wanataka kufanya vitimbi tu? Lakini waliokufuru ndio watakaotegeka.

أَمْ لَهُمْ إِلَٰهٌ غَيْرُ اللَّهِ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٤٣﴾

43. Au wanaye mungu asiye kuwa Mwenyezi Mungu? Ametakasika Mwenyezi Mungu na hao wanaowashirikisha naye.

وَإِن يَرَوْا كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ سَاقِطًا يَقُولُوا سَحَابٌ مَّرْكُومٌ ﴿٤٤﴾

44. Na hata wangeona pande linatoka mbinguni linaanguka wangesema: Ni mawingu yaliyobebana.

## HANA UDHURU MWENYE KUUKANA UTUME WA MUHAMAD

**Aya 29 – 44**

### MAANA

Aya hizi zinaashiria hali ya Mtume **(s.a.w.w)** pamoja na washirikina pale alipowapa mwito wa Tawhid na kutupilia mbali ushirikina.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) alianza kumwambia Mtume wake mtukufu kwa namna zifuatazo:-

1. Basi kumbusha! na wewe, kwa neema ya Mola wako, si kuhani wala mwendawazimu.

Endela na kazi yako ya kulingania kwa Mwenyezi Mungu na kuhadharisha adhabu yake; wala usijali na wayasemayo baadhi ya wapinzani kuwa wewe ni kuhani unayedai kujua ghaibu na wengine wakisema kuwa wewe ni mwendawazimu. Wewe kwa fadhila za Mwenyezi Mungu uko mbali kabisa na madai yao na urongo wao. Utakuwaje kuhani au mwendawazimu na hali Mwenyezi Mungu amekujaalia kuwa ni mwaminifu kwa wahyi wake na akakuchagua kwa risala yake?

2. Au wanasema: mshairi, tunamtazamia kupatilizwa na dahari kwa mauti.

Wengine wakisema ni mshairi anayezungumza kutokana na mawazo. Sema: tazamieni, na mimi pia ni pamoja nanyi katika wanaotazamia. Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimwamrisha Mtume wake kuwaambia kuwa ngojeni na mimi ninangoja, mtajua nani atakayefikwa na adhabu ifedheheshayo na kuwa katika wanaojuta.

3. Au akili zao ndio zinawaamrisha haya ya uzushi na uwongo?

Makusudio ya ya akili zao, neno liliofasiriwa kutoka ‘Ahlam’ yenye maana ya noto, ni matamanio yao ya hadaa.

4. Au wao ni watu waasi?

Wao wanajua fika kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu wa haki na ukweli, lakini wanaikana haki kwa uasi, inadi na kupupia vyeo vyao na chumo lao.

5. Au wanasema: Ameitunga hiyo Qur’an! Bali hawaamini tu haki wala hawajizuii na batili!

Basi na walete masimulizi kama haya ikiwa wao wanasema kweli kuwa Qur’an ni ushairi au ukuhani. Wanao washairi wengi na makuhani.

6. Au wao wameumbwa pasipo kutokana na chochote kwa sadfa tu, hakuna muumbaji wala mpangiliaji, hakuna lengo wala majukumu? Je hakuna chochote kabisa sawa na wanavyopatikana wadudu kwenye uvundo na uchafu?

7. Au wao ndio waumbaji waliojiumba wenyewe kwa uweza wao?

8. Au wameziumba mbingu na ardhi?

**Unaweza kuuliza**: washirikina hawadai kwamba wao wamejiumba wala kuumba wengine; bali Qur'an imenukuu kukiri kwao kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaumba na akaumba mbingu na ardhi. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّنْ خَلَقَهُمْ لَيَقُولُنَّ اللَّـهُ ﴿٨٧﴾

"Na ukiwauliza ni nani aliyewaumba? Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu!"

Juz. 25 (43:87).

Pia amesema:

وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ لَيَقُولُنَّ اللَّـهُ ﴿٦١﴾

"Na ukiwauliza ni nani aliyeumba mbingu na ardhi na akalitiisha jua na mwezi, bila shaka watasema ni Mwenyezi Mungu." Juz. 21 (29:61).

Sasa je, kuna utetezi gani wa kauli yake Mwenyezi Mungu: "Au wao ndio waumbaji au wameziumba mbingu na ardhi?"

**Jibu**: wao kwa upande wa nadharia wanakubali kuwa Mwenyezi Mungu ndiye muumba wa kila kitu, lakini kwa upande wa kimatendo wanafanya kama anavyofanya asiyemwamini Mungu wala kukubali kuwa yuko. Bali matendo yao yanajulisha kuwa wao wanadai ni waumbaji na miungu. Haya ameyadokeza Mwenyezi Mungu kwa kauli yake:

Bali hawana yakini. Wasifu huu unawahusu wengi hivi sasa wanaodai kumwamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.

9. Au wanazo hazina za Mola wako.

Ikiwa wanakubali kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Muumba wa kila kitu, je, basi wanadai kuwa Mungu amewaachia idara ya milki yake, kuchagua manabii wake, kugawanya riziki na umri kwa waja? Umetangulia mfano wake katika Juz. 25 (44:32).

10. Au wao ndio wenye madaraka kwa viumbe wote, atake Mwenyezi Mungu au asitake?

11. Au wanayo ngazi ya kusikilizia?

Ikiwa wao hawadai kitu katika hayo je, basi wanadai kuwa wamepanda kwa Mwenyezi Mungu na wakamsikia akisema kuwa Muhammad ni mwongo?

Basi huyo msikilizaji wao na alete hoja ilio wazi!

Haya ndio mantiki ya haki na uadilifu na ukomo wa kumfanyia haki hasimu. Kila mtu anaweza kudai anavyotaka, hata ilimu ya ghaibu, lakini kwa sharti ya kuleta ushahidi wazi wa madai yake; vinginevyo atakuwa ni mzushi mrongo.

12. Au Yeye Mwenyezi Mungu ana wasichana, na nyinyi mna wavulana?

Hakuna tofauti kabisa baina ya kusema kwao Muhammad ni mshairi, kuhani, mwendawazimu na kusema kwao kuwa Mwenyzi Mungu ana wasichana na wao wana wavulana. Uzushi kwa Mtume hauishilii tu kwa kusema kuwa yeye ni mwendawazimu wala kwa kumnasibishia Mwenyzi Mungu washirika au watoto; bali kila mwenye kuhalalisha haramu au akaharamisha halali atakuwa amemzulia Mwenyezi Mungu na Mtume.

13. Au wewe unawaomba ujira, kwa hiyo wanalemewa na gharama?

Kwanini wamemkadhibisha Mtume wa Mwenyezi Mungu? Je amewalazimisha gharama inayowashinda kuitekeleza?

14. Au wanayo ilimu ya ghaibu, nao wanaandika?

Je, wao ni waandishi wa wahyi mbele ya Mwenyezi Mungu wakisajili riziki na umri na yule watakayemchagua katika manabii, kwa hiyo Mwenyezi Mungu hakuwapa jina la Muhammad kulisajili?

15. Au wanataka kufanya vitimbi tu? Lakini walio kufuru ndio watakaotegeka.

Hii ndio hakika yao. Wao hawataki chochote isipokuwa vitimbi na uovu kwa Muhammad **(s.a.w.w)**, lakini vitimbi vitawarudia wao wenyewe, kwa sababu: "vitimbi viovu havimpati ilia mwenyewe" Juz. 22 (35:43)

16. Au wanaye mungu asiye kuwa Mwenyezi Mungu? Ametaksika Mwenyezi Mungu na hao wanaowashirikisha naye.

Ni nani huyo na yuko wapi huyo mungu ambaye atawaepusha na adhabu ya Mwenyezi Mungu itakapowashukia. Mwenyezi Mungu ametakata kabisa kuwa na mfano na mapinzani.

Na hata wangeona pande linatoka mbinguni linaanguka wangesema: Ni mawingu yaliyobebana.

Hata wangeiona adhabu, ana kwa ana, wangelifanya kiburi na kusema haya ni mawingu na sarabi tu. Mfano wake ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَلَوْ فَتَحْنَا عَلَيْهِم بَابًا مِّنَ السَّمَاءِ فَظَلُّوا فِيهِ يَعْرُجُونَ ﴿١٤﴾ لَقَالُوا إِنَّمَا سُكِّرَتْ أَبْصَارُنَا بَلْ نَحْنُ قَوْمٌ مَّسْحُورُونَ ﴿١٥﴾

"Na lau tungeliwafungulia mlango wa mbingu wakawa wanapanda. Basi wangelisema: Macho yetu yamelevywa; bali sisi ni watu waliorogwa." Juz. 14 (15:14-15).

Kwa ufupi ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakumwachia udhuru wowote yule mwenye kukadhibisha au kuukadhibisha utume wa Muhammad **(s.a.w.w)**, ila akane kuweko Mwenyezi Mungu kabisa.

## BASI WAACHE MPAKA WAKUTANE NA SIKU YAO

**Aya 45 – 49**

فَذَرْهُمْ حَتَّىٰ يُلَاقُوا يَوْمَهُمُ الَّذِي فِيهِ يُصْعَقُونَ ﴿٤٥﴾

45. Basi waache mpaka wakutane na siku yao watakaoangamizwa.

يَوْمَ لَا يُغْنِي عَنْهُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٤٦﴾

46. Siku ambayo hila zao hazitawafaa kitu, wala wao hawatanusuriwa.

وَإِنَّ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا عَذَابًا دُونَ ذَٰلِكَ وَلَـٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٤٧﴾

47. Na hakika waliodhulumu watapata adhabu nyengine isiyokuwa hiyo, lakini wengi wao hawajui.

وَاصْبِرْ لِحُكْمِ رَبِّكَ فَإِنَّكَ بِأَعْيُنِنَا وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ حِينَ تَقُومُ ﴿٤٨﴾

48. Na ingojee hukumu ya Mola wako. Kwani wewe hakika uko machoni mwetu. Na mtakase kwa kumsifu Mola wako unaposimama.

وَمِنَ اللَّيْلِ فَسَبِّحْهُ وَإِدْبَارَ النُّجُومِ ﴿٤٩﴾

49. Na usiku pia msabihi, na zinapokuchwa nyota.

### MAANA

Basi waache mpaka wakutane na siku yao watakaangamizwa.

Bado maneno yanendelea kuhusiana na waliomkadhibisha Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**. Maana ni kuwa usijali ewe Muhammad na ukadhibishaji wao na inadi yao, kwani watafikiwa na siku isiyokuwa na kimbilio la kuepuka maangamizi na adhabu chungu.

Siku ambayo hila zao hazitawafaa kitu, wala wao hawatanusuriwa.

Yaani hakutakuwa na hila ya kujikinga siku hiyo wala hakutakuwa na usaidizi.

Na hakika waliodhulumu watapata adhabu nyengine isiyokuwa hiyo.

Yaani wataadhibiwa adhabu nyingine kabla ya siku ya kiyama. Baadhi ya wafasiri wamesema kuwa hiyo ni adhabu ya kaburi. Wengine wakasema ni yaliyowapata siku ya vita vya Badr. Ama sisi tunayanyamazia aliyoyanya- mazia Mwenyezi Mungu.

Lakini wengi wao hawajui kuwa madhalimu wataadhibiwa kabla ya siku ya Kiyama na ndani ya Siku ya Kiyama.

Na ingojee hukumu ya Mola wako. Kwani wewe hakika uko machoni mwetu.

Makusudio ya hukumu ya Mwenyezi Mungu hapa ni kuwapa muda madhalimu mpaka siku yao waliyoagwa. Machoni mwetu ni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, yuko katika hifadhi ya adha ya maadui na vitimbi vyao.

Na msabihi kwa kumsifu Mola wako unaposimama na usiku pia msabihi, na zinapokuchwa nyota.

Mdhukuru Mwenyezi Mungu katika hali zote kwani kumdhukuru yeye ndio dhikri nzuri. Na amewahidi wenye kumdhukuru ahadi ya ukweli.

### MWISHO WA SURA YA HAMSINI NA MBILI: SURAT AT-TUR

18

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

Sura Ya Hamsini Na Tatu: Surat An-Najm. Imeshuka Makka. Ina Aya 62.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

وَالنَّجْمِ إِذَا هَوَىٰ ﴿١﴾

1. Naapa kwa nyota inapoanguka,

مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ ﴿٢﴾

2. Mwenzenu hakupotea, wala hakukosea.

وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٣﴾

3. Wala hatamki kwa matamanio.

إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ ﴿٤﴾

4. Hayakuwa haya ila ni wahyi uliotolewa;

عَلَّمَهُ شَدِيدُ الْقُوَىٰ ﴿٥﴾

5. Amemfundisha mwenye nguvu sana,

ذُو مِرَّةٍ فَاسْتَوَىٰ ﴿٦﴾

6. Mwenye umbo la sura, akatulia,

وَهُوَ بِالْأُفُقِ الْأَعْلَىٰ ﴿٧﴾

7. Naye yuko upeo wa juu kabisa.

ثُمَّ دَنَا فَتَدَلَّىٰ ﴿٨﴾

8. Kisha akakaribia na akateremka.

فَكَانَ قَابَ قَوْسَيْنِ أَوْ أَدْنَىٰ ﴿٩﴾

9. Akawa umbali wa pinde mbili, au karibu zaidi.

فَأَوْحَىٰ إِلَىٰ عَبْدِهِ مَا أَوْحَىٰ ﴿١٠﴾

10. Akampa wahyi mja wake alichompa wahyi.

مَا كَذَبَ الْفُؤَادُ مَا رَأَىٰ ﴿١١﴾

11. Moyo haukusema uwongo uliyoyaona.

أَفَتُمَارُونَهُ عَلَىٰ مَا يَرَىٰ ﴿١٢﴾

12. Je, mnabishana naye juu ya aliyoyaona?

وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَىٰ ﴿١٣﴾

13. Na alimuona mara nyingine,

عِندَ سِدْرَةِ الْمُنتَهَىٰ ﴿١٤﴾

14. Penye Mkunazi wa mwisho.

عِندَهَا جَنَّةُ الْمَأْوَىٰ ﴿١٥﴾

15. Karibu yake pana Bustani ya makazi.

إِذْ يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشَىٰ ﴿١٦﴾

16. Kilipoufunika huo Mkunazi kilichoufunuika.

مَا زَاغَ الْبَصَرُ وَمَا طَغَىٰ ﴿١٧﴾

17. Jicho halikuhangaika wala halikupetuka mpaka.

لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَىٰ ﴿١٨﴾

18. Hakika aliona katika Ishara kubwa kabisa za Mola wake.

## ALIMWONA KWENYE MKUNAZI WA MWISHO MAANA

**Aya 1 – 18**

### MAANA

Naapa kwa nyota inapoanguka.

Mwenye tafsir Al-Bahrul-muhit ametaja kauli kumi kuhusiana na Aya hii. Iliyo karibu zaidi ni ile isemayo kuwa Makusudio ya nyota ni nyota yoyote, kwa sababu Alif na laam iliyoko katika neno hilo ni za jinsia. Na kwamba maana ya kuanguka nyota ni kuwa zitaanguka na kutawanyika katika anga siku ya kiyama, kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu: "Na nyota zitakapotawanyika." (82:1). Kwa sababu Qur'an inajitafsiri yenyewe. Katika kiapo hiki kuna ishara kuwa mwenye kumkana Muhammad **(s.a.w.w)** atapata malipo yake Siku ya Kiyama.

Mwenzenu hakupotea, wala hakukosea, wala hatamki kwa matamanio. Hayakuwa haya ila ni wahyi uliotolewa.

Mwenzenu, ndiye anayeapiwa, ambaye ni Muhammad **(s.a.w.w)** anatamka na kutenda kwa wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, si kwa shaka wala kwa kutojua, au kupotea wala kwa msukumuo wa matamanio yake. Vipi asitamke na kutenda kulingana na wahyi na hali yeye amekuja kutengeneza na kumaliza ufisadi na tamaa?

### UMBALI WA PANDE MBILI

Aya hizi kuanzia 5 – 18, zinaashiria tukio maalum lisiloweza kujulikana isipokuwa kwa njia ya wahyi. Kwa sababu maudhui yake ni kujitokeza Jibril kwa Mtume mara mbili kwa sura yake halisi aliyomuumba nayo Mwenyezi Mungu na sio sura aliyozoea kuiona Mtume pale anapomletea wahyi.

Maneno yamekuwa mengi sana kuhusiana na Aya hizi; mpaka wengine wakathubutu kutaja wasifu wa Jibril na mbawa zake bila ya hoja wala dalili. Sisi tutafupiliza yale yanayofahamiushwa na dhahiri ya Aya na yanoingia akilini, bila ya kujilazimisha na kauli ya mfasiri au mpokezi; na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuombwa msaada:

1. Amemfundisha mwenye nguvu sana.

Kumfundisha Maana yake ni kumfikishia; yaani Jibril alimfikishia Muhammad **(s.a.w.w)**. Makusudio ya nguvu hapa ni sifa zinazomwandaa Jibril (a.s) kuufikisha wahyi; kama vile kuhifadhi, uaminifu na uhakika; kama kwamba Nabii anausikia moja kwa moja kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Dalili ya hilo ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na hakika hiyo ni uteremsho wa Mola wa walimwengu wote. Ameiteremsha Roho

mwaminifu.” Juz. 19 (26:192-193). Vile vile neno ‘amemfundisha,’ linaashiria hivyo.

Kwa hiyo Maana ni kuwa Jibril mwenye nguvu na mwaminifu, alimfkishia Muhammad **(s.a.w.w)** wahyi kwa uhakika wake kama ulivyo katika ilimu ya Mwenyezi Mungu.

2. Mwenye umbo la sura, akatulia.

Hiyo ni sifa ya Jibril; yaani alimtokea Mtume **(s.a.w.w)** sawasawa kama alivyoumbwa.

3. Naye yuko upeo wa juu kabisa.

Ni huyo huyo Jibril. Yaani alimpomtokezea Mtume kwa sura yake alikuwa amenyooka juu ya anga. Wafasiri wanasema: Upeo wa juu ni mawiyo ya jua; yaani mashariki na upeo wa chini ni magharibi. Kwa hali yoyote iwayo ni kuwa Makusudio yake ni kueleza kuwa Jibril sura yake ilitanda angani; wala si muhimu kuwa anga hiyo ilikuwa mashariki au magharibi.

4. Kisha akakaribia na akateremka. Akawa umbali wa pinde mbili, au karibu zaidi.

Hapa kuna maneno ya kutangulizwa; yaani aliteremka akakaribia. Maana ni kuwa Jibri baada ya kumdhirikia Mtume kama alivyoumbwa na Mwenyezi Mungu na umbo lake kupanda hadi juu, alirudi kwenye sura aliyokuwa akikutana nayo Mtume wakati akimpa wahyi na akamkurubia mpaka akawa kiasi cha umbali wa pinde mbili au chini yake. Ni maarufu kuwa Jibril alikuwa akimjia Mtume kwa sura ya Dahiya Al-Kalbiy

5. Akampa wahyi mja wake alichompa wahyi.

Aliyetoa wahyi ni Mwenyezi Mungu na mja ni Muhammad **(s.a.w.w)**. Maana ni kuwa Jibril baada ya kurudia sura yake aliyokuwa akikutana na Mtume na kumkurubia, Mwenyezi Mungu alimpa wahyi Muhammad **(s.a.w.w)** mambo muhimu kupitia kwa Jibril.

6. Moyo haukusema uwongo uliyoyaona.

Yaani Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alimuona Jibril kwa macho yake, kama alivyomuumba; jicho halikukosea lilichokiona wala moyo hakutuia shaka kilichoonwa na jicho; bali alikuwa na yakini na akasadiki.

Je, mnabishana naye juu ya aliyoyaona?

Wanaambiwa washirikina kuwa je, mnamkadhibisha Muhammad na kubishana naye kwa aliyoyaona kwa macho yake na kuyaamini kwa moyo wake na akili yake; na hali nyinyi mumeujua ukweli wake, uaminifu wake, akili yake na usawa wake?

7. Na alimuona mara nyingine, penye Mkunazi wa mwisho. Karibu yake pana Bustani ya makazi.

Mtume alimuona Jibril mara nyingine. Makusudio ya Mkunazi wa mwisho ni mahali pa mwisho na ukomo wanapopafikia viumbe; hata Malaika. Kundi la wafasiri wamesema kuwa katika mbingu ya saba kuna mti ulio kuume mwa Arshi unaoitwa, Mkunazi wa mwisho!

Kauli hii inahitajia dalili. Vyovyote iwavyo sisi hatuna majukumu ya kuu- jua hasa maadamu Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameunyamazia kuufafanua. Tunavyofahamu kutokana na Aya pamoja na maelezo yaliyokuja kwenye Juz.15 (17:1), ni kuwa Jibril alimchukua Mtume

**(s.a.w.w)** usiku wa Miraji na kuzunguka naye mbinguni mpaka akafikia umbali aliouita Mwenyezi Mungu Mkunazi wa mwisho. Hapo akasimama na hakuendelea.

Ama kuhusu Bustani ya makazi, kauli zimegongana katika tafsiri yake. Lakini dhahiri ni kuwa ni Pepo ya milele aliyoijaalia Mwenyezi Mungu kuwa ni malipo ya wale wanaomcha, kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na ama yule mwenye kuogopa kusimama mbele ya Mola wake, na akaikataza nafsi na matamanio, basi hakika Pepo ndio makazi." (79:40-41). Kwani Qur'an inajifasiri yenyewe.

Maana yanayopatikana ni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alimuona Jibril mara mbili kwa umbo lake, kama alivyo. Mara ya kwanza ni ile iliyoashiriwa na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Naye yuko upeo wa juu kabisa;" na mara ya pili ni katika usiku wa Miraji pale alipozunguka naye mpaka akafika mahali pasipovukwa.

Haya ndiyo yote yaliyojulishwa na dhahiri ya Aya, au tuliyoyafahamu sisi kutokana na dhahiri ya Aya. Zaidi ya hapo – kwa maoni yetu – ni katika mambo ya ghaibu, yaliyofichwa.

Kilipoufunika huo Mkunazi kilichoufunuika.

Neno kufunika tumelifasiri kutokana na neno la kiarabu yaghsha ambalo pia lina maana ya kuja. Inafaa kufasiri Aya kwa maana zote mbili, kwa sababu makusudio yake ni kuwa kwenye Mkunazi wa mwisho kunapatikana maajabu ya athari ya uweza Mwenyezi Mungu na ukuu wake yasiyokuwa na kipimo wala kudhibitiwa na akili, ndio maana Mwenyezi Mungu akayafumba na kuacha kuyafafanua.

Jicho halikuhangaika wala halikupetuka mpaka.

Kabisa! Jicho la Mtume halikuepuka hali halisi. Kila aliloliona kwa Jibril na mbinguni usiku wa Miraji ni haki na kweli.

Hakika aliona katika Ishara kubwa kabisa za Mola wake.

Kuona ishara alizozishuhudia Mtume katika miraji ziko zaidi ya mahisabu yote na wakati na mahali pote, ni muhali kuziona binadamu isipokuwa kwa uweza wa Mwenyezi Mungu na matakwa yake. Tumezungumzia Israi na Miraji katika Juz. 15 (17:1) kifungu cha: "Israi kwa roho na mwili.'

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ ﴿١٩﴾

19. Je, mmemuona Lata na Uzza?

وَمَنَاةَ الثَّالِثَةَ الْأُخْرَىٰ ﴿٢٠﴾

20. Na Manata, mwingine wa tatu?

أَلَكُمُ الذَّكَرُ وَلَهُ الْأُنثَىٰ ﴿٢١﴾

21. Je, nyinyi mnao watoto wa kiume na Yeye ndio awe na watoto wa kike?

تِلْكَ إِذًا قِسْمَةٌ ضِيزَىٰ ﴿٢٢﴾

22. Huo ni mgawanyo wa dhulma!

إِنْ هِيَ إِلَّا أَسْمَاءٌ سَمَّيْتُمُوهَا أَنتُمْ وَآبَاؤُكُم مَّا أَنزَلَ اللَّهُ بِهَا مِن سُلْطَانٍ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَمَا تَهْوَى الْأَنفُسُ وَلَقَدْ جَاءَهُم مِّن رَّبِّهِمُ الْهُدَىٰ ﴿٢٣﴾

23. Hayo hayakuwa ila ni majina mliyowapa nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuteremsha dalili yoyote juu ya hayo. Hawafuati ila dhana tu na kipendacho nafsi. Na kwa hakika uwongofu ulikwishawafikia kutoka kwa Mola wao.

أَمْ لِلْإِنسَانِ مَا تَمَنَّىٰ ﴿٢٤﴾

24. Je, mtu anakipata kila anachokitamani?

فَلِلَّـهِ الْآخِرَةُ وَالْأُولَىٰ ﴿٢٥﴾

25. Ni wa Mwenyezi Mungu mwisho na mwanzo.

وَكَم مِّن مَّلَكٍ فِي السَّمَاوَاتِ لَا تُغْنِي شَفَاعَتُهُمْ شَيْئًا إِلَّا مِن بَعْدِ أَن يَأْذَنَ اللَّـهُ لِمَن يَشَاءُ وَيَرْضَىٰ ﴿٢٦﴾

26. Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipokuwa baada ya Mwenyezi Mungu kutoa idhini kwa amtakaye na kumridhia.

## LATA NA UZZA

**Aya 19 – 26**

### MAANA

Je, mmemuona Lata na Uzza? Na Manata, mwingine wa tatu?

Wanaambiwa washirikina wa kikuraishi waliokuwa wakiabudu masanamu haya na kuyaita ni mabinti wa Mungu, kwa hiyo ndio wakayapa majina yenye ishara ya kike ya herufi ta na alif.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) alizikejeli akili zao kwa kusema:

Je, nyinyi mnao watoto wa kiume na Yeye ndio awe na watoto wa kike? Huo ni mgawanyo wa dhulma!

Mfano wake ni kauli yake Mwenyezi Mungu: "Na wamemfanyia Mwenyezi Mungu yale wanayoyachukia." Juz. 14 (16:62).

Hayo hayakuwa ila ni majina mliyowapa nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuteremsha dalili yoyote juu ya hayo, kwa sababu hayo ni mawe tu hayadhuru wala hayanufaishi.

Yametangulia mazungumzo kuhusu masanamu na ibada yake katika makumi ya Aya. Inatosha kuwa ni kuwarudi wanaoyaabudu na kuyatukuza, kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Hakika wale mnaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu hawatoumba nzi wajapojumuika kwa hilo. Na nzi akiwapokonya kitu hawawezi kukipata kwake. Amedhoofika atakaye na anayetakiwa." Juz. 17 (22:73).

Mwanafasihi mmoja anasema: "Akikunyang'anya nzi maisha yako kwa kukuletea maradhi, ni nani anayeweza kukurudishia uhai huo? Na ikikutoka chembe moja tu ya chakula chako inayogeuka sukari katika matumbo yako, je wakemia wakikusanyika wote wataweza kukurudishia chembe yako?

Hawafuati ila dhana tu na kipendacho nafsi.

Makusudio ya dhana hapa ni ujinga. Mtu anayadhibiti matamanio yake kwa akili yake na ilimu yake. Akiwa ni mjinga au dhaifu wa akili, matamanio yake yatamhukumu na kumwongoza kwenye maangamizi.

Na kwa hakika uwongofu ulikwishawafikia kutoka kwa Mola wao, wakasema nyoyo zetu zimefunikwa na katika masikio yetu mna uziwi. Basi neno la adhabu likawathibitikia.

Je, mtu anakipata kila anachokitamani?

Washirikina walitamani shafaa ya masanamu, ndio Mwenyezi Mungu akawarudi kwa kuwauliza, je, mtu anaweza kupata kila anachotamani? Kwa maneno mengine ni kuwa waabudu masanamu walichanganya ujinga na matamanio yanayopofusha na kutia uziwi, basi ujinga ukapanda juu ya ujinga mwingine.

Ni wa Mwenyezi Mungu mwisho na mwanzo. Ufalme na amri ni yake peke yake duniani na akhera.

Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipokuwa baada ya Mwenyezi Mungu kutoa idhini kwa amtakaye na kumridhia.

Walisema kuwa sisi tunaabudu masanamu ili yatuombee kwa Mungu! Ndio Mwenyezi Mungu (s.w.t) akawaambia kuwa Malaika wa mbinguni pamoja na ukubwa na utukufu wao nao hawataombea isipokuwa kwa idhini yake, vipi mawe yenye uziwi yaweze kuwaombea?

Tumezungumzia kuhusu shafaa katika Juz.1 (2:48) kifungu cha: 'Shafaa.'

19

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

إِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ لَيُسَمُّونَ الْمَلَائِكَةَ تَسْمِيَةَ الْأُنثَىٰ ﴿٢٧﴾

27. Hakika wasioamini Akhera wanawaita Malaika kwa majina ya kike.

وَمَا لَهُم بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئًا ﴿٢٨﴾

28. Nao hawana ujuzi wowote wa hayo isipokuwa wanafuata dhana tu, na hakika dhana haifai kitu mbele ya haki.

فَأَعْرِضْ عَن مَّن تَوَلَّىٰ عَن ذِكْرِنَا وَلَمْ يُرِدْ إِلَّا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿٢٩﴾

29. Basi mwachilie mbali anayeupa kisogo ukumbusho wetu, na wala hataki ila maisha ya dunia.

ذَٰلِكَ مَبْلَغُهُم مِّنَ الْعِلْمِ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعْلَمُ بِمَن ضَلَّ عَن سَبِيلِهِ وَهُوَ أَعْلَمُ بِمَنِ اهْتَدَىٰ ﴿٣٠﴾

30. Huo ndio mwisho wao wa ujuzi. Hakika Mola wako ndiye anayemjua zaidi mwenye kuipotea njia yake, na Yeye ndiye anayemjua zaidi mwenye kuongoka.

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسَاءُوا بِمَا عَمِلُوا وَيَجْزِيَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا بِالْحُسْنَى ﴿٣١﴾

31. Ni vya Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na vilivyo katika ardhi, ili awalipe waliotenda ubaya kwa waliyoyatenda, na waliotenda mema awalipe mema.

الَّذِينَ يَجْتَنِبُونَ كَبَائِرَ الْإِثْمِ وَالْفَوَاحِشَ إِلَّا اللَّمَمَ إِنَّ رَبَّكَ وَاسِعُ الْمَغْفِرَةِ هُوَ أَعْلَمُ بِكُمْ إِذْ أَنشَأَكُم مِّنَ الْأَرْضِ وَإِذْ أَنتُمْ أَجِنَّةٌ فِي بُطُونِ أُمَّهَاتِكُمْ فَلَا تُزَكُّوا أَنفُسَكُمْ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنِ اتَّقَىٰ ﴿٣٢﴾

32. Ambao wanajiepusha na madhambi makubwa na vitendo vichafu, isipokuwa makosa madogo. Hakika Mola wako ni Mkunjufu Naye anawajua sana tangu alipowaumba kutoka kwenye ardhi, na mlipokuwa mimba matumboni mwa mama zenu. Basi msijitakase nafsi zenu, Yeye anamjua sana mwenye takua.

## DHANA HAISAIDI KITU MBELE YA HAIFAI

**Aya 27 – 32**

### MAANA

Hakika wasioamini Akhera wanawaita Malaika kwa majina ya kike.

Waliikadhibisha haki kwa ujinga na inadi. Kila moja kati ya mawili hayo linatosha kuwa ni tafsiri na sababu ya uzushi wao kwa Mwenyezi Mungu kwamba ana washirika, mke na watoto wa kike. Hawakutosheka kusema ana watoto mpaka wakawapa majina maalum.

Nao hawana ujuzi wowote wa hayo isipokuwa wanafuata dhana tu, ndio wakathibitisha vitu visivyokuwako wala kuwa na dalili yoyote isipokuwa njozi tu zinazopita vichwani mwao.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliwarudi kwa kuwaambia kuwa hajui yeye kama ana mabinti aliposema:

قُلْ أَتُنَبِّئُونَ اللَّـهَ بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ سُبْحَانَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١٨﴾

"Sema je, mnamwambia Mwenyezi Mungu asiyoyajua katika mbingu wala katika ardhi? Ametakasika na ametukuka na hao wanaomshirikisha naye." Juz. 11 (10:18).

Na hakika dhana haifai kitu mbele ya haki.

Lau watu wangelifuata dhana, mambo yasingelikwenda sawa katika maisha haya. Imetangulia kwa herufi zake katika Juz. 11 (10:36).

Basi mwachilie mbali anayeupa kisogo ukumbusho wetu, na wala hataki ila maisha ya dunia.

Maneno yaaelekezwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** lakini yanakusudiwa kila mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Maana ni kuwa usiwajadili wale ambao wamezama kwenye uasi na upotevu, wasioamini kitu wala kuona kima chochote isipokuwa nafsi zao na chumo lao:

وَإِن يَرَوْا كُلَّ آيَةٍ لَّا يُؤْمِنُوا بِهَا ﴿٢٥﴾

"Na wakiona kila ishara hawaiamini." Juz. 7 (6:25).

Basi kuna haja gani ya kubishana nao. Tazama kifungu: 'Haki na manufaa' katika Juz. 3 (3:52-54) na kifungu: 'Mjadala wa kijinga na upotevu.' Juz.17 (22: 1-7).

Huo ndio mwisho wao wa ujuzi na haki. Hawana ujuzi, dini dhamiri, haki na msimamo isipokuwa anasa na kutukuza mali. Tazama Juz. 18 (25:7-16). Kifungu: 'Mantiki ya watu wa pesa ni benki na ardhi.'

Hakika Mola wako ndiye anayemjua zaidi mwenye kuipotea njia yake, na Yeye ndiye anayemjua zaidi mwenye kuongoka.

Ewe Muhammad! Mola wako anajua kuwa wale walioukadhibisha unabii wako hawakataziki na upotevu. Vile vile anajua kuwa wewe uko kwenye uongofu na wale wanaokufuata katika waumini. Kwa sababu Yeye amekizunguka kila kitu na ni muweza wa kumlipa mwenye kuamini na kuongoka na adhabu ya mwenye kupotea.

Ni vya Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na vilivyo katika ardhi, ili awalipe waliotenda ubaya kwa waliyoyatenda, na waliotenda mema awalipe mema.

Aya hii ni kemeo na kiaga kwa yule aliyemwashiria Mwenyezi Mungu kwa kauli yake: "Anayeupa kisogo ukumbusho wetu, na wala hataki ila maisha ya dunia."

Njia ya ukemeo ni kuwa dunia na Akhera ziko mikononi mwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu Yeye peke yake ndiye mmiliki wa ulimwengu na vilivyomo ndani yake.

Kwa hiyo atakayeiacha Akhera na akaitafuta dunia na akaihangaikia, tutampa hiyo dunia na katika Akhera hana isipokuwa adhabu; ambapo kila mtu atapata malipo ya matendo yake, ikiwa ni heri basi ni heri na ikiwa ni shari basi ni shari.

Ambao wanajiepusha na madhambi makubwa na vitendo vichafu, isipokuwa makosa madogo. Hakika Mola wako ni Mkunjufu wa maghufira.

Madhambi makubwa ni kama kufru, shirk na dhulma. Na kila linalopituka mpaka kwenye uovu ni katika vitendo vichafu na ni dhambi kubwa pia; kama vile zina na ulawiti. Ama madhambi madogo ni yale ambayo mara nyingi yanampitia mtu; isipokuwa wale maasumu; kama kuangalia na kukaa kwenye meza ya pombe. Tumezungumza kwa ufafanuzi katika Juz.5 (4:31).

Maana ya Aya ni kuwa mwenye kujing'oa kwenye madhambi makubwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) huumpa msamaha na hisani yake hata kama aki-fanya madhambi madogo. Lakini hii haimaanishi kwamba mtu anaruhusiwa kufanya madhambi madogo; hapana! Vinginevyo itakuwa ni halali; isipokuwa ni kwamba mwenye kujiepusha na madhambi makubwa awe na matumaini ya kusamehewa madogo kutoka kwa Mola wake. Vinginevyo ingelikuwa Pepo ni ya maasumu tu.

Imeelezwa katika Nahju-Bbalagha: "Dhambi kubwa ni ile aliyoidharau mtendaji… Na kuyakuza mtu maasi ya mwingine na kuadharau yake na kujiona ana twaa nyingi kuliko mwingine."

Naye anawajua sana tangu alipowaumba kutoka kwenye ardhi, na mlipokuwa mimba matumboni mwa mama zenu. Basi msijitakase nafsi zenu, Yeye anamjua sana mwenye takua.

Ndio! Mwenyezi Mungu anamjua zaidi mtu kuliko anavyojijua yeye mwenyewe vyovyote atakavyokua na ilimu. Haiwezekani mtu kujijua kuliko anavyojuliwa na Mwenyezi Mungu. Kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye aliyemfanya aweko na kumpa uhai, akamficha na atamfufua. Yuko naye akimjua tangu alipokuwa tumboni mwa mama yake mpaka pumzi yake ya mwisho.

Zaidi ya hayo ni kuwa viungo vya mtu hata moyo wake ni shahidi wake mbele ya muumba wake. Shahidi mkali zaidi atakayetamka kumtakasa mtu na kufanya awe katika wenye ikhlasi ni matendo yake mema. Umetangulia mfano wake katika Juz. 5 (4:49) na Juz. 18 (24:21).

﴿أَفَرَأَيْتَ الَّذِي تَوَلَّىٰ ﴿٣٣﴾

33. Je, Umemwona yule aliyegeuka?

﴿وَأَعْطَىٰ قَلِيلًا وَأَكْدَىٰ ﴿٣٤﴾

34. Na akatoa kidogo, kisha akajizuia?

﴿أَعِندَهُ عِلْمُ الْغَيْبِ فَهُوَ يَرَىٰ ﴿٣٥﴾

35. Je, anayo ilimu ya ghaibu, basi ndio anaona?

﴿أَمْ لَمْ يُنَبَّأْ بِمَا فِي صُحُفِ مُوسَىٰ ﴿٣٦﴾

36. Au hakuambiwa yaliyomo katika Vitabu vya Musa?

﴿وَإِبْرَاهِيمَ الَّذِي وَفَّىٰ ﴿٣٧﴾

37. Na vya Ibrahim aliyetimiza ahadi?

﴿أَلَّا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ﴿٣٨﴾

38. Kwamba habebi mbebaji mzigo wa mwingine?

﴿وَأَن لَّيْسَ لِلْإِنسَانِ إِلَّا مَا سَعَىٰ ﴿٣٩﴾

39. Na ya kwamba hatapata mtu ila aliyoyahangaikia.

﴿وَأَنَّ سَعْيَهُ سَوْفَ يُرَىٰ ﴿٤٠﴾

40. Na kwamba mahangaiko yake yataonekana.

﴿ثُمَّ يُجْزَاهُ الْجَزَاءَ الْأَوْفَىٰ ﴿٤١﴾

41. Kisha ndio atalipwa malipo yake kwa ukamilifu.

## MTU HATAPATA ILA ALIYOYAFANYA

**Aya 33 – 41**

### MAANA

Je, Umemwona yule aliyegeuka? Na akatoa kidogo, kisha akajizuia?

Yaani akazuia kutoa. Maana ni kuwa hebu niambie ewe Muhammad kuhusu mtu ambaye ameupa kisogo utajo wa Mwenyezi Mungu, na akawa ametoa kitu kidogo katika mali yake au nafsi yake katika njia ya Mwenyezi Mungu, kisha akajizuia kutoa!

Hii ndivyo inavyofahamisha dhahiri ya Aya. Kisha linakuja swali, kuwa je, Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimkusudia mtu maalum aliyemjua Nabii **(s.a.w.w)**, au alikusudia mfano wa jumla kwa kila atakayekuwa na sifa hizi? Baadhi ya wafasiri wamesema kuwa Aya hii ilimshukia Walid bin Al-Mughira, wengine wakasema ni Uthman Bin Affan. Kauli zote mbili zinahitajia dalili. Kwa hiyo basi Aya inabakia na ujumla wake na kuenea kwa kila mwenye sifa hizo.

Je, anayo ilimu ya ghaibu, basi ndio anaona?

Je, huyu mpingaji anayejizuia kutoa anajua kuwa yeye yuko kwenye amani ya adhabu ya siku ya kiyama mpaka akajasiri kupinga na kujizuia? Na atakuwa ameitoa wapi ilimu hii na hali Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameteremsha katika Kitabu yanayokadhibisha madai yake kama atadai hivyo?

Au hakuambiwa yaliyomo katika Vitabu vya Musa? Na vya Ibrahimu aliyetimiza ahadi?

Hakusikia mpinzani huyu aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu katika Tawrat na maandishi ya Ibrahim ambaye alitimiza ahadi kwa njia ya ukamilifu. Hakusikia kuwa Mwenyezi Mungu ameteremsha katika vitabu viwili hivi, kwamba habebi mbebaji mzigo wa mwingine?

Yaani kila mtu ataadhibiwa kwa dhambi zake na hakuna atakayembebea madhambi yake.

Aya hii imekaririka katika Juz. 8 (6:164), Juz. 15 (17:15), Juz. 22 (35:18) na Juz. 23 (39:7).

Na ya kwamba hatapata mtu ila aliyoyahangaikia.

Makusudio ya kuhangaika hapa ni kufanya amali na harakati katika maisha haya. Aya hii inafahamisha wazi kuwa dini ya Uislamu ni dini ya maisha, kwa sababu inaelezea waziwazi kuwa Mwenyezi Mungu anawangalia waja wake kupitia matendo yao katika maisha ya dunia na anaamiliana nao kwa mujibu wake.

Maana yake ni kuwa kila atakavyofanya mtu kwa ajili ya heri yake na akatatua matatizo yake atakuwa amekuwa karibu na Mwenyezi Mungu na dini ya Mwenyezi Mungu na atastahiki rehema na karama.

Na kadiri atavyoyakimbia maisha akajiweka mbali na matatizo yake kwa kutosheka na takbira, tahalili, kufunga na kuswali, basi atakuwa amejiweka mbali na Mwenyezi Mungu na dini yake na rehema yake.

Na kwamba mahangaiko yake yataonekana.

Yaani Mweneyzi Mungu atamuhisabu kwa mujibu wa matendo yake Siku ya Kiyama. Makusudio ya kuonekana hapa ni kuhisabiwa; vinginevyo ni kuwa Mweneyzi Mungu (s.w.t) anajua kila kitu hata mawazo na wasiwasi.

Kisha ndio atalipwa malipo yake kwa ukamilifu.

Iko wazi haihitaji tafsiri, ni sawa na kauli yake Mweneyzi Mungu Mtukufu:

أَنِّي لَا أُضِيعُ عَمَلَ عَامِلٍ مِّنكُم مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَىٰ ﴿١٩٥﴾

"Kwamba mimi sitapoteza amali ya mfanya amali miongoni mwenu, akiwa mwanamume au mwanamke." Juz. 4 (3:195).

وَأَنَّ إِلَىٰ رَبِّكَ الْمُنتَهَىٰ ﴿٤٢﴾

42. Na kwamba kwa Mola wako ndio mwisho.

وَأَنَّهُ هُوَ أَضْحَكَ وَأَبْكَىٰ ﴿٤٣﴾

43. Na kwamba Yeye ndiye anayeleta kicheko na kilio.

وَأَنَّهُ هُوَ أَمَاتَ وَأَحْيَا ﴿٤٤﴾

44. Na kwamba Yeye ndiye anayefisha na kuhuisha.

وَأَنَّهُ خَلَقَ الزَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ وَالْأُنثَىٰ ﴿٤٥﴾

45. Na kwamba Yeye ndiye aliyeumba jozi, dume na jike,

مِن نُّطْفَةٍ إِذَا تُمْنَىٰ ﴿٤٦﴾

46. Kutokana tone la manii linapomiminwa.

وَأَنَّ عَلَيْهِ النَّشْأَةَ الْأُخْرَىٰ ﴿٤٧﴾

47. Na kwamba ni juu yake ufufuo mwengine.

وَأَنَّهُ هُوَ أَغْنَىٰ وَأَقْنَىٰ ﴿٤٨﴾

48. Na kwamba ni Yeye ndiye anayetosheleza na anayetajirisha.

وَأَنَّهُ هُوَ رَبُّ الشِّعْرَىٰ ﴿٤٩﴾

49. Na kwamba hakika Yeye ndiye Mola wa Shii'ra.

وَأَنَّهُ أَهْلَكَ عَادًا الْأُولَىٰ ﴿٥٠﴾

50. Na kwamba Yeye ndiye aliyewaangamiza A'di wa kwanza.

وَثَمُودَ فَمَا أَبْقَىٰ ﴿٥١﴾

51. Na Thamudi hakuwabakisha.

وَقَوْمَ نُوحٍ مِّن قَبْلُ إِنَّهُمْ كَانُوا هُمْ أَظْلَمَ وَأَطْغَىٰ ﴿٥٢﴾

52. Na kabla yao kaumu ya Nuh. Na hao hakika walikuwa ni madhalimu zaidi, na waasi zaidi.

وَالْمُؤْتَفِكَةَ أَهْوَىٰ ﴿٥٣﴾

53. Na miji iliyopinduliwa, ni Yeye aliyeipindua.

فَغَشَّاهَا مَا غَشَّىٰ ﴿٥٤﴾

54. Vikaifunika vilivyofunika.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكَ تَتَمَارَىٰ ﴿٥٥﴾

55. Basi neema gani ya Mola wako unayoifanyia shaka?

هَـٰذَا نَذِيرٌ مِّنَ النُّذُرِ الْأُولَىٰ ﴿٥٦﴾

56. Hili ni Onyo katika maonyo yale yale ya zamani.

أَزِفَتِ الْآزِفَةُ ﴿٥٧﴾

57. Tukio la karibu limekurubia.

لَيْسَ لَهَا مِن دُونِ اللَّـهِ كَاشِفَةٌ ﴿٥٨﴾

58. Hapana wa kulifichua isipokuwa Mwenyezi Mungu.

أَفَمِنْ هَـٰذَا الْحَدِيثِ تَعْجَبُونَ ﴿٥٩﴾

59. Je, mnayastaajabia maneno haya?

وَتَضْحَكُونَ وَلَا تَبْكُونَ ﴿٦٠﴾

60. Na mnacheka wala hamlii?

وَأَنتُمْ سَامِدُونَ ﴿٦١﴾

61. Nanyi mmeghafilika?

فَاسْجُدُوا لِلَّـهِ وَاعْبُدُوا ﴿٦٢﴾

62. Basi msujudieni Mwenyezi Mungu, na mumwabudu.

## KWA MOLA WAKO NDIO MWISHO

**Aya 42 – 62**

### MAANA

Na kwamba kwa Mola wako ndio mwisho.

Aya hii na zinazofuatia bado zinaungana na zile alizosema Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuwa ziko katika vitabu vya Musa na Ibrahim. Makusudio ya mwisho ni kusimama mtu mbele ya Mola wake kwa ajili ya hisabu ambayo hataepukana nayo.

Na kwamba Yeye ndiye anayeleta kicheko na kilio.

Kicheko ni ishara ya furaha ya watu wa Peponi na kilio ni huzuni ya watu wa motoni. Inawezekana kuwa ni ishara ya silika ya ladha, uchungu, huzuni na furaha aliyompa Mwenyezi Mungu mtu.

Watu wa falsafa wanasema kuwa mtu hawezi kutaharaki isipokuwa kwa mvuto wa ladha; kama vile tendo la ndoa au kwa kuhofia maumivu; kama vile njaa.

### MAADA NA MAISHA

Na kwamba Yeye ndiye anayefisha na kuhuisha.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye anayetoa uhai na kuuchukua. Ama kauli ya mwenye kusema maada ndio asili ya uhai na ndiyo iliyousababisha, hayo ni madai tu yanayokataliwa na msingi wa akili. Kwa sababu maada haina harakati kwa maumbile yake mpaka ipate sababu ya kuibadilisha.

Ni nani mwenye akili anayeweza kukubali kuwa maada pofu imejitengenezea yenyewe macho, masikio na moyo? Ikiwa uhai ni sifa ya maada kwanini kukatokea kukua, harakati, hisia na kufikiri katika baadhi tu, na kwingine kusitokee?

Ikiwa mtu atajibu kuwa baadhi ya maada zina maandalizi ya uhai na nyingine hazina, tutamuuliza: Je, tofauti hii imetoka wapi? Kutoka ndani ya maada yenyewe au kutoka nje? Ikiwa imetoka ndani basi ni lazima kila maada iwe na uhai; vinginevyo itakuwa kitu kimoja kimesababisha kupatikana na kukosekana kwa wakati mmoja. Na ikiwa imesabishwa na sababu ya nje, basi hivyo ndivyo tusemavyo.

Na kwamba Yeye ndiye aliyeumba jozi, dume na jike kutokana tone la manii linapomiminwa.

Mwanamume anashusha manii yake katika mfuko wa uzazi, mimba inatungwa na anapatikana mtoto wa kike au wa kiume. Ni nani basi aliyeleta maandalizi ya mbegu hii mwilini? Ni nani aliyeleta mamilioni ya chembe hai? Je, wataalamu wanaweza kutengeneza chembe moja itakayotoa mtoto wa kike au wa kiume? Bali je, wanaweza kutofautisha chembe itakayotengeneza mtoto wa kiume au wa kike? Ikiwa mbegu za uzazi zinategemea sababu za maumbile, basi sababu hizi zinaishia kwa yule aliyetengeneza maumbile.

Na kwamba ni juu yake ufufuo mwengine.

Juu yake ni juu ya Mwenyezi Mungu. Maana ni kuwa ufufuo hauna budi kuweko.

Na kwamba ni Yeye ndiye anayetosheleza na anayetajirisha.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewapa waja wake na akawafanya wajitosheleze bila ya kuwa na haja ya kuomba wengine na wengine akawapa ya kuwatosheleza na ziada ya kuweka akiba. Mmoja wa wataalamu anasema: "Mwenye kuonja ladha ya kujitosheleza atakuwa amepata fungu la kujitosheleza na kwamba hilo lina utukufu.''

Na kwamba hakika Yeye ndiye Mola wa Shii'ra.

Shiira (Sirius) ni nyota inayoangaza. Mwenyezi Mungu amehusisha kuitaja hapa kwa sababu watu wa wakati wa jahilia walikuwa wakiiabudu. Imesemekana kuwa ni kubwa kuliko Jua kwa mara ishirini na kwamba iko mbali na jua kwa mara milioni zaidi ya sisi tulivyo mbali na Jua.

Na kwamba Yeye ndiye aliyewaangamiza A'di wa kwanza.

Hao ni watu wa Hud. Mazungumzo kuwahusu yamekwishapita huko nyuma mara kadhaa. Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewasifu kuwa wa kwanza kutokana na wale waliokuja baada yao katika umma. Mwenye Majmaulbayan anasema ni kwa sababu walikuja A'di wengine.

Na Thamudi hakuwabakisha, yeyote katika wao.

Hao ni watu wa Swaleh. Vile vile yametangulia maelezo yao na ya watu wa Nuh ambao amewaashiri Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa kusema: Na kabla yao kaumu ya Nuh. Na hao hakika walikuwa ni madhaalimu zaidi, na waasi zaidi kuliko A'di na Thamud.

Na miji ya kaumu ya Lut iliyopinduliwa, ni Yeye aliyeipindua akaizamisha ndani ya ardhi.

Vikaifunika vilivyofunika kwa adhabu.

Basi neema gani ya Mola wako unayoifanyia shaka?

Maneno yanaelekzwa kwa kila mtu.

Hili ni onyo katika maonyo yale yale ya zamani.

Wafasiri wengi wamesema kuwa 'Ishara' hapa ni ya Qur'an au Muhammad **(s.a.w.w)**, kwa hiyo isemwe Hii au Huyu.

Hakuna mwenye shaka kuwa Qur'an na Muhammad **(s.a.w.w)** ni katika maonyo ya mwanzo, lakini pamoja na hayo, tunavyofahamu ni kuwa Mwenyezi Mungu ameashiria yale aliyoyataja miongoni mwa dalili na mawaidha yaliyokusanya mambo muhimu yanayotakikana kuchunguzwa na kuwa ni mafunzo; kama maswala ya kuwa kila mtu peke yake ndiye mwenye majukumu ya makosa yake, kwamba Mwenyezi Mungu anamwangalia kupitia matendo yake, kuwa hakuna chimbuko la uhai isipokuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu tu peke yake na mwisho wa waasi ni maangamizi.

Haya na mengineyo mfano wake ni miongoni mwa maudhui muhimu ya ulimwengu na binadamu. Anapoyataja Mwenyezi Mungu (s.w.t), ili kumfahamisha mtu kuwa Mwenyezi Mungu yuko na ni mkuu, itakuwa kutajwa kwake hasa kunaashiria kuwa maana yake na malengo yake yanajitokeza kwa wataalamu na kwamba wao ndio wana haki zaidi ya kumjua Mwenyezi Mungu, kumwamini na kumcha:

إِنَّمَا يَخْشَى اللَّـهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ ﴿٢٨﴾

"Hakika si mengineyo, wanaomcha Mwenyezi Mungu katika waja wake ni wale wajuzi."

Juz. 22 (35:28).

Tukio la karibu limekurubia.

Makusudio ya tukio hapa ni Kiyama. Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameliisifu kuwa linasogea, kwa vile linakuja na kila linalokuja liko karibu na kila lililopita ni kama halikuwako.

Hapana wa kulifichua isipokuwa Mwenyezi Mungu.

Kulifichua ni hilo tukio la karibu; yaani Kiyama. Unaweza kufasiri kufichua kwa maana ya ilimu; kama kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

يَسْأَلُونَكَ عَنِ السَّاعَةِ أَيَّانَ مُرْسَاهَا ۖ قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا عِندَ رَبِّي ۖ لَا يُجَلِّيهَا لِوَقْتِهَا إِلَّا هُوَ ﴿١٨٧﴾

"Wanauliza hiyo Saa (Kiyama) kutokea kwake kutakuwa lini? Sema: Ujuzi wake uko kwa Mola wangu. Hakuna wa kuidhihirisha kwa wakati wake ila yeye tu." Juz. 9 (7:187).

Pia unaweza kufasiri kwa kauli yake Mwenyezi Mungu mtukufu:

مِن قَبْلِ أَن يَأْتِيَ يَوْمٌ لَّا مَرَدَّ لَهُ مِنَ اللَّـهِ ﴿٤٣﴾

"Kabla ya kufika siku isiyozuilika inayotoka kwa Mwenyezi Mungu." Juz.21 (30:43).

Je, mnayastaajabia maneno haya na mnacheka?

Mananeno haya ni haya mazungumzo ya Kiyama. Imesemkana ni Qur'an. Tafsri zote mbili ni sawa, kwa sabau makafiri walistahajabu ufufuo:

فَقَالَ الْكَافِرُونَ هَـٰذَا شَيْءٌ عَجِيبٌ ﴿٢﴾ أَإِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا ۖ ذَٰلِكَ رَجْعٌ بَعِيدٌ ﴿٣﴾

"Na wakasema makafiri: Hili ni jambo la ajabu! Je, tukifa na tukawa udongo? Marejeo hayo ni ya mbali!" Juz. 26 (50:2-3).

Pia waliistaajabu Qur'an:

أَوَعَجِبْتُمْ أَن جَاءَكُمْ ذِكْرٌ مِّن رَّبِّكُمْ ﴿٦٣﴾

" Je, mnastaajabu kuwafikia mawaidha kutoka kwa Mola? Juz. 8 (7:63).

Wala hamlii? Nanyi mmeghafilika?

Ilikuwa bora mzililie nafsi zenu ambazo mmezidhulumu kwa ukafiri na dhulma:

فَلْيَضْحَكُوا قَلِيلًا وَلْيَبْكُوا كَثِيرًا جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٨٢﴾

"Basi nawacheke kidogo na walie sana, ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyachuma."

Juz. 10 (9:82)

Basi msujudieni Mwenyezi Mungu, na mumuabudu.

Hanafi, Shafi, Shia Imamia na Hambali wamesema ni wajibu kusujudi wakati wa kusomwa Aya hii, kwa sababu Mtume **(s.a.w.w)** alisujudi wakati wa kusomwa kwake na walisujudi waliokuwa pamoja naye, lakini Maliki wakasema kuwa siwajibu.

## MWISHO WA SURA YA HAMSINI NA TATU: SURAT AN-NAJM

20

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

Sura Hamsini Na Nne: Surat Al-Qamar. Imeshuka Makka. Ina Aya 55.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi Mwenye kurehemu.

اقْتَرَبَتِ السَّاعَةُ وَانشَقَّ الْقَمَرُ ﴿١﴾

1. Saa imekaribia, na mwezi umepasuka!

وَإِن يَرَوْا آيَةً يُعْرِضُوا وَيَقُولُوا سِحْرٌ مُّسْتَمِرٌّ ﴿٢﴾

2. Na wakiona Ishara hugeuka upande na husema: Uchawi unaoendelea.

وَكَذَّبُوا وَاتَّبَعُوا أَهْوَاءَهُمْ ۚ وَكُلُّ أَمْرٍ مُّسْتَقِرٌّ ﴿٣﴾

3. Na wamekanusha na wamefuata matamanio yao. Na kila jambo lina wakati maalum.

وَلَقَدْ جَاءَهُم مِّنَ الْأَنبَاءِ مَا فِيهِ مُزْدَجَرٌ ﴿٤﴾

4. Na bila ya shaka zimewajia habari zenye makaripio.

حِكْمَةٌ بَالِغَةٌ ۖ فَمَا تُغْنِ النُّذُرُ ﴿٥﴾

5. Hikima kamili, lakini maonyo hayafai.

فَتَوَلَّ عَنْهُمْ ۘ يَوْمَ يَدْعُ الدَّاعِ إِلَىٰ شَيْءٍ نُّكُرٍ ﴿٦﴾

6. Basi jiepushe nao. Siku atakapoita mwitaji kuliendea jambo linalochusha.

خُشَّعًا أَبْصَارُهُمْ يَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ كَأَنَّهُمْ جَرَادٌ مُّنتَشِرٌ ﴿٧﴾

7. Macho yao yatainama; watatoka makaburini, kama kwamba wao ni nzige waliotawanyika.

مُّهْطِعِينَ إِلَى الدَّاعِ ۖ يَقُولُ الْكَافِرُونَ هَٰذَا يَوْمٌ عَسِرٌ ﴿٨﴾

8. Wanamkimbilia mwitaji; makafiri wanasema: Hii ni siku ngumu.

## MWEZI UMEPASUKA

**Aya 1 – 8**

### MAANA

Saa imekaribia.

Maana yake ni sawa na Aya 57 ya sura iliyopita: "Tukio la karibu limekurubia." Nayo ni kuwa siku ya Kiyama itafika tu, hilo halina shaka.

Na mwezi umepasuka!

Wafasiri wengi wamesema kuwa washirikina walimtaka Mtume wa Mwenyezi Mungu, **(s.a.w.w)** aupasue mwezi mara mbili ikiwa yeye ni mkweli. Basi akamwomba Mola wake, na mwezi ukapasuka vipande viwili, kisha ukarudi kwenye hali yake ya kawaida.

Hakuna mwenye shaka kuwa hili linawezekana, lakini kuwezekana ni jambo jingine na kutokea ni jambo jingine.

Kwa sababu kutokea kunahitajia dalili ya kuthibitisha; wala hakuna dalili ya kuthibitisha; bali dalili ziko kinyume na hivyo; kama ifuatavyo:-

**Kwanza**: Haya hayaafikiani na Aya kadhaa zinazoelezea waziwazi kuwa Mtume **(s.a.w.w)** hakuitikia maoni ya wa shirikina kutaka mambo yasiyokuwa ya kawaida, naye akawajibu kwa mujibu wa amri ya Mwenyezi Mungu:

قُلْ سُبْحَانَ رَبِّي هَلْ كُنتُ إِلَّا بَشَرًا رَّسُولًا ﴿٩٣﴾

"Sema: ametakasika Mola wangu! Kwani mimi ninani isipokuwa ni mwanadamu Mtume!"

Juz. 15 (17:93).

Pia Mwenyezi Mungu amebainisha kuwa wanotaka muujiza wataendela na ukafiri wao hata wakijibiwa maombi yao:

وَمَا مَنَعَنَا أَن نُّرْسِلَ بِالْآيَاتِ إِلَّا أَن كَذَّبَ بِهَا الْأَوَّلُونَ ﴿٥٩﴾

"Na hapana kinachotuzuia kupeleka miujiza ila nikuwa watu wa zamani waliikanusha."

Juz. 15 (17:59).

Akasema tena:

وَإِن يَرَوْا كُلَّ آيَةٍ لَّا يُؤْمِنُوا بِهَا وَإِن يَرَوْا سَبِيلَ الرُّشْدِ لَا يَتَّخِذُوهُ سَبِيلًا وَإِن يَرَوْا سَبِيلَ الْغَيِّ يَتَّخِذُوهُ سَبِيلًا ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَكَانُوا عَنْهَا غَافِلِينَ ﴿١٤٦﴾

"Na wakiona kila Ishara hawaiamini na wakiona njia ya uongofu hawaishi- ki kuwa ndiyo njia, lakini wakiona njia ya upotofu wanaishika kuwa ndiyo njia,. Hayo ni kwa sababu wao wamezikadhibisha ishara zetu na wameghafilika nazo." Juz. 9 (7:146).

Zaidi ya hayo ni kuwa mwenye kutaka visababu hana udhuru wowote baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuwapa changa moto walimwengu wote na wakashindwa; pale aliposema: "Na mkiwa na shaka kwa (hayo) tuliyomteremshia mtumwa wetu, basi leteni sura moja iliyo mfano wake, na muwaite mashahidi wenu badala ya Mwenyezi Mungu ikiwa mnasema kweli." Juz. 1 (2:23).

**Pili**: kupasuka mwezi ni tukio kubwa la kilimwengu, lau lingetokea wangeliona wa mashariki na wa magharibi, na wangeliliandika ulama na wanahistoria wengineo; kama walivyoandika matukio mengineyo.

**Tatu**: Kupasuka mwezi ni katika maudhui ambayo hayathibiti isipokuwa kwa khabar mutawatir na maudhui ya kupasuka mwezi yamekuja kwa Khabar Al-ahd. Tofauti ni kuwa katika Mutawatir wapokezi ni wengi na wanatofautiana hali zao na malengo yao, kwa namna ambayo, kwa kawaida, hawawezi kukongamana wakasema uwongo. Na Ahad ni kinyume na hivyo. Kwa hiyo unaweza kutofautisha kwamba mutawatir inategemewa zaidi kuliko Ahad.

**Nne**: Kauli yake Mwenyezi Mungu 'Na umepasuka mwezi baada ya kauli yake: 'Kimekurubia Kiyama.' Inafahamisha kuwa mwezi utapasuka kitakapokuwa Kiyama na kwamba makusudio ya kupasuka mwezi hapa, ndio yale yaliyo katika kauli yake:

إِذَا السَّمَاءُ انشَقَّتْ ﴿١﴾

"Itakapopasuka mbingu." (84:1).

Na wakiona Ishara hugeuka upande na husema: uchawi unaoendelea usiokuwa na mwisho.

Katika (74:24), Mwenyezi Mungu anamsimulia Walid bin Al-Mughira, kuwa alisema: “Haya si chochote ila ni uchawi ulionukuliwa.”

Na wamekanusha na wamefuata matamanio yao.

Ujinga na hawaa umewapofusha na kila hoja na dalili. Kwa hiyo, pamoja na dalili za wazi, lakini wakakikadhibisha Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kukutana naye.

Na kila jambo lina wakati maalum.

Hili ni kemeo kwa anayeiacha Qur’an. Maana ni kuwa kila kitu kimethibiti katika ujuzi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, hakifichiki kwake jambo lolote likiwamo kuipinga Qur’an na kuachana nayo.

Mfano wake ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: “Na watu wako wameikadhibisha nayo ni haki: Sema nami sikuwakilishwa juu yenu. Kila habari ina wakati maalum na punde mtajua.” Juz. 7 (6:66-67).

Na bila ya shaka zimewajia habari zenye makaripio.

Makusudio ya habari hapa ni kila Aya katika Qur’an yenye mawaidha na mazingatio, mapendekezo na makatazo, au zinazofahamisha njia ya imani, Siku ya Mwisho na wahyi ulioteremshwa kwa Mtume **(s.a.w.w)**.

Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliwabainishia washirikina, kupitia Nabii wake Muhammad **(s.a.w.w)**, dalili za kutosha juu ya haki, pia mawaidha ya kutosheleza ya kuikemea batili.

Hikima kamili.

Kila lilioko katika Qur’an ni hekima iliyofikia ukomo wa mawaidha na dalili juu ya haki, lakini maonyo hayafai kitu, kukiwa na inadi na kung’ang’ania ukafiri na upotevu. Basi jiepushe nao, ewe Muhammad, kwa sababu umewafikishia ujumbe wa Mola wako, lakini hawakukuitikia. Na ukafikisha nasaha, lakini hawakukubali.

Siku atakapoita mwitaji kuliendea jambo linalochusha. Macho yao yatainama; watatoka makaburini. Jambo linalochusha ni linalochukiwa na nafsi na kutochukulika. Makusudio yake hapa ni adhabu.

Hii ni kuwahofisha na kuwapa kiaga wale walioipinga haki, na kwamba wao wana siku ngumu isiyokuwa na kimbilio la adhabu yake, nayo ni siku watakayotoka makaburini kuelekea kwa Mola wao na hisabu, wakiwa madhalili wanyenyekevu, waamejawa na mshangao na kuchanganyikiwa.

Kama kwamba wao ni nzige waliotawanyika kutokana na wingi wao pale Mwenyezi Mungu atakapowafufua wafu na kuwausanya, watakapokutana wa mwanzo hadi wa mwisho.

Hapa kuna ishara ya kuwa ufufuo utakuwa kwa roho na mwili pamoja.

Wanamkimbilia mwitaji.

Yaani watakwenda haraka kwenye hisabu na malipo.

Makafiri wanasema: Hii ni siku ngumu yenye vituko, hatari, maumivu na hofu.

Mfano wake ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtufu:

يَوْمَ يَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ سِرَاعًا كَأَنَّهُمْ إِلَىٰ نُصُبٍ يُوفِضُونَ ﴿٤٣﴾ خَاشِعَةً أَبْصَارُهُمْ تَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ ۚ ذَٰلِكَ الْيَوْمُ الَّذِي كَانُوا يُوعَدُونَ ﴿٤٤﴾

“Siku watakapotoka makaburini kwa upesi; kama kwamba wao wanakimbilia kwenye mradi. Macho yao yatainama, fedhea itawafunika. Hiyo ndiyo Siku waliyokuwa wakiahidiwa.” (70:43-44).

﴿كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ فَكَذَّبُوا عَبْدَنَا وَقَالُوا مَجْنُونٌ وَازْدُجِرَ ﴿٩﴾

9. Kabla yao kaumu ya Nuh walikadhibisha; wakamkadhibisha mja wetu, na wakasema ni mwendawazimu, na akakaripiwa.

﴿فَدَعَا رَبَّهُ أَنِّي مَغْلُوبٌ فَانتَصِرْ ﴿١٠﴾

10. Basi akamwomba Mola wake: Kwa hakika mimi nimeshindwa, basi ninusuru!

﴿فَفَتَحْنَا أَبْوَابَ السَّمَاءِ بِمَاءٍ مُّنْهَمِرٍ ﴿١١﴾

11. Basi tukaifungua milango ya mbingu kwa maji yanayomiminika.

﴿وَفَجَّرْنَا الْأَرْضَ عُيُونًا فَالْتَقَى الْمَاءُ عَلَىٰ أَمْرٍ قَدْ قُدِرَ ﴿١٢﴾

12. Na tukaipasua ardhi kwa chemchem, yakakutana maji kwa jambo liliokadiriwa.

﴿وَحَمَلْنَاهُ عَلَىٰ ذَاتِ أَلْوَاحٍ وَدُسُرٍ ﴿١٣﴾

13. Na tukamchukua kwenye ile ya mbao na misumari.

﴿تَجْرِي بِأَعْيُنِنَا جَزَاءً لِّمَن كَانَ كُفِرَ ﴿١٤﴾

14. Inakwenda kwa macho yetu. Ni malipo kwa alivyokuwa amekanushwa.

﴿وَلَقَد تَّرَكْنَاهَا آيَةً فَهَلْ مِن مُّدَّكِرٍ ﴿١٥﴾

15. Na hakika tuliiacha iwe ni Ishara. Basi je, yupo anayekumbuka?

﴿فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنُذُرِ ﴿١٦﴾

16. Basi ilikuwaje adhabu yangu, na maonyo?

﴿وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِن مُّدَّكِرٍ ﴿١٧﴾

17. Na hakika tumeifanya Qur'an iwe nyepesi kuikumbuka. Basi je yupo anayekumbuka?

## NUH

**Aya 9 – 17**

### MAANA

Katika Aya zilizotangulia Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliashiria kwamba Muhammad **(s.a.w.w)** aliwaonya watu wake, lakini hayakufaa maonyo. Katika Aya tulizonazo anaashiria kuwa hali ya Muhammad **(s.a.w.w)** na watu wake, katika hilo, ni kama hali ya Nuh, na watu wake:

Kabla yao kaumu ya Nuh walikadhibisha; wakamkadhibisha mja wetu.

Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtufu: "wakamkadhibisha ni tafsiri ya kauli yake: "Walikadhibisha." Kama kwamba muulizaji aliuliza: hawa jamaa walimkadhibisha nani? Mwenyezi Mungu (s.w.t) akajibu kuwa wao walimkadhibisha mja wetu Nuh, na wakasema ni mwendawazimu; sawa na walivyosema makuraishi kumwambia Mtume mtufu **(s.a.w.w)**.

Shutuma hii ni ya kawaida kwa wale wanaoshindwa kujibu.

Na akakaripiwa.

Hapa Mwenyezi Mungu anaashiria yale aliyosema katika kauli yake:

﴿قَالُوا لَئِن لَّمْ تَنتَهِ يَا نُوحُ لَتَكُونَنَّ مِنَ الْمَرْجُومِينَ ﴿١١٦﴾

“Wakasema: kama hutakoma ewe Nuh, bila shaka utapigwa mawe.” Juz.19 (26.116).

Walimkemea, wakamzuia kufikisha na wakamtisha kumpiga mawe na kumuua kama ataendelea.

Basi akamwomba Mola wake Mlezi: Kwa hakika mimi nimeshindwa, basi ninusuru!

Watu wa Nuh walipodhikika naye, naye akadhikika nao, alimkimbilia Mola wake na kusema kuwa nimemaliza mbinu zote na kazi yangu ya tabligh imefika ukomo, sasa iliyobaki ni amri yako kwa watu hawa makafiri waovu, basi waadhibu na uinusuru dini yako na mjumbe wako.

Kwa hakika Nuh hakuwaapiza watu wake ila baada ya kukata tamaa nao. Aliendelea kuwalingania kiasi cha miaka elfu kupungua hamsini bila ya mafanikio; kama ilivyoelezwa katika Juz.20 (29:14).

Basi tukaifungua milango ya mbingu kwa maji yanayomiminika. Na tukaipasua ardhi kwa chemchem.

Dua ya Nuh iliitikiwa na Mwenyezi Mungu, akawagharikisha kwa maji yanayotoka mbinguni na yanayotoka ardhini, yakakutana maji kwa jambo liliokadiriwa.

Yaani mvua na chemchem zikachanganyika ikawa ni bahari kubwa kila upande. Hakuna aliyesalimika isipokuwa aliyekuwa katika Jahazi (safina).

Tufani na maangamizi haya yalikuwa ni kwa amri iliyokadiriwa. Kwa hiyo kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: ‘Kwa jambo lililokadiriwa,’ iko katika maana ya kauli yake:

وَكَانَ أَمْرُ اللَّـهِ قَدَرًا مَّقْدُورًا ﴿٣٨﴾

“Na amri ya Mwenyezi Mungu ni kadari iliyokadiriwa.” Juz. 22 (33:38).

Na tukamchukua kwenye ile ya mbao na misumari

Aliyechukuliwa ni Nuh. Maana ni kuwa safina ilikuwa kama majahazi mengineyo, ilitengenezwa kwa mbao na misumari, lakini inakwenda kwa macho yetu, kwa hifadhi na kuilinda. Kwa hiyo ikaokoka na hatari; vinginevyo isingeweza kuhimili mikikimikiki ya tufani.

Ni malipo kwa alivyokuwa amekanushwa.

Neno ‘malipo’ linaashiria sababu zilizowajibisha tufani na kuangamia makafiri.

Na hakika tuliiacha iwe ni Ishara. Lakini je, yupo anayekumbuka?

Yaani Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliiacha habari ya safina iwe ni somo na mawaidha kwa yule anayewaidhika kwa mazingatio.

Basi ilikuwaje adhabu yangu, na maonyo?

Ni kweli kabisa tufani iliangamiza. Ama Nuh, mwenye kutoa bishara na maonyo, alikuwa ni mkweli katika aliyoyafikisha na kuyatolea maonyo.

Na hakika tumeifanya Qur’an iwe nyepesi kuikumbuka.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliiteremsha Qur’an kwa ajili ya ukumbusho na maonyo, na ameyafanya mepesi maana yake kufahamika ili wanufaike nayo, sio watajirike kwa matamshi yake, kuzifanyia dawa Aya zake, au kuzipotoa na kuziuza kwa thamani ndogo.

Basi je yupo anayekumbuka?

Je, watazingatia na kupata onyo, kwa yaliyokuja katika Qur’an, wale wanaoifanyia biashara dini na kuyabadilisha maneno sehemu zake kwa kufuata matamanio yao na malengo yao?

Kisa cha Nuh kimetangulia katika sura Hud, iliyo kwenye Juzuu ya 12, na nyinginezo.

﴿كَذَّبَتْ عَادٌ فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنُذُرِ ﴿١٨﴾﴾

18. A'di walikadhibisha. Basi ilikuwaje adhabu yangu na maonyo?

﴿إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِيحًا صَرْصَرًا فِي يَوْمِ نَحْسٍ مُّسْتَمِرٍّ ﴿١٩﴾﴾

19. Hakika tuliwapelekea upepo mkali katika siku ya Nuhsi iendeleayo.

﴿تَنزِعُ النَّاسَ كَأَنَّهُمْ أَعْجَازُ نَخْلٍ مُّنقَعِرٍ ﴿٢٠﴾﴾

20. Ukiwaangusha watu kama vigogo vya mitende vilivyong'olewa.

﴿فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنُذُرِ ﴿٢١﴾﴾

21. Basi ilikuwaje adhabu yangu na maonyo?

﴿وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِن مُّدَّكِرٍ ﴿٢٢﴾﴾

22. Na hakika tumeifanya Qur'an iwe nyepesi kuikumbuka. Basi je yupo anayekumbuka?

﴿كَذَّبَتْ ثَمُودُ بِالنُّذُرِ ﴿٢٣﴾﴾

23. Thamudi waliwakadhibisha waonyaji.

﴿فَقَالُوا أَبَشَرًا مِّنَّا وَاحِدًا نَّتَّبِعُهُ إِنَّا إِذًا لَّفِي ضَلَالٍ وَسُعُرٍ ﴿٢٤﴾﴾

24. Wakasema: Je tumfuate mtu mmoja miongoni mwetu? Basi hivyo sisi tutakuwa katika upotofu na kichaa!

﴿أَأُلْقِيَ الذِّكْرُ عَلَيْهِ مِن بَيْنِنَا بَلْ هُوَ كَذَّابٌ أَشِرٌ ﴿٢٥﴾﴾

25. Ni yeye tu aliyeteremshiwa huo ukumbusho kati yetu? Bali huyu ni mwongo mwenye kiburi!

﴿سَيَعْلَمُونَ غَدًا مَّنِ الْكَذَّابُ الْأَشِرُ ﴿٢٦﴾﴾

26. Kesho watajua ni nani huyo mwongo mwenye kiburi.

﴿إِنَّا مُرْسِلُو النَّاقَةِ فِتْنَةً لَّهُمْ فَارْتَقِبْهُمْ وَاصْطَبِرْ ﴿٢٧﴾﴾

27. Hakika Sisi tutawapelekea ngamia jike ili kuwajaribu. Basi watazame tu na usubiri.

﴿وَنَبِّئْهُمْ أَنَّ الْمَاءَ قِسْمَةٌ بَيْنَهُمْ كُلُّ شِرْبٍ مُّحْتَضَرٌ ﴿٢٨﴾﴾

28. Na waambie kwamba maji yatagawanywa baina yao; kila sehemu itahudhuriwa.

﴿فَنَادَوْا صَاحِبَهُمْ فَتَعَاطَىٰ فَعَقَرَ ﴿٢٩﴾﴾

29. Basi wakamwita mtu wao akaja akamchinja.

﴿فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِي وَنُذُرِ ﴿٣٠﴾﴾

30. Basi ilikuwaje adhabu yangu na maonyo?

﴿إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ صَيْحَةً وَاحِدَةً فَكَانُوا كَهَشِيمِ الْمُحْتَظِرِ ﴿٣١﴾﴾

31. Hakika tuliwapelekea ukelele mmoja tu, wakawa kama majani makavu yaliyosagika yaliyo zizini.

﴿وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِن مُّدَّكِرٍ ﴿٣٢﴾﴾

32. Na hakika tumeifanya Qur'an iwe nyepesi kuikumbuka, Basi je yupo anayekumbuka?

## HUD NA SWALEH

**Aya 18 – 32**

### MAANA

A'di walikadhibisha. Basi ilikuwaje adhabu yangu na maonyo?

A'di ni kaumu ya Hud. Walimkadhibisha Nabii wao, Mwenyezi Mungu akawaadhibu kwa adhabu chungu. Akabainisha aina hii ya adhabu kwa kusema:

Hakika tuliwapelekea upepo mkali katika siku ya Nuhsi iendeleayo.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliwapelekea upepo wa kimbunga katika siku ngumu na hatari. Uliendelea upepo wa adhabu siku hiyo mpaka ukawamaliza wote.

Ukiwaangusha watu kama vigogo vya mitende vilivyong'olewa.

Kimbunga kiliwang'oa kutoka sehemu zao na kuwatupa chini kama vigogo vya mtende vilivyong'olewa ardhini.

Basi ilikuwaje adhabu yangu na maonyo?

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amelikariri hilo ili kusisitiza kutoa hadhari na maonyo.

Na hakika tumeifanya Qur'an iwe nyepesi kuikumbuka. Basi je yupo anayekumbuka?

Tazama Aya 17 ya sura hii tuliyo nayo, nuku yake na tafsiri yake ni moja tu.

Thamudi waliwakadhibisha waonyaji.

Thamud ni kaumu ya Swaleh. Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameleta tamko la wengi pamoja na kuwa aliyekadhibishwa ni mmoja tu, Swaleh, kwa sababu kumkadhibisha Nabii mmoja ni sawa na kuwakadhibisha manabii wote, kutokana na kuwa risala ni moja na anayewatuma ni mmoja.

Wakasema: Je tumfuate mtu mmoja miongoni mwetu? Basi hivyo sisi tutakuwa katika upotofu na kichaa!

Swaleh ni katika sisi na miongoni mwetu, tumemjua tangu utotoni na ukubwani, vipi tumfuate; wala hakuna anayemfuata na kumsadiki isipokuwa mpotevu. Ndio lau angelikuwa na mali, watumishi na wajakazi, ingelifaa kumfuata.

Ni yeye tu aliyeteremshiwa huo ukumbusho kati yetu?

Haiwezekani kabisa! Itakuwaje na yeye ni mmoja wetu:

وَلَئِنْ أَطَعْتُم بَشَرًا مِّثْلَكُمْ إِنَّكُمْ إِذًا لَّخَاسِرُونَ ﴿٣٤﴾

"Na nyinyi mkimtii mtu kama nyinyi basi hakika mtakuwa hasarani." Juz. 18 (23:34).

Bali huyu ni mwongo mwenye kiburi!

Kwa mantiki yao ni kuwa inatosha kuwa ni mwongo kwa vile anatokana nao na ni miongoni mwao. Kwa hiyo suala ni aina ya mtu na wala sio haki na msingi.

Hili si geni! Ndio mantiki ya watu wa chumo na vyeo, kila mahali na kila wakati na vile vile mantiki ya wajinga na waigaji.

Kesho watajua ni nani huyo mwongo mwenye kiburi, kuwa je, ni Swaleh au wale ambao wamemkadhibisha.

Ndio! Watajua karibu kwamba wao ndio wazushi pale Mwenyezi Mungu atakapowapa mtihani wa ngamia, kisha wamchinje na wapate ghadhabu na adhabu ifedheheshayo.

Hakika Sisi tutawapelekea ngamia jike ili kuwajaribu.

Ni mtihani wa kuwapambanua muovu na mwema.

Basi watazame tu na usubiri.

Ngoja kidogo ewe Swaleh na uvumilie maudhi yao, utaona vile watakavyopatwa na adhabu.

Na waambie kwamba maji yatagawanywa baina yao; kila sehemu itahudhuriwa na atakayehusika.

Wape habari kuwa maji yatagawanywa baina yao na ngamia. Siku moja itakuwa yao na na nyingine ya ngamia.

Basi wakamwita mtu wao akaja akamchinja.

Hawakuwa radhi kugawana maji, ndio wakamwita yule muovu wao zaidi ili amchinje ngamia. Akaitikia yule muovu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Thamud walikadhibisha kwa sababu ya uovu wao. Alipofanya haraka muovu wao zaidi" (91:11-12). Basi walimchinja ngamia na adhabu ikawashukia.

Wametofautiana katika Makusudio ya neno 'taatwa,' tulilolifasiri kwa maana ya 'akaja.' Kuna waliosema kuwa Makusudio yake ni kuwa yule muovu alikunywa pombe kabla ya kuchinja. Wengine wakasema ni kuchukua ala ya kuchinjia. Sio mbali kuwa Makusudio yake hapa ni kuja bila ya kujali.

Basi ilikuwaje adhabu yangu na maonyo?

Yalikuwa ni ya kubomoa. Kukaririka ni msisitizo wa kuhadharisha na kuonya

Hakika tuliwapelekea ukelele mmoja tu, wakawa kama majani makavu yaliyosagika yaliyo zizini.

Walipigwa na ukelele mmoja tu, wakawa kama majani makavu yaliyovunjikavunjika yanayopeperushwa na upepo. Mwenye Al-Manar anasema: "Mara nyingi neno Hashim hutumiwa kwa majani yaliyovunjika vunjika."

Majani haya anayakusanya mwenye zizi kwa ajili ya wanyama wake. Kwa hiyo basi wasifa huu umekuja kwa njia ya majazi, (kufananisha). sio uhakika

Na hakika tumeifanya Qur'an iwe nyepesi kuikumbuka. Basi je yupo anayekumbuka?

Huenda akanufaika na kukaririka huku mwenye kupotea njia. Kimetangulia kisa cha Hud na Swaleh katika Sura ya Hud.

21

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

كَذَّبَتْ قَوْمُ لُوطٍ بِالنُّذُرِ ﴿٣٣﴾

33. Watu wa Lut waliwakadhibisha waonyaji.

إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ حَاصِبًا إِلَّا آلَ لُوطٍ ۖ نَّجَّيْنَاهُم بِسَحَرٍ ﴿٣٤﴾

34. Hakika tuliwapelekea kimbunga cha vijiwe. Isipokuwa wafuasi wa Lut. Tuliwaokoa karibu na alfajiri.

نِّعْمَةً مِّنْ عِندِنَا ۚ كَذَٰلِكَ نَجْزِي مَن شَكَرَ ﴿٣٥﴾

35. Kwa neema inayotoka kwetu. Hivyo ndivyo tunavyomlipa anayeshukuru.

وَلَقَدْ أَنذَرَهُم بَطْشَتَنَا فَتَمَارَوْا بِالنُّذُرِ ﴿٣٦﴾

36. Na hakika yeye aliwaonya mkamato wetu; lakini waliyatilia shaka hayo maonyo.

وَلَقَدْ رَاوَدُوهُ عَن ضَيْفِهِ فَطَمَسْنَا أَعْيُنَهُمْ فَذُوقُوا عَذَابِي وَنُذُرِ ﴿٣٧﴾

37. Na walimtaka awape wageni wake, tukayapofua macho yao. Basi onjeni adhabu na maonyo yangu!

وَلَقَدْ صَبَّحَهُم بُكْرَةً عَذَابٌ مُّسْتَقِرٌّ ﴿٣٨﴾

38. Na iliwafikia asubuhi adhabu ya kuendelea.

فَذُوقُوا عَذَابِي وَنُذُرِ ﴿٣٩﴾

39. Basi onjeni adhabu na maonyo yangu!

وَلَقَدْ يَسَّرْنَا الْقُرْآنَ لِلذِّكْرِ فَهَلْ مِن مُّدَّكِرٍ ﴿٤٠﴾

40. Na hakika tumeifanya Qur'an iwe nyepesi kuikumbuka. Basi je yupo anayekumbuka?

وَلَقَدْ جَاءَ آلَ فِرْعَوْنَ النُّذُرُ ﴿٤١﴾

41. Na waonyaji waliwafikia watu wa Firauni.

كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا كُلِّهَا فَأَخَذْنَاهُمْ أَخْذَ عَزِيزٍ مُّقْتَدِرٍ ﴿٤٢﴾

42. Walizikadhibisha Ishara zetu zote, tukawashika mshiko wa Mwenye nguvu, Mwenye uweza.

## LUT

**Aya 33 – 42**

### MAANA

Watu wa Lut waliwakadhibisha waonyaji, sawa na walivyokadhibisha watu wa Nuh, A'di Thamud na wengineo. Siri yao ni moja tu, mapambano ya haki na batili na uadilfu na dhulma. Kisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) akabainisha aina ya adhabu iliyowashukia watu wa Lut kwa kusema:

Hakika tuliwapelekea kimbunga cha vijiwe.

Yaani aliwatupia vijiwe vilivyochukuliwa na upepo. Vijiwe hivi ndivyo alivyovitaja Mwenyezi Mungu katika Juzuu hii tuliyonayo (51:33).

Isipokuwa wafuasi wa Lut. Hao tuliwaokoa karibu na alfajiri.

Mwenyezi Mungu alimwokoa Lut na wale waliokuwa pamoja naye, pale alipowatoa usiku kutoka kwenye kijiji ambacho watu wake wamekuwa madhalimu.

Kwa neema inayotoka kwetu. Hivyo ndivyo tunavyomlipa anayeshukuru.

Mwenyezi Mungu alimwadhibu aliyeasi na akamneemesha aliyetii kwa kutumia misingi ya uadilifu. Lakini Razi anasema: "Hata kama wangeliaangamizwa watu wa Lut pia ingelikuwa ni uadilifu."

Mwenyezi Mungu ndiye mkweli zaidi wa mazungumzo; naye ndiye aliyesema:

وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ صِدْقًا وَعَدْلًا ۚ لَّا مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِهِ ﴿١١٥﴾

"Na limetimia neno la Mola wako kwa ukweli na uadlifu. Hakuna wa kubadilisha neno lake."

Juz. 8 (6:115).

Yaani uadilifu ni ule uliokwishatimia; vinginevyo ni dhulma.

Na hakika yeye aliwaonya mkamato wetu; lakini waliyatilia shaka hayo maonyo.

Lut aliwahadharisha na adhabu ya Mwenyezi Mungu, lakini wakatia shaka na wakadharau; bali hata walitoa vitisho na:

قَالُوا لَئِن لَّمْ تَنتَهِ يَا لُوطُ لَتَكُونَنَّ مِنَ الْمُخْرَجِينَ ﴿١٦٧﴾

"Wakasema: kama hutakoma ewe Lut, bila shaka utakuwa miongoni mwa watakaotolewa."

Juz. 19 (26:167).

Na walimtaka awape wageni wake.

Walisikia kuwa kuna wageni kwa Lut, kwa hiyo wakaenda kwake haraka na wakamwambia kwa ufidhuli: tupatie wageni wako tuwafanyie uchafu.

Tukayapofua macho yao.

Yaani Mwenyezi Mungu aliyatia upofu macho yao wasiweze kuwaona, kisha akawapelekea adhabu na akawaambia: Basi onjeni adhabu na maonyo yangu ambayo miliyatilia shaka na kuyadharau

Na iliwafikia asubuhi adhabu ya kuendelea.

Iliwafikia adhabu asubuhi, ikaendela hadi ikawamaliza wote.

Basi onjeni adhabu na maonyo yangu!

Haya ameyasema Mwenyezi Mungu (s.w.t) baada ya adhabu ya kupofuka, kisha akayakariri baada ya adhabu ya mawe

Na hakika tumeifanya Qur'an iwe nyepesi kuikumbuka. Basi je yupo anayekumbuka?

Ameikariri Aya hii, ambaye imetukuka hikima yake, mara nne: Ya kwanza ni baada ya kuashiria kisa cha Nuh, ya pili ni baada ya kisa cha Hud, ya tatu baada ya kisa cha Swaleh na ya nne ni hapa baada ya kisa cha Lut.

Lengo ni kupata mazingatio na mafunzo katika kila moja ya visa hivi vine. Kwa sababu ni tosha kabisa katika waadhi na ukumbusho.

Kisa cha Lut kimekwisha tangulia katika sura ya 11, katika Juz.12, na nyinginezo.

Na Waonyaji waliwafikia watu wa Firauni.

Mfano wake ni Aya isemayo:

﴿ثُمَّ بَعَثْنَا مِن بَعْدِهِم مُّوسَىٰ بِآيَاتِنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ ﴿١٠٣﴾

"Kisha baada yao tukamtuma Musa na ishara zetu kwa Firauni na wakuu wake" Juz. 9 (7:103)

Walizikadhibisha Ishara zetu zote; nazo zilikuwa tisa; kama anavyosema Mwenyezi Mungu:

﴿وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ تِسْعَ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ ﴿١٠١﴾

"Hakika tulimpa Musa Ishara tisa zilizo wazi." Juz. 15 (17:101).

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amezitaja tano pale aliposema:

﴿فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الطُّوفَانَ وَالْجَرَادَ وَالْقُمَّلَ وَالضَّفَادِعَ وَالدَّمَ آيَاتٍ مُّفَصَّلَاتٍ ﴿١٣٣﴾

"Basi tukawapelekea tufani na nzige na chawa na vyura na damu kuwa ishara mbalimbali, Juz. 9 (7:133).

Nyingine nne amezitaja katika Aya mbalimbali; nazo ni mkono, fimbo, kufunguka kifundo katika ulimi wa Musa na kupasuka bahari.

Tukawashika mshiko wa Mwenye nguvu Mwenye uweza.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimwangamiza Firauni na watu wake majini na hapo mwanzo alikuwa akiwaambia watu wake: Mimi ndiye Mola wenu mkuu. Basi Mwenyezi Mungu akamuonjesha adhabu ya hizaya ya dunia na adhabu ya Akhera ni kubwa zaidi.

﴿أَكُفَّارُكُمْ خَيْرٌ مِّنْ أُولَٰئِكُمْ أَمْ لَكُم بَرَاءَةٌ فِي الزُّبُرِ ﴿٤٣﴾

43. Je, Makafiri wenu ni bora kuliko hao, au yameandikwa vitabuni kuwa nyinyi mtaachwa?

﴿أَمْ يَقُولُونَ نَحْنُ جَمِيعٌ مُّنتَصِرٌ ﴿٤٤﴾

44. Au ndio wanasema: Sisi ni wengi tutashinda?

﴿سَيُهْزَمُ الْجَمْعُ وَيُوَلُّونَ الدُّبُرَ ﴿٤٥﴾

45. Wingi wao huu utashindwa, na watasukumwa nyuma.

﴿بَلِ السَّاعَةُ مَوْعِدُهُمْ وَالسَّاعَةُ أَدْهَىٰ وَأَمَرُّ ﴿٤٦﴾

46. Bali Saa ndio miadi yao, na Saa hiyo ni nzito sana na chungu zaidi.

﴿إِنَّ الْمُجْرِمِينَ فِي ضَلَالٍ وَسُعُرٍ ﴿٤٧﴾

47. Hakika wakosefu wamo katika upotofu na mioto.

﴿يَوْمَ يُسْحَبُونَ فِي النَّارِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ ذُوقُوا مَسَّ سَقَرَ ﴿٤٨﴾

48. Siku watakapokokotwa Motoni kifudifudi: Onjeni mguso wa Jahannamu!

﴿إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَاهُ بِقَدَرٍ ﴿٤٩﴾

49. Kwa hakika tumekiumba kila kitu kwa kipimo.

﴿وَمَا أَمْرُنَا إِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَمْحٍ بِالْبَصَرِ ﴿٥٠﴾

50. Na amri yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.

﴿وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا أَشْيَاعَكُمْ فَهَلْ مِن مُّدَّكِرٍ ﴿٥١﴾

51. Na bila ya shaka tumekwisha waangamiza wenzenu. Je, yupo anayekumbuka?

﴿وَكُلُّ شَيْءٍ فَعَلُوهُ فِي الزُّبُرِ ﴿٥٢﴾

52. Na kila kitu walichokifanya kimo vitabuni.

﴿وَكُلُّ صَغِيرٍ وَكَبِيرٍ مُّسْتَطَرٌ ﴿٥٣

53. Na kila kidogo na kikubwa kimeandikwa.

﴿إِنَّ الْمُتَّقِينَ فِي جَنَّاتٍ وَنَهَرٍ ﴿٥٤

54. Hakika wenye takua watakuwa katika Mabustani na mito.

﴿فِي مَقْعَدِ صِدْقٍ عِندَ مَلِيكٍ مُّقْتَدِرٍ ﴿٥٥

55. Katika makalio ya haki kwa Mfalme Mwenye uweza.

## KILA KITU TUMEKIUMBA KWA KIPIMO

**Aya 43 – 55**

### MAANA

Je, Makafiri wenu ni bora kuliko hao?

Maneno yanaelekezwa kwa Muhammad **(s.a.w.w)**. Hao ni watu wa uma zili- zotangulia walioangamia kwa sababu ya kufuru na inadi yao. Katika Aya zilizotangulia Mwenyezi Mungu ametaja aina za adhabu zilizowapata.

Maana ni kuwa nyinyi sio bora zaidi ya tuliowaangamiza; bali nyinyi ni waovu zaidi na wenye uasi zaidi kwa Mwenyezi Mungu. Je, mmejiaminisha yasiwapate yale yaliyowapata wenzenu au yameandikwa vitabuni kuwa nyinyi mtaachwa? Je, Mwenyezi Mungu ameteremsha katika kitabu chochote miongoni mwa vitabu vyake kuwa nyinyi mtasalimika na adhabu yake?

Au ndio wanasema: Sisi ni wengi tutashinda?

Hivi nyinyi mnadai kwa ni kundi kubwa lilisiloshindwa?

Wingi wao huu utashindwa, na watasukumwa nyuma.

Iliposhuka Aya hii washirikina ndio waliokuwa na nguvu, kwa vile walikuwa wengi. Ama waislamu walikuwa ni mmoja mmoja wadhaifu. Mshirikina yeyote alikuwa na uwezo wa kumuudhi Mwislamu.

Lakini hazikupita siku na mambo yakageuka, washirikina wakasukumwa nyuma, Uislamu na waislamu wakawa juu, na ikabainika kwa ukaribu na umbali kuwa kauli yake Mwenyezi Mungu: 'Wingi wao huu utashindwa,' kuwa ni kweli. Hii peke yake ni ubainifu mkataa kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) anatamka kupitia kwenye ulimi wa Mtume wake mtukufu **(s.a.w.w)**.

Bali Saa ya Kiyama ndio miadi yao, na Saa hiyo ni nzito sana na chungu zaidi.

Neno 'yao,' linawarudia wote, kuanzia kaumu ya Nuh mpaka makafiri wa Kiarabu ambao walimkadhibisha Muhammad **(s.a.w.w)**. Maana ni kuwa kila adhabu iliyowapata makafiri duniani, si chochote kulinganisha na adhabu ya Akhera. Kila balaa isiyokuwa Moto hiyo ni salama.

Hakika wakosefu wamo katika upotofu na mioto. Siku watakapokokotwa Motoni kifudifudi waambiwe: Onjeni mguso wa Jahannamu!

Hii ni tafsiri na ubainifu wa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: 'Na Saa hiyo ni nzito sana na chungu zaidi.' Watu wa motoni hawatatosheka na vituko vyake tu, bali Malaika wa adhabu watawahamishia kwenye adhabu mbalimbali; kama vile kuvutwa kifudifudi, makomeo ya chuma na mengineyo yasiyoelezeka.

Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo.

Aya ya pili inasema:

﴿وَخَلَقَ كُلَّ شَيْءٍ فَقَدَّرَهُ تَقْدِيرًا ﴿٢﴾

"Na ameumba kila kitu na akakikadiria kipimo." Juz. 18 (25:2).

Ya tatu inasema:

﴿وَكُلُّ شَيْءٍ عِندَهُ بِمِقْدَارٍ ﴿٨﴾

"Na kila kitu kwake ni kwa kipimo." Juz. 13 (13:8).

Ya nne:

﴿الَّذِي خَلَقَ فَسَوَّىٰ ﴿٢﴾ وَالَّذِي قَدَّرَ فَهَدَىٰ ﴿٣﴾

"Ambaye ameumba akalinganisha sawa na Ambaye amekadiria na akaongoza." (87:2-3).

Na kuna Aya nyinginezo nyingi zinazofamisha kuwa hakuna kitu chochte kilichopo ila kimekadiriwa kwa kipimo maalum na sifa zisizozidi wala kupungua vile inavyotakikana na kwamba kila kilichomo ndani yake kitakuwa kimepangwa kwa mpangilio mzuri na kuweka mahali panapolingana na wadhifa na umuhimu wake.

Tukitafuta kilichosababisha hivyo kinachokubalika kiakili, hatupati isipokuwa utashi wa Mwenyezi Mungu ambao uko nyuma ya kila kitu. Anasema Conte: "Maumbile ni kama kazi ya usanii. Kuitolea dalili ya chimbuko lake ni sawa na kutolea dalili athari pale ilipotokea."

**Unaweza kuuliza**: Hiwezekani kuwa nidhamu hii imetokana na kazi ya sadfa?

**Jibu**: Sadfa kama lilivyo jina lake, haiwezekani kukaririka. Kuyafasiri matukio kwa sadfa, itakuwa ni kukimbia. Hayo ni kwa hukumu ya akili na uhalisia. Ndio maana wakasema maulama kuwa, hakimbilii kwenye sadfa ila mwenye kushindwa.

Zaidi ya hayo, kama nadharia hii ingelikuwa sahihi basi ilimu isingelikuwa na maana kabisa. Kwa sababu ilimu ina misingi maalumu; vinginevyo itakuwa si ilimu. Kinyume na sadfa ambayo huwa haina maaudhui maalumu, na kama itakuwa na maaudhui maalum, basi itakuwa nayo siyo sadfa.

Ikiwa sadfa ni batili, basi madhehebu ya wanaosema kuwa maada ndio asilili ya kila kitu nayo yatakuwa ni batili.

Ni nani mwenye akili anayeweza kukubali kuwa ulimwengu umepatikana kwa sadfa, kila kilichomo ndani yake ikiwemo kanunui na nidhamu imepatikana kwa sadfa na maada nayo imepatikana kwa sadfa? Hapa ndio tunakuta tafsiri ya kauli ya msahiri: "Kila kitu ni ishara kwake kutambulisha umoja wake."

Pia tafsiri ya aliyesema: "Uwezekano si zaidi ya ulivyo." Yaani kila kitu kimewekwa mahali panaponasibiana nacho, lau kitaepuka hata kiasi cha unywele basi itabainika kasoro na upungufu.

Na amri yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.

Hiki ni kinaya cha kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) akitaka kukileta kitu ni kiasi cha kutaka tu, wala hahitajii wakati hata ule wa kupepesa jicho au chini yake. Ametaja kupepesa jicho kwa kiasi cha kuleta karibu maana tu.

Kwa maneno ya wanafalsafa ni kuwa mnasaba wa matakwa yake Mwenyezi Mungu kwa anachokitaka ni kama mnasaba wa kupatikana kinachopatikana.

Na bila ya shaka tumekwishawaangamiza wenzenu. Je, yupo anayekumbuka?

Katika wakati uliopita walikuweko wenzenu waliojiona kama mnavyojiona nyinyi enyi washirikina wa kiarabu; wakawakadhibisha mitume wao kama nyinyi mnavyomkadhibisha Muhammad (s.a.w.), Mwenyezi Mungu akawapondaponda kabisa. Basi chukuueni somo kwao kabla ya kuchukuliwa somo nyinyi.

Na kila kitu walichokifanya kimo vitabuni. Na kila kidogo na kikub- wa kimeandikwa.

Si kauli wala kitendo, kiwe kidogo au kikubwa kitakuwa kimethibitishwa, kwa aliyekitenda, katika ilimu ya Mwenyezi Mungu. Mwenye faida ni yule anayejihisabu kabla ya kuhisabiwa.

Hakika wenye takua watakuwa katika Mabustani na mito. Katika makalio ya haki kwa Mfalme Mwenye uweza.

Wenye takua ni wale waliojiangalia na wasijiingize kwenye maangamizi kwa kumuasi Mwenyezi Mungu. Wakajihisabu kwa kila dogo na kubwa, wakawa ni wenye kukurubishwa kwa Mwenyezi Mungu.

## MWISHO WA SURA YA HAMSINI NA NNE: SURAT AL-QAMAR

22

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

Sura Ya Hamsini Na Tano: Surat Ar-Rahman. Ina Aya 78.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

الرَّحْمَـٰنُ ﴿١﴾

1. Mwingi wa Rehema.

عَلَّمَ الْقُرْآنَ ﴿٢﴾

2. Amefundisha Qur'an.

خَلَقَ الْإِنسَانَ ﴿٣﴾

3. Amemuumba mtu,

عَلَّمَهُ الْبَيَانَ ﴿٤﴾

4. Akamfundisha ubainifu.

الشَّمْسُ وَالْقَمَرُ بِحُسْبَانٍ ﴿٥﴾

Jua na mwezi ni kwa hisabu.

وَالنَّجْمُ وَالشَّجَرُ يَسْجُدَانِ ﴿٦﴾

6. Na mimea yenye kutambaa, na miti, inanyenyekea.

وَالسَّمَاءَ رَفَعَهَا وَوَضَعَ الْمِيزَانَ ﴿٧﴾

7. Na mbingu ameziinua, na ameweka mizani,

أَلَّا تَطْغَوْا فِي الْمِيزَانِ ﴿٨﴾

8. Ili msidhulumu katika mizani.

وَأَقِيمُوا الْوَزْنَ بِالْقِسْطِ وَلَا تُخْسِرُوا الْمِيزَانَ ﴿٩﴾

9. Na wekeni mizani kwa haki, wala msipunje katika mizani.

وَالْأَرْضَ وَضَعَهَا لِلْأَنَامِ ﴿١٠﴾

10. Na ardhi ameiweka kwa ajili ya viumbe.

فِيهَا فَاكِهَةٌ وَالنَّخْلُ ذَاتُ الْأَكْمَامِ ﴿١١﴾

11. Humo yamo matunda na mitende yenye mafumba.

وَالْحَبُّ ذُو الْعَصْفِ وَالرَّيْحَانُ ﴿١٢﴾

12. Na nafaka zenye makapi, na mrehani.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿١٣﴾

13. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

## AMEMUUMBA MTU AKAMFUNDISHA UBAINIFU

**Aya 1 – 13**

### MAANA

Mwingi wa Rehema

Katika sura hii Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja neema kadhaa kwa waja wake. Ameanza kwa kwa neno Mwingi wa rehma, kwa vile linaashiria neema na fadhila.

Amefundisha Qur'an.

Yaani ameiteremsha. Qur'an inafana na ulimwengu katika njia kadhaa; miongoni mwazo ni hizi zifutazo:

• Qur'an ni katika maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na ulimwengu umepatakina kwa neno 'Kuwa.'

• Kila moja kati ya Qur'an na ulimwengu unafahamisha kwa hisia uwezo na ukuu wa Mwenyezi Mungu. Ulimwengu unaonekana kwa macho na Qur'an inasikiwa kwa masikio. Ndio mmoja wa waumini akasema kuwa Mwenyezi Mungu ana vitabu viwili: kimoja kinasomwa na kusikiwa nacho ni Qur'an na kingine kinaonekana na kuguswa nacho ni ulimwengu.

• Ulimwengu na Qur'an ni katika uweza wa Mwenyezi Mungu pekee yake hakuna anayeweza kuleta mafano wake.

• Qur'an na ulimwengu ni katika neema kubwa aliyoileta Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa mtu. Ananeemeka na heri za ardhi na mbingu na anaongoka kwa Qur'an kueleka kwenye raha na wema wa nyumba mbili.

Kwa hiyo Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemneemesha mtu kwa jua, mwezi, ardhi, mvua, upepo, mimea, miti, wanyama na mengineyo yasiyokuwa na mwisho.

Amemuumba mtu. Akamfundisha ubainifu.

Makusudio ya ubainifu ni kila linalofahamisha makusudio ya kutamka, hati kuchora au ishara. Hata hivyo kusema, ndio kiungo muhimu zaidi cha ubainifu na chombo chake ni ulimi ambao ndio kiungo kitiifu zaidi kwa mtu, chenye harakati nyingi zaidi na chepesi. Hakijui kuchoka wala kutaabika. Sifa hizi hazipatikani katika viungo vingine.

Ubainifu, hasa maneno, ni katika neema kuu zaidi. Kwayo mtu anaeleza makusudio yake, kufahamu makusudio ya wengine, kujibizana nao kwa upendo, kutekeleza haja zake na za wengine.

Ubainifu unabainisha kufuru na imani, inajikita ilimu, fasihi na fani mbalimbali na kujulikana dini. Baadhi ya ulama wanasema: Kila matumizi ya ilimu yanaelezea ubainifu. Hakuna kitu chochote ila kinatumia ilimu.

Jua na mwezi ni kwa hisabu.

Yaani vinakwenda kwa nidhamu kamili na kanuni thabiti. Kwa nidhamu hii ndio yanahifadhika maisha katika ardhi, ikatofautiana misimu na zikajulikana nyakati.

Na mimea yenye kutambaa, na miti, inanyenyekea.

Neno 'mimea yenye kutambaa' tumelifasiri kutokana na neno la kiarabu annajm kama walivyosema hivyo wafasiri wengi. Kwa sababu Mwenyezi Mungu (s.w.t) amelitaja pamoja na mti kwa mkabala wa jua na mwezi.

Maana ya kusujudi ni kuwa yote hiyo inafahamisha kuweko Mwenyezi Mungu na ukuu wake kutokana na usanii wa hali ya juu kabisa. Tazama kifungu cha maneno:

وَإِن مِّن شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ ﴿٤٤﴾

Na pana kila kitu ila kinamtakasa kwa sifa zake.' katika Juz. 15 (17:44) .

Na mbingu ameziinua, na ameweka mizani.

Makusudio ya mbingu hapa ni kila kilichomo ndani yake miongoni mwa sayari. Na mizani ni kila hakika ya vitu na vipimo vyake vinavyojulikana; viwe vya kimaada kama vile makopo, mita na mizani au vya kimaana kama vile wahyi na misingi ya kiakili na maumbile.

Vile vile makusudio ni kuwa ulimwengu huu wa maajabu umepangika vizuri. Kwa sababu Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameziweka sayari kwenye sehemu zake zinapotakikana; kiasi ambacho lau kama sayari itasogea kidogo tu zaidi ya sehemu yake ilipopangiwa, basi nidhamu ya uliwengu ingelivurugika na kubadilika kila kitu.

Pia hakuna jamii inayoweza kuwa sawa isipokuwa kwa kufuata mizani ya maadili.

Ili msidhulumu katika mizani. Na wekeni mizani kwa haki, wala msipunje katika mizani.

Dhulma ni kupora na kunyang'anya, kupunja ni kutotekeleza haki kwa anayestahiki na kuweka mizani kwa haki ni kutojipunja wala kuwapunja wengine. Ni muhali kupatikana utulivu katika jamii itakayopuuza haki na uadilifu.

Kwa muhtasari ni kuwa Aya hii, pamoja na ufupi wake, ni kuwa imeashiria yale yanayotimiza na yanayoweka nidhamu ya ulimwengu na jamii. La kwanza ni nidhamu ya ulimwengu aliyoitimiza Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa ukamilifu. Ya pili ni nidhamu ya sharia aliyoiwajibisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa waja wake, waichunge na waitekeleze kwa mujibu wake.

Na ardhi ameiweka kwa ajili ya viumbe kuwa ni tandiko na kutafutia maisha. Humo yamo matunda mengi na vyakula vinginevyo na vinywaji na mitende yenye mafumba yanayopasuka na kutoa matunda yanapofikia kuiva.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amehusisha kutaja mti wa mtende kutokana na umuhimu wake kwa waarabu wakati huo[1].

Na nafaka zenye makapi.

Nafaka ni kwa ajili ya chakula cha binadamu na makapi ni kwa ajili ya wanyama.

Na mrehani kwa ajili ya manukato na kujipamba.

Mrehani ni ule mti maarufu unaoitwa hivyo, lakini imesemekena kuwa makusudio yake hapa ni kila mmea wenye harufu nzuri.

Chakula, matunda na maua yote hayo ni katika heri za ardhi na baraka zake alizowaneemesha Mwenyezi Mungu waja wake, lakini wao wanaishi kwa kuziharibu na ufisadi.

Basi ni ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Wawili hapa anaambiwa jinni na mtu kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu: 'Kwa ajili ya viumbe,' inayochanganya aina mbili hizi za viumbe, na pia kauli itakayokuja badae. "Tutawakusudia enyi wazito wawili."

Maana ni kuwa, je anaweza kukana yeyote, katika majini na watu, neema alizozitaja Mwenyezi Mungu (s.w.t)? Vipi anaweza kuzikataa na yeye yumo ndani yake?

---

1.Hata hivyo kuna maoni kuwa bado una umuhimu hadi sasa na baadae kutokana na ubora wa lishe yake yenye faida nyingi za kiafya -Mtarjumu.

خَلَقَ الْإِنسَانَ مِن صَلْصَالٍ كَالْفَخَّارِ ﴿١٤﴾

Amemuumba mtu kwa udongo mkavu kama uliookwa.

وَخَلَقَ الْجَانَّ مِن مَّارِجٍ مِّن نَّارٍ ﴿١٥﴾

15. Na akawaumba majini kwa ulimi wa moto.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿١٦﴾

16. Basi ni ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

رَبُّ الْمَشْرِقَيْنِ وَرَبُّ الْمَغْرِبَيْنِ ﴿١٧﴾

17. Mola wa mashariki mbili na wa magharibi mbili.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿١٨﴾

18. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ يَلْتَقِيَانِ ﴿١٩﴾

19. Anaziendesha bahari mbili zikutane;

بَيْنَهُمَا بَرْزَخٌ لَّا يَبْغِيَانِ ﴿٢٠﴾

20. Baina yao kipo kizuizi, haziingiliani.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٢١﴾

21. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

يَخْرُجُ مِنْهُمَا اللُّؤْلُؤُ وَالْمَرْجَانُ ﴿٢٢﴾

22. Katika hizo bahari mbili zinatoka lulu na marijani.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٢٣﴾

23. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

وَلَهُ الْجَوَارِ الْمُنشَآتُ فِي الْبَحْرِ كَالْأَعْلَامِ ﴿٢٤﴾

24. Na ni vyake Yeye hivi viendavyo baharini vilivyoundwa kama vilima.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٢٥﴾

25. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٢٦﴾

26. Kila kilicho juu yake kitatoweka.

وَيَبْقَىٰ وَجْهُ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٢٧﴾

28. Na itabakia dhati ya Mola wako Mwenye utukufu na ukarimu.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٢٨﴾

28. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

يَسْأَلُهُ مَن فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ كُلَّ يَوْمٍ هُوَ فِي شَأْنٍ ﴿٢٩﴾

29. Vinamwomba Yeye vilivyo katika mbingu na ardhi. Kila siku Yeye yumo katika mambo.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٠﴾

30. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

## KILA SIKU YUMO KATIKA MAMBO

**Aya 14 – 30**

### MAANA

Amemuumba mtu kwa udongo mkavu kama uliookwa.

Makusudio ya mtu ni Adam baba wa watu.

Katika Juz. 14 (15: 26 – 31) Tumechanganya Aya nne; ambazo ni:

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ مِن صَلْصَالٍ مِّنْ حَمَإٍ مَّسْنُونٍ ﴿٢٦﴾

"Na hakika tulimuumba mtu kutokana na udongo mkavu kwa matope meusi yenye kufinyangwa." Juz. 14 (15:26).

وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ مِنَ الْمَاءِ بَشَرًا ﴿٥٤﴾

"Yeye ndiye aliyemuumba mtu kutokana na maji" Juz. 19 (25:54).

كَمَثَلِ آدَمَ خَلَقَهُ مِن تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ كُن فَيَكُونُ ﴿٥٩﴾

"Ni kama mfano wa Adam; alimuumba kutokana na udongo, kisha akamwambia kuwa akawa." Juz.3 (3:59) .

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُم مِّن طِينٍ ﴿٢﴾

"Yeye ndiye aliyewaumba kwa udongo." Juz. 7 (6:2)

Huko tulithibitisha kuwa hakuna njia ya kujua asili ya mtu isipokuwa kwa wahyi utokao kwa aliyemuumba mtu. Na katika Juz. 8 (7:11) tumedokeza majibu ya nadharia ya Darwin.

Na akawaumba majini kwa ulimi wa moto.

Mara nyingi tumesema kuwa tunaamini kuweko majini kwa vile wahyi umeyathibitisha na akili haikani. Katika kufasiri kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na majini tumewaumba kwa moto wenye joto kali."

Juz. 14 (15:27), tulisema kuwa wataalamu wamegundua aina ya vidudu ambavyo haviishi isipokuwa katika hewa ya sumu na aina nyingine haiwezi kupata uhai isipokuwa kwenye visima vya mafuta na vitu vinavyowaka.

Maana ni kuwa katika viumbe hai kuna vinavyotokana na maji na vinavyotokana na moto. Vile vile kuna vilivyo katika ulimwengu wa kuonekana na vilivyo kwenye ulimwengu wa ghaibu.

Basi ni ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Ni kwa kuumbwa mtu kutokana na udongo au kuumbwa jini kutokana na ulimi wa moto?

Maana ya ulimi wa moto ni moto bila ya moshi. Nahofia wale wanaolazimisha wahyi uafikiane na sayansi wasiseme kuwa ulimi wa moto ni ishara ya kugunduliwa petroli na sipiriti!

Kukaririka kauli yake Mwenyezi Mungu: "Basi ni ipi katika neema za Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili," ni kwa kukaririka sababu ambazo ni neema zenye kuulizwa; sawa na unavyoweza kumwambia uliyemsaidia mambo tofauti: Nimekuokoa na adui yako aliyekuweza na

nikakupa pesa, sasa ni lipi kati ya haya mawili unalolikataa? Tena nikakusomeshea watoto wako na nikakujengea nyumba, ni lipi kati ya haya mawili unalolikataa?

Kwa hiyo basi hakuna kukaririka wala msisitizo wa kitu kimoja; isipokuwa ni vitu mabalimbali.

Mola wa mashariki mbili na wa magharibi mbili.

Makusudio ya mashariki mbili na magharibi mbili ni mashariki ya jua na mwezi na magahribi ya jua na mwezi. Maana haya ndiyo yanayokuja haraka akilini na si mengineyo.

Hakuna mwenye shaka kwamba uhai mwingi unahitajia kuangaziwa na kuchwewa na jua na mwezi; bali wamesema kuwa maisha hayayezi kuwa ardhini bila ya hivyo.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Je, neema ya kuangaziwa au ya kuchwewa.

Anaziendesha bahari mbili zikutane; baina yao kipo kizuizi, haziingiliani.

Neno Bahari tumelifasiri kutokana na neno la kiarabu bahr lenye maana ya maji mengi, yawe tamu au chumvi. Makusudio ya bahari mbili hapa ni maji ya bahari na ya mito.

Makusudio ya kizuizi hapa ni uweza wa Mwenyezi Mungu unaofanya zisichanganyike zikageuzana. Tazama tafsiri ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَهُوَ الَّذِي مَرَجَ الْبَحْرَيْنِ هَـٰذَا عَذْبٌ فُرَاتٌ وَهَـٰذَا مِلْحٌ أُجَاجٌ وَجَعَلَ بَيْنَهُمَا بَرْزَخًا وَحِجْرًا مَّحْجُورًا ﴿٥٣﴾

"Naye ndiye aliyezichanganya bahari mbili, hii ni tamu mno na hii ni chumvi sana, na akaweka kinga kati yake na kizuizi kizuiacho." Juz. 19 (25:53).

Bahari zina manufaa mengi na faida kwa viumbe wa Mwenyezi Mungu na waja wake.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Ni neema ya bahari au mito au nyingineyo?

Katika hizo bahari mbili zinatoka lulu na marijani.

Wafasiri wengi wametatizika kufasiri Aya hii. Hilo ni kwa kuwa wao walikata kauli kuwa lulu haipatikanai isipokuwa kwenye maji chumvi tu, na Mwenyezi Mungu anasema kuwa inatoka kwenye maji chumvi na maji tamu. Wakatafuta visingizio vya kuleta taawili.

Lakini Razi amesema: "Inawezekana vipi kuamua kuwa lulu inatoka baharini tu, ikiwa waliotembea wameshindwa hata kuyajua yaliyoko nchi kavu wataweza kujua yaliyoko majini?

Ile kuwa wazamiaji hawakutoa lulu isipokuwa baharini, hakulazimishi kuwa haiwezi kupatikana kwingine. Dhahiri ya maneno ya Mwenyezi Mungu ndiyo inayofaa kuzingatiwa kuliko maneno ya watu."

Sisi tunaunga mkono mantiki hii ya sawa, na inaungwa mkono na Sheikh Maraghi katika tafsiri yake aliposema: "Imethibitika katika ugunduzi wa sasa kwamba, kama inavyotolea lulu kutoka katika maji chumvi, vilevile inaweza kutolewa katika maji tamu. Pia marijani; ingawaje sana sana huwa zinatoka kwenye maji chumvi."

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Je ni neema hii ndio manyoikadhibisha?

Shia Imamiya wameambiwa kuwa wao wanaitakidi kuwa makusudio ya bahari mbili ni Ali na Fatima, kizuizi ni Muhammad **(s.a.w.w)** na lulu na marijani ni Hasan na Husein.

Mimi kwa wasifu wangu kuwa ni mshia ninakana kabisa madai haya wanayobandikizwa shia na kwamba wao wanaharamisha tafsiri ya undani. Ikiwa atapatikana mwenye rai hiyo basi itakuwa ni rai yake binafsi.

Hii pia inapatikana kwa sunni; kama ilivyoelezwa katika tafsiri zao; ikiwemo Addurил manthur ya Suyut wa madhehebu ya Shafiy, anasema: "Ametoa Ibn Mardawayh kutoka kwa Ibn Abbas, kwamba bahari mbili ni Ali na Fatima, kizuizi ni Nabii na lulu na marijani ni Hasan na Husein. Vile vile ameyatoa haya kutoka kwa Anas bin Malik."

Ya kushangaza zaidi kuliko haya ni yale aliyoyanukuu Ismail Haqqi, kati- ka tafsiri yake Ruhul-bayan, kutoka kwa baadhi ya ulama kuwa nusu ya wanane aliowaashiria Mwenyezi Mungu katika kauli yake:

وَيَحْمِلُ عَرْشَ رَبِّكَ فَوْقَهُمْ يَوْمَئِذٍ ثَمَانِيَةٌ ﴿١٧﴾

"Na wanane juu ya hawa watachukua Arshi ya Mola wako," (69:17),

Kuwa ni Abu Hanifa, Shafiy, Malik na Hambali!

Na ni vyake Yeye hivi viendavyo baharini vilivyoundwa kama vilima.

Maana ni kuwa vyombo vya majini vinatembea kwa manufaa ya watu.

Umetangulia mfano wake katika Aya kadhaa ikiwemo Juz. 21 (31:31).

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Je, ni kule kuumbwa kwenu na kuumbwa mali ghafi ya vyombo vya majini au ni kwa kutembea majini n.k.?

Kila kilicho juu yake kitatoweka. Na itabakia dhati ya Mola wako Mwenye utukufu na ukarimu.

Yeye ambaye imetukuka heshima yake, yuko hai kwa dhati yake; kama ambavyo amepatikana kwa dhati yake, na kila mwenye kupatikana kwa dhati hawezi kutoweka wala kubadilika. Yeye Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndio chimbuko la uhai na anayeutoa.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Je, ni utukufu wake au ukarimu wake na yasiyokuwa hayo?

### MWENYEZI MUNGU NA MTU NA IBN AL-ARABIY

Muhyiddin Ibn Al-arabiy, katika Futuhatul-Makkiyya kuhusiana na kauli yake Mwenyezi Mungu: 'Mwenye utukufu na ukarimu,' ana maneno haya yafutayo:

"Hakika Mwenyezi Mungu ameunganisha ukarimu baada ya utukufu, kwa sababu mtu akisikia wasifa wa Mwenyezi wa utukufu bila ya ukarimu, basi atakata tamaa ya kufika kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa vile hajioni kuwa ana nafasi yoyote mbele ya Mtukufu.

"Ndio akaondoa Mwenyezi Mungu dhana hii, kwa mtu, kwa kuuunganisha ukarimu kwenye utukufu, kwa sababu maana ya sifa mbili hizi ni kuwa Mwenyezi Mungu hata kama ni mtukufu, lakini Yeye anamkirimu mtu na kumwangalia kwa jicho la huruma kwa kumfadhili na kumkirimu.

"Mtu akijua nafasi yake hii kwa Mwenyezi Mungu, basi anahisi ukarimu wake na kutambua kuwa lau asingelikuwa ni mkarimu asingejishughulisha

na usaidizi huu. Hapo anazidi kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa sababu naye anajikuta ni mtukufu mbele ya Mwenyezi Mungu."

Tunaunganisha kauli ya Ibn Al-arabi, kwamba mwenye kukana kuweko Mwenyezi Mungu atakuwa ameiangusha nafsi na mazingatio yote na kuikana dhati yake na utukufu wake bila ya kutaka. Kwa sababu atakuwa amemkosea yule aliyemfanya aweko na kumtukuza, na atastahiki adhabu:

وَمَن جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَى الَّذِينَ عَمِلُوا السَّيِّئَاتِ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٨٤﴾

"Na Mwenye kutenda uovu hawalipwi wanaotendao uovu ila yale waliyokuwa wakiyatenda." Juz. 20 (28:84).

Vinamwomba Yeye vilivyo katika mbingu na ardhi.

Makusudio ya kuomba hapa ni mahitajio. Maana ni kuwa viumbe vyote vinamuhitajia Mwenyezi Mungu katika kubakia kwake na katika hali zote; kama vinavyomuhitajia katika asili ya kuweko kwake, na kwamaba Yeye anavisaidia kuweko, lau anaviacha kwa muda wa kupepesa jicho tu, kusingelikuwa na kitu.

Kila siku Yeye yumo katika mambo.

Makusudio ya siku hapa ni wakati bila ya kuwa na mpaka. Maana ni kuwa hakuna chochote kinachokuwa ila kinagura kutoka hali moja hadi nyingine wakati wote. Ndio maana ikasemwa: "Ni muhali kudumu hali." Na vyenye kuweko vinamuhitajia Mwenyezi Mungu katika hali zote. Mwenye nguvu anamhitajia Yeye katika kubakia nguvu zake, na mdhaifu pia anamhitajia kuondoa udhaifu wake.

Hiyo haimaanishi kuwa mtu aache kuhangakia na kufanya kazi kwa kumwachia Mwenyezi Mungu, hapana! Mwenyezi Mungu (s.w.t.) ameamrisha na akahimiza kuhangaika; ndiye aliyesema:

وَأَن لَّيْسَ لِلْإِنسَانِ إِلَّا مَا سَعَىٰ ﴿٣٩﴾

"Na ya kwamba hatapata mtu ila aliyoyahangaikia." (53:39).

Maana yake hasa ni kuwa mtu afanye matendo kwa kuamini kuwa nyuma yake kuna nguvu iliyojificha ikimsaidia kufanya kazi na kumwandalia njia ya kufaulu.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Je, ni huko kuwasaidia kila wakati au ni neema nyinginezo?

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

سَنَفْرُغُ لَكُمْ أَيُّهَ الثَّقَلَانِ ﴿٣١﴾

31. Tutawakusudia enyi wazito wawili.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٢﴾

32. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

يَا مَعْشَرَ الْجِنِّ وَالْإِنسِ إِنِ اسْتَطَعْتُمْ أَن تَنفُذُوا مِنْ أَقْطَارِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ فَانفُذُوا لَا تَنفُذُونَ إِلَّا بِسُلْطَانٍ ﴿٣٣﴾

33. Enyi makundi ya majini na watu! Mkiweza kupenya kwenye mbingu na ardhi, basi penyeni! Hamtapenya ila kwa madaraka.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٤﴾

34. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

يُرْسَلُ عَلَيْكُمَا شُوَاظٌ مِّن نَّارٍ وَنُحَاسٌ فَلَا تَنتَصِرَانِ ﴿٣٥﴾

35. Mtapelekewa muwako wa moto na ufukizo; wala hamtanusurika.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٦﴾

36. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

فَإِذَا انشَقَّتِ السَّمَاءُ فَكَانَتْ وَرْدَةً كَالدِّهَانِ ﴿٣٧﴾

37. Itakapopasuka mbingu ikawa nyekundu kama mafuta.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٣٨﴾

38. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

فَيَوْمَئِذٍ لَّا يُسْأَلُ عَن ذَنبِهِ إِنسٌ وَلَا جَانٌّ ﴿٣٩﴾

39. Siku hiyo hataulizwa dhambi zake mtu wala jini.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٤٠﴾

40. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

يُعْرَفُ الْمُجْرِمُونَ بِسِيمَاهُمْ فَيُؤْخَذُ بِالنَّوَاصِي وَالْأَقْدَامِ ﴿٤١﴾

41. Watajulikana wakosefu kwa alama zao, basi watakamatwa kwa nywele zao za utosi na kwa miguu.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٤٢﴾

42. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

هَٰذِهِ جَهَنَّمُ الَّتِي يُكَذِّبُ بِهَا الْمُجْرِمُونَ ﴿٤٣﴾

43. Hii ndiyo Jahannamu ambayo wakosefu wakiikadhibisha.

﴿يَطُوفُونَ بَيْنَهَا وَبَيْنَ حَمِيمٍ آنٍ ﴿٤٤

44. Watakuwa wakizunguka baina ya hiyo na maji ya moto yanayochemka.

﴿فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٤٥

45. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

## HAMTAPENYA ILA KWA MADARAKA

**Aya 31 – 45**

### MAANA

Tutawakusudia enyi wazito wawili.

Makusudio ya kuwakusudia hapa ni kuwahisabu, na hicho ni kiaga kwa kila mwenye kufanya dhambi katika wazito wawili ambao ni watu na majini.

Katika Bahru Al-muhit cha Abu hayan Al-andalusi imeelezwa: "Wameitwa watu na majini kuwa ni wazito kwa sababu ya uzito wao juu ya ardhi. Katika Hadith limetumika neno hilo pale iliposemwa: 'Hakika mimi ninawachia vizito viwili: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu, Ahlu bayt wangu,' vimeitwa hivyo kwa sababu ya utukufu wao."

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Je, ni uweza wake wa kufufua na kuhisabu au ni nini? Hisabu na malipo ni katika neema kubwa kwa viumbe; vinginevyo mwenye kudhulumiwa angelikuwa na hali mbaya zaidi kuliko aliyedhulumu.

Enyi makundi ya majini na watu! Mkiweza kupenya kwenye mbingu na ardhi, basi penyeni! Hamtapenya ila kwa madaraka.

Kabisa hakuna kuokoka na kukutana na Mwenyezi Mungu ila kwa tawfiki inayotoka kwake kwenye toba na kujing'oa kwenye dhambi.

Haya ndio makusudio ya kauli yake Mwenyezi Mungu: 'Ila kwa madaraka.' Kwa sababu toba ni ngome inayomkinga mwenye kutubia kwa ikhlasi na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na adhabu yake.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Je, ni uweza wake kwenu au ni hadhari yake au mengine?

Mtapelekewa muwako wa moto na ufukizo; wala hamtanusurika.

Wamesema kuwa muwako hapa, lililofasiriwa kutokana na neno shuwadh, ni muwako wa moto bila ya moshi. Na ufukizo, lililotokana na nuhas ni moshi bila ya moto. Vyovyote iwavyo, maana yanayopatikana kutokana na Aya ni kuashiria vituko vya kiyama na machngu yake, na kwamba mkosefu hataokoka na machungu na vituko hivi kwa uombezi wala usaidizi.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Je, ni adhabu ya mwenye kupituka mipaka au ni nini?

Itakapopasuka mbingu ikawa nyekundu kama mafuta.

Mbingu na vilivyomo ndani yake miongoni mwa sayari vitayeyuka kama yanavyoyeyuka mafuta kwenye moto na rangi ya myeyuko huu itakuwa kama wekundu wa waridi.

Lengo la kufananisha huku na mengineyo yaliyokuja katika Aya nyingine ni kuashiria kuharibika ulimwengu na kubomoka kwake Siku ya Kiyama.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Je, ninani dhalimu mkubwa na muovu zaidi kuliko yule mwenye kukadhibisha ukweli na akaikalia juu haki?

Siku hiyo hataulizwa dhambi zake mtu wala jini.

Tukiunganisha Aya hii na ile isemayo: "Na wasimamisheni. Hakika hao wataulizwa" Juz. 23 (37:24), inatubainikia kuwa Siku ya Kiyama kuna sehemu watu wataulizwa yale waliyokuwa wakiyafanya na sehemu nyingine hakutakuwa na maswali wala majibu, bali ni kungoja maswali na hisabu. Tazama Juz. 22 (36:55-68).

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Je, ni kwa kusimama kuonyeshwa hisabu au ni kusimama kuingoja? Yote hayo ni dhiki na uchungu, hilo halina shaka, lakini malipo ni katika neema itokayo kwa Mwenyezi Mungu kwa vile Watajulikana wakosefu kwa alama zao, basi watakamatwa kwa nywele zao za utosi na kwa miguu.

Yaani wakosefu watakuwa na alama za kuwatambulisha na kuwapambanua na watu wema, zaidi ya hayo Malaika wa adhabu watawafunga utosi na miguu pamoja na kuwatupa Motoni kifudifudi.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Katika mawaidha na makanyo?

Hii ndiyo Jahannamu ambayo wakosefu wakiikadhibisha.

Hili ni jawabu sahihi zaidi kwa mwenye kukadhibisha adhabu ya Mwenyezi Mungu, nalo ni kutumbukizwa ndani yake:

وَنَقُولُ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذُوقُوا عَذَابَ النَّارِ الَّتِي كُنتُم بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿٤٢﴾

"Na tutawaambia wale ambao wamedhulumu: onjeni adhabu ya moto wa Jahannam mliokuwa mkiukadhibisha." Juz. 22 (34:42).

Watakuwa wakizunguka baina ya hiyo na maji ya moto yanayochemka.

Hiyo ni Jahannam. Maji ya moto ni kinywaji.

Kukisifia kuwa kinachemka ni kuonyesha kuwa kinywaji hiki kitafikia kiwango cha joto kiasi ambacho mnywaji atahisi kama kwamba kiko motoni.

Maana ni kuwa hakuna kazi kwa wakosefu isipokuwa kuzunguka baina ya Moto au kunywa kinywaji cha Moto.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Je, ni adhabu ya Moto au ni kinywaji cha Moto? Yote hayo mawili ni katika neema ya Mwenyezi Mungu, kwa sababu ni hukumu ya uadlifu na upanga wa haki.

وَلِمَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ جَنَّتَانِ ﴿٤٦﴾

46. Na mwenye kuogopa kusimama mbele ya Mola wake atapata Bustani mbili.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٤٧﴾

47. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

ذَوَاتَا أَفْنَانٍ ﴿٤٨﴾

48. Zenye matawi yaliyotanda.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٤٩﴾

49. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

فِيهِمَا عَيْنَانِ تَجْرِيَانِ ﴿٥٠﴾

50. Ndani yake zimo chemchem mbili zinazopita.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥١﴾

51. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

فِيهِمَا مِن كُلِّ فَاكِهَةٍ زَوْجَانِ ﴿٥٢﴾

52. Humo katika kila matunda zimo namna mbili.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٣﴾

53. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

مُتَّكِئِينَ عَلَىٰ فُرُشٍ بَطَائِنُهَا مِنْ إِسْتَبْرَقٍ وَجَنَى الْجَنَّتَيْنِ دَانٍ ﴿٥٤﴾

54. Wakiegemea matandiko yenye vitambaa vya hariri nzito; na matunda ya Bustani hizo
yapo karibu.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٥﴾

55. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

فِيهِنَّ قَاصِرَاتُ الطَّرْفِ لَمْ يَطْمِثْهُنَّ إِنسٌ قَبْلَهُمْ وَلَا جَانٌّ ﴿٥٦﴾

56. Humo watakuwamo wanawake watulizao macho; hajawagusa mtu kabla yao wala jini.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٧﴾

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

كَأَنَّهُنَّ الْيَاقُوتُ وَالْمَرْجَانُ ﴿٥٨﴾

58. Kama kwamba wao ni yakuti na marijani.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٥٩﴾

59. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

هَلْ جَزَاءُ الْإِحْسَانِ إِلَّا الْإِحْسَانُ ﴿٦٠﴾

60. Hakuna malipo ya ihsani ila ihsani?

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٦١﴾

61. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

وَمِن دُونِهِمَا جَنَّتَانِ ﴿٦٢﴾

62. Zaidi ya hizo mbili ziko Bustani mbili nyingine.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٦٣﴾

63. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

مُدْهَامَّتَانِ ﴿٦٤﴾

64. Za kijani kibivu.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٦٥﴾

65. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

فِيهِمَا عَيْنَانِ نَضَّاخَتَانِ ﴿٦٦﴾

66. Mna chemchem mbili zinazofurika.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٦٧﴾

67. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

فِيهِمَا فَاكِهَةٌ وَنَخْلٌ وَرُمَّانٌ ﴿٦٨﴾

68. Mna humo matunda, na mitende na komamanga.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٦٩﴾

69. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

فِيهِنَّ خَيْرَاتٌ حِسَانٌ ﴿٧٠﴾

70. Wamo wanawake wema wazuri.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٧١﴾

71. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

حُورٌ مَّقْصُورَاتٌ فِي الْخِيَامِ ﴿٧٢﴾

72. Wanawake wazuri wanaotawishwa katika mahema.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٧٣﴾

73. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

لَمْ يَطْمِثْهُنَّ إِنسٌ قَبْلَهُمْ وَلَا جَانٌّ ﴿٧٤﴾

74. Hajawagusa mtu kabla yao wala jini.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٧٥﴾

75. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

مُتَّكِئِينَ عَلَىٰ رَفْرَفٍ خُضْرٍ وَعَبْقَرِيٍّ حِسَانٍ ﴿٧٦﴾

76. Wameegemea juu ya matakia ya kijani na mazulia mazuri.

فَبِأَيِّ آلَاءِ رَبِّكُمَا تُكَذِّبَانِ ﴿٧٧﴾

77. Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

تَبَارَكَ اسْمُ رَبِّكَ ذِي الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٧٨﴾

78. Limekuwa na baraka jina la Mola wako, Mwenye utukufu na ukarimu.

## HAKUNA MALIPO YA HISANI ILA HISANI

**Aya 46 – 78**

### MAANA

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuhofisha na kumpa kiaga yule mwenye kupetuka mipaka na akafanya uovu, sasa anamtuliza yule mwenye takua na akalisadikisha tamko jema, na kumwahidi Pepo iliyo na sifa kubwa kwa chakula chake, kinywaji chake, huri laini wake, miti yake, mito yake, samani zake na vipambo vyake kwa namna ambayo haina mfano wala hatuijui.

Nyingi katika Aya hizi ziko wazi hazihitajii tafsiri; mbali ya kuwa ni kukariri yaliyotangulia. Kwa hiyo tutafupiliza tafsiri ila kukiwa na haja ya kurefusha.

Na mwenye kuogopa kusimama mbele ya Mola wake atapata Bustani mbili.

Makusudio ya kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu ni kuwa yeye ni msimamizi wa kila nafsi akijua siri yake na dhahiri yake. Imepokewa kutoka kwa Imam Ja'far Assadiq (a.s) amesema: **"Mwenye kujua kuwa Mwenyezi Mungu anamuona na kusikia anayoyasema, na likamzuia hilo kufanya maovu, atakuwa ameogopa kusimama mbele ya Mola wake."**

Wafasiri wana kauli kadhaa kuhusu maana ya Bustani mbili. Iliyo karibu zaidi na ufahamu ni bustani katika Pepo, kwa sababu neno Pepo limefasiriwa kutoka neno la kiarabu janna lenye maana ya bustani. Hilo linatiliwa nguvu na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu katika wasifu wake zenye matawi yaliyotanda; yaani matawi yenye majani na matunda.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Je, nyinyi majini na watu mnakanusha neema hizi tulizozitaja. Kila swali linalokuja kwa tamko hili, basi inayoulizwa ni neema aliyoitaja Mwenyezi Mungu (s.w.t) kabla ya swali; kwa hiyo hakuna haja ya kutaja na kubainisha kinachouliziwa.

Ndani yake zimo chemchem mbili zinazopita.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Maana yako wazi, lakini pamoja na hayo mfasiri mmoja amesema: kupita maana yake ni kutawanyika. Mwingine akasema: yaani zinapita baina ya miti. Wa tatu akasema chemchem moja inaitwa tasnim na nyingine inaitwa salsabil.

Wanne naye akasema: zinapita ni kwa ambaye macho yake yanatiririka machozi kwa kumhofia Mwenyezi Mungu.

Hakuna chimbuko la tafsiri hizi isipokuwa hamu ya kusema tu. Kwa nini wana hamu ya kusema? Ni kwa vile tu wao ni wafasiri.

Humo katika kila matunda zimo namna mbili.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Tunda moja linaweza kuwa na aina mbili; kama zabibu kavu na mbichi, tende mbichi na za kuiva[1] na matofaha ya tamu na yasiyokuwa tamu.

Wakiegemea matandiko yenye vitambaa vya hariri nzito; na matunda ya Bustani hizo yapo karibu.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili? Mfano wake ni Aya isemayo: "Vishada vyake viko karibu." (69:23).

Humo watakuwamo wanawake watulizao macho; hajawagusa mtu kabla yao wala jini.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Humo, ni humo Peponi; na kabla yao, ni kabla ya hao waume wa Hurilaini. Maana ni kuwa Hurilaini hawataangalia isipokuwa waume zao, pia watakuwa ni bikra kama walivyumbwa.

Kama kwamba wao ni yakuti na marijani kwa urembo na uzuri.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

### UJIRA NI HAKI NA ZIADA NI FADHILA

Hakuna malipo ya ihsani ila ihsani?

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Kila wanaloliona watu kuwa ni hisani au wema basi kwa Mwenyezi ni hivyo hivyo, kwa Sharti yakuwa lisikataliwe na akili iliyo salama wala kukatazwa na sharia; kama ilivyokuwa wakati wa jahilia, walikuwa wakiona ni wema na jambo zuri kuabudu masanamu na kuwadhulumu wanyonge, hasa wanawake.

Mpaka leo hii bado kuna mamilioni ya watu wanaoona ni hisani kuabudu masanamu na watu wakimfanya Mwenyezi Mungu ana watoto na washirika. Hakuna mwenye shaka kuwa hii ni desturi mbaya sana.

Ikiwa mtu atafanya jambo na watu wakaliona ni zuri na lisikataliwe na akili na sharia, basi mwenye kuilifanya anastahiki ujira na karama kutoka kwa Mwenyezi Mungu na atamzidisha ziada ya anayostahiki:

لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ ﴿٢٦﴾

"Kwa wafanyao wema ni wema na ziyada." Juz. 11(10:26).

Kundi katika wanatiolojia wamesema kuwa thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa tendo la wajibu ni fadhila sio malipo wala haki. Wengine wakasema, bali ni malipo na haki.

Imam Ali (a.s) anasema: **"Ingelikuwa kuna yeyote mwenye haki lakini wengine hawana haki juu yake, ingelikuwa hivyo kwa Mwenyezi Mungu tu peke yake, sio kwa viumbe wake, kutokana na uwezo wake kwa waja wake na kwa uadilifu kwa kila linalopita katika hukumu yake.**

**Lakini amejaalia haki yake kwa waja wake ni kumtii na akajalia malipo yao yawe juu yake, kwa kuwaongezea malipo kwa fadhila na kupanua ile ziyada kwa wanaostahiki."**

Maana yake ni kuwa Mwenyezi Mungu ana haki yake naye anayo haki ya wengine. Hakuna linalofahamisha hivyo kuliko kauli hiyo ya Imama Ali (a.s).

---

1. Katika lugha ya kiarabu hizi zina majina yake maalumu; kama inab na zabib, na tamri na rutab -Mtarjumu.

Kwa hiyo haki ya Mwenyezi Mungu ni kutiiwa na waja wake na haki ya watiifu kwake, Yeye ambaye imetukuka hikima yake, ni malipo kulingana na matendo. Zaidi ya hayo ni fadhila kutoka kwake Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Hii inaafikiana na hukumu ya kiakili na maumbile, kwani watu wote wanaona ni fadhila na hisani ukimlipa aliyekufanyia kazi zaidi ya malipo yake na stahiki yake. Lakini ukimlipa bila ya ziada wala upungufu basi wewe ni mtekelezaji, lakini sio mhisani wala makarimu.

Zaidi ya hayo Uislamu, kwa misingi yake na matawi yake, unajengeka kwenye fikra ya uadilifu. Na ujira wa kazi ni haki ya wajibu kuitekeleza katika mantiki ya uadilifu na hukumu yake.

Zaidi ya hizo mbili ziko Bustani mbili nyingine.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Yaani katika Pepo kuna kuzidiana kulingana na imani za waumini na kutofautiana na matendo yao. Haya ndiyo yanayopelekea mantiki ya haki na misingi ya uadilifu. Kwa hiyo inatubainikia kuwa Bustani mbili zilizotajwa mwanzo ni za wale wenye imani ya nguvu, wenye kazi iliyo na manufaa zaidi na wenye juhudi zaidi ya wengine, na hizi mbili zilizotajwa sasa ni za walio chini ya hapo.

Za kijani kibivu.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Yaani rangi yake inaeleka weusi kutokana na kuiva sana.

Mna chemchem mbili zinazofurika.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Yaani zinachimbuka maji. Ama zile zilizotajwa mwanzo maji yake yanapita. Kama ambavyo bustani mbili zilozitajwa mwanzo ni tofauti na zilizotajwa baadae vile vile chemchem.

Mna humo matunda, na mitende na komamanga.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Baadhi ya wafasiri wamesema kuwa tende na komamanga sio matunda ndio maana kukawa na maunganisho. Razi anasema kuwa katika matunda kuna ya Ardhini, kama vile matango n.k. na kuna yaliyo kwenye miti, kama vile tende n.k. Kwa hiyo kuunganisha kunakuwa kwa mahususi kwenye jumla.

Wamo wanawake wema wazuri.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Yaani wazuri wa umbo na tabia.

Wanawake wazuri wanaotawishwa katika mahema.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Mwenye Majmaul'bayan anasema maana yake ni kutwawishwa kwenye makuba wanayojengewa wanawake wanaotawa nyumbani. Wengine wakasema kuwa makusudio ni mahema hasa; kwani yako mengine yanashinda majumba kwa uzuri. Kauli hii ndio iliyo karibu na dhahiri ya Aya.

Hajawagusa mtu kabla yao wala jini.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Yaani bado ni bikra. Imetangulia kwa herufi zake katika Aya 56 ya Sura hii. Wameegemea juu ya matakia ya kijani na mazulia mazuri.

Basi ni ipi katika neema ya Mola wenu mnayoikanusha nyinyi wawili?

Yaani kwenye mito ya kuegemea.

limekuwa na baraka jina la Mola wako, Mwenye utukufu na ukarimu.

Mwenyezi Mungu ana utukufu na ukubwa, ikiwa ni pamoja na ukarimu na fadhila kwa viumbe wake. Tazama kifungu cha 'Mwenyezi Mungu na mtu na Ibn A-arabi'.

Katika Aya 27 ya sura hii tuliyo nayo.

## MWISHO WA SURA YA HAMSINI NA TANO: SURAT AR-RAHMAN

24

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

Sura Ya Hamsini Na Sita: Surat Al-Waaqia. Imeshuka Makka. Ina Aya 96.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu

إِذَا وَقَعَتِ الْوَاقِعَةُ ﴿١﴾

1. Litakapotukia hilo Tukio.

لَيْسَ لِوَقْعَتِهَا كَاذِبَةٌ ﴿٢﴾

2. Hapana cha kukanusha kutukia kwake.

خَافِضَةٌ رَّافِعَةٌ ﴿٣﴾

3. Literemshalo linyanyualo.

إِذَا رُجَّتِ الْأَرْضُ رَجًّا ﴿٤﴾

4. Itakapotikiswa ardhi kwa mtikiso,

وَبُسَّتِ الْجِبَالُ بَسًّا ﴿٥﴾

5. Na milima itaposagwasagwa,

فَكَانَتْ هَبَاءً مُّنبَثًّا ﴿٦﴾

6. Iwe mavumbi yanayopeperushwa.

وَكُنتُمْ أَزْوَاجًا ثَلَاثَةً ﴿٧﴾

7. Na nyinyi mtakuwa namna tatu.

فَأَصْحَابُ الْمَيْمَنَةِ مَا أَصْحَابُ الْمَيْمَنَةِ ﴿٨﴾

8. Basi watakuwepo wa kuume; je, ni yapi ya wa kuume?

وَأَصْحَابُ الْمَشْأَمَةِ مَا أَصْحَابُ الْمَشْأَمَةِ ﴿٩﴾

9. Na wa kushoto; je, ni yapi ya wa kushoto?

وَالسَّابِقُونَ السَّابِقُونَ ﴿١٠﴾

10. Na waliotangulia ndio waliotangulia.

أُولَٰئِكَ الْمُقَرَّبُونَ ﴿١١﴾

11. Hao ndio watakaokaribishwa

فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿١٢﴾

12. Katika Bustani zenye neema

ثُلَّةٌ مِّنَ الْأَوَّلِينَ ﴿١٣﴾

13. Fungu kubwa katika wa mwanzo,

وَقَلِيلٌ مِّنَ الْآخِرِينَ ﴿١٤﴾

14. Na wachache katika wa mwisho.

عَلَىٰ سُرُرٍ مَّوْضُونَةٍ ﴿١٥﴾

15. Watakuwa juu ya viti vya fahari vilivyodariziwa.

مُّتَّكِئِينَ عَلَيْهَا مُتَقَابِلِينَ ﴿١٦﴾

16. Wakiviegemea wakielekeana.

يَطُوفُ عَلَيْهِمْ وِلْدَانٌ مُّخَلَّدُونَ ﴿١٧﴾

17. Watawazunguukia vijana wa milele.

بِأَكْوَابٍ وَأَبَارِيقَ وَكَأْسٍ مِّن مَّعِينٍ ﴿١٨﴾

18. Kwa vikombe na mabirika na bilauri za vinywaji kutoka chemchem safi.

لَّا يُصَدَّعُونَ عَنْهَا وَلَا يُنزِفُونَ ﴿١٩﴾

19. Hawataumwa kichwa kwa hivyo wala hawataleweshwa.

وَفَاكِهَةٍ مِّمَّا يَتَخَيَّرُونَ ﴿٢٠﴾

20. Na matunda wayapendayo,

وَلَحْمِ طَيْرٍ مِّمَّا يَشْتَهُونَ ﴿٢١﴾

21. Na nyama ya ndege kama wanavyotamani.

وَحُورٌ عِينٌ ﴿٢٢﴾

22. Na Mahurulaini.

كَأَمْثَالِ اللُّؤْلُؤِ الْمَكْنُونِ ﴿٢٣﴾

23. Walio kama mfano wa lulu zilizohifadhiwa.

جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٢٤﴾

24. Ni malipo kwa waliyokuwa wakiyatenda.

لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا تَأْثِيمًا ﴿٢٥﴾

25. Humo hawatasikia upuzi wala maneno ya dhambi.

إِلَّا قِيلًا سَلَامًا سَلَامًا ﴿٢٦﴾

26. Isipokuwa maneno ya Salama, Salama.

## LITAKAPOTUKIA TUKIO

**Aya 1 – 26**

### MAANA

Litakapotukia hilo Tukio. Hapana cha kukanusha kutukia kwake.

Makusudio ya tukio hapa ni Kiyama. Katika maisha ya duniani kuna wanaoisadiki Akhera na wanaoikanusha. Lakini ikashafikia wakati wake na kutekelezewa kila nafsi iliyoyachuma, hapo ndio wataikubali na kukiri.

Kwanini? Kwa vile tukio lake ndilo Literemshalo linyanyualo. Linawainamisha wakosefu na kuwainua wenye takua.

Itakapotikiswa ardhi kwa mtikiso, Na milima itaposagwasagwa, Iwe mavumbi yanayopeperushwa.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anaashiria kuharibika ulimwengu. Ardhi itavunjwavunjwa na tetemeko na majabali yatageuka vumbi.

Na nyinyi mtakuwa namna tatu:

Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu atawakusanya watu na kuwafanya makundi matatu:

Basi watakuwepo wa kuume; je, ni yapi ya wa kuume?

Ni ambao kesho watapewa vitabu vyao kwa mikono yao ya kuume. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na ama atakayepewa kitabu chake kwa mkono wake wa kuume, atasema: Haya someni kitabu changu! Hakika nilijua kuwa nitapokea hisabu yangu.

فَأَمَّا مَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ فَيَقُولُ هَاؤُمُ اقْرَءُوا كِتَابِيَهْ ﴿١٩﴾ إِنِّي ظَنَنتُ أَنِّي مُلَاقٍ حِسَابِيَهْ ﴿٢٠﴾ فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَّاضِيَةٍ ﴿٢١﴾

Basi ama atakaye pewa kitabu chake kwa mkono wake wa kulia, atasema: Haya someni kitabu changu! Hakika nalijua ya kuwa nitapokea hisabu yangu. Basi yeye atakuwa katika maisha ya kuridhiwa." (69:19-21).

Kundi, hata kama ni katika watakaookoka, lakini sio kama kundi la tatu.

Na wa kushoto; je, ni yapi ya wa kushoto?

Hawa ni wale watakopewa vitabu vyao kwa mikono yao ya kushoto. Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema:

وَأَمَّا مَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِشِمَالِهِ فَيَقُولُ يَا لَيْتَنِي لَمْ أُوتَ كِتَابِيَهْ ﴿٢٥﴾ وَلَمْ أَدْرِ مَا حِسَابِيَهْ ﴿٢٦﴾ يَا لَيْتَهَا كَانَتِ الْقَاضِيَةَ ﴿٢٧﴾

"Na ama atakayepewa kitabu chake kwa mkono wake wa kushoto, atasema: laiti nisingelipewa kitabu changu wala nisijue nini hisabu yangu. Laiti mauti yangelikuwa ni ya kumaliza."

(69:25-27).

Na waliotangulia ndio waliotangulia.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amesema waliotangulia, lakini hakubainisha wametangulia kwenye jambo gani; hata hivyo amebainisha mahali pengine: "Hakika wale ambao humwogopa Mola wao wanamnyenyekea. Na wale ambao wanaamini ishara za Mola wao. Na wale ambao hawamshirikishi Mola wao.

Na wale ambao wanatoa walichopewa na hali nyoyo zao zinaogopa kwa kuwa watarejea kwa Mola wao. Hao ndio wanokimbilia kwenye kheri na ndio watakaotangulia kuzifikia." Juz. 18 (23: 57-61).

Kwa hiyo basi waliotangulia ni wale wanaomwamini Mwenyezi Mungu peke yake bila ya kuwa na mshirika, na wakaamini siku ya mwisho, wala wasipuuze kumtii kwa kuhofia ghadhabu na adhabu yake, na wakawa wanajitolea mhanga ulio ghali kwa kutaka radhi na thawabu zake.

Hao ndio watakaokaribishwa katika Bustani zenye neema.

Wana hadhi kubwa ya kukaribishwa kwenye utukufu wake mtukuka na wana fungu kubwa la neema yake.

Fungu kubwa katika wa mwanzo, Na wachache katika wa mwisho.

Wametofautiana wafasiri kuwa ni nani hao wa mwanzo, wa mwisho na wachache? Kuna waliosema kuwa makusudio ya wa kwanza ni walioami- ni na wakatangulia kwenye heri kabla ya Muhammad **(s.a.w.w)**. Wengine wakasema wote wa kwanza na wa mwisho ni katika umma wa Muhammad **(s.a.w.w)**.

Tuonavyo sisi ni kwamba wa kwanza ni ishara ya zama za uislamu wa dhahabu, pale ulipokuwa na nguvu na madaraka na waislamu wakawa wanauamini kwa kauli na vitendo wakiupigania kwa roho na mali. Na

wengine ni ishara ya waumini wachache katika zama za baadae. Kauli hii inasadikishwa na kauli ya Imam Ali (a.s):

**"Zitakuja zama kwa watu haitabakia Qur'an isipokuwa maandishi tu, na Uislamu isipokuwa jina lake. Misikiti yao itajengwa vizuri, lakini itakuwa mibovu ya uongofu. Wakazi wake na waamirishaji wake ndio watakuwa washari zaidi katika watu wa ardhi.**

**Kutoka kwao itatokea fitna na kwao itaishia hatia. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Ninaapa nitawapelekea hawa fitna nimwache mpole hana la kufanya."**

Watakuwa juu ya viti vya fahari vilivyodariziwa.

Vitakuwa vimefuwa kulingana na mili ya watu wa Peponi iliyo myororo na nyuso zenye kunyinyirika.

Wakiviegemea wakielekeana.

Hawana shughuli wala fikra ya familia.

Watawazunguukia vijana wa milele Kwa vikombe na mabirika na bilauri za vinywaji kutoka chemchem safi.

Vikombe vyenye asali safi, pombe ya ladha kwa wanywaji, mvinyo wenye kusiliwa. Katika kuyapata basi nawashindane wenye kushindana.

Hawataumwa kichwa kwa hivyo wala hawataleweshwa.

Vinywaji hivyo havimwondolei mnywaji akili yake wala hataumwa na kichwa.

Na matunda wayapendayo, na nyama ya ndege kama wanavyotamani. Na Mahurulaini, walio kama mfano wa lulu zilizohifadhiwa.

Kinywaji safi, nyama freshi, matunda aina kwa aina, wanawake wazuri, matandiko na viti. Ni raha na utulivu. Yote hayo ni malipo kwa waliyo kuwa wakiyatenda ya heri na masilahi ya umma bila ya riya wala kupigiwa ngoma au nzumari.

Humo hawatasikia upuzi wala maneno ya dhambi. Isipokuwa maneno ya Salama, Salama.

Watasikia wapi upuzi na porojo na peponi hakuna matamshi isipokuwa heri tu. Yote haya ni ya wale waliotangulia. Ama watu wa kuume Mwenyezi Mungu (s.w.t) amebainisha fungu lao, katika Aya zifuatazo.

وَأَصْحَابُ الْيَمِينِ مَا أَصْحَابُ الْيَمِينِ ﴿٢٧﴾

27. Na wa kuume; je, ni yapi ya wa kuume?

فِي سِدْرٍ مَّخْضُودٍ ﴿٢٨﴾

28. Katika mikunazi isiyo na miba,

وَطَلْحٍ مَّنضُودٍ ﴿٢٩﴾

29. Na migomba iliyopangiliwa,

وَظِلٍّ مَّمْدُودٍ ﴿٣٠﴾

30. Na kivuli kilichotanda,

وَمَاءٍ مَّسْكُوبٍ ﴿٣١﴾

31. Na maji yanayomiminika,

وَفَاكِهَةٍ كَثِيرَةٍ ﴿٣٢﴾

32. Na matunda mengi;

لَّا مَقْطُوعَةٍ وَلَا مَمْنُوعَةٍ ﴿٣٣﴾

33. Hayakatiki wala hayakatazwi,

وَفُرُشٍ مَّرْفُوعَةٍ ﴿٣٤﴾

34. Na matandiko yaliyonyanyuliwa.

إِنَّا أَنشَأْنَاهُنَّ إِنشَاءً ﴿٣٥﴾

35. Hakika Sisi tumewaumba upya.

فَجَعَلْنَاهُنَّ أَبْكَارًا ﴿٣٦﴾

36. Na tutawafanya bikira,

عُرُبًا أَتْرَابًا ﴿٣٧﴾

37. Wanaopenda, walio marika.

لِّأَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٣٨﴾

38. Kwa ajili ya watu wa kuume.

ثُلَّةٌ مِّنَ الْأَوَّلِينَ ﴿٣٩﴾

39. Fungu kubwa katika wa mwanzo.

وَثُلَّةٌ مِّنَ الْآخِرِينَ ﴿٤٠﴾

40. Na fungu kubwa katika wa mwisho.

## WA KUUME

**Aya 27– 40**

### MAANA

Na wa kuume; je, ni yapi ya wa kuume?

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kutaja karama na neema aliyowaandalia waliotangulia, sasa anataja aliyowaandalia wale walio chini yao kuume. Amewaita wa kuume, kwa vile watapewa vitabu vyao kwa mikono yao ya kuume, kama ilivyotangulia kuelezwa. Hili lifutalo ndilo fungu lao katika Pepo.

Katika mikunazi isiyo na miba, na migomba iliyopangiliwa; yaani ndizi zilizopandana Na kivuli kilichotanda kisichokuwa na muda. Na maji yanayomiminika bila ya kukatika. Na matunda mengi kwa idadi na aina.

Hayakatiki wala hayakatazwi,

Miti ya duniani inazaa kwa msimu na mtunda yanakuwa ni ya mwenye mti tu, akimpa anayemtaka. Lakini miti ya Akhera matunda yake ni ya kudumu na yanatumiwa na kila mtu.

Na matandiko yaliyonyanyuliwa.

Yaani vitanda vya juu. Ajabu ni kauli ya mfasiri mmoja aliyesema urefu wa kitanda kwenda juu ni masafa ya miaka mia tano.

Hakika Sisi tumewaumba Mahurulaini upya, Na tutawafanya bikira wanaopenda waume zao, walio marika.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewaandalia watu wa kuume wanawake bikra, wanaowapenda waume zao na wote wakiwa na umri mmoja.

Mfasiri mmoja amekadiria umri wao kuwa miaka 33. na kimo cha dhiraa sitini kwa dhiraa saba; sawa na alivyokuwa Adam, kulingana na kauli yake mfasiri huyo.

Lengo la kuashiria haya ni kutanabahisha kuwa baadhi ya tafsiri haifai kuzitegemea, kwa sababu ni kusema bila ya ujuzi.

Kwa ajili ya watu wa kuume.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amekariri kwa kiasi cha kusisitiza kwamba aliyoyataja ni ya watu wa kuume.

Fungu kubwa katika wa mwanzo na fungu kubwa katika wa mwisho.

Maneno yanaanza tena, kwamba watu wa kuumeni kuna waliokuwa katika zama zilizotangulia na wengine wa zama zitakazokuja; nao kwa kawaida watakuwa ni wachache kuliko watu wa kushoto:

وَقَلِيلٌ مِّنْ عِبَادِيَ الشَّكُورُ ﴿١٣﴾

“Ni wachache katika waja wangu wanaoshukuru.” Juz. 22 (34:13).

وَأَصْحَابُ الشِّمَالِ مَا أَصْحَابُ الشِّمَالِ ﴿٤١﴾

41. Na wa kushoto; je, ni yapi ya wa kushoto.

فِي سَمُومٍ وَحَمِيمٍ ﴿٤٢﴾

42. Katika upepo wa moto, na maji yanayochemka.

وَظِلٍّ مِّن يَحْمُومٍ ﴿٤٣﴾

43. Na kivuli cha moshi mweusi.

لَّا بَارِدٍ وَلَا كَرِيمٍ ﴿٤٤﴾

44. Si baridi wala starehe.

إِنَّهُمْ كَانُوا قَبْلَ ذَٰلِكَ مُتْرَفِينَ ﴿٤٥﴾

45. Hakika hao walikuwa kabla ya haya wakiishi maisha ya anasa.

وَكَانُوا يُصِرُّونَ عَلَى الْحِنثِ الْعَظِيمِ ﴿٤٦﴾

46. Na walikuwa wakishikilia kiapo kikubwa.

وَكَانُوا يَقُولُونَ أَئِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظَامًا أَإِنَّا لَمَبْعُوثُونَ ﴿٤٧﴾

47. Na walikuwa wakisema: Tutakapokufa na tukawa udongo na mifupa, ati ndio tutafufuliwa?

أَوَآبَاؤُنَا الْأَوَّلُونَ ﴿٤٨﴾

48. Au baba zetu wa zamani?

قُلْ إِنَّ الْأَوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ ﴿٤٩﴾

49. Sema: Hakika wa zamani na wa mwisho,

لَمَجْمُوعُونَ إِلَىٰ مِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ﴿٥٠﴾

50. Bila ya shaka watakusanywa kwa wakati wa siku maalumu.

ثُمَّ إِنَّكُمْ أَيُّهَا الضَّالُّونَ الْمُكَذِّبُونَ ﴿٥١﴾

51. Kisha nyinyi, mliopotea, mnaokadhibisha,

لَآكِلُونَ مِن شَجَرٍ مِّن زَقُّومٍ ﴿٥٢﴾

52. Kwa yakini mtakula mti wa Zaqqum.

فَمَالِئُونَ مِنْهَا الْبُطُونَ ﴿٥٣﴾

53. Na kwa huo mtajaza matumbo.

فَشَارِبُونَ عَلَيْهِ مِنَ الْحَمِيمِ ﴿٥٤﴾

54. Na juu yake mtakunywa maji yanayochemka.

فَشَارِبُونَ شُرْبَ الْهِيمِ ﴿٥٥﴾

55. Tena mtakunywa kama wanavyo kunywa ngamia wenye kiu.

هَـٰذَا نُزُلُهُمْ يَوْمَ الدِّينِ ﴿٥٦﴾

56. Hii ndiyo karamu yao Siku ya Malipo.

## NA WA KUSHOTO

**Aya 41 – 56**

### MAANA

Na wa kushoto; je, ni yapi ya wa kushoto.

Mwenyezi Mungu (s.w.t), kwanza, ametaja malipo makubwa aliyowandalia waliotangulia, kisha rehema na thawabu alizowaandalia wa kuume. Sasa, katika Aya hizi tulizo nazo anataja aina kwa aina ya adhabu itakayowapata watu wa kushoto; miongoni mwazo ni kuwa wao watakua katika upepo wa moto, na maji yanayochemka. Upepo wa moto utavutwa ndani ya mwili na kuchemsha nyama na damu na watakunywa maji yanayochemka tumboni.

Na kivuli cha moshi mweusi.

Neno moshi mweusi tumelifasiri kutokana na neno la kiarabu yahmum ambalo pia lina maana ya weusi tititi wa kitu chochote na pia moshi mwingi. Maana yanafaa kwa moja wapo au yote pamoja

Si baridi wala starehe.

Ni kivuli lakini hakileti baridi wala kukinga joto, sawa na anayekimbilia kwenye mchanga wa kuchoma.

Hakika hao walikuwa kabla ya haya wakiishi maisha ya anasa.

Walipetuka mipaka wakawafanyia uovu waja wa Mwenyezi Mungu na miji yao; wakapora riziki za viumbe na wakastarehe kadiri walivyotaka, kuanzia mavazi ya gharama, chakula kitamu, kinywaji kinachoshuka hadi makazi ya fahari. Basi malipo mbele ya Mwenyezi Mungu yamekuwa ni adhabu ya kuungua, kinywaji cha moto, chakula cha zaqqum, upepo wa kuunguza na kivuli ni moshi.

Na walikuwa wakishikilia kiapo kikubwa.

Imesemekana kuwa ni madhambi makubwa. Lakini kauli ya kiapo chao cha uongo kuwa hakuna ufufuo wala malipo, ndiyo iliyo karibu; kama alivyowasimulia Mwenyezi Mungu (s.w.t) pale aliposema: Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu kwa viapo vyao vya nguvu (kwamba) Mwenyezi Mungu hatawafufua wafu.” Juz. 14 (16:38).

Kiapo chao hiki ni matokeo ya shirki yao, kwa hiyo basi inafaa kufasiri Aya tuliyo nayo kwa maana ya shirki.

Na walikuwa wakisema: Tutakapokufa na tukawa udongo na mifupa, ati ndio tutafufuliwa? Au baba zetu wa zamani?

Walisema, kwa madharau, kuwa kweli mchanga unaweza kugeuka kuwa mtu? Wamesahau kuwa Mungu aliwaumba kutokana na mchanga kisha tone la manii.

Sema: Hakika wa zamani na wa mwisho, bila ya shaka watakusanywa kwa wakati wa siku maalumu.

Waambie ewe Muhammad! Ndio, Mwenyezi Mungu atawakusanya kesho viumbe ili kuchambua hisabu na malipo ya matendo. Au kama Mwenyezi Mungu angeliwaacha tu hivi hivi bila ya makemeo wala maswali, angelikuwa ni dhalimu na anayefanya mchezo. Ametukuka sana Mwenyezi Mungu na wanayoyasema madhalimu.

Umetangulia mfano wake katika Aya kadhaa; zikiwemo: Juz. 13 (13:5), Juz. 15 (17:49) na Juz. 18 (23:81-83).

Kisha nyinyi, mliopotea, mnaokadhibisha, Mmepotea mkaacha njia ya haki, mkaikanusha haki na mkabishana kijinga, basi malipo yenu kwa yakini mtakula mti wa Zaqqum. Na kwa huo mtajaza matumbo.

Sisi hatujui mti huu na kuna mengi tusiyoyajua, lakini tuna uhakika kuwa unaashiria, adhabu mbaya. Mwenyezi Mungu (s.w.t) amefananisha mashada yake na vichwa vya shetani. Tazama Juz. 22 (37:62).

Na juu yake mtakunywa maji yanayochemka.

Chakula chao ni kichungu kuliko shubiri, kinanuka kuliko mzoga na kinywaji chao ni chumvi.

Tena mtakunywa kama wanavyokunywa ngamia wenye kiu.

Neno kiu tumelifasiri kutokana na neno la kiarabu him ambalo lina maana ya ngamia mwenye kiu au ugonjwa wa kiu kisichokwisha.

Hii ndiyo karamu yao Siku ya Malipo.

Hii ni ishara ya hali ya watu wa kushoto. Siku ya malipo ni siku ya kiyama. Karamu ni chakula na kinywaji anachoandaliwa anayekuja. Ni karamu mbaya ya kinywaji, kivazi na hata malazi. Fauka ya hayo mikono itafungwa shingoni na kukutanishwa utosi na nyayo. Tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu na mwisho mbaya.

نَحْنُ خَلَقْنَاكُمْ فَلَوْلَا تُصَدِّقُونَ ﴿٥٧﴾

57. Sisi tumewaumba; basi mbona hamsadiki?

أَفَرَأَيْتُم مَّا تُمْنُونَ ﴿٥٨﴾

58. Je, mnaiona mnayoitoneza?

أَأَنتُمْ تَخْلُقُونَهُ أَمْ نَحْنُ الْخَالِقُونَ ﴿٥٩﴾

59. Je, mnaiumba nyinyi, au tunaiumba Sisi?

نَحْنُ قَدَّرْنَا بَيْنَكُمُ الْمَوْتَ وَمَا نَحْنُ بِمَسْبُوقِينَ ﴿٦٠﴾

60. Sisi tumewawekea mauti. Na Sisi hatushindwi,

عَلَىٰ أَن نُّبَدِّلَ أَمْثَالَكُمْ وَنُنشِئَكُمْ فِي مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦١﴾

61. Kuwaleta wengine badala yenu na kuwaumba nyinyi kwa umbo msilolijua.

وَلَقَدْ عَلِمْتُمُ النَّشْأَةَ الْأُولَىٰ فَلَوْلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٦٢﴾

62. Na bila ya shaka mlikwisha jua umbo la kwanza, tena mbona hamkumbuki?

أَفَرَأَيْتُم مَّا تَحْرُثُونَ ﴿٦٣﴾

63. Je, Mnaona mnayolima?

أَأَنتُمْ تَزْرَعُونَهُ أَمْ نَحْنُ الزَّارِعُونَ ﴿٦٤﴾

74. Je, ni nyinyi mnayoyaotesha au ni Sisi ndio wenye kuotesha?

لَوْ نَشَاءُ لَجَعَلْنَاهُ حُطَامًا فَظَلْتُمْ تَفَكَّهُونَ ﴿٦٥﴾

75. Tungelitaka tungeliyafanya mapepe, mkabaki mnastaajabu,

إِنَّا لَمُغْرَمُونَ ﴿٦٦﴾

66. Hakika sisi tumegharamika.

بَلْ نَحْنُ مَحْرُومُونَ ﴿٦٧﴾

67. Bali sisi tumenyimwa.

أَفَرَأَيْتُمُ الْمَاءَ الَّذِي تَشْرَبُونَ ﴿٦٨﴾

68. Je, mnayaona maji mnayoyanywa?

أَأَنتُمْ أَنزَلْتُمُوهُ مِنَ الْمُزْنِ أَمْ نَحْنُ الْمُنزِلُونَ ﴿٦٩﴾

69. Je, ni nyinyi mnayoyateremsha kutoka mawinguni au ni Sisi ndio wenye kuyateremsha?

لَوْ نَشَاءُ جَعَلْنَاهُ أُجَاجًا فَلَوْلَا تَشْكُرُونَ ﴿٧٠﴾

70. Tungelipenda tungeliyafanya ya chumvi kali. Basi mbona hamshukuru?

أَفَرَأَيْتُمُ النَّارَ الَّتِي تُورُونَ ﴿٧١﴾

71. Je, mnauona moto mnaouwasha?

أَأَنتُمْ أَنشَأْتُمْ شَجَرَتَهَا أَمْ نَحْنُ الْمُنشِئُونَ ﴿٧٢﴾

72. Ni nyinyi mliouumba mti wake au Sisi ndio Wenye kuuumba?

نَحْنُ جَعَلْنَاهَا تَذْكِرَةً وَمَتَاعًا لِّلْمُقْوِينَ ﴿٧٣﴾

73. Sisi tumeufanya uwe ni ukumbusho na manufaa kwa wenye kusikiliza.

فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٧٤﴾

74. Basi lisabihi jina la Mola wako aliye Mkuu.

## JE, MNAONA MAKULIMA MNAYOYAPANDA

**Aya 57 – 74**

### MAANA

Sisi tumewaumba; basi mbona hamsadiki?

Waliamini na wakakubali kuwa Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaumba, lakini wakakana na kukadhibisha kwamba wao baada ya mauti watarudishwa kwa ajili ya hisabu na malipo. La kwanza kwa itikadi, linawezekana ama la pili kwao ni muhali.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) akawarudi kuwa kuanza kuumba na kurudisha baada ya mauti ni hali moja tu, kulingana na uweza wa Mwenyezi Mungu; bali kurudisha ni rahisi zaidi. Kwani kuumba ni kuleta kitu kisichokuwepo kabisa, na kurudisha ni kukusanya viungo vilivyotawanyika.

Kwa hiyo basi inawalazimu moja ya mambo mawili: Ama muamini yote mawili au muyakate yote. Mwenye kuamini moja na akaacha jingine atakuwa amejipinga yeye mwenyewe. Hii inaitwa dalili ya kulazimiana baina ya vitu viwili, haiepukani na nyingine. Kwa hiyo moja inaitolea dalili nyingine kichanya na kihasi.

Kisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) akapiga mifano ya kuumba kwake inayofahamisha uwezekano wa kuweko ufufuo; kama ifutavyo:-

1. Je, mnaiona mbegu ya uzazi mnayoitoneza? Je, mnaiumba nyinyi, au tunaimba Sisi?

Ni nani aliyewaumba kutokana na manii yenu kuwa mtu aliyekamilika viungo vyake na silika yake. Ni nyinyi au Mwenyezi Mungu? Mmeshusha manii katika mfuko wa uzazi wa mwanamke tu na kazi yenu ikaisha. Ni nani aliyeyageuza manii kuwa pande la damu nalo kuwa pande la nyama kisha kuwa mifupa na mifupa kuvikwa nyama n.k.? Ikiwa mtasema yote hiyo ni kazi ya asili ya maumbile peke yake, tutawauliza:

Ni nani aliyeyaleta hayo maumbile? Mkijubu kuwa yamejileta yenyewe, tutawauliza: Ni nani aliyempa mtu uhai, hisia na utambuzi? Mkisema ni hayo maumbile, tutawauliza: Hayo yana uziwi na upofu, na asiyekuwa nacho hawezi kutoa.

Mkiendelea kusema kuwa uhai umetokea kwenye maada bila ya makusudio, nasi tutawaambia kuwa maneno haya nayo yametokea bila ya makusudio. Na akili haikubali tafsiri yoyote ya maisha na nidhamu ya ulimwengu isipokuwa kwa sababu ya kiakili iliyofanya. Na haiwezekani kuweko sababu zizizokuwa na ukomo; vinginevyo kupatikana kusingekuwa na athari.

Sisi tumewawekea mauti.

Mwenye kumiliki mauti ndio huyo huyo anayemiliki uhai.

Na Sisi hatushindwi kuwaleta wengine badala yenu na kuwaumba nyinyi kwa umbo msilolijua.

Hakika Mwenyezi Mungu (s.w.t) hashindwi, wala hapitwi na lolote; na yeye ni muweza wa kila jambo. Na kwa uweza wake amehamisha kukosekana kwenye kupatikana. Lau Mwenyezi Mungu angelitaka kuwabadilisha waasi kuwa watu wengine wanaomtii, angelifanya hilo wala hakuna wa kulizuia analolitaka.

Hapa kuna makemeo na kiaga kwa yule anayepinga mwito wa haki:

وَإِن تَتَوَلَّوْا يَسْتَبْدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُونُوا أَمْثَالَكُم ﴿٣٨﴾

"Na mkigeuka atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi."

Juz. 26 (47:38).

Na bila ya shaka mlikwishajua umbo la kwanza, tena mbona hamkumbuki?

Mmejua kuumbwa kwenu kusikotokana na kitu chochote; sasa je tutashindwa kuvikusanya viungo vyenu na kuvirudisha kama vilivyokuwa baada ya baada ya kutawanyika?

Tafsiri fasaha zaidi ya Aya hii ni kauli ya Imam Ali (a.s): "Nashangazwa na yule anayepinga ufufuo wa mwisho na hali anaona ufufuo wa kwanza!"

2. Je, Mnaona mnayolima? Je, ni nyinyi mnayoyaotesha au ni Sisi ndio wenye kuotesha?

Mtu anatafuta mbegu, analima anapanda na kumwagilia maji, hilo halina shaka. Lakini hiyo mbegu, miche, maji, ardhi na mengineyo, kama jua na hewa yametoka wapi? Wakisema; yametokana na kitendo cha maada isiyokuwa na akili, nasi tutawajibu: Kauli yenu hiyo inatokana na asiyekuwa na akili.

Tungelitaka tungeliyafanya mapepe, mkabaki mnastaajabu, Mkisema: Hakika sisi tumegharimika.

Yaani tumetaabika sana na kugharimika kutayarisha mashamba na wala hatukunufaika na chochote. Na mtaendelea kusema: Bali sisi tumenyimwa riziki. Hakuna kitu kinachotia uchungu kwenye nafsi kuliko kuhisi kunyimwa.

3. Je, mnayaona maji mnayoyanywa? Je, ni nyinyi mnayoyateremsha kutoka mawinguni au ni Sisi ndio wenye kuyateremsha?

Mwenyezi Mungu (s.w.t) anaashiria kuwa Yeye ndiye aliyeleta maumbile yanayosababisha mvua. Maana ni kuwa maji haya, ambayo ni asili ya uhai, na ambayo mtu hana budi nayo kwa hali yoyote, ni nani aliyesababisha kupatikana kwake na kuyapangilia? Ni nyinyi au ni yule ambaye ameumba kila kitu na akakipangilia?

Mwenyezi Mungu amezindua, kwenye Aya nyingi. kwamba Yeye atafufua wafu; kama anavyoifufua ardhi kwa mvua:

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنَّكَ تَرَى الْأَرْضَ خَاشِعَةً فَإِذَا أَنزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَتْ ۚ إِنَّ الَّذِي أَحْيَاهَا لَمُحْيِي الْمَوْتَىٰ ۚ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٩﴾

"Na katika Ishara zake ni kwamba unaiona ardhi imetulia, lakini tunapoiteremshia maji mara unaiona inashtuka na kututumka. Bila ya shaka

aliyeihuisha ardhi ndiye atakayehuisha wafu. Hakika Yeye ni Muweza juu ya kila kitu.” Juz. 24 (41:39).

Tungelipenda tungeliyafanya ya chumvi kali. Basi mbona hamshukuru?

Neno chumvi kali tumelifasiri kutokana na neno la kiarabu ujaj lenya maana ya chumvi kali iliyofikia kufanya kitu kiwe kichungu.

Maana ni kuwa lau Mwenyezi Mungu angelitaka angeliyafanya maji kuwa na chumvi sana yasiyoweza kuwa na manufaa ya kunywewa wala kulimi- wa, lakini ameyafanya tamu baridi, kwa ajili ya kuwahurumia. Pamoja na kuwa neema hii inataka kushukuriwa, lakini bado Mwenyezi Mungu anamlipa mwenye kushukuru.

4. Je, mnauona moto mnaouwasha?

Moto ni neema sawa na maji. Lau si huo mtu asingeliweza kupiga hata hatua moja katika maisha yake; mpaka siku yake ya mwisho angelibakia akiishi na wanyama mwituni.

Ni nyinyi mliouumba mti wake au Sisi ndio Wenye kuuumba?

Moto unasabishwa na vitu mbali mabali; miongoni mwavyo ni kuni, makaa ya mawe, mafuta umeme na mengineyo watakayoyagundua wataalamu baadae au wasiyagundue, Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi.

Umetajwa mti katika Aya kwa njia ya kufananisha tu. Wafasiri wamesema kuwa waarabu walikuwa wakipekecha vijiti kutoa moto, ndio maana Mwenyezi Mungu akaleta mfano unaoendana na maisha ya wakati huo.

Sisi tumeufanya uwe ni ukumbusho na manufaa kwa wenye kusikiliza.

Neno kusikiliza tumelifasiri kutokana na neno muqwin ambalo wafasiri wametofatiana katika tafsiri yake. Tabari anasema: “Wametofautiana wafasiri katika maana ya neno muqwin. Kuna waliosema ni wasafiri na waliosema ni wasikilizaji.”

Sisi tumechagua wenye kusikiliza kwa vile moto unawanufaisha wasafiri na wasiokuwa wasafiri.

Basi lisabihi jina la Mola wako aliye Mkuu.

Maneno yanaelekezwa kwa Mtume wakikusudiwa watu wote. Maana ni mtukuze na umtakase Muumba Mkuu na kila yasiyofanana na ukuu wake. Waislamu wanaisoma tasbihi katika rukui zao. Ama kwenye sujudi zao wanasoma tasbihi iliyoko (87:1).

فَلَا أُقْسِمُ بِمَوَاقِعِ النُّجُومِ ﴿٧٥﴾

75. Basi naapa kwa maanguko ya nyota.

وَإِنَّهُ لَقَسَمٌ لَّوْ تَعْلَمُونَ عَظِيمٌ ﴿٧٦﴾

76. Na hakika bila ya shaka hiki ni kiapo kikubwa, lau mngelijua!

إِنَّهُ لَقُرْآنٌ كَرِيمٌ ﴿٧٧﴾

77. Hakika hii bila ya shaka ni Qur’an Tukufu,

فِي كِتَابٍ مَّكْنُونٍ ﴿٧٨﴾

78. Katika Kitabu kilichohifadhiwa.

لَّا يَمَسُّهُ إِلَّا الْمُطَهَّرُونَ ﴿٧٩﴾

79. Hapana akigusaye ila waliotakaswa.

تَنزِيلٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٨٠﴾

80. Ni uteremsho unaotoka kwa Mola wa walimwengu wote.

أَفَبِهَـٰذَا الْحَدِيثِ أَنتُم مُّدْهِنُونَ ﴿٨١﴾

81. Je, ni maneno haya ndiyo nyinyi mnayafanyia udanganyifu?

وَتَجْعَلُونَ رِزْقَكُمْ أَنَّكُمْ تُكَذِّبُونَ ﴿٨٢﴾

82. Na mnafanya riziki yenu kuwa mnakadhibisha?

فَلَوْلَا إِذَا بَلَغَتِ الْحُلْقُومَ ﴿٨٣﴾

83. Basi mbona itakapofika kwenye koo.

وَأَنتُمْ حِينَئِذٍ تَنظُرُونَ ﴿٨٤﴾

84. Na nyinyi wakati huo mnatazama,

وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنكُمْ وَلَـٰكِن لَّا تُبْصِرُونَ ﴿٨٥﴾

85. Na Sisi tuko karibu zaidi naye kuliko nyinyi, lakini hamuoni,

فَلَوْلَا إِن كُنتُمْ غَيْرَ مَدِينِينَ ﴿٨٦﴾

86. Na lau kuwa nyinyi hamumo katika mamlaka,

تَرْجِعُونَهَا إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿٨٧﴾

87. Kwa nini hamuirudishi, ikiwa nyinyi mnasema kweli?

فَأَمَّا إِن كَانَ مِنَ الْمُقَرَّبِينَ ﴿٨٨﴾

88. Basi akiwa miongoni mwa waliokaribishwa.

فَرَوْحٌ وَرَيْحَانٌ وَجَنَّتُ نَعِيمٍ ﴿٨٩﴾

89. Itakuwa ni raha, na manukato, na Bustani zenye neema.

وَأَمَّا إِن كَانَ مِنْ أَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٩٠﴾

90. Na akiwa katika watu wa kuume.

فَسَلَامٌ لَّكَ مِنْ أَصْحَابِ الْيَمِينِ ﴿٩١﴾

91. Basi ni Salama kwako uliye miongoni mwa watu wa kuume.

وَأَمَّا إِن كَانَ مِنَ الْمُكَذِّبِينَ الضَّالِّينَ ﴿٩٢﴾

92. Na ama akiwa katika waliokadhibisha wapotovu,

فَنُزُلٌ مِّنْ حَمِيمٍ ﴿٩٣﴾

93. Basi karamu yake ni maji yanayochemka,

وَتَصْلِيَةُ جَحِيمٍ ﴿٩٤﴾

94. Na kutiwa Motoni.

إِنَّ هَـٰذَا لَهُوَ حَقُّ الْيَقِينِ ﴿٩٥﴾

95. Hakika hii ndiyo haki yenye yakini.

فَسَبِّحْ بِاسْمِ رَبِّكَ الْعَظِيمِ ﴿٩٦﴾

96. Basi lisabihi jina la Mola wako aliye Mkuu.

## HAPANA AIGUSAYE ILA WALIOTAKASWA

**Aya 75 – 96**

### MAANA

Basi naapa kwa maanguko ya nyota, na hakika bila ya shaka hiki ni kiapo kikubwa, lau mngelijua!

## LUGHA

Wafasiri wengi wamesema kuwa herufi la hapa ni ziyada kiirabu ya nahau; kama ilivyo katika Aya ya mwisho ya Juzuu hii tuliyo nayo (57:29) na “Nini kilichokuzuia kumsujudia.” Juz. 8 (8:12). Wengine wamesema kuwa herufi La hapa ni ya asili, na kwamba maana yake ni ‘Siapi,’ kwa vile jambo liko wazi nilislohotajia kiapo.

Kauli sahii ni ya mwanzo, kwa dalili ya kuli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: “Na hakika bila ya shaka hiki ni kiapo kikubwa, lau mngelijua!” inayofahamisha kuwa Mwenyezi Mungu ameapa hasa.

Katika Juz. 23 (37:1), tumesema kuwa Mwenyezi Mungu anaweza kuapia chochote katika viumbe wake, kwa sababu kila kiumbe kinafahamisha kuweko muumba, ujuzi wake na hikima yake; sikwambii tena ikiwa kinachoapiwa athari yake inaonyesha zaidi mpangilio wa ulimwengu na nidhamu yake na kuhifadhika kwake na kubakia; kama vile kuwekwa nyota sehemu zake na mpangilio wake; kiasi ambacho lau itasogea moja tu kutoka sehemu yake kwa nafasi ya unywele mmoja tu, basi kila kitu kitaharabika. Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: ‘lau mngelijua!,’ inaashiria kuwa watu wengi hawajui hakika hii; hasa wale wa zama za mwanzomwanzo.

## UISLAMU NA WANAFIKRA WAKUU WA ULAYA

Hakika hii bila ya shaka ni Qur’an Tukufu.

Ndio! Hii ni Qur’an tukufu inayotosheleza miongozo na dalili zote, ni ponyo la ugonjwa wa ujinga na upotevu, inaongoza kwenye vituo vya heshima na salama na ni mkombozi wa vifungo vya dhulma na utumwa.

Siri ya sifa zote hizi na nyinginezo ni kuwa Qur’an inatekeleza mahitajio yote ya maisha, na inafungamanisha dini na matendo, katika maisha ya dunia, kwa ajili ya maisha mazuri ya usawa yasiyokuwa na matatizo wala uadui. Hata wema wa Akhera pia hawezi kuupata ila mwenye ikhlasi na akafanya matendo mema. Kabisa! Hakuna njia ya kwenda kwa Mwenyezi Mungu wala kuokoka isipokuwa kwa matendo yenye kunufaisha:

فَأَمَّا الزَّبَدُ فَيَذْهَبُ جُفَاءً ۖ وَأَمَّا مَا يَنفَعُ النَّاسَ فَيَمْكُثُ فِي الْأَرْضِ ﴿١٧﴾

“Ama povu linakwenda bure; ama kinachowafaa watu hukaa kwenye ardhi.” Juz. 13 (13:17).

Ndio maana Waislamu wamekongamana kwa kauli moja kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakuweka sharia wala hataweka sharia ila kwa heri ya mtu na masilahi yake, na kwamba haiwezekani kabisa kuweka sharia itakayokuwa na madhara kwa mtu yoyote vyovyote awavyo.

Ikiwa itadaiwa kuwa ni sharia ya Qur’an na haiendani na misingi hii, basi hiyo itakuwa imetokana na ujinga wa wajinga au wasingiziaji wanaobandika mambo. Aya zinazofahamisha hivyo zinahisabika kwa makumi; miongoni mwazo ni hizi zifuatazo:

Kauli yake Mwenyezi Mungu kupitia Nabii wake Shua’yb:

إِنْ أُرِيدُ إِلَّا الْإِصْلَاحَ ﴿٨٨﴾

“Sitaki ila kutengeneza.” Juz. 12 (11:88).

مَا يُرِيدُ اللَّـهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُم مِّنْ حَرَجٍ وَلَـٰكِن يُرِيدُ لِيُطَهِّرَكُمْ وَلِيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكُمْ ﴿٦﴾

“Mwenyezi Mungu hapendi kuwatia katika taabu lakini anataka kuwatakasa na kutimiza neema yake juu yenu.” Juz.6 (5:6).

إِنَّ اللَّـهَ بِالنَّاسِ لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٤٣﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu, kwa watu, ni Mpole, Mwenye kurehemu.” Juz. 2 (2:143).

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا ۚ فِطْرَتَ اللَّـهِ الَّتِي فَطَرَ النَّاسَ عَلَيْهَا ۚ لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ اللَّـهِ ۚ ذَٰلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ وَلَـٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾

“Basi uelekze uso wako sawa sawa kwenye dini – ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo dini ya sawa sawa, lakini watu wengi hawajui.” Juz. 21 (30:30).

Huu ndio uhakika wa Uislamu na uhalisia wake, ulio katika kitabu cha Mwenyezi Mungu na ujuzi wake. Hakuna kitu ndani yake isipokuwa kile anachokihitajia mtu kwa silika yake na maumbile safi aliyozaliwa nayo yanayomtofautisha na viumbe vingine vyote, lakini sio kujiingiza kwenye tamaa dhulma uchokozi n.k.

Hakika hii wameigundua wanafalsafa na wanafsihi wengi wa Ulaya. Wakautukuza Uislamu na wakamsifia Mtume **(s.a.w.w)**; si kwa lolote ila ni kwa msukumo wa heri, haki na uadilifu.

Lau tungelikuwa na nafasi tungelitaja kauli zao nyingi, lakini yasiyowezakana yote hayaachwi yote. Tutachagua kauli za baadhi yao; kama vile: Mjarumani Goeth, Mfaransa Amrtin, Mrusi Tolstoy na Mwingereza Bernad Show. Wote hawa kama unavyooona wanatofautiana katika uta- maduni, mwelekeo na jinsia zao.

Goethe alisoma Qur’an, akatambua yaliyomo ndani yake na akaitukuza. Alifanya hafla usiku wa Laylatul-qadr ambao Qur’an iliteremshwa. Alisoma Historia ya Mtume **(s.a.w.w)**, akatunga kasida ya Muhammad na akaandika tamthilia ya Muhammad **(s.a.w.w)**.

Miongoni mwa kauli zake ni: “Ikiwa Uislamu ni kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu na sio kwenye hawa na matamanio, basi tuishi kwenye Uislamu na tufeni kwenye Uislamu.”

Amrtin, Mshairi mkubwa wa Kifaransa, anasema: “Maisha ya Muhammad **(s.a.w.w)** yote yanafahamisha kuwa hakudhamiria kudanganya au kuishi kwenye ubatilifu… Hakika yeye ni mwongozi wa watu kwenye akili na ni muasisi wa dini isiyokuwa na uzushi.”

Tolstoy, mwanafalsafa ya binadamu kutoka Urusi, anasema: “Katika mambo yasiyo na shaka ni kuwa Muhammad ameihudumia jamii kwa huduma tukufu. Inatosha kuwa ni fahari, kwamba yeye ameongoza mamia ya mamilioni kwenye nuru ya haki utulivu na amani na akaupa ubinadamu njia ya maisha. Hiyo ni kazi kuu ambayo haiwezi isipokuwa yule aliyepewa nguvu na ilhamu kutoka mbinguni.”

Mwanafisihi wa kimataifa kutoka Uingerza, Bernad Show anasema: “Ni lazima isemwe kuwa Muhammad ni mwokozi wa mtu… Mimi ninaamini kwamba lau hivi sasa angelitawala ulimwengu mtu mfano wake, angelifaulu kutatua matatizo kwa namna ambayo ingeuleta ulimwengu kwenye amani

na raha…Hakika Muhammad ni mkamilifu zaidi ya watu waliopita na watakaokuja, wala haifikiriwi kupatikana mfano wake katika watakaokuja.”

Kauli ya Show kuwa Muhammad ni mkamilifu zaidi ya watu waliopita na watakaokuja, inamaanisha kuwa risala ya Muhammad **(s.a.w.w)** haifikiwi na risala ya manabii waliotangulia; hata Isa na Ibrahim.

Na aliposema: “Wala haifikiriwi kupatikana mfano wake katika watakaokuja.” Maana yake ni kuwa hakuna yeyote baada ya Muhammad **(s.a.w.w)** anayeweza kuleta jipya lenye faida au manufaa zaidi ya alilolileta Muhammad.

Vile vile anamaanisha kuwa mwito wa Muhammad hauhitajii dini wala sharia au nidhamu nyingine; bali hizo nyingine ndizo zinauhitajia.

Kila mmoja wetu anajua kuwa Bernad Show ni katika wanafikra wakubwa wa ulaya aliyetokea katika karne ya ishirini, karne ya maendeleo ya atom na anga; na kwamba ushahidi wake huu ni matokeo ya utafiti mrefu, fikra ya kina na upembuzi yakinifu.

Ushuhuda huu wa Bernad ni ibara au tafsiri nyingine ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٠٧﴾

“Na hatukutuma ila uwe ni rehema kwa walimwengu wote.” Juz. 17 (21:107).

Yaani walimwengu wote kila wakati na kila mahali. Vile vile tafsiri ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَلَـٰكِن رَّسُولَ اللَّـهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ ﴿٤٠﴾

“Bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na mwisho wa mitume.” Juz. 22 (33:40).

Vile vile ushahidi wa Show, ni dalili mkataa ya ukweli wa waislamu katika itikadi yao, kwamba Muhammad ni mkamilifu zaidi ya watu waliopita na watakaokuja, wala haifikiriwi kupatikana mfano wake katika watakaokuja; kama anavyosema.

Je, baada ya hayo yote wanasemaje vijana wanokana dini ya mababa na mababu zao, kuhusiana na kauli ya Bernad Show? Je, wao wana ujuzi zaidi, wana hamu zaidi ya ubinadamu kuliko yeye au wao wanazungumza kwa kutumia fikra za maadui wa Uislamu na ubinadamu bila ya kujitambua?

Katika Kitabu kilichohifadhiwa.

Wametofautiana katika kuhifadhiwa Kitabu. Kuna waliosema kimehifadhiwa na mchanga na vumbi; kama ilivyoelezwa katika Tafsir Attabari. Wengine wakasema kimehifadhiwa katika Lawh mahfudh.

Tuonavyo sisi ni kuwa hakuna haja ya mzozo huu, kwa sababu Mwenyezi Mungu (s.w.t) amebaainisha maana ya hifadhi hii kwa kusema:

Hapana akigusaye ila waliotakaswa. Ni uteremsho unaotoka kwa Mola wa walimwengu wote.

Yaani Qur’an ni wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu sio kutoka kwa shetani, wala si uchawi au ngano za watu wa kale; kama wanavyodai walahidi.

Wameafikiana wana fikh wa madhehbu kuwa ni haramu kugusa maandishi ya Qur’an isipokuwa kwa aliyetwahara mwenye udhu. Wakatofautiana katika kuiandika na kuisoma kwa asiyekuwa twahara.

Hanafi wamesema haifai kuiandika, lakini inajuzu kuisoma kwa moyo. Shafii wakasema haijuzu kuiandika wala kuisoma isipokuwa kama ni kwa kukusudia dhikri; kama kusoma Bismillah kwenye chakula. Maliki nao wakasema haijuzu kuiandika, lakini inajuzu kusoma kwa moyo au kwa kuiangalia. Hambali wamesema haijuzu kuiandika, lakini inajuzu kuichukua kwa kuiziba na kizuizi.

Shia Imamiyah wamesema si haramu kwa mwenye janaba kusoma Qur'an na inajuzu kuandika, isipokuwa sura nne za Azaim, zenye sijda ya wajib, ambazo ni: Alaq. Annajm, Alif lamim Sajjda na Sajda (96, 53, 41 na 32).

Je, ni maneno haya ndiyo nyinyi mnayafanyia udanganyifu?

Makusudio ya maneno hapa ni Qur'an. Kauli hii inaelekezwa kwa wanafiki ambao walifanya udanganyifu; wakadhihirisha kuikubali Qur'an na nyoyoni wanaikataa.

Na mnafanya riziki yenu kuwa mnakadhibisha?

Makusudio ya riziki hapa ni neema na kukadhibisha ni kuikataa. Maana ni kuwa Qur'an ni neema kwenu kutoka kwa Mwenyezi Mungu enyi wadanganyifu, vipi mnaikabili kwa kuikana na kuikufuru.

Kundi katika wafasiri wamesema: mvua iliponyesha walikuwa wakisema: hii ni kazi ya maumbile, kwa hiyo ikawa huko ni kukufuru neema ya Mwenyezi Mungu, na ndio wakateremshiwa Aya hii.

Lakini kauli hii iko mbali na maana. Kwa sababu mazungumzo yanahusiana na Qur'an si mvua.

Basi mbona itakapofika kwenye koo, na nyinyi wakati huo mnatazama!

Itakapofika kwenye koo ni roho. Hilo limefahamika kutokana na mfumo wa maneno unavyokwenda. Nyinyi wanaambiwa waliokaribu na anayekata roho, awe ni katika jamaa zake au la.

Maana ni mtakuwaje nyinyi wanafiki mmoja wenu akifikiwa na mauti na roho ikafika kooni huku mnamwangalia mkitamani aendelee kuishi, je mtakuwa na uwezo na kumrudishia uhai na afya yake?

Na Sisi tuko karibu zaidi naye kuliko nyinyi, lakini hamuoni.

Naye ni huyo anayekata roho. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) anayajua yanayompitia mwenye kukata roho, na jinsi nyinyi mnavyoshindwa kumwokoa na mnavyoona uchungu kumkosa, lakini nyinyi hamjui kuwa Mwenyezi Mungu yuko kila mahali kwa ilimu yake na uweza wake.

Na lau kuwa nyinyi hamumo katika mamlaka, kwanini hamuirudishi, ikiwa nyinyi mnasema kweli?

Ikiwa nyinyi mko huru, kama mnavyodai, na hamtaulizwa lolote wala hakuna yoyote anayeweza kuwalazimisha kitu, basi kwanini hamyazuii mauti na mkazirudisha roho kwenye mili yenu? Kwa sababu mnavyomaanisha ni kuwa Mwenyezi Mungu hamiliki mauti, uhai, ufufuo wala hisabu.

Basi akiwa miongoni mwa waliokaribishwa, itakuwa ni raha, na manukato, na Bustani zenye neema.

Mwanzoni mwa sura hii Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewagawanya watu siku ya kiyama kwenye aina tatu, waliotangulia wenye kukaribishwa, watu wa kuume na wa kushoto.

Katika Aya hii anataja kuwa mwenye kukata roho akiwa ni katika waliotangulia basi atakuwa mwenye amani na neema ya milele. Aliyowaandalia wenye kutangulia ameyataja katika Aya ya 12 na zinazofuatia katika sura hii tuliyo nayo.

Na akiwa katika watu wa kuume, basi ni Salama kwako uliye miongoni mwa watu wa kuume.

Akiwa mkata roho ni katika aina ya pili ambayo ni watu wa upande wa kuume, basi malaika watampa bishara ya salama na raha. Mwenyezi Mungu ameyataja aliyowaandalia hawa katika Aya 27 na zinazofutia katika sura hii tuliyo nayo.

Na ama akiwa katika waliokadhibisha wapotovu, basi karamu yake ni maji yanayochemka, na kutiwa Motoni.

Anayekata roho akiwa ni katika aina ya tatu ambao ni watu wa kushoto, basi makazi yake ni Jahannam ambayo ni makazi mabaya kabisa. Maandalizi ya hawa, Mwenyezi Mungu ameyataja katika Aya 41 na zinazofuatia katika sura hii tuliyo nayo.

Hakika hii ndiyo haki yenye yakini isiyokuwa na shaka yoyote. Katika baadhi ya vitabu vya kisufi imeelezwa kuwa utambuzi uko mafungu matatu: Utambuzi wa ilimu ya yakini; kama kujua kuweko moto kutokana na moshi unaofuka, kujua kwa jicho la yakini; kama kuuona moto wenyewe hasa na kujua kwa haki ya yakini; kama kuungua kwenye huo moto.

Basi lisabihi jina la Mola wako aliye Mkuu.

Imetangulia kwa herufi zake katika Aya ya 75 ya sura hii.

## MWISHO WA SURA YA HAMSINI NA SITA: SURAT AL-WAAQIA

26

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

Sura Ya Hamsini Na Saba: Al-Hadid. Imeshuka Madina. Ina Aya 29.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

سَبَّحَ لِلَّـهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١﴾

1. Vinamsabihi Mwenyezi Mungu vilivyo katika mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima.

لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ يُحْيِي وَيُمِيتُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢﴾

2. Yeye ndiye Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi. Anahuisha na anafisha. Na Yeye ni Mwenye uweza wa kila kitu.

هُوَ الْأَوَّلُ وَالْآخِرُ وَالظَّاهِرُ وَالْبَاطِنُ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٣﴾

3. Yeye ndiye wa Mwanzo na ndiye wa Mwisho, naye ndiye wa Dhahiri na wa Batini, naye ndiye Mjuzi wa kila kitu.

هُوَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِي الْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنزِلُ مِنَ السَّمَاءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنتُمْ وَاللَّـهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٤﴾

4. Yeye ndiye aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita; kisha akastawi juu ya Arshi. Anayajua yanayoingia katika ardhi, na yanayoteremka kutoka mbinguni, na yanayopanda humo. Naye yuko pamoja nanyi popote mlipo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona mnayoyatenda.

لَّهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَإِلَى اللَّـهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٥﴾

5. Ufalme wa mbingu na ardhi ni wake. Na mambo yote yanarejeshwa kwa Mwenyezi Mungu.

يُولِجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُولِجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ وَهُوَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٦﴾

6. Huuingiza usiku katika mchana, na huuingiza mchana katika usiku. Na Yeye ni Mwenye kuyajua yaliomo vifuani.

آمِنُوا بِاللَّـهِ وَرَسُولِهِ وَأَنفِقُوا مِمَّا جَعَلَكُم مُّسْتَخْلَفِينَ فِيهِ فَالَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَأَنفَقُوا لَهُمْ أَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿٧﴾

7. Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake; na toeni katika alivyowafanyia nyinyi kuwa ni waangalizi wake. Basi walioamini miongoni mwenu, na wakatoa, wana malipo makubwa.

## NDIYE WA MWANZO NA NDIYE WA MWISHO

**Aya 1 – 6**

### MAANA

Katika Juz. 14 (16:49), Mwenyezi Mungu anasema: “Vinamsujudia Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini.”

Kumsabihi Mwenyzi Mungu na kumsujudia ni kukiri uweza wa Mwenyezi Mungu mtukufu na hikima yake. Kukiri huku kunakua katika hali mbili: Moja ni kwa lugha ya kusema na nyingine ni kwa lugha ya hali. Mtu huwa anatumia hali zote mbili, lakini viumbe vingine visivyoweza kutamka huwa vinasujudi na kusabihi kwa lugha ya hali. Kwa sababu hakuna kiumbe chochote isipokuwa kinafahamisha kuweko mwenye kukifanya na kukipa sura. Tazama Juz. 15 (15:44) kifungu cha 'Kila kitu kinamsabihi.'

Katika vitabu vya sera, Hadith na Tafsiri imeelezwa kuwa Fatima binti wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akifanya kazi zote za nyumbani yeye mwenyewe, akimuhudumia mumewe na watoto wake. Siku moja akamweleza baba yake hali yake, naye akaona athari ya juhudi yake kwenye mikono yake. Basi akamtaka ampatie mjakazi katika mateka wa vita ili amsaidie kazi za nyumbani.

Mtume akasema: sitakupa mjakazi na hali kuna mwingine anafunga tumbo lake kwa njaa. Kisha akaendelea kusema: Unaonaje nikikufahamisha jambo lilio na heri zaidi kuliko mjakazi – kusabihi Mwenyezi Mungu mara 33, kumhimidi mara 33 na kumfanyia takbira mara 34. Fatima akasema: Nimeridhia ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Tasbihi hii inajulikana kwa jina la Tasbih Zahra.

Yeye ndiye Mwenye ufalme wa mbingu na ardhi. Anahuisha na anafisha.

Kama kwamaba muulizaji ameuliza kwanini vikamsabihi Mwenyezi Mungu vilivyo katika ardhi na mbingu? Na Yeye ni Mwenye uweza wa kila kitu. Analolitaka hua na asilolitaka haliwi.

Yeye ndiye wa Mwanzo bila ya kuanza kulikokuwa kabla yake na kutoka kwake ndio chanzo cha kila kitu. Na ndiye wa Mwisho, bila ya kuweko na ukomo baada yake na kwake Yeye ndio mwisho wa kila kitu.

Naye ndiye wa Dhahiri kwa athari na vitendo sio kwa kuhisiwa. Na wa Batini, akili na dhana haziwezi kufikiria hakika yake; isipokuwa anadhihiri kwa athari zake.

Kwenye Nahjul-balagha imesemwa: "Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye ameonyesha athari za mamlaka yake na ukuu wa ukubwa wake, zilizozubaisha mboni za macho kwa maajabu yake na kuzuia dhana za nafsi kujua hakika ya sifa zake... amekuwa karibu akawa mbali na amekua juu akawa chini. Kuwa kwake kumetangulia nyakati, na kupatikana kwake kumetangulia kukosekana, na ukale wake umetangulia kuanza."

Naye ndiye Mjuzi wa kila kitu.

Ni mjuzi wa kila kitu kwa vile ameumba kila kitu.

Yeye ndiye aliyeziumba mbingu na ardhi katika siku sita; kisha akastawi juu ya Arshi.

Makusudio ya siku ni mikupuo, kustawi ni kutawala na arshi ni ufalme. Umetangulia mfano wake katika Juz. 8 (7:54), 11 (10:3), 12 (11:7), 19 (25:59) na 21 (32:4).

Anayajua yanayoingia katika ardhi miongoni mwa hazina, mbegu na maji; hata milipuko ya mabomu ardhini wanayoilipua maadui wa Mwenyezi Mungu na wa ubinadamu, Mwenyezi Mungu anaijua hakika yake na atahri yake. Pia anajua lengo lake kuwa ni kutawala waja wa Mwenyezi Mungu na kuwawafanya wawanyenyekee na wakuze viwanda vya silaha.

Vile vile Mwenyezi Mungu anayajua na yanayotoka humo, ikiwemo mimea wadudu na maji. Hata mafuta pia Mwenyezi Mungu anajua yanatoka kwenye ardhi gani, mikono inayoyatoa, mashirika yanayoyapora na vita vinavyosababishwa nayo. Na yanayoteremka kutoka mbinguni, yakiwemo maji theluji, nuru na heri nyinginezo.

Pia amewajua wale waliokwenda kwenye mwezi ili waweze kupata nyenzo watakayoitumia kuhodhi baraka za mbinguni na kuwanyima waja wa Mwenyezi Mungu; sawa na walivyoifanyia ardhi na heri zake. Lakini Mwenyezi Mungu ambaye imetukuka hikima yake, aliwarudisha nyuma kwa visigino vyao kwenye jaribio la tatu na wakarudi utupu.

Na yanayopanda humo.

Vile vile Mwenyezi Mungu (s.w.t) anajua yanayoendelea kwenye anga za juu, hata ndege za ujajusi na zile zinazobeba makombora na setilaiti zinazozunguka juu ya ardhi kwa malengo ya kishetani; kama vile ujasusi, na ugaidi kwa walala hoi na kuwapora riziki zao.

Naye yuko pamoja nanyi popote mlipo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona mnayoyatenda. Ufalme wa mbingu na ardhi ni wake. Na mambo yote yanarejeshwa kwa Mwenyezi Mungu.

Huu ni ukemeo na utisho kwa kila taghuti na dhalimu, kuwa matendo yake yamehifadhiwa mbele ya Mwenyezi Mungu na kwamba amewekwa rahani na atahisabiwa hisabu ya ndani na nzito na kuadhibiwa adhabu chungu.

Huuingiza usiku katika mchana, na huuingiza mchana katika usiku. Na Yeye ni Mwenye kuyajua yaliomo vifuani.

Sayari zinataharaki na misimu inageuka, kuna msimu sehemu ya usiku inachukuliwa na mchana na mwingine mchana unachukuliwa na usiku na pia kuna siku unakuwa sawa usiku na mchana. Umetangulia mfano wake katika Juz. 3 (3:27), 17 (22:61), 21: (31:29) na 22 (34:13).

وَمَا لَكُمْ لَا تُؤْمِنُونَ بِاللَّـهِ ۙ وَالرَّسُولُ يَدْعُوكُمْ لِتُؤْمِنُوا بِرَبِّكُمْ وَقَدْ أَخَذَ مِيثَاقَكُمْ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿٨﴾

8. Na mna nini hata hamumwamini Mwenyezi Mungu na hali Mtume anawaita mumwamini Mola wenu? Naye amekwishachukua ahadi yenu, ikiwa nyinyi ni waumini.

هُوَ الَّذِي يُنَزِّلُ عَلَىٰ عَبْدِهِ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ لِّيُخْرِجَكُم مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ۚ وَإِنَّ اللَّـهَ بِكُمْ لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿٩﴾

9. Yeye ndiye anayemteremshia mja wake Aya zinazobainisha wazi ili awatoe gizani muingie kwenye nuru. Na hakika Mwenyezi Mungu kwenu ni Mpole, Mwenye kurehemu.

وَمَا لَكُمْ أَلَّا تُنفِقُوا فِي سَبِيلِ اللَّـهِ وَلِلَّـهِ مِيرَاثُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ لَا يَسْتَوِي مِنكُم مَّنْ أَنفَقَ مِن قَبْلِ الْفَتْحِ وَقَاتَلَ ۚ أُولَـٰئِكَ أَعْظَمُ دَرَجَةً مِّنَ الَّذِينَ أَنفَقُوا مِن بَعْدُ وَقَاتَلُوا ۚ وَكُلًّا وَعَدَ اللَّـهُ الْحُسْنَىٰ ۚ وَاللَّـهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿١٠﴾

10. Na mna nini hata hamtoi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na hali urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa miongoni mwenu wenye kutoa kabla ya Ushindi na wakapigana vita. Hao

wana daraja kubwa zaidi kuliko wale waliotoa baadae na wakapigana. Na wote hao Mwenyezi Mungu amewaahidi wema. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda.

مَّن ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّـهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضَاعِفَهُ لَهُ وَلَهُ أَجْرٌ كَرِيمٌ ﴿١١﴾

11. Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, ili amrudishie maradufu, na apate ujira mzuri.

## TOENI KATIKA ALIVYOWAFANYA NI WAANGALIZI

**Aya 7 – 11**

### MAANA

Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake; na toeni katika alivyowafanyia nyinyi kuwa ni waangalizi wake. Basi walio amini miongoni mwenu, na wakatoa, wana malipo makubwa.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amehimiza kutoa na akapendekeza kwa mifumo mbali mbali. Akakemea na kumtishia kwa adhabu kali mwenye kufanya ubahili na akazuia. Miongoni mwa mifumo ya kuhimiza kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu ni Aya hii tuliyo nayo ambayo imeweka sawa imani ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kutoa.

Usawa huu unaashiria kwamba mwenye kufanya ubakhili na akazuia basi amemkufuru Mwenyezi Mungu na Mtume wake kimatendo; hata kama atawamini kinadharia. Vile vile Aya inaashiria kwamba wanachotoa matajairi sio mali yao; isipokuwa wao ni mawakala tu.

Imepokewa riwaya kutoka kwa sahaba mtukufu Abu dharr, kwamba yeye siku moja alitoka na Mtume kuelekea upande wa Uhud. Mtume **(s.a.w.w)** akamwambia: Unauona mlima huu ewe Abu dharr? Akasema: ndio ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mimi sipendi kuwa na dhahabu mfano wake, kisha nitoe katika njia ya Mwenyezi Mungu na nife nibakishe kareti mbili. Abu dhar akasema: sio mirundo miwili ya dhahabu ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Akasema: Hapana karati mbili[1].

Tazama kifungu cha maneno 'Matajiri ni mawakala sio wenyewe' katika Juz. 4 (3:180).

Na mna nini hata hamumwamini Mwenyezi Mungu na hali Mtume anawaita mumwamini Mola wenu? Naye amekwishachukua ahadi yenu, ikiwa nyinyi ni Waumini.

Makusudio ya ahadi hapa ni amali kutokana na inavyofahamisha dalili mkataa. Dalili hizo ziko nyingi sana, tumetangulia kuzitaja pale tunapofasiri Aya za kilimwengu; miongoni mwazo ni zile tulizozitaja katika Juz. 15 (17:83) kifungu cha 'Mwenyezi Mungu na ilimu ya chembe hai;' kama ambavyo tumetaja dalili za utume wa Muhammad **(s.a.w.w)**, katika kufasiri Aya zinazoashiria hivyo; ikiwemo tuliyoyataja punde katika Aya ya 77 ya sura iliyopita kwenye juzuu hii tuliyo nayo, kifungu cha 'Uislamu na wanafikra wakuu wa Ulaya.'

Maana yanayopatikana ya Aya tuliyo nayo ni: vipi nyinyi mnapinga mwito wa Mtume kwenye imani ya Mwenyezi Mungu au kwenye lile linalowapa maisha na hali zimekuwako dalili za kutosha za kuweko

1. Karati moja ni sawa na 0.2gm.

Mwenyezi Mungu na umoja wake na ukweli wa Mtume katika mwito wake na unabii wake?

Razi anasema: kutokana na dalili hizo zilivyohukumia wajibu wa kufanya amali, zimekuwa na msisitizo zaidi ya kiapo, ndio maana Mwenyezi Mungu (s.w.t) akauita ahadi.

Yeye ndiye anayemteremshia mja wake Aya zinazobainisha wazi ili awatoe gizani muingie kwenye nuru.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amemtuma Muhammad **(s.a.w.w)** kwa hoja za kutosheleza na mawaidha ili awatoe kwenye utuiifu wa shetani kwenda kumtii Mwingi wa rehema – kutoka kwenye upotevu na ufisadi kwenda kwenye uongofu na utengeneo. Mtume akawahofisha na nguvu ya Mwenyezi Mungu na adhabu yake, kama wakipinga, na akawaahidi wema na thawabu nyingi kama wataitikia mwito na kumtiii; akawaambia:

Na hakika Mwenyezi Mungu kwenu ni Mpole, Mwenye kurehemu.

Mwenyezi Mungu ni mpole kwa waja, mwenye huruma, mwema na mkarimu.

Anawafanyia upole bila ya wao kujua na kuwaandalia njia ya heri bila ya kudhania na anawaneemesha, lakini wao wanafanya jeuri.

Na mna nini hata hamtoi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na hali urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu?

Mali yote iliyo mikononi mwa mtu ni ya kuazima tu atawaachia wa baada yake. Inaendelea hivi mpaka mtu wa mwisho; akishaondoka atakuwa hana mrithi isipokuwa Mwenyezi Mungu: "Hakika sisi tutairithi ardhi na walio juu yake na kwetu sisi watarejeshwa," Juz. 16 (19:40).

Ikiwa hali ni hiyo basi ubahili ni wa nini? Kwani kujizuia kutoa katika njia ya Mwenyezi Mungu? Katika Nahjul-balagha anasema: "Namshangaa bahili anayeulilia ufukara alioukimbia na unampita utajiri alioutaka. Duniani anaishi maisha ya kifukara na akhera atahisabiwa hisabu ya matajri."

Hawawi sawa miongoni mwenu wenye kutoa kabla ya Ushindi na wakapigana vita.

Mkabala wake ni na waliotoa baada ya ushindi wa Makka.

Ufufanuzi wa maana ni kuwa kitu kinaweza kupimwa kwa vipimo na kwa aina; kama vyakula vinywaji, mavazi na vipambo. Thamani ya vitu hivi na mfano wake hukadiriwa kwa kipimo chake na kwa manufaa yake pamoja. Vingine vinapimwa kwa idadi tu; kama vile upigaji kura. Kura ya mjinga na mtaalamu, ya muovu na mwadilifu zote ni sawa katika kumfikisha mgombea kwenye uongozi au bungeni, au kutomfikisha.

Vingine vinapimwa kwa aina tu; kama vile dawa inayopimwa kwa athari ya kuponesha kwake au kinga yake.

Kutoa nako kuko namna kama hii. Mtu anaweza kutoa maelfu kwa ajili ya sehemu ya kuabudu, lakini asiwe na malipo ya yule aliyetoa mkate kumpa mwenye njaa.

Ndio maana Mwenyezi Mungu (s.w.t) akakana usawa wa aliyetoa na akapigana kabla ya ushindi wa Makka na aliyetoa baada ya ushindi wa Makka. Waislamu kabla ya ushindi wa Makka walikuwa na dhiki na haja sana na huku makafiri wakiwa kwenye utajiri na nguvu, lakini baada ya ushindi ilikuwa kinyume – ukafiri ulidhoofika na Uislamu ukawa na nguvu.

Hao wana daraja kubwa zaidi kuliko wale waliotoa baadae na wakapigana. Na wote hao Mwenyezi Mungu amewaahidi wema. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda.

Hao ni ishara ya wale waliotangulia. Maana ni kuwa kila mmoja kati ya waliotangulia na waliofuatia ana ujira na thaawabu lakini kwa kutofautiana:

وَلِكُلٍّ دَرَجَاتٌ مِّمَّا عَمِلُوا وَلِيُوَفِّيَهُمْ أَعْمَالَهُمْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٩﴾

"Na wote watakuwa na daraja zao mbalimbali kwa waliyoyatenda na ili awalipe kwa vitendo vyao." Juz. 26 (46:19).

Kwa maneno mengine ni kuwa waliotangulia wenye kukaribishwa ndio aina hii ya kwanza ambao Mwenyezi Mungu amewataja katika Aya ya 10 ya sura iliyotangulia. Na watu wa kuume ni katika aina hii ya pili. Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewataja katika Aya ya 67 ya sura hiyo.

Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema, ili amrudishie maradufu, na apate ujira mzuri.

Makusudio ya kukopesha hapa ni kutoa, kwa sababu Mwenyezi Mungu haihitajii mkopo anajitosheleza. Katika Nahjul-balagha kuna maelezo haya: "Mwenyezi Mungu hakuwataka msaada kwa sababu ya unyonge wala hawataki mkopo kwa sababu ya kuishiwa.

Anawataka msaada na hali ana majeshi ya mbingu na ardhi na Yeye ni Mwenye nguvu Mwenye hikima. na anawataka mkopo na hali ana hazina za mbingu na ardhi na Yeye ni mwenye kujitosha msifiwa. Ametaka kuwajaribu ni nani mwenye matendo mazuri zaidi kwenu."

Umetangulia mfano wake na tafsiri yake kwa ufafanuzi katika Juz. 2 (2:245).

27

## TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

يَوْمَ تَرَى الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ يَسْعَىٰ نُورُهُم بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَبِأَيْمَانِهِم بُشْرَاكُمُ الْيَوْمَ جَنَّ اتٌ
تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٢﴾

12. Siku utakapowaona waumini wanaume na waumini wanawake, nuru yao inakwenda mbele yao, na kuume kwao: Furaha yenu leo ni Bustani zipitiwazo na mito chini yake kukaa humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa.

يَوْمَ يَقُولُ الْمُنَافِقُونَ وَالْمُنَافِقَاتُ لِلَّذِينَ آمَنُوا انظُرُونَا نَقْتَبِسْ مِن نُّورِكُمْ قِيلَ ارْجِعُوا وَرَاءَكُمْ
فَالْتَمِسُوا نُورًا فَضُرِبَ بَيْنَهُم بِسُورٍ لَّهُ بَابٌ بَاطِنُهُ فِيهِ الرَّحْمَةُ وَظَاهِرُهُ مِن قِبَلِهِ الْعَذَابُ ﴿١٣﴾

13. Siku wanafiki wanaume na wanafiki wanawake watapowaambia walioamini: Tuangalieni ili tupate mwangaza katika nuru yenu. waambiwe: Rejeeni nyuma yenu mkaitafute nuru! Utiwe baina yao ukuta wenye mlango - ndani yake mna rehema, na upande wake wa nje kuna adhabu.

يُنَادُونَهُمْ أَلَمْ نَكُن مَّعَكُمْ قَالُوا بَلَىٰ وَ لَـٰكِنَّكُمْ فَتَنتُمْ أَنفُسَكُمْ وَتَرَبَّصْتُمْ وَارْتَبْتُمْ
وَغَرَّتْكُمُ الْأَمَانِيُّ حَتَّىٰ جَاءَ أَمْرُ اللَّـهِ وَغَرَّكُم بِاللَّـهِ الْغَرُورُ ﴿١٤﴾

14. Watawaita wawaambie: Kwani hatukuwa pamoja nanyi? Watawaambia: Ndiyo, lakini mlijifitini wenyewe, na mkangojea, na mkatia shaka na matamanio yakawadanganya, Mpaka ilipokuja amri ya Mwenyezi Mungu ya na mdanganyifu akawadanganya katika Mwenyezi Mungu.

فَالْيَوْمَ لَا يُؤْخَذُ مِنكُمْ فِدْيَةٌ وَلَا مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا مَأْوَاكُمُ النَّارُ هِيَ مَوْلَاكُمْ وَبِئْسَ
الْمَصِيرُ ﴿١٥﴾

15. Basi leo haitapokelewa kwenu fidia, Wala kwa wale walio kufuru. Makaazi yenu ni Motoni; na ni marejeo maovu yalioje!

### NDANI YAKE NI REHMA NA NJE YAKE NI ADHABU

**Aya 12 – 15**

### MAANA

Katika Aya iliyotangulia Mwenyezi Mungu (s.w.t) amesema kuwa mwenye kuamini na akatoa sabili kwa ajili ya radhi yake Mwenyezi Mungu Mtukufu, atakuwa na ujira mzuri. Sasa hapa anaubainisha ujira huo kwa kusema:

Siku utakapowaona waumini wanaume na waumini wanawake, nuru yao inakwenda mbele yao, na kuume kwao:

Wenye takuwa waliojitolea, dunini walikuwa wakienda kwa mwongozo wa Mola wao. Siku ya hisabu na malipo mwongozo huu wa Mwenyezi Mungu utawaangazia mwanga hasa wa kuhisiwa, kama inavyoashiria Aya kwa neno utawaona na neno kuume kwao; yaani utaona nuru yao kwa macho yako; kama unavyoona taa anavyoichukuwa mtu mkononi na kuifanya anavyotaka.

Kwa maneno mengine ni kuwa, waliifanyia kazi nuru hii duniani kwa bidii na ikhlasi, wakaikuta Akhera iko mbele yao ikiwangazia masafa.

Furaha yenu leo ni Bustani zipitiwazo na mito chini yake kukaa humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa.

Kesho waongofu watatoka makaburini mwao na kutembea kwenye mwangaza utakaowafichulia njia ya amani. Na kabla ya kufika mwisho utawajia mwito: Furahini kwa Pepo. Kuna furaha gani zaidi inayoweza kulingana na Pepo ya milele na neema yake? Na ni kufuzu gani kukubwa kuliko huku?

Siku wanafiki wanaume na wanafiki wanawake watapowaambia walioamini: Tuangalieni ili tupate mwangaza katika nuru yenu.

Neno kuangalia tulilolifasiri kutokana na neno la kiarabu nadhr lina maana ya kuona kwa macho, kutaamali au kuhurumia[1]1. Sio mbali kuwa maana ya kuangalia hapa ni hii ya kuhurumia. Mwenyezi Mungu (s.w.t) amelitumia neno hili kwa maana haya ya kuhurumia aliposema:

وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّـهُ وَلَا يَنظُرُ إِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ﴿٧٧﴾

"Wala Mwenyezi Mungu hatasema nao wala hatawaangalia." Juz. 3 (3:77).

Waongofu duniani walikuwa kwenye nuru ya Mola wao na Akhera watakuwa hivyo hivyo:

وَالَّذِينَ اهْتَدَوْا زَادَهُمْ هُدًى وَآتَاهُمْ تَقْوَاهُمْ ﴿١٧﴾

"Na ambao wameongoka anawazidishia uongofu wao na anawapa takua yao" Juz.26 (47:17).

Na wanafiki duniani walikuwa katika viza vya hawaa na mtamanio, basi wao siku ya kiyama watakuwa kwenye giza juu ya giza:

وَمَن كَانَ فِي هَـٰذِهِ أَعْمَىٰ فَهُوَ فِي الْآخِرَةِ أَعْمَىٰ وَأَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٧٢﴾

"Na aliyekuwa kipofu katika hii, basi Akhera atakuwa kipofu zaidi na aliyepotea njia."

Juz. 15 (17:72).

Hekima yake Mwenyezi Mungu Mtukufu imetaka wanafiki waone nuru ya waongofu ikiwaangazia mbele yao, ili wazidi uchungu juu ya uchungu; kisha uchungu utazidi pale watakapotaka usaidizi kwa waumini kuwa waende kwenye njia yao waambiwe: Rejeeni nyuma yenu mkaitafute nuru!

Hili ndilo jawabu lao: rudini kwa rafiki yenu shetani na mtafute nuru kutoka kwake. Yuko nyuma yenu leo kama alivyokuwa nyuma yenu jana.

Nuru hii ni ya yule aliyeifanyia kazi duniani na katika Akhera yake. Mwenye kuyanunua maisha ya dunia kwa Akhera, basi hatatoka katika giza isipokuwa kwenye ubaya zaidi.

Utiwe baina yao ukuta wenye mlango - ndani yake mna rehema, na upande wake wa nje kuna adhabu.

Makusudio ya ukuta ni kizuizi na rehema ni Pepo. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu amewaneemesha waumini kwa Pepo na akawaadhibu wanafiki kwa adhabu ya Moto. Baina ya Pepo na Moto kuna kizuizi kilicho na pande mbili.

1.Hata kwenye lugha ya kiswahili pia kuangalia kuna maana hayo –Mtarjumu.

Watawaita wawaambie: Kwani hatukuwa pamoja nanyi?

Wanafiki watazungumza kwa lugha ya maneno au lugha ya hali kuwa sisi duniani tulikuwa tukifunga na kuswali na kufanya mliyokuwa mkiyafanya nyinyi, kwanini nyinyi mmeingia Peponi na sisi tukaingia motoni?

Watawaambia: Ndiyo, lakini mlijifitini wenyewe.

Makusudio ya kujifitini ni kujiangamiza. Waumini watawajibu, ndio mlikuwa pamoja na sisi mkifunga na kuswali, lakini mliziangamiza nafsi zenu kwa uwongo na unafiki na mkangojea balaa iwafike waumini, na mkatia shaka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kauli zake, na matamanio yakawadanganya, pale mlipodhani kwamba hadaa yenu na unafi- ki wenu utawavusha salama bila ya hisabu na adhabu.

Mpaka ilipokuja amri ya Mwenyezi Mungu ya kukutana naye kwa hisabu na malipo, na mdanganyifu akawadanganya katika Mwenyezi Mungu na mkamsadiki shetani na ahadi yake kuwa mtasalimika na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu na adhabu yake.

Basi leo haitapokelewa kwenu fidia, wala kukubaliwa toba wala hamtaweza kuikimbia adhabu:

فَلَن يُقْبَلَ مِنْ أَحَدِهِم مِّلْءُ الْأَرْضِ ذَهَبًا وَلَوِ افْتَدَىٰ بِهِ ۗ أُولَـٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ وَمَا لَهُم مِّن نَّاصِرِينَ ﴿٩١﴾

"Basi haitakubaliwa kwa yeyote katika wao hata fidia ya dhahabu kwa kujaza ardhi lau angelitoa. Hao watapata adhabu iumizayo, wala hawatakua na wasaidizi." Juz. 3 (3:91).

Wala kwa wale walio kufuru.

Vile vile haitakubaliwa fidia na toba kutoka kwa wale waliodhihirisha kufuru bila ya kufanya hadaa na unafiki kama nyinyi.

Makaazi yenu ni Motoni. Hakuna kukimbia wala usaidizi isipokuwa Jahannam ndio bora kwenu; na ni marejeo maovu yalioje!

أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ آمَنُوا أَن تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ اللَّـهِ وَمَا نَزَلَ مِنَ الْحَقِّ وَلَا يَكُونُوا كَالَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلُ فَطَالَ عَلَيْهِمُ الْأَمَدُ فَقَسَتْ قُلُوبُهُمْ ۖ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ فَاسِقُونَ ﴿١٦﴾

16. Je, bado haujafika wakati kwa walioamini zikanyenyekea nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na haki iliyoteremka? Wala wasiwe kama waliopewa Kitabu kabla yao, muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikasusuwaa, na wengi wao ni mafasiki.

اعْلَمُوا أَنَّ اللَّـهَ يُحْيِي الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا ۚ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ ﴿١٧﴾

17. Jueni kwamba Mwenyezi Mungu huifufua ardhi baada ya kufa kwake. Tumewabainishia Ishara ili mpate kutia akili.

إِنَّ الْمُصَّدِّقِينَ وَالْمُصَّدِّقَاتِ وَأَقْرَضُوا اللَّـهَ قَرْضًا حَسَنًا يُضَاعَفُ لَهُمْ وَلَهُمْ أَجْرٌ كَرِيمٌ ﴿١٨﴾

18. Kwa hakika wanaume wanaotoa sadaka, na wanawake wanaotoa sadaka, na wakamkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mzuri, watazidishiwa maradufu na watapata ujira mzuri.

وَالَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّـهِ وَرُسُلِهِ أُولَـٰئِكَ هُمُ الصِّدِّيقُونَ ۖ وَالشُّهَدَاءُ عِندَ رَبِّهِمْ لَهُمْ أَجْرُهُمْ وَنُورُهُمْ ۖ وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَـٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿١٩﴾

19. Na waliomwamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake, hao ndio wakweli hasa; Na Mashahidi mbele ya Mola wao, watapata ujira wao na nuru yao. Na waliokufuru na wakakadhibisha Ishara zetu, hao ndio watu wa Motoni.

## JE, BADO HAUJAFIKA WAKATI KWA WALIOAMINI

**Aya 16 – 19**

### MAANA

Je, bado haujafika wakati kwa walioamini zikanyenyekea nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na haki iliyoteremka?

Kuunganisha haki iliyoteremka juu ya kumbuka Mwenyezi Mungu ni kwa kitafsiri; kwamba hakuna tofauti baina ya kinachounganishwa na kinachounganisha isipokuwa matamshi tu. Makusudio ya walioamini ni kundi katika wao.

Kabla ya kuleta ubainifu wa Aya, tunatanguliza maelezo kuwa imani inatofautiana kwa nguvu na udhaifu. Kuanzia imani inayomwajibisha aliye nayo kuwa maasumu; kama manabii; hadi imani ya uaminifu; kama vile baadhi ya maswahaba, hadi walio na daraja ya chini na kuendela chini zaidi.

Makusudio ya walioamini hapa ni wale waliotosheka na imani ya juu juu sio ya ndani na kwa dhahiri sio kwa hali halisi, wala haliwashughulishi jambo lolote la watu na masilahi ya umma.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amelizindua kundi hili la waumini kwenye Aya za jihadi alizoziteremsha katika Kitabu chake na kuhimiza kufanya uadilifu, kuinusuru haki na watu wake na kuwasuluhishia watu. Amewazindua kwenye hakika ya dini kwa mfumo huu wa upole 'Je, bado haujafika wakati,' ili waweze kusikia na kuwa na akili?

Wala wasiwe kama waliopewa Kitabu kabla yao, muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikasusuwaa.

Watu wa Kitabu ni wayahudi na wanaswara. Kususuwaa nyoyo zao ni kinaya cha kugeuka kwao baada ya Musa. Vile vile wanaswara baada ya Isa, basi nanyi waislamu msigeuke baada ya Muhammad **(s.a.w.w)**; kama walivyogeuka watu wa Kitab hapo mwanzo. Mfano wa Aya ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِ الرُّسُلُ أَفَإِن مَّاتَ أَوْ قُتِلَ انقَلَبْتُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ ﴿١٤٤﴾

"Hakuwa Muhammad ila ni Mtume; wamekwishapita Mitume kabla yake. Je, akifa au akiuliwa mtarudi nyuma? Juz. 4 (3:144)

Na wengi wao ni mafasiki.

Makusudio ya ya wengi ni viongozi wa kiyahudi na kinaswara (kikiristo) walioipotoa Tawrat na Injil kwa kupupia vyeo na chumo.

Jueni kwamba Mwenyezi Mungu huifufua ardhi baada ya kufa kwake.

Wafasiri wengi wamesema kuwa huku ni kufananisha nyoyo zilizosusuwaa na ardhi iliyokufa na kwamba Yeye Mwenyezi Mungu anaipa uhai ardhi kwa mvua vile vile ataziongoza nyoyo zilizosusuwaa kwa mawaidha.

Tuonavyo sisi ni kuwa huu ni utisho na onyo kwa wale watakaogeuka baada ya Muhammad **(s.a.w.w)** – kwamba Yeye Mwenyezi Mungu

Mtukufu atawafufua; sawa na anavyoifufua ardhi, na atawalipa kuritadi kwao baada ya nabii wao.

Maana haya yanatiwa nguvu na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu iliyokuja moja kwa moja inayosema: Tumewabainishia Ishara ili mpate kutia akili. Hakika nyinyi mtaulizwa siku ya Kiyama yale mliyoyazusha baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**.

Kwa hakika wanaume wanaotoa sadaka, na wanawake wanaotoa sadaka, na wakamkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mzuri, watazidishiwa maradufu na watapata ujira mzuri.

Husomwa bila ya shadda katika herufi swad kwa maana ya waumini na husomwa kwa shadda kwa maana ya wanaotoa sadaka.

Makusudio ya mkopo mwema ni kutoa sadaka kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa hiyo hakuna kukaririka. Makusudio ya ujira mzuri ni kuwa nuru yao iko mbele yao siku ya Kiyama kuongezea mahurilaini makasri n.k.

Umetangulia mfano wake katika Aya 11 ya sura hii na Juz. 2 (2:245)

Na waliomwamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na wakatenda kwa mujibu wa imani yao, hao ndio wakweli hasa; yaani waliodumu na ukweli katika imani yao kwa kauli na vitendo, na ukweli ni njia ya uokovu kwa kila maangamizi.

Na Mashahidi mbele ya Mola wao, watapata ujira wao na nuru yao.

Mashahidi ni wale waliouliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu. Ama ujira wao mbele ya Mola wao, ameibainisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa kauli yake: "Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwamba wao wapate Pepo, wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, kwa hiyo wanaua na kuuawa. Ni ahadi aliyojilazimisha kwa haki katika Tawrat na Injil na Qur'an."Juz. 11 (9:111).

Ama nuru yao ameiashiria katika Aya ya 12 ya sura hii. Mtume **(s.a.w.w)** anasema: "Hakuna yeyote atayeingia Peponi kisha akapenda kutoka kwenda duniani, hata kama atakuwa na ardhi na vilivyomo ndani yake, isipokuwa shahidi. Atatamani arudi duniani auawe mara kumi, kutokana na karama aliyoiona kwa Mwenyezi Mungu.

Na waliokufuru na wakakadhibisha Ishara zetu, hao ndio watu wa Motoni.

Hii ni desturi ya Qur'an kulinganisha wenye takuwa na wakosefu na thawabu zao na adhabu zao kwa kusudia kupendekeza na kuhadharisha.

Umetangulia mfano wake katika Aya kadhaa; ikiwemo ile iliyo katika Juz.7 (6:32). Dunia inayoshutumiwa katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kupitia kwa mitume wake, ni ile dunia inayotafutiwa matamanio, starehe, mchezo, upuzi, kiburi na kujifaharisha. Ama dunia ambayo haja za wahitaji zinatekelezwa, udhalimu unapingwa na kunufaika ndani ya dunia hiyo na Akhera, basi hiyo haishutumiwi.

# TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

اعْلَمُوا أَنَّمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَلَهْوٌ وَزِينَةٌ وَتَفَاخُرٌ بَيْنَكُمْ وَتَكَاثُرٌ فِي الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ ۖ كَمَثَلِ غَيْثٍ أَعْجَبَ الْكُفَّارَ نَبَاتُهُ ثُمَّ يَهِيجُ فَتَرَاهُ مُصْفَرًّا ثُمَّ يَكُونُ حُطَامًا ۖ وَفِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ شَدِيدٌ وَمَغْفِرَةٌ مِّنَ اللَّهِ وَرِضْوَانٌ ۚ وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ ﴿٢٠﴾

20. Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo, na upuzi, na pambo, na kujifaharisha baina yenu na kushindana kwa wingi wa mali na watoto. Ni kama mfano wa mvua ambayo huwafurahisha wakulima mimea yake, kisha hunyauka ukayaona yana rangi ya njano kisha yakawa makapi. Na akhera kuna adhabu kali na maghufira kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi. Na maisha ya dunia si chochote ila ni starehe ya udanganyifu.

سَابِقُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا كَعَرْضِ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أُعِدَّتْ لِلَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ ۚ ذَٰلِكَ فَضْلُ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ ۚ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٢١﴾

21. Kimbilieni maghufira ya Mola wenu, na Pepo ambayo upana wake ni kama upana wa mbingu na ardhi, iliyowekewa waliomwamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake. Hiyo ndiyo fadhila ya Mwenyezi Mungu, humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu.

مَا أَصَابَ مِن مُّصِيبَةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي أَنفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَابٍ مِّن قَبْلِ أَن نَّبْرَأَهَا ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٢٢﴾

22. Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwishaandikwa katika Kitabu kabla hatujaziumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.

لِّكَيْلَا تَأْسَوْا عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ وَلَا تَفْرَحُوا بِمَا آتَاكُمْ ۗ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿٢٣﴾

23. Ili msihuzunike kwa kilicho wapotea, wala msifurahi kwa alichowapa. Na Mwenyezi Mungu hampendi kila anayejivuna, anayejifaharisha.

الَّذِينَ يَبْخَلُونَ وَيَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبُخْلِ ۗ وَمَن يَتَوَلَّ فَإِنَّ اللَّهَ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٢٤﴾

24. Ambao wanafanya ubakhili, na wanaamrisha watu wafanye ubakhili. Na anayegeuka, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha, Msifiwa.

## MAISHA YA DUNIA NI MCHEZO NA UPUZI

**Aya 20 – 24**

### MAANA

Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo, na upuzi, na pambo, na kujifaharisha baina yenu na kushindana kwa wingi wa mali na watoto.

Mwenye kufuatilia Aya za Qur'an yenye hikima, ataona kuwa thawabu za Mwenyezi Mungu zimewekewa wanaoamini, wakatenda mema duniani na wakatekeleza haki na wajibu; na kwamba hakuna nyenzo ya kufikia wema wa Akhera isipokuwa kazi ya manufaa katika maisha ya dunia.

Ni kama mfano wa mvua ambayo huwafurahisha wakulima mimea yake, kisha hunyauka ukayaona yana rangi ya njano kisha yakawa makapi.

Sifa hii inalingana na dunia kwa sababu haiudumu kwenye hali moja. Inakuwa kijani kisha manjano, inakuwa ngumu kisha laini na inatoa na kuzuia. Lau itampa mtu kila analolipenda, basi muda mchache tu inamnyang'anya kila kitu mpaka maisha yake yeye mwenyewe na ya watu wake.

Vile vile mfano unaendana na sifa za mtu duniani. Anakuwa kijana mwenye nguvu ya mifupa, kushupaa nyama yake na kuwa nyororo ngozi; kisha anazeeka na kuwa mnyonge, nyama zinasinyaa, mifupa inakuwa dhaifu na ngozi kuwa manjano. Kila siku zinavyoendelea ndivyo anavyozidi kuwa katika hali mbaya mpaka anakuwa kama makapi na kumalizika.

Ikiwa dunia iko hivi na mtu naye anakuwa hivyo, basi lililo bora kwake ni kuyafanyia kazi maisha ya daima isiyokwisha neema yake wala kuzeeka mkazi wake.

Na akhera kuna adhabu kali na maghufira kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kutaja kuwa dunia haidumu raha yake wala tabu yake, sasa anataja kuwa Akhera ni thabiti kwenye hali moja tu. Neema yake ni ya kudumu na adhabu yake pia ni ya kudumu. Kwa vile inayosababisha neema ni radhi ya Mwenyezi Mungu na sababu ya moto ni ghadhabu zake na zote hizo ziko.

Na maisha ya dunia si chochote ila ni starehe ya udanganyifu.

Razi anamnukuu sahaba mtukufu Said bin Jubayr, kwamba amesema katika kufasiri Aya hii: "Dunia ni starehe ya udanganyifu kama ikikufanya upuuze kuitafuta Akhera, lakini kama itakupa mwito wa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu na kuitafuta Akhera, basi itakuwa ni starehe nzuri na nyenzo bora."

Sahaba huyu mtukufu ni katika wanafunzi wa Mtume **(s.a.w.w)** waliokuwa karibu naye.

Kimbilieni maghufira ya Mola wenu, na Pepo ambayo upana wake ni kama upana wa mbingu na ardhi, iliyowekewa waliomwamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake.

Makusudio ya maghufira hapa ni sababu zake; kama vile toba na matendo mema. Baadhi ya wafasiri wamesema, ikiwa upana ni hivyo je, urefu? Wengine wakasema: imegunduliwa kuwa umbali wa ulimwengu hauna mwisho. Kwa hiyo basi upana utakuwa ni wa uhakika sio majazi.

Sisi hatufahamu upana isipokuwa ni ibara ya utukufu wa Pepo na upana wake usiokuwa na kiwango. Umetangulia mfano wake katika Juz. 4 (3:133).

Hiyo ndiyo fadhila ya Mwenyezi Mungu, humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu kwa watu, lakini watu wengi hawashukuru.

Hakuna mwenye shaka kwamba utiifu ni sababu ya kuzidishiwa fadhila, bali ndio sababu ya fadhila ya Mwenyezi Mungu na radhi yake siku ya hukumu.

Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwishaandikwa katika Kitabu kabla hatujaziumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.

Maana ya dhahiri ya Aya hii yanaonyesha kuwa masaibu yote yanatoka kwa Mwenyezi Mungu; ni sawa yawe ni katika aina ya majanga ya

maumbile; kama matetemeko na mafuriko, au yawe ya kijamii; kama vile vita ufukara na uadui.

Lakini haya siyo makusudio yake moja kwa moja kwa hukumu ya wahyi na akili. Ufafunuzi ni kama ufuatavyo:-

## MASAIBU NA MWENYE IDHLAL

Mwenye Idhlal katika kufasiri Aya hii anasema: "Tamko kwa kuliachia kilugha halihusiani na heri au shari. Kila msiba unaotokea kwenye ardhi yote au kwenye nafsi ya mtu au wanaoambiwa, utakua uko katika kitabu tangu azali kabla ya kudhihiri ardhi na kudhihiri nafsi."

Tunamuuliza mwenye Idhlal: ukiwa kweli unategemea dhahiri ya tamko na kuliachia kilugha, mbona hukufanya hivyo ulipokuwa unafasiri Aya hii: "Na misiba iliyowasibu ni kwa sababu ya ilivyotenda mikono yenu." Juz. 25 (42:30). Je, umesahau katika tafsiri yako kuwa ulisema ninanunukuu: "Kila msiba uliomsibu mtu una sababu zake kutokana na ilivyofanya mikono yake." Jalada la 7, uk.38, Juzuu ya 25.

Je, utakuwa unategemea dhahiri ya tamko na kuliachia kilugha hata kama hilo litafanya Aya mbili zigongane?

Je, pia utategemea dhahiri ya tamko likiwa litagongana na hukumu ya akili na uhalisia, na kufahamisha kuwa Mwenyezi Mungu ana mkono, uso, usikizi na macho?

Je, uzayuni na ukoloni ambao ni chimbuko la masaibu na mabalaa yanayopatikana hivi sasa yanatokana na wao au yanotokana na Mwenyezi Mungu?

Ni jambo lisilowezekana kutokea mgongano baina ya Aya mbili kiuhakika ni kiuhalisi. Pia ni jambo lisilowezekana kugongana Aya na hukumu ya akili. Itakuwaje hivyo na hali imetokea kwa mwenye hikima mwenye ujuzi?

Ikitokea dhahiri ya Aya kugongana na Aya nyingine au kugongana na hukumu ya kiakili, tutajua dhahiri hii siyo aliyoikusudia Mwenyezi Mungu Mtukufu; isipokuwa ameliachia tamko kutegemea desturi yake ya kuleta ibara; kama kuleta ibara ya watu wa Kitabu kwa maana ya mayahudi na wanaswara. Au kuleta ibara kutokana na ilivyozoeleka kiakili; kama uweza wa Mwenyezi Mungu kuuletea ibara ya mkono. Au kuleta ibara kutegema Aya nyingine; kama Aya hizi zifuatazo:-

وَمَا أَصَابَكُم مِّن مُّصِيبَةٍ فَبِمَا كَسَبَتْ أَيْدِيكُمْ ﴿٣٠﴾

"Na misiba iliyowasibu ni kwa sababu ya ilivyotenda mikono yenu." Juz. 25 (42:30).

وَمَا ظَلَمَهُمُ اللَّـهُ وَلَـٰكِنْ أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿١١٧﴾

"Na Mwenyezi Mungu hakuwadhulumu, lakini wanajidhulumu wenyewe." Juz. 4 (3:117).

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ ﴿٤١﴾

"Ufisadi umedhihiri bara na baharini kwa sababu ya iliyoyafanya mikono ya watu."

Juz.21 (30:41).

Aya zote hizi na maana yake ni dalili mkataa kwamba makusudio ya Aya tuliyonayo siyo ya kidhahiri ya lugha na kwamba Mwenyezi Mungu ameiacha hivyo kwa kutegema aliyoyasema katika Aya hizo nyingine.

Kwa hiyo basi makusudio ya misiba ya ardhi, katika Aya tuliyonayo, ni majanga ya kimaumbile; kama vile matetemeko n.k. Na makusudio ya masaibu ya nafsi ni baadhi ya magonjwa yasiyokuwa na kinga wala hadhari n.k.

Ama makusudio ya misiba katika Aya zile tatu ni masaibu yanayotokana na binadamu mwenyewe; kama vile dhulma vita njaa n.k.

Ili msihuzunike kwa kilichowapotea, wala msifurahi kwa alichowapa.

Imam Aliy (a.s) anasema: "Zuhudi yote iko katika matamshi mawili katika Qur'an; kisha akasoma Aya hii na akaendelea kusema: "Asiyekata tamaa kwa yaliyopita wala asifurahi kwa yanayokuja atakuwa ameichukua zuhudi kwa pande zake mbili."

Hakuna asiyehuzunika na kufurahi; hata mitume pia. Isipokuwa makusudio ni furaha isimwingize mtu kwenye batili na huzuni isimtoe kwenye haki. Imethibiti kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kwamba yeye alisema wakati wa mauti ya mwanawe Ibrahim: **"Jicho linalia na moyo unahuzunika wala hatusemi isipokuwa yanayomridhisha Mola wetu. Nasi tunakuhuzunikia ewe Ibrahim."**

Na Mwenyezi Mungu hampendi kila anayejivuna, anayejifaharisha.

Hakuna kitu kinachofahamisha ujinga kuliko kiburi na kujiona. Imam Aliy (a.s) anasema: "Ana nini binadamu na kujifaharisha? Mwanzo wake ni tone la manii na mwisho wake ni mzoga. Hawezi kujipa riziki wala kujikinga na mauti."

Ambao wanafanya ubakhili, na wanaamrisha watu wafanye ubakhili.

Anayefanya ubakhili na akawaamuru wengine wafanye ubakhili, ndiye aliyekusudiwa katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

مَّنَّاعٍ لِّلْخَيْرِ مُعْتَدٍ أَثِيمٍ ﴿١٢﴾ عُتُلٍّ بَعْدَ ذَٰلِكَ زَنِيمٍ ﴿١٣﴾

"Mwenye kuzuia heri arukaye mipaka mwenye dhambi, mgumu, juu ya hayo ni mshenzi."

(68:12-13).

Razi anasema hizi ni sifa za mayahudi. Ikumbukwe kuwa Razi alifariki mwaka 606 AH.

Umetangulia mfano wake katika Juz. 5 (4:37).

Na anayegeuka, basi Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujitosha, Msifiwa.

Bakhili hajidhuru ila yeye mwenyewe, na Mwenyezi Mungu (s.w.t) hayamdhuru maasi ya mwenye kuasi wala haumnufaishi utiifu wa mwenye kutii. Umetangulia mfano wake katika Juz. 26 (47:37).

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ ۖ وَأَنزَلْنَا الْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنَافِعُ لِلنَّاسِ وَلِيَعْلَمَ اللَّـهُ مَن يَنصُرُهُ وَرُسُلَهُ بِالْغَيْبِ ۚ إِنَّ اللَّـهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢٥﴾

Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili wazi wazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na mizani, ili watu wasimamie uadilifu, na tumeteremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu, na ili

Mwenyezi Mungu amjue anayemnusuru Yeye na Mitume wake kwa ghaibu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye kushinda.

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا وَإِبْرَاهِيمَ وَجَعَلْنَا فِي ذُرِّيَّتِهِمَا النُّبُوَّةَ وَالْكِتَابَ فَمِنْهُم مُّهْتَدٍ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ
فَاسِقُونَ ﴿٢٦﴾

26. Na hakika tulimtuma Nuh na Ibrahim, na tukaweka katika dhuriya zao Unabii na Kitabu. Basi wapo miongoni mwao walioongoka, na wengi katika wao ni mafasiki.

ثُمَّ قَفَّيْنَا عَلَىٰ آثَارِهِم بِرُسُلِنَا وَقَفَّيْنَا بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ وَآتَيْنَاهُ الْإِنجِيلَ وَجَعَلْنَا فِي قُلُوبِ الَّذِينَ
اتَّبَعُوهُ رَأْفَةً وَرَحْمَةً وَرَهْبَانِيَّةً ابْتَدَعُوهَا مَا كَتَبْنَاهَا عَلَيْهِمْ إِلَّا ابْتِغَاءَ رِضْوَانِ اللَّـهِ فَمَا رَعَوْهَا حَقَّ
رِعَايَتِهَا فَآتَيْنَا الَّذِينَ آمَنُوا مِنْهُمْ أَجْرَهُمْ وَكَثِيرٌ مِّنْهُمْ فَاسِقُونَ ﴿٢٧﴾

27. Kisha tukafuatisha nyuma yao Mitume wetu, na tukamfuatisha Isa bin Maryam, na tukampa Injili. Na tukajaalia katika nyoyo za waliomfuata upole na rehema. Na utawa wameuzua wao. Hatukuwaandikia hayo, ila kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Lakini hawakuufuata inavyotakiwa kuufuata. Basi wale walioamini katika wao tuliwapa ujira wao. Na wengi wao ni mafasiki.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّـهَ وَآمِنُوا بِرَسُولِهِ يُؤْتِكُمْ كِفْلَيْنِ مِن رَّحْمَتِهِ وَيَجْعَل لَّكُمْ نُورًا
تَمْشُونَ بِهِ وَيَغْفِرْ لَكُمْ وَاللَّـهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٨﴾

28. Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na muaminini Mtume wake, atawapa sehemu mbili katika rehema yake, na atawajaalia muwe na nuru ya kwenda nayo, na atawaghufiria. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

لِّئَلَّا يَعْلَمَ أَهْلُ الْكِتَابِ أَلَّا يَقْدِرُونَ عَلَىٰ شَيْءٍ مِّن فَضْلِ اللَّـهِ وَأَنَّ الْفَضْلَ بِيَدِ اللَّـهِ يُؤْتِيهِ مَن
يَشَاءُ وَاللَّـهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٢٩﴾

29. Ili watu wa Kitabu wajue kwamba wao hawana uweza wowote juu ya fadhila za Mwenyezi Mungu. Na fadhila zote zimo mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye fadhila kuu.

## CHUMA KINA NGUVU NYINGI

**Aya 25 – 29**

### MAANA

Kwa hakika tuliwatuma Mitume wetu kwa dalili waziwazi, na tukateremsha Kitabu pamoja nao na Mizani, ili watu wasimamie uadilifu.

Kila ambalo unajulikana uhakika kwalo basi hilo ni mizani, ni sawa uwe ni wahyi, akili au hisia; kama vile majaribio na ushuhuda. kwa hiyo basi kuunganisha mizani kwenye Kitabu ni kuunganisha mahsusi kwenye ujumla; mfano wa kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: “Na alichopewa Musa na Isa na manabii kutoka kwa Mola wao.”

Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu aliwatuma mitume kwa hoja zinazojulisha juu ya utume wao na risala yao na kwa lile litakalowaongoza watu kwenye haki na uadilifu, ili wawe katika njia iliyonyooka.

Na tumeteremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu.

Wafasiri wa kale walisema katika kufasiri Aya hii kuwa chuma ni nguvu katika vita, watu wanatengeneza panga na diraya. Pia wanatengeneza visu shoka na sindano. Mifano hii ilikuja kuakisi zama zao na maisha yao. Sisi tungelikuwa wakati wao, nasi tungelisema kama walivyosema. Na wao wangelikuwa zama zetu wangelisema: Chuma ni uti wa mgongo wa maisha katika nyanja zote.

Nyenzo za mawasiliano ya nchi kavu angani na baharini zinatokana nacho. Pia vyombo kadha anavyovihitaji mtu tajiri au fukara, madaraja, majengo, kuta na maghala, vyote vinahitajia chuma. Lau si chuma mtu asingelijua umeme na petrol. Chuma ni msingi wa ilimu nyinyi za kisasa, bali ndio kila kitu cha maendeleo ya karne ya ishirini.

Na ili Mwenyezi Mungu amjue anayemnusuru Yeye na Mitume wake kwa ghaibu.

Yaani atakayenusuru mafunzo ya mitume wa Mwenyezi Mungu hata kama hakuwaona.

Kila kitu katika maisha haya kina pande mbili: chanya na hasi; manufaa na madhara. Ikiwa chuma kina manufaa hayo, ya kumhudumia mtu, tuliyoyataja, basi vie vile kina madhara ya kumwangamiza mtu. Kabla ya kugunduliwa chuma mauji yalikuwa ni kwa makumi, lakini baada ya kugunduliwa mauji yamekuwa kwa mamilioni.

Hofu na utisho wanaoishi nao wa magharibi na wa mashariki, damu inayomwagika kama mito huko Cambodia, Laos, Vietnam, Guatemala na mashariki ya kati[1], maangamizi yote haya na mengineyo ni natija ya nguvu ya silaha ya shari ya chuma dhidi ya wananchi na harakati za ukombozi.

Hapa ndio tunatambua siri ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na tumeteremsha chuma chenye nguvu nyingi na manufaa kwa watu. Na ili Mwenyezi Mungu amjue anayemnusuru Yeye na Mitume wake kwa ghaibu."

Yaani ameumba chuma ili awatie mtihani waja wake kwa yaliyomo ndani ya nyoyo zao ya heri na shari, na kudhihirisha wazi kwenye ulimwengu, ili apambanuke muovu ambaye anaifanya nguvu ni nyenzo ya kutekeleza matamanio yake na malengo yake, na apambanuke mwema ambaye anaona nguvu ni neema ya Mwenyezi Mungu na kuitumia kwa manufaa ya watu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema yake.

Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mwenye kushinda.

Atawaadhibu mataghuti madhalimu kwa mikono ya wenye haki ambao hawataki katika maisha haya isipokuwa uhuru, uadilifu na kuishi wote kwa utulivu na amani.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa mapinduzi dhidi ya dhulma yanayotokea leo kila pembe ya ardhi. Hakuna mwenye shaka kwamba mapinduzi haya yana nguvu za Mwenyezi Mungu, hayatazuilika maadamu yanatafuta haki na uadilifu. Ama malipo ya mataghuti huko Akhera ni Jahannam, makao mabaya kabisa.

Na hakika tulimtuma Nuh na Ibrahim, na tukaweka katika dhuriya zao Unabii na Kitabu.

---

1. Mwandishi hapa alikuwa katika mwaka wa 1970.

Mwenyezi Mungu alimtuma Nuh na Ibrahim kulingania kwenye haki, kila mmoja akafikisha risala ya Mola wake akapigana jihadi na maadui wa Mwenyezi Mungu; kama ilivyo habari ya Nuh katika Juz. 12 (11:25-49) na kuhusu Ibrahim katika Juz. 17 (21:51-74).

Basi wapo miongoni mwao walioongoka, na wengi katika wao ni wapotovu.

Yaani katika kizazi chao kuna baadhi ni wema, lakini wengi wao walikuwa bila dini wala dhamiri; kama walivyo watoto wa ulama wa dini.

Kisha tukafuatisha nyuma yao Mitume wetu, wengine wengi.

Baada ya Nuh na Ibrahim, Mwenyezi Mungu (s.w.t) alituma mitume wengi; kama vile Hud, Swaleh, Musa n.k.

Na tukamfuatisha Isa bin Maryam, na tukampa Injili.

Waliendelea kufuatana mitume hadi Isa (a.s) akiwa na Injil. Wakati huo ilikuwa ni mwongozo na nuru.

Na tukajaalia katika nyoyo za waliomfuata upole na rehema.

Hao ni wale waliomfuta Bwana Masih na wakayatumia mafunzo yake kwa nukuu na kwa kiroho bila ya kugeuza yale yanayotamaniwa na nafsi zao. Hilo linaashiriwa na neno wakamfuata. Tazama mwanzo wa Juzuu ya saba.

Na utawa wameuzua wao. Hatukuwaandikia hayo, ila kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Lakini hawakuufuata inavyotakiwa kuufuata.

'Ila' hapa ni kwa maana ya lakini. Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu hakuwaelezea utawa, isipokuwa viongozi wa kinaswara ndio waliouanzisha kwa madai kuwa unawakurubisha kwa Mwenyezi Mungu kwa vile unawaweka mbali na dunia na starehe zake.

Pamoja na kuwa Mwenyezi Mungu hakuwaamuru utawa, bali amewahalalishia riziki njema; hata hivyo bado wao hawakujilazimisha na zuhudi ya utawa, bali waliufanya ni nyenzo ya matamanio na kutawala. Aya hii inafahamisha kuwa hakuna utawa katika Uislamu wala katika dini aliyokuja nayo Bwana Masih.

Basi wale walioamini katika wao tuliwapa ujira wao.

Hao ni wale waliokuwa wafuasi wa Isa halisi na ukweli, waliokuwa wakiamini kwa kauli na vitendo kwamba umasihi ni upendo na huruma, ni usafi na ubinadamu, sio ubaguzi na chuki, dhulma na unyanyasaji, vita na mapinduzi, kuanzisha vita na vurugu wala sio silaha za maangamizi. Pia wakaamini kuwa Umasihi sio nembo za uongo kuzuia uhuru, kueneza hofu na wasiwasi katika nyoyo za waja wa Mwenyezi Mungu.

Na wengi wao ni mafasiki wakiongozwa na kambi ya ukoloni mambo leo na maadui nambari moja wa ubinadamu ambao wana sifa zote zinazowatoa kwenye umasihi wa kihaki na ukweli.

Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu.

Yaani enyi ambao mmemkubali Mwenyezi Mungu, fanyeni kwa mujibu wa kuuamini kwenu. wala matendo yenu yasiende kinyume na kauli zenu.

Na muaminini Mtume wake. Mtiini Muhammad **(s.a.w.w)** na mfuate sera yake na mwongozo wake.

Atawapa sehemu mbili katika rehema yake.

Makusudio ya rehema hapa ni thawabu. Maana ni kuwa mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na akatenda kwa mujibu wa

imani yake atakuwa na aina mbili ya tahawabu: thawabu za imani na thawabu za matendo.

Na atawajalia muwe na nuru ya kwenda nayo siku ya Kiyama.

Ambaye Mwenyezi Mungu hatamjalia nuru siku hii atahangaika kwenye giza na atatokeza kwenye machungu.

Na atawaghufiria. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

Atawasamehe maasi yaliyopita, kwa vile Yeye ni mwingi wa maghufira mwenye kurehemu. Ibn Al-arabi anasema katika Futuhat: "Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakutanishi maghufira na toba wala na matendo mema, kwa hiyo hapana budi rehema na maghufira imwendee kwenye kuifanyia israf nafsi yake." Na rehema yake imekienea kila kitu.

Ili watu wa Kitabu wajue kwamba wao hawana uweza wowote juu ya fadhila za Mwenyezi Mungu.

Makusudio ya kuwa hawana uweza ni kuwa wao hawatapata chcochote katika fadhila za Mwenyezi Mungu siku ya kiyama.

Maana ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) kesho atawaghufiria waliomwamini Muhammad **(s.a.w.w)**. Na mwenye kufanya mema atampa ujira wake mara mbili, kwa sababu Yeye Mwenyezi Mungu ni mkarimu. Vile vile wajue mayahudi kuwa na manaswara waliokataa kumwamini Muhammad **(s.a.w.w)** kwamba wao hawana fungu la maghufira na rehema yake, kwa vile wamejizuia kumsadiki Muhammad **(s.a.w.w)**.

Na fadhila zote zimo mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye fadhila kuu.

Anayowafadhili wale ambao wamemwamini Muhammad **(s.a.w.w)**, wala hakuna wa kuzuia alilolitaka, kwa sababu kila kitu kiko mikononi mwake naye ni muweza wa kila kitu.

### SHARTI YA KUCHAPA

Sharti ya kuchapa au kusambaza ni kutaja rejeo hili. haki zote zimehifadhiwa na Taasisi ya Al-Hasanain Taasisi ya Imamu Husein (a.s)

Site ya Al-Imaamaini Al-Hassanaini (a.s) ya usambazaji wa utamaduni wa Kiislamu na mafunzo ya Kidini.

### MWISHO WA JUZUU YA ISHIRINI NA TATU

## YALIYOMO

**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA MBILI** ........ **1**
IMEANDIKWA NA: SHEIKH MUHAMMAD JAWAD MUGHNIYYA ........ 1
IMETAFSIRIWA NA: SHEIKH HASAN MWALUPA ........ 1
IMEHARIRIWA NA: USTADH ABDALLAH MOHAMED ........ 1
IMEPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: UKHT PILI RAJABU ........ 1
UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI ........ 1
MAKOSA YA CHAPA ........ 2
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........ **3**
IKO WAPI DALILI IKIWA NYINYI NI WA KWELI? ........ 3
MAANA ........ 3
KUABUDU MASANAMU WAKATI MAENDELEO YA KUFIKA ANGANI ........ 4
AU WANASEMA WAMEYATUNGA? ........ 6
MAANA ........ 6
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........ **9**
KUWAFANYIA WEMA WAZAZI WAWILI ........ 9
MAANA ........ 9
ALIYEWAAMBIA WAZAZI WAKE AKH! ........ 12
MAANA ........ 12
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........ **14**
HUD ........ 15
MAANA ........ 15
MAJINI WANASIKILZA QUR'AN ........ 17
MAANA ........ 17
JE, HAYA SI KWELI? ........ 19
MAANA ........ 19
MWISHO WA SURA YA ARUBAINI NA SITA: SURAT AL-AHQAF ........ 20
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........ **21**
AMININI TULIYOMTEREMSHIA MUHAMMAD ........ 21
MAANAA ........ 21

24 ........ MKIMNUSURU MWENYEZI MUNGU ATAWANUSURU
24 ........................................................... MAANA
25 ............................................ DOLA YA KIISLAMU
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA**
**28 ........................................................... TATU**
28 ...................................................... SIFA ZA PEPO
28 ........................................................... MAANA
31 ........................................ UTIIFU NA KAULI NJEMA
31 ........................................................... MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA**
**33 ........................................................... TATU**
33 ...................................... JE HAWAIZINGATI QUR'AN?
33 ........................................................... MAANA
36 ..................................... MSIBATILISHE AMALI ZENU
36 ........................................................... MAANA
37 .................................... QUR'AN NA SIASA YA VITA
MWISHO WA SURA YA ARUBAINI NA SABA: SURAT
39 ................................................. MUHAMMAD
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA**
**40 ........................................................... TATU**
40 .............................................. TUMEKUPA USHINDI
40 ........................................................... MAANA
43 ...................................... NA AWAADHIBU WANAFIKI
43 ........................................................... MAANA
44 ............................... BAIA YA RIDHWAN CHINI YA MTI
44 ................................................ KISA KWA UFUPI
46 ............................... MABEDUI WALIOBAKI NYUMA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA**
**48 ........................................................... TATU**
48 .......................................... TUACHENI TUWAFUATE
48 ........................................................... MAANA
50 ..................................... WALIPOKUBAI CHINI YAMTI
50 ........................................................... MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA**
**53 ........................................................... TATU**
53 ....................... WALIOWAZUIA NA MSIKITI MTAKATIFU
53 ........................................................... MAANA
55 .............................................. MRUIYA YA MTUME

MAANA ........................................................ 55
MASWAHABA NA QUR'AN .................................... 56
JE, SHIA ITHANAASHARIA WANA TAFSIRI YA NDANI? .... 58
MWISHO WA SURA YA ARUBAINI NA NANE: SURAT AL-FATH ........................................................ 59
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........................................................ **60**
MSINYANYUE SAUTI ZENU KULIKO SAUTI YA NABII ........ 60
MAANA ........................................................ 60
AKIWAJIA FASIKI NA HABARI YOYOTE, ICHUNGUZENI ..... 62
MAANA ........................................................ 62
MWENYEZI MUNGU AMEWAPENDEKEZEA IMANI ........... 63
MAANA ........................................................ 63
NA IKIWA MAKUNDI MAWILI KATIKA WAUMINI YANAPIGANA ........................................................ 64
MAANA ........................................................ 64
UDUGU WA KIDINI NA UDUGU WA KIBINADAMU ......... 65
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........................................................ **67**
KAUMU ISIDHARAU KAUMU NYINGINE ........................ 67
MAANA ........................................................ 67
VIPI UTAPATA MARAFIKI? .................................... 68
DHANA, UJASUSI NA KUSENGENYA ............................ 69
MAANA ........................................................ 69
DHANA ........................................................ 69
UJASUSI ........................................................ 70
KUSENGENYA .................................................. 71
MTUKUFU ZAIDI YENU NI MWENYE TAKUA ZAIDI .......... 73
MAANA ........................................................ 73
MWISHO WA SURA YA ARUBAINI NA TISA: SURAT AL-HUJURAT ........................................................ 75
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........................................................ **76**
NAAPA KWA QUR'AN TUKUFU .................................. 76
MAANA ........................................................ 76
MWENYE KULA NA MWENYE KULIWA ......................... 77
KWANI TULICHOKA KWA KUUMBA KWA KWANZA? .......... 80
MAANA ........................................................ 80

**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........ **83**
ANAYEKATAZA HERI ........ 83
MAANA ........ 84
SIKU ATAKAPONADI MWENYE KUNADI ........ 87
MAANA ........ 87
MWISHO WA SURA YA HAMSINI: SURAT QAF ........ 88
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........ **89**
NAAPA KWA ZINAZOTAWANYA ........ 89
MAANA ........ 90
HAKI YA MWENYE KUOMBA NA ASIYEOMBA ........ 92
MAANA ........ 92
MWENYEZI MUNGU NA MAARIFA YA HISIA ........ 93
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........ **96**
BASI MAKUSUDIO YENU NI NINI ENYI MLIOTUMWA? ........ 97
MAANA ........ 97
KILA KITU TUMEUMBA DUME NA JIKE ........ 99
MAANA ........ 99
MWISHO WA SURA YA HAMSINI NA MOJA: SURAT ADH-DHARIYAT ........ 102
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........ **103**
NAAPA KWA MLIMA ........ 104
LUGHA ........ 104
MAANA ........ 104
WATU WA PEPONI ........ 106
MAANA ........ 106
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........ **109**
HANA UDHURU MWENYE KUUKANA UTUME WA MUHAMAD ........ 110
MAANA ........ 110
BASI WAACHE MPAKA WAKUTANE NA SIKU YAO ........ 112
MAANA ........ 113
MWISHO WA SURA YA HAMSINI NA MBILI: SURAT AT-TUR ........ 113

**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........................................................... **114**
ALIMWONA KWENYE MKUNAZI WA MWISHO MAANA .... 115
MAANA ........................................................... 115
UMBALI WA PANDE MBILI ................................. 115
LATA NA UZZA ................................................ 118
MAANA ........................................................... 118
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........................................................... **120**
DHANA HAISAIDI KITU MBELE YA HAIFAI .................. 120
MAANA ........................................................... 120
MTU HATAPATA ILA ALIYOYAFANYA ....................... 123
MAANA ........................................................... 123
KWA MOLA WAKO NDIO MWISHO ............................ 125
MAANA ........................................................... 125
MAADA NA MAISHA ........................................... 125
MWISHO WA SURA YA HAMSINI NA TATU: SURAT AN-NAJM ........................................................... 128
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........................................................... **129**
MWEZI UMEPASUKA ........................................... 129
MAANA ........................................................... 129
NUH ............................................................... 132
MAANA ........................................................... 132
HUD NA SWALEH ............................................... 135
MAANA ........................................................... 135
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........................................................... **137**
LUT ............................................................... 137
MAANA ........................................................... 137
KILA KITU TUMEKIUMBA KWA KIPIMO ....................... 140
MAANA ........................................................... 140
MWISHO WA SURA YA HAMSINI NA NNE: SURAT AL-QAMAR ........................................................... 142
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA TATU** ........................................................... **143**
AMEMUUMBA MTU AKAMFUNDISHA UBAINIFU ........... 143
MAANA ........................................................... 143

147 ............................ KILA SIKU YUMO KATIKA MAMBO
147 ........................................................ MAANA
149 ....... MWENYEZI MUNGU NA MTU NA IBN AL-ARABIY
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA**
**151 ........................................................ TATU**
152 ......................... HAMTAPENYA ILA KWA MADARAKA
152 ........................................................ MAANA
156 ..................... HAKUNA MALIPO YA HISANI ILA HISANI
156 ........................................................ MAANA
157 ...................... UJIRA NI HAKI NA ZIADA NI FADHILA
MWISHO WA SURA YA HAMSINI NA TANO: SURAT AR-
159 ........................................................ RAHMAN
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA**
**160 ........................................................ TATU**
161 ........................................ LITAKAPOTUKIA TUKIO
161 ........................................................ MAANA
164 ........................................................ WA KUUME
164 ........................................................ MAANA
166 ............................................... NA WA KUSHOTO
166 ........................................................ MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA**
**168 ........................................................ TATU**
169 ................ JE, MNAONA MAKULIMA MNAYOYAPANDA
169 ........................................................ MAANA
172 ................... HAPANA AIGUSAYE ILA WALIOTAKASWA
172 ........................................................ MAANA
173 ........................................................ LUGHA
173 .......... UISLAMU NA WANAFIKRA WAKUU WA ULAYA
MWISHO WA SURA YA HAMSINI NA SITA: SURAT AL-
177 ........................................................ WAAQIA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA**
**178 ........................................................ TATU**
178 ................ NDIYE WA MWANZO NA NDIYE WA MWISHO
178 ........................................................ MAANA
181 ....... TOENI KATIKA ALIVYOWAFANYA NI WAANGALIZI
181 ........................................................ MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA**
**184 ........................................................ TATU**

184 .........NDANI YAKE NI REHMA NA NJE YAKE NI ADHABU
184 ........................................................ MAANA
187 ......... JE, BADO HAUJAFIKA WAKATI KWA WALIOAMINI
187 ........................................................ MAANA
**TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA ISHIRINI NA**
**189** .............................................................. **TATU**
189 ....................MAISHA YA DUNIA NI MCHEZO NA UPUZI
189 ........................................................ MAANA
191 ............................ MASAIBU NA MWENYE IDHLAL
193 ................................ CHUMA KINA NGUVU NYINGI
193 ........................................................ MAANA
196 ....................................... SHARTI YA KUCHAPA
196 ................ MWISHO WA JUZUU YA ISHIRINI NA TATU
197 .................................................... YALIYOMO